Rehma ya Ajabu

Urithi na Tunu ya Kimaadili
ya Mtume Muhammad ﷺ

Othman Nuri TOPBASH

ERKAM
PUBLICATIONS

Istanbul - 2022

© Kimechapwa na Erkam 2022 / 1443 H

REHMA YA AJABU

Othman Nuri Topbash

Jina la Asili:	Öyle Bir Rahmet ki
Mwandishi:	Othman Nuri Topbash
Msimamizi Mkuu:	Abdi Mohamed Adam
Mfasiri:	Ibrahimu H. Kabuga
Mhariri:	Saad Abdullah
Msanifu jalada:	Altinoluk Graphics
Kupangiliwa vizuri na:	Sarkhan Isgandarov Nijat Garibov
ISBN:	978-9944-83-687-6
Mchapaji:	Erkam Printhouse
Anuani:	Ikitelli Organize Sanayi Bölgesi Mah. Atatürk Bulvarı, Haseyad 1. Kısım No: 60/3-C Başakşehir, Istanbul, Turkey
Simu:	(+90-212) 671-0700 pbx (+90-212) 671-0748
Barua pepe:	info@islamicpublishing.org
Tovuti:	www.islamicpublishing.org
Language:	Swahili / Kiswahili

ERKAM PUBLICATIONS

Rehma ya Ajabu

Urithi na Tunu ya Kimaadili ya Mtume Muhammad ﷺ

Othman Nuri TOPBASH

ERKAM PUBLICATIONS

YALIYOMO

DIBAJI 9
UTANGUL IZI 15
Mifano Kutoka Katika Maisha Ya Mtume ﷺ
FAIDA ZA MAADILI YALIYOTUKUKA – 1 29
Mifano Kutoka Katika Maisha Ya Mtume ﷺ
FAIDA ZA MAADILI YALIYOTUKUKA – 2 45
Mifano Kutoka Katika Maisha Ya Mtume ﷺ
FAIDA ZA MAADILI YALIYOTUKUKA – 3 57
KUWAPENDA WATU WA NYUMBA YA MTUME ﷺ 73
Upendo na Urafiki 73
Watu wa Nyumba ya Mtume (Ahlul-Bayt) 74
Salman ni Katika Sisi 76
Tabia na Mwenendo wa Watu wa Nyumba ya Mtume ﷺ 78
Kuwapenda Watu wa Nyumba Ya Mtume ﷺ 82
Mauaji Yaliyozitikisa Mbingu 83
HAKI NA UADILIFU - 1 87
Kusamehe katika uadilifu 90
HAKI NA UADILIFU - 1 101

Kinyume cha Uadilifu ni Dhulma.....102
Mfano Bora wa Uadilifu.....105
Hata Kama Angekuwa Binti Yangu Fatimah….....105
Kushikamana na Uadilifu.....107
Kuwatendea Uadilifu Watoto.....109
Kutoa Haki kwa umakini kuwapa wale wanaostahiki.....110
Kupinga dhulma na uonevu 113
DHIMA.....119
Msijiangamize.....127
AMANA 135
TAFAKKUR 151
Tafakuri ya Kimaada na Tafakuri ya Kiroho 151
Malezi na Makuzi ya roho.....152
Tafakuri ya Mtukufu Mtume ﷺ..... 155
Uoni wa Kipofu: Mfano wa tafakuri.....157
Kusoma Kitabu cha Maisha na Uhai 157
Kuugundua msingi: Tasawwuf 159
Kukitafakari kifo.....160
MIALE YA HEKMA KUTOKA KATIKA
BUSTANI YA MOYO WA RUMI 165
Subira na Uvumilivu.....168
Kutafuta njia za kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu.....170
Kuitakasa nafsi.....173
Tamaa, saratani ya moyo.....174
Sadaka: ponyo la nyoyo na furaha ya Dunia na Akhera.....177

MWEZI MTUKUFU WA RAMADHAN
Mafunzo ya Kiroho kwa ajili ya Maisha.....181
Qur'an na Mwezi wa Ramadhan 182
Mwezi wa Ramadhan ni fursa ya uhai 183
Kushikamana na Funga.....184
Kuwa Mja Mwenye Udhati wa Moyo (Ikhlas).....187
Usiku wenye Cheo Kitukufu.....191
Sikukuu ya Eid.....193
ISRAFU -1
Katika imani, itikadi na ibada 197
Israfu katika imani na itikadi.....199
Israfu katika Swala 203
ISRAFU -2
Katika muda.....213
Matumizi mabaya (israfu) ya muda.....214
ISRAFU -3
Katika elimu 227
ISRAFU -4
Katika maadili.....245
ISRAFU -5
Katika tafakuri 261
ISRAFU -6
Katika Riziki na Sadaka.....279
ISRAFU -7
Katika Afya na Matumizi ya chakula na Vinywaji 293

"HAKUNA UDHURU WA KUKIUKA MPAKA WA HALALI NA HARAMU"

Mahojiano kuhusu Utambuzi wa Kiislamu Katika Ulimwengu wa Biashara.....309

Kuna aina Ngapi za Kipato? 311

Aina nyingine ni ipi? 311

Uislamu unapendekeza njia gani?.....313

Unashauri uangalifu, umakini na hatua zipi?.....314

Inaonekana kwamba Waislamu wanaoshikamana na maagizo ya kidini sasa wanabadili msimamo wao.....315

Tunawezaje kufanikisha hili, ilhali pesa ni msingi wa ubepari na kila kitu kinatawaliwa na ubepari? 317

Mheshimiwa Ustadh! Kuwa tajiri inaonekana kuwa mtihani mgumu. 318

DIBAJI

Himidi na sifa zote njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehma, Mwenye kurehemu, anayeamiliana nasi kwa huruma na kututendea wema na ukarimu, akatusamehe dhambi na makosa yetu. Rehma na amani ziwe juu ya bwana na mwalimu wetu, Mtume Muhammad ﷺ, aliyetumwa kama rehma kwa walimwengu, na ndiye tabibu, kiongozi na kiombezi wa wanadamu.

Kila kitu ki lichopo ulimwenguni kipo kwa sababu ya upendo na rehma ya Mwenyezi Mungu, Naye huamiliana na wanadamu kwa ukarimu na hisani maalumu. Hata wale wasiokuwa na imani huvuta pumzi na kupata riziki kwa sababu ya rehma na huruma ya Mwenyezi Mungu. Japokuwa ulimwengu hushuhudia aina mbalimbali za ukatili, ufisadi na uasi, lakini ulimwengu huo unaendelea kupata riziki kupitia rehma ya Mwenyezi Mungu isiyokuwa na kikomo.

Ni dhahiri kuwa mwenyezi Mungu anapenda rehma na huruma, kwa maana huruma ya Mwenyezi Mungu inaishinda hasira na ghadhabu Yake. Mwenyezi Mungu anamsifu na kumuelezea mjumbe Wake wa mwisho, Mtume Muhammad ﷺ[1] kuwa ni rehma kwa

1. *Salla Allahu 'alayhi wa sallam,* ni dua ambayo husomwa baada ya jina la Mtume, na kifupi chake kitakuwa kikielezewa kwa alama ya ﷺ. Ama kwa mitume wengine tutatumia neno *'alayhi as-salam,* yaani "amani iwe juu yake" na tutatumia alama ya عليه السلام.

walimwengu kwa kusema: "Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote." (Al-Anbiya, 21: 107)

Kila kitu hunufaika na rehma hii, lakini wanadamu ndio wanaopata faida kubwa zaidi. Fadhila zote tunazopewa ni tunu tunazopewa na Mwenyezi Mungu ambazo huchomoza kutoka katika Jua hilo la Rehma. Uzuri na mandhari yenye kupendeza ya Maumbile na mazingira ni vielelezo vya rehma hiyo. Ni kwa rehma hiyo ya ajabu ambapo kwamba mbawa za kipepeo zenye kupendeza, umaridadi na uzuri wa mawaridi yenye kuchanua, ulaini wa maua ya majira ya kuchipua, uzuri wa wanadamu na sifa za kimungu ambazo zimewatengeneza watu wengi wa tukufu, yote hayo ni picha na nuru itokanayo na rehma hiyo. Wanadamu hawawezi kufikia furaha na wokovu isipokuwa tu kwa kufuata viwango vya juu vya maadili yaliyooneshwa na Mtu Bora kabisa, Mtume Muhammad ﷺ, ambaye ni kiongozi wa kipekee na wa aina yake kwa wanadamu.

Hivyo, viumbe vyote ni wadeni wake. Tunaweza kulipa deni hili kwa kumtumia salamu na kwa kumpenda sana. Kumpenda kunahitaji pia kuwapenda wale anaowapenda, na hivyo kuwapenda watu wa familia yake kunatakiwa pia kuwe na nafasi katika nyoyo zetu. Miongoni mwao ni makhalifa walioongoka: Sayyidna Abu Bakr, Allah awe radhi naye,[2] ambaye alipewa cheo cha "Msadikishaje"; Sayyidna Umar رضي الله عنه, ambaye alikuwa mfano wa haki na uadilifu; Sayyidna Uthman رضي الله عنه, aliyekuwa mnara wa utambuzi na uaminifu; na Sayyidna Ali رضي الله عنه, Mlango wa Elimu, aliyekuwa akipendwa sana na Mtume ﷺ. Yatupasa kufurahia na kufuata misingi na kanuni tulizorithi kutoka kwao wote.

Misingi na kanuni hizo za maisha zinaweza kumuokoa mwanadamu dhidi ya unyama na ukatili, na hatimaye kumuokoa dhidi ya

2. *Radhiyallahu 'anhu/anha*, ni maneno ya dua ambayo hutamkwa pindi yanapotajwa majina ya Maswahaba wa Mtume, na yatakuwa yakielezewa kwa ufupi kwa kutumia alama ya رضي الله عنه.

adhabu ya milele, na kutuongoza kuelekea kwenye zama za ustawi. Kutozijua kanuni na misingi hiyo ni janga kubwa kwa maadili na uadilifu, wema, maarifa na ujuzi. Jamii na serikali yake, hata hivyo, vitaweza kuwa imara iwapo tu vitakuwa vimesimama kwenye jiwe la msingi la elimu, maadili na uadilifu. Tutaweza kuwajibika kwa uhalisia huu iwapo tu tutakuwa tayari kuzifuata tunu hizo sahihi.

Yatupasa kutafakari kwa kina ili kuziunga mkono kikamilifu tunu hizo. Tafakuri hiyo yaweza tu kupatikana katika mazingira ya kimaanawi (kiroho), sio katika mazingira yalisongwa na mafuriko ya tamaa za ubinafsi. Hivyo ni jambo muhimu sana kuzipa malezo akili na moyo ndani ya mwanga wa ujumbe utokao kwa Mwenyezi Mungu. Mtu anaweza kufikia kiwango cha nuru kwa kusuhubiana na watu wema au kwa kufuata muongozo wa kiroho wa walimu wetu wenye ujuzi. Miongoni mwao ni mwalimu wetu kiongozi, Hadhrat Mawlana Jalaluddin Rumi, Mwenyezi Mungu aitakase siri yake,[3] ambaye ana vipaji vikubwa kabisa vya kuwapeleka watu kwenye ukomavu.

Maisha yanayopambwa kwa neema na Baraka za kiroho na kimaanawi yanatakiwa kujaa rehma, huruma na upole. Baraka hizo huanzia kwa Mtume Muhammad ﷺ, ambaye ni *rehma kwa walimwengu*. Mtume wa Rehma ametupatia zawadi ya misingi na kanuni za maisha kwa kila wakati tunaoishi. Miongoni mwa kanuni hizo muhimu sana katika zama hizi ni kujiweka huru dhidi ya tabia ya matumizi mabaya.

Leo hii ni rahisi sana kushuhudia matumizi mabaya ya imani na matendo, matumizi mabaya ya muda na wakati, matumizi mabaya ya elimu, matumizi mabaya ya hisia za kimaadili, matumizi mabaya ya tafakuri ya kimaanawi na kiroho, matumizi mabaya ya uhai na kujitolea, na matumizi mabaya ya afya na riziki, bila kutaja matumizi mabaya ya nafsi za wanadamu wenyewe.

3. *Qaddasallahu sirrahu/sirraha:* maneno ambayo hutamkwa kama dua kwa ajili ya viongozi wa kiroho, na yatakuwa yakielezewa kwa ufupi kwa alama ya (q.s).

Waislamu hawana budi kuyajutia yote haya. Hatuna budi kufanya juhudi ya kuwalea, kuwafundisha na kuwaelimisha watoto wetu, ambao Mwenyezi Mungu ametukabidhi kama amana, ili wapate kuishi katika mazingira ya kimaanawi ya Qur'an na katika sunna za Mtume, kama kizazi chenye imani. Waislamu yawapasa kuuangalia msitari uliopo baina ya halali na haramu katika mazingira yote, waviweke pembeni visingizio visivyokuwa na maana.

Mapenzi ya kupenda rasilimali na mali nyingine za kidunia yametutawala, ilhali ilitakiwa sisi ndio tuzitawale hizo mali. Sadaka, huruma, uungwana na kuwatanguliza wengine vinatakiwa kuwa alama ya Waislamu. Tunatakiwa kuvuta pumzi, kutenda, kuongea kwa rehma na huruma nyakati zote kama alivyofanya Mtume ﷺ. Kama tunataka kupata hadhi ya kuingia Peponi, basi yatupasa kuzihuisha nafsi zetu. Tuna hitajio kubwa kabisa la misingi na kanuni hizo zilizooneshwa katika maisha ya Mtume wa Rehma. Tunatakiwa kuamka na kuzinduka iwapo tunataka kuzipata nafsi zetu halisi!

Kitabu hiki kinalenga kumsaidia msomaji kujua jinsi maisha yetu yanatakiwa kuandaliwa katika safari ya kuelekea kwenye maisha halisi na ya kweli. Matoleo ya mwanzo ya baadhi ya sura yalichapishwa katika jarida la kila mwezi la *Altinoluk.*

Tunamuomba Mwenyezi Mungu ayapokee maombi yetu na atulipe kwa nia yetu njema na atuhurumie.

Mola wetu! Tunaomba msaada wako ili tufikie tabia za Mtume ﷺ ambaye daima alikuwa *mpole na mwenye huruma kwa waumini* (Tawbah, 9: 128).

Tunakuomba utujaalie rehma na huruma Yako!

Amiin….

Utangulizi

Tunahitajika kuziweka maishani mwetu tabia za kimaadili za Mtume ﷺ ili kulipa deni la shukrani zetu kwake na kuilinda imani yetu katika mazingira ya kiroho na kimaanawi. Kumtii Mwenyezi Mungu ndio jambo la kwanza kabisa; kisha hufuata utii na usikivu kwa Mtume ﷺ, ambaye ni fakhari ya milele ya ulimwengu, kwa sababu upendo na huruma yake kwa umma wake ni mkubwa sana kuliko ule wa mama kwa mwanaye.

UTANGULIZI

Mola wetu hakumtuma Mtume ﷺ *ila awe ni rehma kwa walimwengu*. Ni rehma kuu ya ajabu ambayo kwamba viumbe vyote viliumbwa kwa sababu ya uwepo wake, na viumbe wote wamepewa daraja kulingana na mapenzi yao kwake.

- Ni rehma ya ajabu kwa sababu huruma na upole wake vili-wazunguka wanadamu wote, na hata viumbe wote pia.

- Ni rehma kuu na ya ajabu kwa sababu alitolewa zawadi kwa nyoyo na akili zote kama chemchem ya uhai, upendo na hekma; elimu na maarifa; akapambwa kwa Baraka zisizokuwa na kikomo.

- Ni rehma ya ajabu kiasi kwamba Qur'an Tukufu, ambayo ni muongozo unaowaongoza watu kwenye njia sahihi, iliterem-shwa kupitia kwake.

- Rehma kuu ya ajabu kiasi kwamba alikuwa na daraja ya kipekee miongoni mwa Mitume wote. Ndiye kipenzi zaidi kwa Mwenyezi Mungu. Alipewa zawadi ya Safari ya Usiku wa Kiroho kupitia katika mbingu mpaka mbele ya Mwenyezi Mungu.

- Ni rehma ya ajabu kwa kuwa bila yeye ulimwengu wote ungegeuka kuwa jangwa lenye ukiwa.

- Ni rehma kuu ya ajabu kwa sababu asili ya viumbe ilianza kwa kuumbwa kwake. Mitume wote waliomtangulia walikuwa wakitambua utukufu wa kuumbwa kwake.

- Ni rehma ya ajabu kwa kuwa uzuri wote ni picha ya uzuri wake. Hakuna ua linalochanua bila kupata sehemu ya nuru yake. Hakuna ua linalofunguka bila mwanga wa nuru yake. Yeye ni tumba la waridi, lililotengenezwa kwa maada tukufu, ambalo halinyauki, bali huzidi kustawi siku hadi siku.

- Ni rehma ya ajabu ambayo kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ametangaza ubora na thamani yake kwa kumsifu.

Sifa ya Mwenyezi Mungu kwake inazidi sifa nyingine zote. Mwenyezi Mungu Mtukufu anatangaza kuwa Yeye Mwenyewe, pamoja na malaika Wake, humtakia rehma Mtume – ambaye ni fakhari na uzuri wa milele wa ulimwengu huu – kabla ya kuamuru kuwa waumini wote wamtakie rehma na kumsalimu kwa salamu (al-Ahzab, 33: 56)

Neema iliyoje kwetu sisi kupata heshima ya kuletewa Mtume Aliyeteuliwa miongoni mwa mitume 124,000 waliotumwa na Mwenyezi Mungu! Hakika Baraka hiyo kutoka kwa Mwenyezi Mungu ni Baraka ya kipekee na ya aina yake. Hivyo, yatupasa kushukuru na kuziweka wazi shukrani zetu. Kuwa mfuasi wa Sultan wa Mitume wote ni heshima kubwa, lakini pia inawapa Waislamu jukumu zito wanalotakiwa kulibeba juu ya mabega yao, kwa maana Mwenyezi Mungu ametangaza kuwa kumtii au kumuasi Mtume ni sawa na kumtii au kumuasi Mwenyezi Mungu Mwenyewe.

Waislamu yawapasa kuonesha shukrani kwa kushikamana zaidi na Mtume ﷺ kuliko kitu kingine chochote kile katika ulimwengu huu na kwa kumpenda zaidi kuliko tunavyojipenda.

Tunatakiwa kumsifu Mtume kwa kumtakia rehma pindi jina lake linapotajwa; kwa kunufaika kiroho kutokana na mfano wa maisha yake; na kwa kumpenda. Tunatakiwa kumheshimu kama kiigizo na rejea yetu kwa ajili ya kuanzisha shakhsia na mtindo wetu wa maisha ya Kiislamu. Huruma yake kuu katika ulimwengu huu ni jambo la kuigwa, na uombezi wake siku ya mwisho ni jambo tutakalolihitajia kwa ajili ya wokovu wetu.

Tunawajibika kuanzisha mfumo wa maisha unaoturuhusu kuungana naye katika matendo na kauli zetu zote, kwa sababu *kila mtu atakuwa pamoja na Yule anayempenda*, na hivyo tunatakiwa kuwafanya wale anaowapenda kuwa kama mfano. Kadiri tunavyoshikamana na sunna za Mtume, ndivyo tunavyozidisha mapenzi yetu kwake na kuhisi kuwa yu karibu na nyoyo zetu. Kadiri tunavyozidi kumjua na kumkumbuka, ndivyo tunavyozidi kujisogeza zaidi kwake. Kwa hivyo tunatakiwa kuzitekeleza kwa ukaribu zaidi tabia na shakhia yake kamilifu, kumfuata kwa kushikamana na maadili yake bora na kumjaza ndani ya nyoyo zetu.

Mtume wetu hakupewa malezi na wanadamu, bali Mwenyezi Mungu. Alilelewa vyema kiasi kwamba alionesha na kudhihirisha kiwango cha juu kabisa cha shakhsia ya mwanadamu. Alitumwa kwa watu wote kama mkalimani wa ulimwengu usioonekana na usiojulikana, na kama mwalimu wa shule kuu ya Mola Mwenyezi. Hakuna kitabu kinachoweza kuuelezea kikamilifu uzuri wake usiokuwa na kikomo, lakini tutasimulia baadhi ya mifano.

Mtume Muhammad ﷺ: alishughulishwa sana na hali ya umma wake

Huruma aliyokuwa nayo Mtume ﷺ kwa umma wake ilikuwa kubwa zaidi kuliko hata huruma anayohisi mama kwa mwanaye. Qur'an Tukufu inasema:

Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma. (Tawbah, 9: 128)

Mtume ﷺ aliomba dua nyingi mno za rehma na huruma kwa ajili ya umma wake. Siku moja Mtume ﷺ alilia huku akiomba: "Ewe Mwenyezi Mungu! Unusuru umma wangu, wape huruma Yako!." Mwenyezi Mungu Mtukufu akamwambia malaika Jibril amuulize Mtume kwa nini alikuwa akilia. Jibril alipomuuliza Mtume ﷺ kuhusu machozi yake, akasema kuwa alilia kwa kuuonea huruma umma wake. Pindi Jibril aliporejesha jawabu hili, Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema: "Ewe Jibril! Mpe Muhammad habari hii njema: 'Tutakufanya kuwa mwenye furaha, hutahuzunika kwa ajili ya watu wako." (Muslim, Iman, 364)

Ibn Mas'ud anasimulia kisa kimoja kinachoonesha kiwango cha huruma kilichooneshwa na Mtume ﷺ kwa umma wake.

Siku moja, Mtume ﷺ alisema: "Ewe Ibn Mas'ud! Tusomee aya za Qur'an!" Nami nikamjibu: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Qur'an iliteremshwa kwako. Haistahiki kwangu kukusomea!" Mtume akasema: "Ninapenda kuiskiliza Qur'an ikisomwa na mtu mwingine." Hapo nikaanza kusoma Surat Nisa'. Nilipokuwa nikisoma aya isemayo, *"Basi itakuwaje pindi tukiwaletea kutoka kila umma shahidi, na tukakuleta wewe kuwa shahidi wa hawa?"* (Nisa', 4: 41), Mtume ﷺ akasema, "Ni bora usimamishe kisomo!" Nilimtazama Mtume nikaona machozi yakibubujika kutoka machoni mwake. (Bukahri, Tafsir 4/9; Muslim, Musafirin, 247)

Kisa hiki kinaonesha jinsi Mtume alivyokuwa akishughulishwa na umma wake. Siku ya Kiyama, patasemwa:

Soma kitabu chako! Nafsi yako inakutosha leo kukuhisabu. (Isra, 17:14) na dhambi za watu zitafunuliwa. Mtume ﷺ ambaye alikuwa na moyo wa huruma kwa umma wake, alitoa machozi kwa maana aya hiyo ilimkumbusha kile tutakachokuwa tukikabiliana nacho Siku ya Kiyama.

Siku moja Mtume ﷺ alisema: "Mwenyezi Mungu aliniahidi mambo mawili. Jambo la kwanza ni, *Mwenyezi Mungu hakuwa wa kuwaadhibu nawe umo pamoja nao*. La pili ni, *wala Mwenyezi Mungu si wa kuwaadhibu na hali ya kuwa wanaomba msamaha* (Anfal, 8: 33). Nitakapoondoka nitauachia umma wangu ahadi ya pili, ambayo itawaokoa dhidi ya adhabu ya Mwenyezi Mungu mpaka Siku ya Kiyama." (Tirmidhi, Tafsir, 8/3082)

Ni matumaini yetu kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu atawanusuru dhidi ya Moto waja Wake wanaompenda Mtume ﷺ kwa nyoyo zao zote. Pia tunatumai kuwa hatakubali nyoyo hizo zichomwe na moto.

Visa hivi ni mifano michache tu miongoni mwa mifano mingi ya huruma ya Mtume isiyokuwa na kikomo ambayo alikuwa nayo kwa umma wake. Daima tunatakiwa kuuangaza ulimwengu wetu wa ndani ili kuona tumefanikiwa kiasi gani katika kufuata sunna zake na kuenda sambamba na huruma yake.

Mtume Muhammad ﷺ: mwenye staha

Kwa Muhammad ﷺ, Utume haukumaanisha ukuu usiokuwa wa kudumu. Japokuwa kuna mitume waliokuwa wafalme, alipendelea kuwa mja wa Mwenyezi Mungu kuliko kuwa mfalme.[4]

4. Haythami, *al-majmauz-Zawaid,* IX:192.

Alijishughulisha zaidi na matatizo ya umma wake. Alitoa msaada kwa watu wenye shida. Alitenga sehemu maalumu kwenye pembe ya msikiti kwa ajili watu maskini katika Maswahaba zake na yeye mwenyewe akawa anawatunza Maswahaba hao ambao walifanya juhudi kubwa sana katika kujifunza dini ya uislamu.

Unyenyekevu wake ulikuwa wa kipekee. Kamwe hakujishughulisha na maslahi binafsi. Kitu pekee kilichomshughulisha ni kuwasaidia watu kupata njia ya kweli ili waweze kufikia wokovu hapa duniani na kesho Akhera.

Bibi Aisha ﵂ alizungumzia kuhusu jinsi Mtume ﷺ alivyomsaidia katika kazi za nyumbani. "Usiku mmoja baba yangu, Abu Bakr, alituagizia mguu wa nyama ya kondoo. Mtume alinishikia wakati nikijaribu kumkata, nami pia nikamshikia wakati akimkata." Mtu mmoja katika wasikilizaji alimuuliza Aisha iwapo walikuwa wakifanya kazi hiyo gizani. Bibi Aisha akajibu: "Pindi tunapokuwa na mafuta ya kuweka katika taa, tulipendelea kutumia mafuta hayo kwa ajili ya chakula. Familia ya Mtume ilikuwa ikikaa miezi kadhaa bila kuwa hata na kipande cha mkate, au bila kuwasha jiko kwa ajili ya kupika chakula." (Ahmad, VI: 217; Ibn Sa'd, I: 1405).

Mtume Muhammad ﷺ: Mwenye ukarimu

Siku moja, mtu mmoja alimuomba Mtume ﷺ ampe kitu cha kula. Mtume ﷺ akasema: "Sina ninachoweza kukupa, lakini unaweza kununua kitu kwa jina langu, nami nitalipa baadaye nitakapokuwa na pesa." Sayyidna Umar ﵁ alisikia mazungumzo hayo. Hakupenda kumuona Mtume ﷺ katika tabu. Akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kama unacho unaweza kutoa, lakini kama huna huna hulazimiki kutoa. Mbele ya Mwenyezi Mungu huwajibiki kutoa kile usichokuwa nacho!"

Mtume ﷺ hakufurahishwa na maneno ya Umar ؓ. Kuona hivyo, Swahaba mwingine akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, baba na mama yangu wawe fidia kwako! Unatakiwa kutoa. Usihofu kwamba Mola wa ulimwengu atakukatia riziki yako!" Mtume ﷺ akatabasamu kwa maneno haya, kwa maana yalioangazia kile alichokitaka. Akajibu: "Ninatakiwa kufanya hivyo kwa namna yoyote ile." (Haythami, X, 242).

❁

Maskini anapokuja kwa Mtume ﷺ, kwanza alikuwa akiulizia nyumbani mwake kama kuna chochote. Akijulishwa kuwa hakuna chochote zaidi ya maji, alikuwa akiwataka Maswahaba kukidhi haja ya maskini huyo. Asingeishia hapo, bali angeridhika pale anapoona kuwa mahitaji hayo yametekelezwa. Mfano mwingine wa aina hii unasimuliwa na Anas ؓ:

"Kuna mali ililetwa kwa Mtume ﷺ kutoka Bahrain. Mtume ﷺ akasema: "Mali yote iwekwe msikitini." Mtume wa Mwenyezi Mungu hakuwa amepokea mali kubwa kama hiyo hapo kabla… alielekea msikitini kwa ajili ya swala. Baada ya kumaliza kuswali, alisimama pembezoni mwa mali hiyo na kuitoa kwa kila aliyepita mpaka ikaisha." (Bukhari, Salat, 42)

Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akipata raha katika kuwafurahisha waumini kwa kukidhi mahitaji yao. Siku moja alisema: "Malaika Jibri ameniletea ujumbe kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu akisema: "*Hakika nimekuchagulieni dini hii* [Uislamu] *na nimeridhia iwe dini yenu."* Ukarimu na maadili mema ndiyo yanayoendana na dini. Inyanyueni dini hii kwa sifa hizi mbili katika kipindi chote ambacho mtaishi kama Waislamu." (Haythami, VIII, 20; Ali al-Muttaqi, al-Kanz, VI: 392). Hivyo ni wajibu wetu kufuata misingi ya kimaadili iliyooneshwa na Mtume ﷺ ili tuweze kuinyanyua dini yetu na kuziokoa imani zetu kiroho na kimaanawi.

Utii wetu wa kwanza lazima tuuelekeze kwa Mwenyezi Mungu, kisha kwa Mtukufu Mtume ﷺ. Hakika Mtume ndiye aliyeuombea umma wake kabla ya kujiombea, na alipokuwa akitoa sadaka ya kuchinja alikuwa pia akiwatolea vichinjwa wale wote wasioweza kugharamia ibada hiyo katika umma wake.[5] Utii wetu hufikia kilele chake pale tunapoifanya njia ya maisha yake kuwa chanzo cha kiroho kwa ajili ya mwenendo na matendo yetu kutokana na kuvutwa na upendo wetu mkubwa kwake. Mtukufu Mtume ﷺ alielezea jinsi anavyowapenda wafuasi wa kweli kabisa katika umma wake wanaofuata mwendo na njia yake: "Kuna watu wanaonipenda sana watakuja baada yangu. Watakuwa tayari kutoa mali zao na kuzitoa dhabihu familia zao kwa ajili ya kupata nafasi ya kuniona." (Muslim, Jannah, 12)

❁

Tukishindwa kufuata misingi iliyowekwa na Mtume ﷺ, tutapata hasara mbalimbali na hata kupoteza maisha yetu kwa kukabiliwa na migongano yenye kuumiza baina ya misukumo yetu ya ndani na ile ya nje. Hii ni kwa sababu Mwenyezi Mungu amemuumba mwanadamu akiwa na jozi mbili za tabia na sifa: zile zinazotuvuta na kutupeleka Kwake, na zile zinazotutoa kwake, zikatupeleka kwenye uchafu na uovu. Qur'an Tukufu inasema:

"Kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake. Hakika amefanikiwa aliye itakasa." (Surah Shams: 8-9)

Ulimwengu wa ndani wa wale ambao hawajalelewa kiroho kwa nuru ya Qur'an na sunna za Mtume ﷺ ni kama misitu yenye wanyama wengi, wakali na wapole. Kila mtu, kulingana maumbile yake, ana sifa za mnyama. Kuna wenye hila na ujanja kama mbweha, baadhi ni wakali na wakatili kama mbwa mwitu, baadhi

5. Abu Dawud, Adhahi, 3-4; Ibn Sa'd, I,249.

ni wenye pupa na ulafi kama mchwa, na wengine ni wenye sumu kali kama nyoka. Baadhi watakung'ata utakapowashambulia, wengine watainyonya damu yako, na wengine watatabasamu mbele ya uso wako huku wakikubg'ata mgongoni. Kila mnyama ana moja kati ya tabia na sifa hizi, sifa ambayo humtofautisha na mnyama mwingine.

Watu wasioweza kujiokoa kutoka katika utumwa wa mielekeo ya tamaa za nafsi zao dhalili hawawezi kujenga shakhsia imara. Baadhi yao wana sifa na tabia za mnyama mmoja au wawili, huku wengine wakiwa na tabia za wanyama wengi. Na kwa kuwa ulimwengu wa ndani wa watu umezienea tabia zao, mtu mwenye busara anaweza kugundua aina gani ya tabia na sifa aliyonayo mtu husika.

Je, mfumo wa ukomonisti, ulioasisiwa kwenye msingi wa damu za watu milioni 20, sio zao ulimwengu wa ndani wa unyama? Je mapramidi, yaliyojengwa kwa ajili ya maiti ya Fir'an mmoja tu kwa gharama maisha ya wafanyakazi wasiokuwa na idadi waliozikwa wakiwa hai, sio minara ya uonevu, dhulma na ukatili? Mambo ya kale yanatoa mafunzo na mazingatio kwa wale ambao bado ni wajinga, lakini leo hii bado unaweza kushuhudia, kwa urahisi kabisa, mifano kayaya na mingi mno ya dhulma na ukatili ambao unaweza kumshangaza hata mbweha mwenye ukali wa hali ya juu kabisa. Yote inaonesha kuwa iwapo jamii itatawaliwa na watu wenye tabia za chura, basi madimbwi yataenea kila mahali. Iwapo itatawaliwa na watu wenye tabia za nyoka, basi watu wote wataumizwa na sumu yake: hofu na wasiwasi vitatawali. Na iwapo jamii itatawaliwa na watu wenye tabia za mawaridi na huruma, mabustani ya mawaridi yataenea kila mahali: jamii itapata amani ya kweli.

Yote haya yanaonekana kutoka katika historia. Katika historia, Mtume Muhammad ﷺ, bwana wa mitume wote, ndiye aliyekuwa

mtu wa kipekee, kwani ndiye aliyezibadilisha zama na eneo kuwa bustani. Kwa kipindi chote cha miaka 23 ya kazi yake, aliupa ubinaadamu zawadi ya bustani isiyonyauka. Katika kipindi cha utume wake, haki na batili vilikuwa wazi kabisa. Aliujenga na kuuimarisha ufahamu na utambuzi wa wanadamu kuhusu Muumba, ulimwengu, mazingira na maumbile yenyewe. Watu wakajua kuwa ulimwengu huu ni uwanja wa kutahiniwa. Jamii iliyokuwa ya kijinga na ya kijahiliya isiyojua kitu ikabadilika kuwa jamii iliyojengwa kwa msingi wa elimu, ujuzi na maarifa.[6] Waumini wakaanza kujua kuwa mwili wa mwanadamu unatokana na tone la maji, kwamba ndege anatokana na yai, na kwamba miti na majani hutokana na mbegu. Waumini wakaanza kuitafakari hekma, mantiki na maaba ya uumbaji, na nyoyo zao zikatoka nje na kusafiri kuelekea kwenye anga ya hekima.

Mafunzo na malezi ya Mtume ﷺ ndiyo yaliyoiruhusu jamii aliyoiongoza kuwa na kiwango cha juu kabisa cha huruma, kujitolea kwa moyo, kujitoa na hisia ya uadilifu. Mtume ﷺ akawa kitovu cha urafiki ambao uhai wake ulijengwa kwenye msingi wa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu. Nyoyo zote zilijazwa msisimko wa udadisi. Kila mtu aliuliza: "Mwenyezi Mungu anataka tufanye jambo gani? Mtume ﷺ angependa kutuona tukiwa katika hali gani?" Kwa namna hii, usiku ulibadilika kuwa mchana, majira ya kiangazi yakabadilika kuwa majira ya kuchipua. Hivyo, zama hizo za historia ya mwanadamu zikawa Zama halisi za Dhahabu.

Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa neema kubwa ambayo kwa uwepo wake, mashimo mengi ya giza yalijazwa nuru tukufu. Kampeni kali ambayo imekuwa ikifanywa dhidi yake kutoka zama moja hadi nyingine zinatokana na ujinga wa wahusika na nia zao mbaya.

6. Tazama Surat az-Zumar, 39:9.

Kila kiumbe hai huishi katika mazingira yanayoafikiana na maumbile yake. Kanuni hii ya kimaumbile inawahusu binaadamu pia. Nyuki wanahitaji maua yenye kuchanua, na hawawezi kuishi bila maua hayo. Panya huishi katika maeneo machafu na hawawezi kustahmili kuishi katika mabustani ya mawaridi. Kwa namna hiyo, roho adhimu hulelewa kwa utukufu utokao kwa Hakika na Dhati ya Muhammad. Nafsi chafu huishi katika uchafu.

Sayyidna Abu Bakr ﷺ alikuwa akitazama uso wa Mtume ﷺ na kusema kwa mshangao mkubwa: "Yaa rabb! Uzuri ulioje!" Kile ambacho Abu Bakr alikuwa akikishuhudia ni ulimwengu wake wa ndani ulioakisiwa katika wajihi wa Mtume ﷺ. Hivyo, Mtume ﷺ aliposema: "Sijapata kutumia mali ya yeyote kama nilivyotumia mali ya Abu Bakr", Abu Bakr alijibu huku machozi yakimtoka: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Je mali yangu si mali yako?" (Ibn Maja, Muqaddimah, 11). Maneno haya ni ushahidi wa wazi kwamba Abu Bakr alikuwa amejifunga kikamilifu kwa Mtume ﷺ kiasi cha kuungana naye. Aliufanya ulimwengu wake wa ndani kuwa kioo kwa Mtume ﷺ. Kwa upande mwingine, Abu Jahl, adui mkubwa wa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, alikuwa akiuchukia sana uso wa Mtume ﷺ. Alipokuwa akiutazama uso wa Mtume, hakuwa akipata picha chanya, bali alikuwa akizibwa na ukafiri na dhulma zake. Kila mtu aliiona shakhsia yake ya kweli, ulimwengu wake wa ndani, katika uso wa Mtume ﷺ.

Mitume ni kama vioo vyenye kung'ara. Katika vioo hivyo, kila mtu huweza kuiona sura na picha yake, yaani ulimwengu wake wa ndani. Kioo hakimdanganyi mtu anayekitazama. Vioo huakisi picha ya kweli ya Yule anayevitazama.

Yajulikana wazi kuwa ndimi zenye sumu na maandiko yaliyokosa hisia vinawajeruhi sana watu wa dini wasiokuwa na hatia, ambao wanampenda sana Mtume ﷺ. Wale waliojichukulia njia ya

kuwa maadui wa Waislamu, Qur'an na Mtume ﷺ, punde watakabiliwa na kisasi cha Mwenyezi Mungu Mtukufu. Yeye ndiye mlinzi wa dini ya Uislamu.

Ieleweke kuwa haiwezekani kuifuta silika ya ndani ya mwanadamu kuelekea kwenye jambo sahihi. Mwenyezi Mungu Mtukufu amemjaalia mwanadamu njaa ya kimaanawi na kiroho. Juhudi zozote zitakazofanywa kueneza imani ya kumkana Mungu haziwezi kuzaa matunda, na maua mazuri ya dini, yaliyopandikizwa katika kina cha ndani cha roho ya mwanadamu, yataibuka na kustawi. Hitajio la waja la kuwa karibu na Mola wao kamwe haliwezi kuzuiliwa. Hisia hizo kuu haziwezi kusimamishwa, kwa sababu nguvu itokayo kwa Mungu ndiyo iliyoziweka. Silika ya ndani ya mwanadamu ni kuwa karibu na Mwenyezi Mungu na kuihitajia dini.

Ewe Mwenyezi Mungu ziangaze nyoyo na macho yetu kwa nuru ya Mtume ﷺ! Tusaidie tuwe miongoni mwa umma wa Sultani wa Mitume! Zijaalie nyoyo zetu furaha kuu kutoka katika anga ya Zama za dhahabu za Mtume! Tufanye kuwa waja wenye ikhlasi na usafi wa moyo mbele Yako, na tuwe watu wanaostahiki kuwa wafuasi wa Mtume ﷺ!

Amiin…

SURA YA 1

Mifano Kutoka Katika Maisha Ya Mtume ﷺ

Faida Za Maadili Yaliyotukuka - 1

Yatupasa kuifanya shakhsia ya mfano ya Mtume wa Mwenyezi Mungu kuwa muongozo katika nyakati zetu zote za maisha yetu. Kila rehma tunayomuombea Mtume ﷺ inalenga kutupatia mwanga kutoka katika maisha yake ya kimaanawi. Muislamu yeyote anayefanikiwa kuzishika tabia hizo tukufu za Mtume ﷺ kama vile unyenyekevu, staha na unyoofu anaweza kuifikia furaha na wokovu wa kweli kwa urahisi kabisa.

SURA YA 1

Mifano Kutoka Katika Maisha Ya Mtume ﷺ

FAIDA ZA MAADILI YALIYOTUKUKA – 1

Muumini hawezi kustawisha mwenendo kamili wa kiroho isipokuwa tu pale atakaposhikamana na maadili yaliyotukuka ya Mtume ﷺ. Lengo hili linaweza kufikiwa kulingana na kiwango cha upendo alichonacho kwa Mtume ﷺ, fakhari ya ulimwengu, na jinsi anavyokiheshimu kiigizo hicho.

Kutoka katika ulimi mtukufu wa Mtume ﷺ wanadamu waliyasikia maneno kutoka mbinguni yaliyozitibu na kuzinawirisha nyoyo. Kupitia kwa Mtukufu Mtume ﷺ, ambaye ni fakhari ya viumbe, binaadamu wamejaaliwa bahari isiyokuwa na kikomo ya msamaha. Ni kwa sababu ya Mtume, bwana wa ulimwengu, ambapo jamii ya binaadamu wanaitwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa maneno: "*Enyi waja Wangu*!"

Sisi kama watu wa Muhammad ﷺ, tunachotakiwa kufanya mbele ya Baraka hizi za Mwenyezi Mungu ni kuishi kulingana na mwenendo wake, kufanya kwa moyo mmoja kile alichotuamrisha na kuacha yale aliyotukataza.

Mwenyezi Mungu Mtukufu alimpa Mtume Muhammad ﷺ daraja ya juu na yenye kuheshimika kabisa, "cheo chenye kusifika", (*al-maqam al-mahmud*). Vilevile Mwenyezi Mungu alimuandaa Mtume kwa ajili ya nafasi hiyo yenye kuheshimika. Kwa kuwa

Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa *mpole na mwenye huruma* sana kwa watu wake, alitulingania na kutuita kuungana naye, yaani yatupasa kufuata njia ambayo Mwenyezi Mungu alimuonesha. Zifuatazo ni baadhi ya nasaha zake. Mtume ﷺ alisema: "Mola wangu aliniusia kumcha katika nyakati zote, katika siri au dhahiri. Ninawausia kunifuata katika hilo."[7] Katika kufuata muongozo huu, alikuwa mwangalifu mno katika kutekeleza amri za Mwenyezi Mungu, akasema: "Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, hakika mimi ni mwenye kumuogopa, kujisalimisha kwake na kumheshimu Mwenyezi Mun gu kuliko yeyote miongoni mwenu!" (Sahih Bukhari, Nikah, 1).

❀

Alipokuwa akitaka kuondoka katika kundi la watu, Mtume ﷺ alikuwa akiomba dua na kusema: "Ewe Mwenyezi Mungu! Tupe sehemu ya khofu itakayotukinga dhidi ya madhambi!" (Tirmidhi, Da'wat, 79)

❀

Mtukufu Mtume ﷺ alipata heshima ya kumtambua Mwenyezi Mungu kwa undani zaidi kuliko binadamu mwingine yeyote. Siku moja aliwaambia Maswaha: "Lau kama mngejua ninayoyajua, mngecheka kidogo na kulia sana." Maswahaba waliposikia maneno haya waliangua vilio. (Bukhari, Tafsir 5/12)

❀

Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaahidi pepo waja Wake wanamuogopa na kumcha katika siri na dhahiri. Qur'an Tukufu inasema:

7. Kuhusu maneno haya ya Mtukufu Mtume ﷺ, tazama: Ibrahim Canan, *Hais Ansiklopedis,* XVI, 252, namba 5838.

"Na ama yule anaye ogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake Mlezi, na akajizuilia nafsi yake na matamanio, basi huyo, Pepo itakuwa ndiyo makaazi yake!" (Nazi'at, 79: 40-41)

Na

"Haya ndiyo mnayo ahidiwa kwa kila mwenye kurejea kwa Mwenyezi Mungu na akajilinda. Mwenye kumwogopa Mwingi wa Rehema hali kuwa hamwoni, na akaja kwa moyo ulioelekea" (Qaaf, 50: 32-33)

Na

"Mbavu zao zinaachana na vitanda kwa kumwomba Mola wao Mlezi kwa khofu na kutumaini, na hutoa kutokana na tulivyo waruzuku." (Sajdah, 32:16)

Nyakati za usiku kwa Mitume na Marafiki wa Mwenyezi Mungu, ambazo huzitumia kumuomba Mwenyezi Mungu kwa khofu na kutumaini huruma Yake, huwa na mwanga kuliko mchana, kwa maana nyakati hizo za usiku huwa zimejazwa utulivu na hali ya kiroho itokanayo na kusujudu huku wakiwa wanalia.

❁

Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Mola wangu aliniamuru kuhukumu kwa uadilifu, wakati wa hasira au wakati wa amani. (Nami ninawausia hayo hayo)." Wakati wa ghadhabu na hasira, mtu anaweza kuuacha msimamo wa wastani na kuwa na msimamo mkali, na akahukumu kwa uonevu na bila uadilifu. Lakini tunatakiwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na kuwa na subira na stahmala, tusielekee kwenye uonevu, dhulma na ubabe.

❁

Mola wetu anatueleza ndani ya Qur'an Tukufu:

"Enyi mlio amini! Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ijapo kuwa ni juu ya nafsi zenu…" (Nisaa, 4: 135)

Na

"…hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanao hukumu kwa haki." (Hujurat, 49: 9)

❁

Akigusia masuala mbalimbali, Mtume ﷺ anasema: "Kuna masharti matatu ya kupata wokovu: kutenda uadilifu wakati wa hasira na amani; kutumia kiasi, sio tu wakati ukiwa huna kitu, bali pia wakati ukiwa nacho; na kumuogopa Mwenyezi Mungu katika siri na dhahiri. (Haythami, I: 90)

❁

Siku moja mtu mmoja mwenye hadhi ya juu alikuja kwa Mtume ﷺ na kumuomba asimuadhibu mwizi. Mtukufu Mtume ﷺ akamjibu: "Ningetekeleza hukumu hiyo hata kama mhusika akiwa ni binti yangu Fatimah." (Bukhari, Anbiya 54; Muslim, Hudud 8, 9).[8]

❁

Uadilifu ni jambo la msingi sana kwa ajili ya ustawi wa mtu na jamii kwa ujumla. Hivyo, Sayyidna Umar رضي الله عنه anasema: "uadilifu ni msingi wa serikali yenye mafanikio."

❁

Wakati wa utawala wa Umar ibn Abdul-Aziz, aliyetewala kwa kipindi cha miaka miwili na nusu pekee katika kipindi cha utawala wa miaka 92 ya banu Umayya na ambaye anachukuliwa kuwa Khalifa wa tano wa uislamu, watu wa dola ya Bani Umayya

8. Bukhari, al-Maghazi 53; Nasaai, al-Qat' al-Sariq, 6, VIII, 72-74.

waliishi katika amani na usalama kwa sababu ya utawala uliokuwa na usawa na uadilifu. Ukatili hauleti amani, na dola haziwezi kusimama bila uadilifu. Kisa cha mhandisi wa Kikristo aliyemshitaki Sultani wa Dola ya Othamniyya, Muhammad wa pili, ni mfano mzuri wa kihistoria kuhusu jambo hili. Pamoja na kuwa hakimu wa mahakama, Hizir Bey, alikuwa rafiki wa karibu wa sultani, hukumu yake ilikuwa dhidi ya sultani. Kisa hiki kinaonesha jinsi Wauthmaniyya walivyouchukulia uadilifu kama msingi wa utawala.

❁

Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Mola wangu aliniusia kuwa na matumizi ya kiasi katika umasikini na katika utajiri. (Nami nakuusieni vivyo hivyo)." Mwenyezi Mungu akituandikia kuwa maskini au matajiri, vyovyote itakavyokuwa, yatupasa kuwa na matumizi ya kiasi, na tusifanye isirafu na kuwa na matumizi mabaya. Mtukufu Mtume ﷺ alituusia kujua umuhimu wa utajiri kabla hatujakabiliwa na umaskini.[9]

Mwenyezi Mungu Mtukufu anatueleza na kutuonesha jinsi ya kuwa na matumizi ya kiasi:

"… wala usitumie ovyo kwa fujo. Hakika wabadhirifu ni ndugu wa Mashet'ani. Na Shet'ani ni mwenye kumkufuru Mola wake Mlezi." (Isra, 17: 26-27)

"Wala usiufanye mkono wako kama uliofungwa shingoni mwako, wala usiukunjue wote kabisa, utabaki ukilaumiwa muflisi." (Isra, 17: 29)

❁

9. Hakim, *al-Mustadrak,* IV: 341.

Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Wale wenye kuwa na matumizi ya kiasi na kujiepusha na israfu kamwe hawatafukarika." (Ibn Hanbal, I: 477)

Na, "Mwenye kumuomba Mwenyezi Mungu amuamulie baina ya mambo mawili au zaidi kwa kufanya swala ya ushauri (*istikahara)*[10]* hatahuzunika; na mwenye kutaka ushauri hatajuta; na mwenye kuwa na matumizi ya kiasi hatafukarika." (Haythami, *al-Majmu'ah al-zawaid,* II: 280). Muumini anatakiwa kutambua kuwa milki yote ni ya Mwenyezi Mungu, na kwamba mwanadamu, kama khalifa wa Mwenyezi Mungu, amepewa fursa ya umiliki wa mali za kidunia kwa muda tu. Tutumie kile tu tunachokkihitajia, na kilichobaki tukitumie katika njia ya Mwenyezi Mungu.

Qur'an Tukufu inasema:

"…Na wanakuuliza watoe nini? Sema: Kilicho chepesi." (Baqarah, 2: 219)

❀

Mtume wetu ﷺ alitushauri na kutuusia kuwa matajiri wa moyo hata kama hatutakuwa matajiri wa mali: "Jiokoeni na moto kwa kutoa sadaka, hata kama itakuwa nusu ya tende. Kama hamtapata hata kiasi hicho basi jiokoeni na Moto kwa kusema maneno mazuri." (Bukhari, Adab 34)

❀

Ustawi na maendeleo ya kweli huja kwa kutoa katika njia ya Mwenyezi Mungu. Mtu anaweza kutoa huduma na kutoa katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa kutumia tu njia za halali, na pia isiwe kwa kutaka manufaa ya kimaada. Mtukufu Mtume ﷺ anas-

10. Kutaka msaada wa Mwenyezi Mungu kwa njia ya swala na ndoto.

ema kuhusu jambo hili: "Mali bora ni ile ya halali na yenye manufaa, katika mikono ya mtu mwema." (Ibn Hanbal, IV: 202)

Waumini wa kweli na wema wana huruma na upendo. Huruma inatutaka tutoe kile tulichonacho kuwapa wale wasiokuwanacho. Kwa hakika, huruma inataka tukimbilie kuwahudumia wanyonge na wenye shida. Huruma na ukarimu humletea Muislamu utulivu wa kimaanawi na kiroho hapa duniani na kumpatia ukombozi huko Akhera.

Wale wenye kuwa na utajiri na wakawa wenye kushukuru, na wale walio maskini na wakawa na subira, wote ni watu muhimu sana. Makundi yote mawili ni makundi ya waja wenye thamani kubwa mno mbele ya Mwenyezi Mungu. Matajiri wakarimu na wenye kushukuru, na maskini wenye heshima na subira, wote wana hadhi sawa ya ubinaadamu, na wote wanapata radhi za Mwenyezi Mungu. Lakini, wenye wenye utajiri lakini wakawa na kiburi na ubakhili; na wale wenye umaskini lakini wakaasi na kutokuwa na subira, wote ni wabaya katika Uislamu. Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akisema: "Mola wangu! Ninajilinda kwako dhidi ya shari ya mali na umaskini." (Muslim, Dhikr 49). Hivyo, wale wenye tabia za kiroho za kuridhika, kutosheka na unyenyekevu ndio matajiri wa kweli. Na mtu hawezi kupata furaha ya utajiri huo isipokuwa kwa kutoa katika njia ya Mwenyezi Mungu.

Ilipoanza kampeni ya kukusanya rasilimali katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Vita vya Tabuk, Maswahaba waliokuwa maskini na ambao hawakuwa matajiri walifanya juhudi kubwa sana kushiriki katika kampeni hiyo kwa kujitolea kwa njia

mbalimbali ikiwa ni pamoja na wao wenye kujitolea nafsi zao au kutoa kidogo walichokuwa nacho. Miongoni mwa Maswahaba hao ni Abu ‘Aqil ﷺ ambaye alipata ndoo mbili za tende kwa kufanya kazi usiku mzima. Ndoo moja aliipeleka nyumbani na nyingine akaitoa kwa jili ya vita vya Tabuk. Mtume ﷺ alimwambia: “Mwenyezi Mungu azifanye kuwa maradufu ndoo hizi, ile uliyoipeleka nyumbani nahileuliyoileta hapa!” (Tabari, Tafsir, X: 251).

Mtume ﷺ anasema: “Siku moja dirhamu moja ya sadaka ilipata thawabu kuliko dirhamu laki moja!” Maswahaba wakauliza: “Ilitokeaje hiyo?” Mtukufu Mtume ﷺ akajibu: “Mtu mmoja alikuwa na dirham mbili tu katika mali yake. Alichukua nusu yake – yaani dirham moja - na kuitoa sadaka. Mtu mwingine, ambaye alikuwa tajiri sana, alichukua dirhamu laki moja katika mali yake na kuitoa sadaka.” (Nasai, Zakat, 49). Mtu wa kwanza alitoa nusu ya alichokuwa nacho. Mtu wa pili alitoa zaidi ya Yule wa kwanza, lakini sadaka yake ilikuwa sehemu ndogo ya mali yake. Hivyo, thamani ya sadaka zetu haitokani na kiwango tunachokitoa, bali hutokana na hisia tunayokuwa nayo katika kujitolea. Kisa kifuatacho pia kinaashiria juu ya ukweli huu:

Mtu mmoja alikuja kwa Sayyidna Uthman ﷺ akasema: “Enyi wenye mali! Hakika ninawastaajabia. Mnapata Baraka zote kwa kutoa sadaka, kuwakomboa watumwa na kwenda hijja!”

Sayyidna Uthman akamuuliza: “Kweli watustaajabia?”

Akasema: “ndiyo, kwa hakika ninawastaajabia mno!”

Sayyidna Uthman akajibu: “Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba dirham moja ya sadaka inayotolewa na maskini katika mazingira magumu ina thamani zaidi kuliko dirham elfu moja zinazotolewa na tajiri.” (Ali al-Muttaqi, VI, 612/17098)

Sheikh Sa'di anatoa ushauri na wosia ufuatao kuhusu jambo hili: "Mwenyezi Mungu Mtukufu haifungi milango ya wema na kheri dhidi ya yeyote. Hivyo, tambua kwamba wema wa kila mtu hupimwa kulingana na uwezo wake. Sadaka ndogo inayotolewa na maskini ina thamani kubwa zaidi kuliko kiwango kikubwa kinachotolewa na tajiri. Mguu wa nzige ni mzigo mkubwa kwa sisimizi."

Hivyo, thamani ya sadaka au kujitolea hupimwa kulingana na kiwango cha ikhlasi kilichohusika. Kiasa cha mashahidi watatu wa Uislamu waliokufa katika Vita vya Yarmuk, ambapo kila mmoja alipendelea mwenzake aanze kunywa kikombe cha maji kabla yake na hivyo wote kufariki dunia, ni mfano mzuri katika suala hili.

❁

Siku zote shauku ya Maswahaba ilikuwa ni kujipambanua kwa tabia na mwenende wa kimaadili wa Mtume ﷺ. Kwa namna hii waliweza kufikia kilele cha huruma na maisha ya unyoofu (*zuhd*). Waliishi katika kujitoa kwa moyo moja kwa moja, wakifuata misingi ya maisha ya Mtukufu Mtume ﷺ. Walijizuia na aina zote za ubadhirifu na israfu. Tajiri miongoni mwao walikuwa wenye kushukuru, na maskini walikuwa wenye kusubiri na kustahmili. Mwenendo usiokuwa na ubinafsi uliooneshwa na Mtume ﷺ katika ugawaji wa ngawira za vita ni mfano wa jinsi alivyokuwa mwenye kushukuru katika nyakati za neema, na kufunga kwake jiwe kwenye tumbo lake ili kutosikia maumivu ya njaa ni mfano wa jinsi alivyokuwa na subira wakati wa umaskini au anapokuwa hana kitu.

❁

Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Mwenyezi Mungu aliniusia kuwatembelea jamaa zangu hata kama hawataki kuwa karibu nami. (Nami ninawausia vivyo hivyo)." Mwenyezi Mungu Mtukufu

anawataka waja Wake kudumisha uhusiano na familia na kuamiliana nao kwa wema. Katika kusisitiza umuhimu wa kuwatembelea ndugu na jamaa, Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Mwenyezi Mungu alinituma kudumisha ujamaa (udugu), kuvunja masanamu, na kuthibitisha Umoja wa Mwenyezi Mungu, na kutomfanyia washirika." (Muslim, Musafirin, 294)

Ni wajibu kwetu, kwa mujibu wa imani yetu, kudumisha mawasiliano na familia na tutumie upole na ulaini kuwajuza yale ambayo Mwenyezi Mungu anataka tuyafanye, hata kama majibu yao hayatakuwa sawa na wasiwasi wetu kwao. Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Kuwafanyia wema ndugu zako haina maana kwamba wajibu wako kwao umetekelezwa. Yule atekelezaye wajibu huo huendelea kuwatendea wema licha ya kutorejeshewa wema wake, na kuwa karibu na wale ambao hawataki kuwa karibu nao." (Bukhari, Adab 15; Abu Dawud, Zakah, 45)

❁

Kwa mara nyingine, Mtukufu Mtume ﷺ ni mfano bora kabisa wa jambo hili. Kila alipochinja mnyama alikuwa akiagiza sehemu ya nyama kwenda kwa ndugu wa mkewe, Khadijah رضي الله عنها. (Bukhari, Manaqib al-Ansar, 20)

❁

Sehamu nyingine, Mtukufu Mtume ﷺ alisema: "Jifunze mti wa familia yako ili uendeleze uhusiano na wanafamilia yako." (Ali al-Muttaqi, al-Kanz, X: 220, naba 29162)

❁

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an kwamba wale wanaopuuza kuwatembelea jamaa zao na hawawaulizii watakuwa wenye khasara:

"Wanao vunja ahadi ya Mwenyezi Mungu baada ya kwisha ifunga, na wakayakata aliyo amrisha Mwenyezi Mungu kuungwa, na wakafanya uharibifu katika nchi; hao ndio wenye khasara." (al-Baqara, 2: 27)

"[Enyi wanafiki!] Basi yanayo tarajiwa kwenu mkitawala ndio mfisidi katika nchi na muwatupe jamaa zenu? Hao ndio Mwenyezi Mungu aliowalaani, na akawatia uziwi, na akawapofoa macho yao." (Surat Muhammad, 47: 22-23)

Naye Mtukufu Mtume ﷺ anasema kuwa wale wanaopuuza kuwatembelea jamaa zao watakuwa katika hasara kubwa. Anasema: "Wale wenye kukata pingu za udugu hawastahiki Pepo." (Bukhari, Adab, 11) Pia akasema: "Siku ya Kiyama Mwenyezi Mungu Mtukufu atayaadhibu makundi mawili ya watu: madhalimu na wale wanaowatupa ndugu zao. Makundi haya mawili pia ndio yanayostahili sana kuadhibiwa katika maisha ya duniani." (Abu Dawud, Adab, 43; Tirmidhi, Qiyamah, 57)

❁

Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Mwenyezi Mungu aliniamuru kuwapa wale walioninyima. (Nami nakuusieni kufanya hivyo)." Qur'an Tukufu inasema:

"Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu." (Fussilat, 41: 34)

Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Usikate uhusiano na Yule anayekukatia uhusiano! Mpe Yule aliyekunyima! Msamehe Yule aliyekuumiza!" (Ibn Hanbal, IV: 148, 158)

❁

Katika mwaka wa pili wa Hijra, watu wa Makka walipata shida sana ya njaa na ukame. Mtukufu Mtume ﷺ aliwasaidia, japokuwa walikuwa wamempiga vita kwa muda wa miaka ishirini, akawatumia dhahabu, shayiri na tende. Abu Sufyan ndiye aliyepokea msaada huu na kuugawa kwa maskini wa Kiqurayshi.

Mwanadamu amepewa maumbile ya kutambua fadhila anayotendewa pamoja na muamala mzuri. Sifa hizo humlainisha hata adui. Hata Abu Sufyan, adui mkubwa wa Mtukufu Mtume ﷺ, alihisi kulainika kwa sababu ya wema aliokuwa amewafanyiwa watu maskini wa Makka. Alisema: "Mwenyezi Mungu amlipe mtoto wa ndugu yangu [Mtume alikuwa mpwa wa Abu Sufyan]! Ametekeleza haki ya udugu wake." (Yaqubi, *al-Tarikh*, II: 56)

❀

Watu wengi waliingia katika Uislamu kutokana na tabia adhimu za moyo wa Mtukufu Mtume ﷺ

❀

Kisa cha Nabi Yusufu عليه السلام ni mfano mwingine kuhusu jambo hili. Ndugu zake walimtupa kisimani kwa sababu ya wivu na husda. Lakini miaka mingi baada ya tukio hilo, Nabii Yusufu عليه السلام aliwatendea wema pindi alipokutana nao katika kasri la mfalme wa Misri akiwa kama waziri. Kutokana na wema wake aliowatendea, wakasema:

"…Wallahi! Mwenyezi Mungu amekufadhilisha wewe kuliko sisi, na hakika sisi tulikuwa wenye kukosa." (Yusuf, 12: 91)

❀

Ni wajibu kwetu kutafuta njia ya kuingia ndani ya nyoyo za wale tunaotaka kuwaongoza kwenye njia ya kweli na wema. Njia rahisi kabisa ni kuwa na ukarimu, huruma na kusamehe.

Ili tuwe waumini wa kweli na kupendwa na Mwenyezi Mungu yatupasa kutenda yafuatayo:

- Daima tuwe na hofu ya kumuogopa Mwenyezi Mungu ndani ya nyoyo zetu;
- Kutenda haki na uadilifu wakati wote, wakati wa hasira au amani;
- Kutoa katika njia ya Mwenyezi Mungu, kuwa na matumizi ya wastani wakati wote, tunapokuwa na mali na tunapokuwa maskini;
- Kuwasiliana na ndugu;
- Kuonesha heshima hata kwa wale wasiotuheshimu; na tuwasamehe hata wale wanaotuonea.

Ewe Mwenyezi Mungu tunakuomba utuongoze tuweze kufuata wosia wa Mtukufu Mtume ﷺ kama kivuli kinavyomfuata mwenye nacho! Tupambe kwa mwendo wa kimaadili wa Mtume ﷺ, ambaye ni mfano mkuu kwa wanadamu, na tujumuishe kuwa miongoni mwa waja Wako wema!

Amiin!

SURA YA 2

Mifano Kutoka Katika Maisha Ya Mtume ﷺ

Kaida Za Maadili Yaliyotukuka - 2

Yatupasa kuzingatia kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwaumba wanaadamu na kuwapa silika na mfumo wa kuhitajiana. Kila jamii ina matajiri na masikini, pia ina wenye nguvu na wanyonge. Unaweza kuuliza: "Kwa nini Mwenyezi Mungu Mtukufu aliruhusu na kukubali watu wawe maskini?" Na jibu ni rahisi: Mwenyezi Mungu amewakabidhi maskini kuwa amana kwa matajiri.

SURA YA 2

Mifano Kutoka Katika Maisha Ya Mtume ﷺ

KAIDA ZA MAADILI YALIYOTUKUKA – 2

Upendo huambatana na kila kitu kinachomhusu anayependwa. Mlima wa Uhud, kwa mfano, sio mlima wa kawaida katika akili za Waislamu, kwa sababu Mtukufu Mtume ﷺ aliupenda. Mji wa Madina ulikuwa mji wa kawaida, lakini ukapata Baraka baada ya tukio la Hijrah, pale Mtukufu Mtume ﷺ alipogura kutoka Makka na kwenda kuishi huko. Mji huo wenye nuru ukawa ni mji unaopendwa na Waislamu kwa sababu ulifungamanishwa na Mtukufu Mtume ﷺ.

Kumpenda Mwenyezi Mungu Mtukufu kunahitaji kukipenda kile anachokipenda zaidi, nacho ni Mtume ﷺ. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an Takatifu:

"Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni…" (Al-I Imran, 3: 31)

Kwa hivyo basi, mwenye kufanya juhudi ya kumfuata Mwenyezi Mungu na Mtume Wake bila shaka atahesabiwa kuwa ni miongoni mwa waja wanaopendwa, kwa fadhila za Mwenyezi

Mungu Mtukufu. Kushikamana na njia ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake kutawapeleka waumini kwenye sifa za kimaanawi kama vile kuonesha upendo na huruma kwa viumbe wote kwa ajili ya Muumba, watashirikiana na waumini wengine katika rasilimali mbalimbali, wataongeza uwezo wa kuwasamehe wengine na kuwaangalia viumbe kupitia jicho la Muumba.

Maswahaba waliuchukulia muunganiko wa kiroho na kimaanawi pamoja na Mtume ﷺ kuwa ni Baraka kubwa zaidi katika ulimwengu huu, wakawa kama vipepeo wanaoizunguka miale ya mwanga: hivyo wakapata fadhila adhimu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na wale Waislamu ambao, katika kipindi chote cha historia, waliakisi na kuonesha ndani mwao mwenenndo na tabia adhimu za Mtukufu Mtume ﷺ walizipevusha sifa za asili za kuumbwa kwao, na mwenye adhimu wa imani na maadili kwa wanadamu.

Tiba mujarrabu kabisa kwa ugonjwa wa moyo ni kumpenda na kumfuata Mtukufu Mtume ﷺ kwa kuustaajabia mwenendo wake wa ajabu usiokuwa wa kawaida.

Kwa kuwa shauku ya Mtukufu Mtume ﷺ ni kutaka kuungana na umma wake Peponi, anatutaka tuchunge kanuni na sheria za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Qur'an Tukufu:

"Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma." (Tawbah, 9: 128)

Hivyo basi, hatuna budi ila kusikiliza yale ambayo Mtukufu Mtume ﷺ anatuusia kuyafuata ili tuweze kuungana naye kwenye bwawa la Kawthar, ambalo ndio eneo lenye kuheshima zaidi Peponi. Ufuatao ni baadhi ya wosia wake kwetu:

Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Mola wangu aliniusia kutafakari ninapokuwa katika ukimya. (Nami nawausia hayo hayo)."[11]

Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwajaalia viumbe wote uwezo wa kufikri kulingana na vipawa vyao. Katika viumbe hai wote, isipokuwa binaadamu na majini, uwezo huu upo katika mfumo wa silika za kimaumbile kwa ajili ya uhai wa miili yao. Silika huwasaidia wanyama kujipatia chakula, kujitetea na kuzaliana.

Wanadamu, kwa upande mwingine, wamejaaliwa uwezo wa kutafakari. Uwezo huu hutusaidia kuwa karibu na Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuwa waja Wake wanaoheshimika. Hatupaswi kuutumia uwezo huu kwa kutafuta anasa za mpito tu hapa duniani. Kwa hakika hilo ni kosa kubwa mno kwa binaadamu!

Kadiri mtu anavyozidi kutafakari juu ya maajabu ya uumbaji na kuongeza umakini katika kutafakari, ndivyo anavyozidi kupata ladha ya upendo wa Mwenyezi Mungu na amani ya Akhera.

Kutafakari ni nyenzo kubwa kabisa inayotuwezesha kupata uwezo wetu kamili wa kimaanawi. Kuanzia mwanzo mpaka mwisho, Qur'an Tukufu, ambayo muongozo mkubwa wa wokovu, inatutaka tutafakari kwa kina juu ya hekma inayopatikana katika kuumbwa kwa mwanadamu, katika usanifu wa ulimwengu, na katika maneno yake yenyewe yaliyojaa miujiza. Qur'an imeteua maneno maalumu katika kuelezea maonyo yake kama vile, "*Je hamfikiri?" "Je hamtafakari?" "Je hamuielewi mifano iliyotolewa na Qur'an kwa ajili ya watu"* Hivyo mwenye kutaka kuishi maisha yanayoendana na hadhi ya mwanadamu hana budi kuingia katika ulimwengu wa kutafakari uliooelekezwa na unaoongozwa na Qur'an Tukufu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an:

11. İbrahim Canan, *Hadis Ansiklopedisi*, XVI, 252, no. 5838.

"Je! Hawajifikirii nafsi zao? Mwenyezi Mungu hakuumba mbingu na ardhi na viliomo ndani yake ila kwa Haki na kwa muda maalumu…" (Surat Rum, 30: 8)

"Kwani tulichoka kwa kuumba mara ya kwanza. Bali wao wamo katika shaka tu juu ya umbo jipya. Na hakika tumemuumba mtu, nasi tunayajua yanayo mpitikia katika nafsi yake. Na Sisi tuko karibu naye kuliko mshipa wa shingoni mwake." (Surat Qaaf, 50: 15-16)

Daima Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akitafakari juu ya Mwenyezi Mungu, Muumba wa Ulimwengu. Alikuwa akitafakari kwa muda mrefu bila kutikisika au kuhama. Vilevile aliulingania umma wake kwenye kutafakari juu ya viumbe na uumbaji,[12] na akatangaza kuwa tafakuri ni aina ya ibada yenye thamani ya kipekee.[13]

Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Mola wangu aliniusia kwamba mazungumzo yangu yawe ya *dhikr* ya kumkumbuka Mwenyezi Mungu. (Nami nawausia hivyo hivyo)."

Wale wanaopenda huwa na hamu ya kuwakumbuka na kuwataja wanaowapenda. Kadiri unavyomkumbuka unayempenda, ndivyo upendo unavyoongezeka. Hivyo wale waliowahi kuonja ladha ya imani kwa Mwenyezi Mungu watajitahidi kuongeza upendo wao kwa kumkumbuka.

Kumkumbuka Mwenyezi Mungu haina maana ya kuyasoma tu majina Yake matukufu, bali kuungiza upendo wetu Kwake ndani ya nyoyo zetu, katikati ya dhamiri na akili zetu. Ni kwa sababu hiyo kwamba Qur'an Tukufu inasema:

"…Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!" (Ra'd, 13: 28)

12. Daylami, II, 56.
13. Ali al-Muttaqi, *al-Kanz al-Ummal*, XVI, 121.

Bibi Aisha ﵂ anasimulia kuwa *daima* Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa katika hali ya kumkumbuka Mwenyezi Mungu.[14] Allah Mtukufu anatutaka tumfuate Mtume ﷺ katika hilo:

"… Na mdhukuru Mola Mlezi wako kwa wingi na mtakase jioni na asubuhi." (Ali- Imran, 3: 41)

"Mkisha sali basi mkumbukeni Mwenyezi Mungu mkisimama, na mkikaa, na mnapo jinyoosha kwa kulala…" (Nisaa, 4: 103)

Katika aya hii Mwenyezi Mungu Mtukufu anawaamuru waja wake waungane Naye kwa nyoyo zao muda wote, na wasiache kumkumbuka na kumdhukuru Mwenyezi Mungu hata wakati wa vita, wakati wa hofu na wakati wa hatari.

Kumdhukuru Mwenyezi Mungu ni jambo muhimu sana katika kuufanya moyo uendelee kuwa kwenye njia iliyonyooka. Qur'an Tukufu inasema:

"Wala msiwe kama wale walio msahau Mwenyezi Mungu, na Yeye akawasahaulisha nafsi zao. Hao ndio wapotovu." (Hashr, 59: 19)

Mwenyezi Mungu aliwaambia Musa na Harun ﵇ walipokwenda kwa Fir'auni:

"Nenda, wewe na ndugu yako, pamoja na ishara zangu, wala msichoke kunikumbuka." (Surat Ta Ha, 20: 42)

Muumini ambaye moyo wake humkumbuka na kumdhukuru Mwenyezi Mungu kwa kusema: "Ewe Mola wangu!" hawezi kuzungumza uongo bali atazungumza ukweli, atafanya kila kitu kwa uadilifu, na kuwaonea huruma viumbe wote, kwa sababu sifa za Mwenyezi Mungu kama vile Mwingi wa Rehma na Mwenye

14. Muslim, Hayd 117.

kurehemu zitajionesha na kujidhihirisha ndani ya muumini anayemkumbuka Mwenyezi Mungu na kuyadhukuru majina Yake.

Mwenye kumdhukuru Mwenyezi Mungu akauunganisha moyo wake na Mwenyezi Mungu hufikia kwenye kilele cha juu kabisa cha ibada. Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Tofauti baina ya mtu anayemdhukuru Mwenyezi Mungu na yule asiyemdhukuru ni kama tofauti iliyopo baina ya mtu aliye hai na mfu." (Bukhari, Da`awat 66)

❀

Mtukufu Mtume ﷺ anasema tena kuwa: "Mola wangu aliniusia kujifunza na kuzingatia pindi ninapotazama uumbaji Wake. (Nami ninawasia hivyo)."

Mwenyezi Mungu Mtukufu anawasifu waja wanaotazama uumbaji Wake kwa jicho la mazingatio na anatangaza kuwa anawafanya wazielewe ishara Zake. Aya za Qur'an zinawataka na kuwahimiza wanadamu kuyaona mambo yote yanayotokea kuwa ni mafunzo na mazingatio:

"Je! Hawamtazami ngamia jinsi alivyo umbwa? Na mbingu jinsi ilivyo inuliwa? Na milima jinsi ilivyo thibitishwa? Na ardhi jinsi ilivyo tandazwa?" (Surat al-Ghaashiyah, 88: 17-20)

"Kwani hawakutembea katika ardhi wakaona ulikuwaje mwisho wa walio kuwa kabla yao? Mwenyezi Mungu aliwaangamiza, na kwa makafiri hawa itakuwa mfano wa hayo." (Surat Muhammad, 47: 10)

Maarifa ya juu kabisa, katika sayansi na kiroho, ni kuwa na uelewa mkubwa wa ukweli wa uhai. Mawlana Jalaluddin Rumi (q.s) katika maneno yake kama vile "nilipikwa nikaungua" anaashiria kufikia kwake daraja hii. Katika kitabu chake maarufu cha

Mathnawi anazungumza na tabia za viumbe na kuakisi juu ya hisia zao, huku akitafsiri hali zao. Miongoni mwa mazungumzo hayo ya kimaanawi ni pale anapozungumza na kuongea na uawaridi.

Waridi lilipata manukato yake kwa kuendeleza usuhuba wake na mwiba. Lisikilize waridi utayajua hayo! Sikia linavyosema: Kwa nini niwe na wasiwasi ninapokuwa pamoja na mwiba? Nilijifunza kutabasamu kwa kuuvumilia mwiba mbaya. Kwa kuwa pamoja na mwiba hu nilipata uwezo wa kuupa ulimwengu harufu nzuri na manukato.

Yunus Emre, Sufi wa Kituruki, alifanya mazungumzo na alizeti. Alitamka maneno ya hekma na siri za ulimwengu kupitia ulimi na lugha ya alizeti.

Sa'di al-Shirazi anasema: "Kwa akili zenye werevu, kila jani la kila mti linatoa kitabu cha maarifa ya Mwenyezi Mungu. Kwa akili zenye ujinga, miti yote kwa pamoja haitoi hata jani moja."

Sifa hizo za kimaanawi kama vile tafakuri, kumdhukuru Mwenyezi Mungu, na kuchukua mafunzo kutoka kwenye uumbaji wa viumbe mbalimbali ni sharti la ukamilifu wa kiroho kupitia utakaso wa ulimwengu wa ndani. Mtukufu Mtume ﷺ alitambua kuwa Mwenyezi Mungu alimuusia kuboresha sifa hizo kwa nguvu zote naye akauusia umma wake kuwa makini katika masuala hayo.

Imam Rabbani analieleza hili kwa ufasaha: "Muumini mzuri ni yule aliyebarikiwa kufuata mfano wa Mtume! Juhudi ndogo tu inayofanywa kwa imani madhubuti na isiyotetereka hupata hadhi ya kuwa juhudi kubwa na adhimu katika zama hizi ngumu kwa Uislamu…" (*Al-Maktubat* al-Rabbani, barua 44)

Mwenyezi Mungu atujaalie sisi wote kuwa miongoni mwa waja Wake wenye bahati ambao hufuata kikamilifu mfano wa Mtume ﷺ. Mfumo wa maisha unaofuata njia ya Mtukufu Mtume ﷺ humuongoza mhusika kwenye wokovu hapa duniani na kesho akhera. Tiba pekee ya kupata furaha inapatikana ndani ya taratibu na tabia ya huruma ya Mtukufu Mtume ﷺ. Tiba hiyo huyabadilisha mateso ya dunia kuwa wokovu wa milele, machozi ya maumivu hubadilika kuwa tabasamu la milele.

Adhama ya kidini tunayoifurahia katika ulimwengu huu inatakiwa kuunganishwa na ukweli huu mtukufu, hapo tunaweza kutunukiwa furaha ya milele. Misingi hii inajumuisha tafakuri, kumdhukuru Mwenyezi Mungu na kutazama na kutaamali katika uumbaji wa viumbe mbalimbali. Pia inajumuisha kuyapamba maisha yetu kwa hali ya kimaadili ya Mtukufu Mtume ﷺ kwa uungwana wa kuwatanguliza wenzetu na kushirikiana na wenzetu.

Yatupasa kutambua kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwaumba wanaadamu ili wahitajiane. Kila jamii ina tajiri na maskini, na ina wenye ngubu na wanyonge. Unaweza kuuliza: “Kwa nini Mwenyezi Mungu amekubali na kuruhusu watu wawe maskini?” Na jibu ni rahisi: Mwenyezi Mungu aliwakabidhi maskini kuwa amana kwa matajiri. Jukumu hili ambalo matajiri wamepewa kulitekeleza limetolewa na Mwenyezi Mungu Mwenyewe.

Lau matajiri na wale wenye nguvu wangaetafakari kuwa wanaweza kujikuta katika nafasi ya wanyonge na maskini kwa urahisi kabisa, wangewasaidia wale walio katika mazingira magumu na kutekeleza jukumu lao kwa kuwaonyeeshea masikini mikono ya msaada. Kwa maana maisha ya duniani ni muda mfupi – si chochote ukiyalinganisha na maisha ya milele ya Akhera. Wakati huo huo, maskini wanaweza kufikia wokovu huko Akhera kwa kuwa wenye subira na kumshukuru Mwenyezi Mungu hapa duniani.

Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, ambaye uhai wangu uko mikononi mwake, kwamba hamtaingia peponi mpaka mhurumiane." Maswahaba wakasema: "Ewe Mtume wa Allah! Hakika sisi tunahurumiana." Mtukufu Mtume ﷺ akasema: "Sina maana ya kuhurumiana nyinyi kwa nyinyi pekee. Ninamaana kuwa na huruma kwa viumbe wote – huruma inayojumuisha jumla ya viumbe wote!" (Hakim, IV,185/7310).

Hivyo, yatupasa kusikiliza vilio vinavyotoka katika jamii yetu. Shughuli yetu kubwa yatakiwa kuwa ni kuwahurumia na kuwasaidia wagonjwa na vikongwe wanaoishi katika ukiwa, yatima, vijana walioathirika na madawa ya kulevya, na wale wanaotaabika kwa sababu ya kutengwa kikabila na kidini.

Furaha yetu hupatikana pale tunapoinyoosha mikono na nyoyo zetu kwa fakiri na maskini. Waislamu ni kama viungo vya mwili mmoja, hivyo kila mtu anayetenganishwa nasi ni kama kiungo kinachotenganishwa na mwili wetu. Katika kuwahimiza Waislamu kudumisha msimamo huo wa umoja, Mtukufu Mtume ﷺ alisema: "Waislamu ni kama mwili mmoja katika kupenda, kuhurumiana na kuteteana. Kiungo kimoja cha mwili kinapoumwa, viungo vingine vya mwili hupata tabu kwa kukesha na kuwa na homa." (Bukhari, Adab 27; Muslim, Birr 66).

Tufanye nini ili kufikia furaha ya dini, ambapo mwanadamu atapata ukombozi na uso wa bashasha ya Uislamu, wajinga wakaamka na waliotengwa wakafurahi? Yatupasa kulifikiria sana hilo. Yatupasa kutumia muda kufikria juu ya furaha ya kidini kwa Waislamu wanaoonewa na kuhuzunishwa ulimwenguni kote. Aina gani ya kadi ya salamu tunayotakiwa kuwatumia? Tutafanyaje kuzinyoosha nyoyo na kuzipeleka dua zetu kwa Waislamu wanaokandamizwa, kwa yatima, kwa maskini wanajiona kama ndege waliovunjika mbawa? Je tunaweza kuwafanya watabasamu

angalau mara moja? Hilo linaweza kutupatia raha ya kupata furaha ya kweli.

Furaha ya kweli ambayo huwapeleka watu kwenye ukombozi wa kweli itapatikana tu pindi tutakapotoa majibu ya chanya ya maswali hayo. Furaha iliyoje kwa wale wanaoishi kwa mujibu wa maadili ya Mtume!

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tuwe na hisia za masumbuko ya Waislamu wenzetu ulimwenguni kote, azifanye nyoyo zetu ziwakumbuke na kuwafikia kupitia misaada mbalimbali na kwa dua. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aifanye milango ya Akhera kuwa sikukuu ya milele iliyopambwa kwa furaha ya kiroho na kimaanawi!

Amiin…

SURA YA 3

Mifano Kutoka Katika Maisha Ya Mtume ﷺ

Kaida Za Maadili Yaliyotukuka - 3

Ili kuisambaza dini hii vizuri, mja anahitaji kuwa na moyo mnyenyekevu uliopambwa kwa hekma za Qur'an na uso wenye furaha unaoonesha na kuakisi tabia ya bashasha ya Uislamu. Mtu huyo anapaswa kuwa alama ya kila zuri na jema na azungumze lugha ya moyo.

SURA YA 3

Mifano Kutoka Katika Maisha Ya Mtume ﷺ

KAIDA ZA MAADILI YALIYOTUKUKA – 3

Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwaomba viumbe wote, hasa wanadamu, akawapa silika ya upendo. Maendeleo ya kiroho ambayo wanadamu huyafikia hutegemea kiwango ambacho tunaelekeza upendo wetu kwa Mwenyezi Mungu na kwenye kutenda matendo mema katika dunia hii ambayo ni chumba cha darasa ambacho ndani yake tunatahiniwa na Mwenyezi Mungu. Lengo la kipekee na la mwisho la uhai na maisha ni upendo ambao utazifanya nyoyo zetu zipate makao na makazi ya amani, yaani Mwenyezi Mungu, ambaye alitupulizia roho Yake ndani mwetu. Kila aina ya upendo wa kiistiari na usiodumu ambao huelekezwa kwa vitu visivyokua sahihi hupotelea katika vichochoro vya giza. Kama upendo wetu haumfikii Mwenyezi Mungu, utakuwa umepotea bure na hautakuwa na chochote zaidi ya kuuchosha moyo.

Mawlana Jalaluddin Rumi anaelezea ujinga wetu kuhusu suala hili: "Haishangazi kumuona kondoo akimkimbia mbwa mwitu, kwa sababu mbwa mwitu ni adui wa kondoo. Kinachoshangaza ni kumuona kondoo akimpenda mbwa mwitu!"

Maumbile na ustawi wetu vinatutaka tuufanye upendo wa kumpenda Mwenyezi Mungu kuwa kitovu cha uhai na maisha yetu. Hivyo, upendo mwingin wote wa kiistiari unapaswa kutujengea ngazi ya kuelekea kwenye upendo wa kumpenda Mwenyezi Mungu. Hili ni lengo la kwanza na la asili la kuumbwa kwa mwanadamu.

Njia fupi na rahisi zaidi ya kuufikia upendo wa Mwenyezi Mungu ni kumpenda Mtume ﷺ, kipenzi cha Allah. Lengo hili linaweza kufikiwa kwa kumfuata katika kila kipengele cha maisha. Mwitikio wetu kwake unatakiwa kuwa kwa msingi wa upendo: mpendaji anatakiwa kupenda kila kitu kinachopendwa na mpendwa wake. Msimamo huu wa nidhamu ya kumtanguliza Mwenyezi Mungu ndio msingi wa kumpenda.

Upendo wa kumpenda Mtukufu Mtume ﷺ hujidhihirisha kwa kuwa na utulivu katika ibada, staha katika mahusiano binafsi, upole katika maadili, ulaini wa moyo, ung'aavu wa uso, hali ya kiroho katika maongezi, na kina katika mtazamo na uelewa. Chemchem pekee inayoweza kutoa uzuri wote huu ni Muhammad ﷺ.

Kwa hakika, nyoyo zetu zinaweza kufaidika kikamilifu na moyo wa Mtukufu Mtume ﷺ iwapo tu tutakuwa kama vipepeo wanauozunguka mwanga. Mawlana Jalaluddin Rumi anatupa mifano kadhaa ya jinsi upendo wa Mwenyezi Mungu ulivyoenea na kusambaa katika ulimwengu. Mifano hii inatupatia fursa ya kuupima upendo wetu kwa Mtume ﷺ:

Nondo wasiokuwa na idadi huchupa ndani ya moto kwa ajili ya upendo. Hupapatika ndani ya moto na kuungua, huku wakisema katika lugha ya hali zao: "Kuwa kama mimi!"

Mshumaa huwaka na kulia. Hujisalimisha mbele ya moto na kuteseka sana. Hutoa mwanga huku ukinyauka kwa machozi.

Mshumaa husema: "Ni kazi bure kutumia dhahabu na fedha kwa ajili ya kujinufaisha. Kama wataka faida ya kimaanawi, ungua na uyeyuke kama mimi!"

Mtume ﷺ ambaye tunampenda sana alilia tena na tena, akasema, "Umma wangu, umma wangu!" Upendo na huruma aliyokuwa nayo kwa umma wake ni zaidi ya upendo na huruma ya mama kwa wanaye. Daima alikuwa na wasiwasi kuhusu hali ya umma wake Siku ya Kiyama, na alipata mateso mengi ili kuwaokoa watu wake. Alisema, "Nilikumbwa na masaibu na mateso makubwa katika njia ya Mwenyezi Mungu ambayo hayakumpata yeyote kabla yangu." (Tirmidhi, Qiyamah 34/2472).

Mtukufu Mtume ﷺ aliwaambia Maswahaba: "Kuweni makini! Hakika uwepo wangu ni kinga kwenu, na nitaendelea kuwa hivyo baada ya mauti yangu. Nitaendeleakuwaombea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, nikisema, 'Umma wangu, Umma wangu!' mpaka itakapopulizwa parapanda ya mwisho." (Ali al-Muttaqi, al-Kanz al-Ummah, juzuu 14, uk. 414).

Yatupasa kumpenda kwa dhati Mtukufu Mtume ﷺ kwa ajili ya maisha yetu ya akhera kuliko tunavyozipenda nafsi zetu, kwa maana alitwambia, "Muumini atafufuliwa pamoja na Yule anayempenda" (Bukhari, Adab 96). Waislamu wote wanatakiwa kuonesha mshikamano na umma wa Mtume ﷺ kwa kuwa aliupenda sana… Mshikamano huo unaonesha ni kwa kiasi gani tunampenda.

Hapa Mtukufu Mtume ﷺ anatuusia mambo mawili ambayo tunaweza kuyatumia kama mtaji na rasilimali ya kuwekeza kwa ajili ya dunia na akhera yetu.

1. "Mola wangu aliniusia kumsamehe kila anayenitendea ubaya (mimi binfasi). (Hivyo ninawausia kunifuata katika hilo.)"[15]

15. İbrahim Canan, *Hadis Ansiklopedisi*, XVI, 252, no. 5838.

Msamaha huwa na thamani pale mtu anaposamehe hali ya kuwa anauwezo wa kuadhibu lakini yeye akaamua kusamehe. Tabia hiyo huonesha upendo wetu kwa viumbe kwa ajili ya upendo wetu kwa Muumba wa viumbe hivyo. Muislamu anatakiwa kuwa na unyenyekevu wa kutosha kumfanya aachane na kisasi, na kumuachia Mwenyezi Mungu hukumu ya wakosaji hao Siku ya Hukumu. Kitendo hicho cha kusamehe ni kitendo cha ukomavu wa moyo uliotakasika na ni sifa ya waumini safi wenye staha. Muumini anapoendelea kuwasamehe wale wanaomkosea, naye hupata msamaha kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Sayyidna Umar ﵁ anasema, "Asiyewahurumiwa watu hatahurumiwa. Asiyesamehe hatasamehewa" (Bukhari, al-Adab al-Mufrad, uk. 415, 371).

Nafsi zetu hazipendi kusamehe. Hivyo, kusamehe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni amali yenye ubora mkubwa sana. Kwa kuwa thamani ya amali hutegemeana na ugumu wake, Mwenyezi Mungu mtukufu huutambua msahamaha wetu kwa kiwango tunachojitahidi kusamehe.

Mtu mmoja aliyekuwa na udhaifu wa kuishinda ghadhabu yake alimtaka Mtukufu Mtume ﷺ amuusie. Mtukufu Mtume ﷺ akamwambia, "Usikasirike!" Mtu huyo akarudia swali hilo mara tatu. Katika mara zote hizo, jibu la Mtukufu Mtume ﷺ halikubadilika. (Bukhari, Adab 76)

Mtukufu Mtume ﷺ aliutaka umma wake kuimarisha tabia ya kusamehe. Alisema, "Msiwe kama wale wasemao, 'watu wakitutendea wema, nasitutawatendea wema. Wakitutendea ubaya, tutawatendea ubaya.' Fanyeni mazoea ya kuwatendea wema wale wanaowatendeeni wema na vivyo hivyo kwa wale wanaowatendeeni ubaya!" (Tirmidhi, Birr 63/2007). Kuna methali moja ya Kituruki inagusia suala hilo hilo: "Watu duni ndio hurejesha wema kwa

wema- wale wakomavu hurejesha wema wanapotendewa ubaya.” Kwa hakika amali hiyo ni mbinu na njia ya mafunzo ya kimaanawi na ya kiroho.

Pindi adui anapofanya ubaya halafu akarejeshewa wema, moyo wake unaweza kulainika na uhasama ukayeyuka. Kwa kusamehe, aduia anaweza kuwa rafiki, na rafiki akazidi kuwa rafiki wa karibu zaidi.

Qur’an Tukufu inasema;

“Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu.” (Fussilat, 41:34)

Ibn Abbas ﷺ anasema katika kuitafsiri aya hiyo: “Kifungu kisemacho “*lilio jema zaidi*” kina maana ya kuwa na subira na uvumilivu wakati wa hasira, na kusamehe pindi unapotendewa ubaya. Mwenyezi Mungu huwaokoa wale wenye kuweza kufanya hivyo, akawafanya maadui zao wasalimu amri na kuwa marafiki.” (Bukhari, Tafsir 41/1)

Historia imethibitisha kuwa binadamu amenufaika mno na tabia ya kusamehe. Kusamehea kuwaepusha wanadamu na shari, dhulma na unyanyasaji, ikawaamsha wengi kutoka kwenye ujahili wa kimaadili… Mojawapo katika matukio hayo lilitokea pindi Mtukufu Mtume ﷺ alipoifungua Makka na kutangaza msamaha kwa watu wa mji huo. Aliwahutubia watu hao waliokuwa wamekusanyika kwenye Kaabah: “Enyi watu wa Makkah! Mnadhani nitafanya jambo gani juu yenu?”

Wakajibu: “Tunatarajia wema kutoka kwako. Kwani wewe ni ndugu mwenye moyo wa ukarimu na ni mwana wa ndugu yetu pia. Tunaamini unatujali!..”

Mtukufu Mtume ﷺ akasema: "Ninawaambia yale yaliyosemwa na Nabii Yusufu kuwaambia ndugu zake: '*Leo hapana lawama juu yenu. Mwenyezi Mungu atakusameheni, naye ni Mwingi wa kurehemu kuliko wote wanao rehemu*.' (Yusufu, 12: 92)"

Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa na uwezo wa kuwachukua kama mateka waabudu wa Makka ambao walikuwa wamewatesa Waislamu kwa miaka mingi, lakini badala yake aliwasamehe na kuwaacha huru.[16] Nyoyo za waabudu masanamu zililainika na wengi wao wakaishia kuingia katika Uislamu.

❁

Wakati bibi Zaynab, binti mpendwa wa Mtukufu Mtume ﷺ, alipokuwa akihamia Madina kwenda kuungana na baba yake, mtu mmoja aitwaye Habbar ibn Aswad alimtupia mkuki. Zainab alidondokea juu ya jiwe na kuumia vibaya sana. Alikuwa mjamzito na hivyo ujauzito wake uliharibika kutokana na tukio hilo. Baadaye alifariki dunia kutokana na majeraha na maumivu aliyoyapata. Pindi Waislamu walipoikamata Makka, Habbar ambaye alikuwa ameshafanya jinai nyingine nyingi dhidi ya Waislamu alikimbia.

Siku moja, Mtukufu Mtume ﷺ akiwa amekaa pamoja na Maswahaba, Habbar alikuja mbele yake. Alisilimu na kuomba msamaha kwa makosa na jinai zake alizowahi kuzitenda. Mtukufu Mtume ﷺ alimsamehe na kuwakataza Maswahaba wasimtendee ubaya kwa makosa aliyokuwa ameyatenda huko nyuma.[17] Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an:

"Shikamana na kusamehe, na amrisha mema, na jitenge na majaahili." (`Araf, 7: 199)

16. Ibn Hisham, IV, 32; Waqidi, II, 835; Ibn Saad, II, 142-143.
17. Waqidi, al-Maghazi, II, 857-858.

Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akisamehe makosa yote binafsi yanayotendwa dhidi yake. Hata hivyo, alikuwa akihakikisha haki inatendeka kama makosa husika yamefanywa dhidi ya jamii. Katika hali hiyo, hakuwa akimruhusu mtu kuingilia kati kwenye adhabu dhidi ya mhalifu. Kama uhalifu uliofanywa umeilenga jamii moja kwa moja, basi haki za watu lazima zilindwe. Kama uhalifu dhidi ya umma ukisamehewa, basi hatua hiyo hufungua milango ya dhulma kutendeka zaidi.

Miongoni mwa sifa za kipekee za Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akisamehe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Aliwasamehe hata wale waliomnyanyasa na kumtesa wakati akifikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu, akawaombea kwa Mwenyezi Mungu awaongoze kwenye njia yake na awape hadhi na heshima ya Uislamu. Siku moja Mtukufu Mtume ﷺ alipigwa mawe na waabudu masanamu wa Taif. Malaika Jibril عليه السلام akamjia na kuwambia kuwa alikuwa tayari kuwaangamiza watu hao kama ataombwa kufanya hivyo. Lakini Mtukufu Mtume ﷺ alimjibu: "Hapana! Ninatumai kupata kizazi kutoka watu hawa ambacho kitamuabudu Mwenyezi Mungu peke yake." (Bukhari, Bad` al-Khalq 7; Muslim, Jihad 111) Haukupita muda mrefu, watu wa Taif wakaingia katika Uislamu kutokana na dua hii ya Mtukufu Mtume ﷺ.

❁

Mtu mmoja aitwaye Mistah, maskini aliyekuwa akipata msaada wa kifedha kutoka kwa Abu Bakr رضي الله عنه, aliungana na watu waovu waliomzushia bibi Aishah, binti wa Abu Bakr. Kitendo kilichofanywa na Mistah kilimuumiza sana Abu Bakr. Uzushi na tuhuma hizo zilimuathiri mama wa ummah, binti wa Abu Bakr na mke wa Mtukufu Mtume ﷺ. Abu Bakr رضي الله عنه aliudhika sana kwa kitendo cha Mistah na kuapa kuwa hatamsaidia tena. Mistah na familia yake

wakaumizwa sana na hatua hiyo ya Abu Bakr. Mwenyezi Mungu akateremsha aya ifuatayo:

"…Je! Nyinyi hampendi Mwenyezi Mungu akusameheni?" (Nur, 24:22).

Abu Bakr aliposikia aya hiyo akasema: "Naam, ninataka kusamehewa!" Alitubu kutokana na hasira yake, akaendelea kumpatia Mistah msaada wa kifedha kama zamani (Bukhari, Maghazi 34; Muslim, Tawbah 56).

Mwenyezi Mungu ndiye msamehevu mkuu. Waislamu hupata furaha ya kusamehe kwa kadiri ya upendo wa kumpenda Mwenyezi Mungu ulio katika nyoyo zao. Wale wapendao kuonja ladha ya kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu wanatakiwa kusamehe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Ushindi wa kiroho na kimaanawi huwaendea wale wanaowasamehe kwa hiari watu wanaowakosea…

2. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu daima alikuwa akiwausia umma wake kuwa: "Mola wangu ameniusia kuamrisha mema na kukataza mabaya. "Nami nawausia kunifuata katika kufanya hivyo."

Kuamrisha mema na kukataza mabaya ndiyo kazi kubwa na muhimu sana ambayo mtu anaweza kuifanya kwa ajili ya watu. Huduma hiyo ni matokeo ya kuwapenda viumbe kwa ajili ya Muumba. Kwa hali hiyo, kuwaita na kuwalingania watu kwenye njia sahihi ni kazi tukufu. Kazi hiyo imeitwa kuwa ni "kazi ya mitume." Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an Tukufu:

"Na kwa yakini tutawauliza wale walio pelekewa Ujumbe, na pia tutawauliza hao Wajumbe." (Surah `Araf, 7:6)

Mtume Muhammad ﷺ alijipa jukumu la kuwaita na kuwalingania watu kwenye njia ya haki. Wakati wa Hijja yake ya mwisho

ijulikanayo kama "Hijja ya Kuaga", aliwauliza watu iwapo alikuwa amefanya kazi yake kikamilifu. Kwa kuwa sisi ni umma wake, kazi yake ni kazi yetu pia.

Qur'an Tukufu inasema:

"Na ni nani mbora wa kusema kuliko aitaye kwa Mwenyezi Mungu na akatenda mema, na akasema: Hakika mimi ni katika Waislamu?" (Fussilat, 41/33).

"Na uwe kutokana na nyinyi umma unao lingania kheri na unao amrisha mema na unakataza maovu. Na hao ndio walio fanikiwa." (Al `Imran, 3/104)

Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba, Mwenyezi Mungu akimuongoza kwenye Uislamu mtu mmoja kupitia mkono wako ni bora kwako kuliko kumiliki ngamia wekundu [mali iliyokuwa na thamani zaidi wakati huo]." (Bukhari, Ashab al-Nabi 9)

Furaha iliyoje kwa waumini watakaopata thawabu na malipo hayo adhimu! Mtukufu Mtume ﷺ anasema tena: "Mwenye kulingania kwenye njia ya haki hupata thawabu sawa na wale wanaomfuata, bila kunpuguzwa malipo ya wale wanaomfuata." (Muslim, `Ilm 16)

Malipo na thawabu zitokanazo na matendo yanayofanywa kwa ikhlasi na kutaka radhi za Mwenyezi Mungu pekee huwa ni kubwa zaidi. Hivyo, ni wajibu wetu kuwaonya makafiri na waislamu wajinga ambao hawana imani thabiti, na kuwataka kufuata njia ya kweli. Bila shaka hili litakuwa na msaada kwao na tutapata Baraka na neema kwa kuwaita na kuwalingania kwenye njia ya Mwenyezi Mungu.

Kwa hakika, kazi na juhudi zetu za kuwalingania na kuwaita watu kwenye njia ya Mwenyezi Mungu ni ishara tosha kuwa tuna ikhlasi katika imani yetu. Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Mwenye kushuhudia uovu, basi aurekebishe kwa mkono wake. Kama

hawezi, basi kwa maneno. Na kama hataweza, basi alichukie moyoni mwake. Na hilo chaguo la mwisho ndio kiwango cha chini kabisa cha imani." (Muslim, Iman 78)

Kuna maonyo makali kwa wale wanaopuuzia kuwaita watu kwenye njia ya kweli. Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu ambaye nafsi yangu iko mikononi Mwake, kwamba mtakapoacha kuamrisha mema na kukatazama mabaya, Mwenyezi Mungu atawateremshia ghadhabu Yake. Baada ya hapo mtaomba kusamehewa, lakini dua zenu hazitajibiwa." (Tirmidhi, Fitan 9)

Hata hivyo, tunatakiwa kuchunga kanuni na misingi ya kuwaita na kuwalingania watu kwa Mwenyezi Mungu. Vinginevyo, juhudi zetu zinaweza kuleta athari hasi badala ya kuwa na faida na athari chanya. Tunatakiwa kujua kwa undani kabisa maana ya jambo sahihi na jambo jema. Mtu mjinga asiyejua kile anachokifanya lazima kitakumbwa na makosa kimuundo na kimaudhui.

Msingi wa daawah nzuri ni elimu, maarifa na moyo safi. Bila maarifa na hekma hatuwezi kupata mafanikio, inakuwa kama mwenyeji anayempa mgeni wake kikombe kitupu kisichokuwa na kitu.

Haifai kwa mtu mtovu wa maadili na aliyeathiriwa na ubinafsi na umimi kujishughulisha na kazi ya kuwaita watu kwa Mwenyezi Mungu. Mtu kama huyo anaweza kusababisha matokeo mabaya kabisa. Ili aweze kutangaza dini hii vizuri, anahitaji kuwa na moyo mnyenyekevu uliopambwa kwa hekma za Qur'an Tukufu na wajihi unaoakisi tabia ya Uislamu ya kutabasamu. Anatakiwa kuwa alama ya mema na mazuri, na kuzungumza kwa lugha ya moyo.

Kazi ya kuwalingania na kuwaita watu kwa Mwenyezi Mungu inatakiwa kuambatana na wema na ukarimu pamoja na tabia ya Uislamu ya huruma. Sifa hizo zitawafanya wale wanaomsikiliza

wawe tayari kuupokea ujumbe anaotaka kuwapatia. Kwa sababu ni tabia yetu sisi wanadamu kuupokea vizuri muamala mzuri na tabia ya heshima tunayofanyiwa.

Mtu anayewalingania na kuwaita watu kwa Mwenyezi Mungu anatakiwa kutoyaangalia makosa na dosari za zamani za wale anaowalingania, kwa maana wasikilizaji wana haki ya moja kwa moja ya kujifunza ujumbe huo. Mlinganiaji hatakiwi kumbagua mtu katika ujumbe wake, bali anatakiwa kutambua kuwa miti mingi humea kutoka katikati ya mawe, na kwamba huruma na ukarimu wa Mwenyezi Mungu hauna mipaka wala ubaguzi.

Mtukufu Mtume ﷺ hakuwafungia milango ya ujumbe wa Uislamu watu kama Habbar ibn Aswad, ambaye alisababisha kifo cha binti wa Mtukufu Mtume ﷺ, bibi Zaynab; au Ikrimah ibn Abi Jahl aliyefanya kila aina ya matendo ya uadui dhidi ya Waislamu mpaka ilipofunguliwa Makkah; au Wahshi aliyemuua ami wa Mtukufu Mtume ﷺ, Sayyidna Hamza رضي الله عنه; au Hind, mke wa Abu Sufyan, aliyelitafuna kinyama ini la Sayyidna Hamza رضي الله عنه. Haidhuru kama mtu anayelinganiwa ana kashfa nzito kama za Fir'auni: hatakiwi kubaguliwa katika wito wa kuwalingania watu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mwenyezi Mungu Mtukufu alipomuamuru Nabii Mussa عليه السلام kwenda kwa Fir'auni, ambaye alijitangaza kuwa ni mungu, alimpa maagizo ya kumlingania Fir'auni kwa ulaini.

Mwenye kuwalingania na kuwaita watu kwenye Uislamu anatakiwa kuhubiri na kutangaza ukubwa wa rehma na hurma ya Mwenyezi Mungu kwa wakosefu ambao wamekata tamaa ya kusamehewa. Qur'an Tukufu inasema:

"Sema: Enyi waja wangu walio jidhulumu nafsi zao! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu. Na rejeeni kwa Mola wenu Mlezi, na silimuni

kwake, kabla ya kukujieni adhabu. Kisha hapo hamtanusuriwa." (Zumar, 39:53-4)

Tunatakiwa kuwa na maneno mazuri na yenye hekma wakati wa kuwaita kwa Mwenyezi Mungu wale watu ambao wanajiona kuwa wamekwama katika maisha yaliyojaa dhambi.

Hivyo ni wajibu wetu kama waumin kujitahidi sana kuwalingania na kuwaita watu kwa Mwenyezi Mungu bila kuwapuuza. Tunatakiwa kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kama matokeo ya juhudi zetu. Tusiifanye kazi hii kwa ubinafsi, tukiwaza "kujiokoa" sisi wenyewe. Bali tunatakiwa kufanya juhudi ya kuhakikisha misingi ya Uislamu inajulikana na kutangazika kwa watu wote.

Moyo una uwezo mkubwa sana wa kusoma maana na siri za viumbe. Mwenyezi Mungu Mtukufu ameonesha hekma kubwa kupitia viumbe Vyake, na ameviumba kwa idadi isiyokuwa na kikomo. Ulimwengu ni darasa lenye kuvutia kwa wale waliotunukiwa tunu na utayari wa kujifunza. Marafiki hao wa Mwenyezi Mungu kama Mawlana Jalaluddin Rumi na Yunus Emre wamekuwa wanafunzi nyota katika darasa hili. Walipata hekma za kimaanawi kutoka katika siri za ulimwengu huu, na kwa kile walichojifunza, waliendelea kutawanya manukato ya kiroho na kimaanawi kwenye nyoyo zenye shauku.

Mola wetu aliufungua ulimwengu wote kama kitabu ambacho ndani yake tunatakiwa kujifunza.

Mola wetu ameweka masomo mengi ndani viumbe vyote, kwa ajili ya nyoyo zenye kuwa na hisia na macho yenye kuweza kuona. Ishara yake inatuvuta na kutupeleka kwenye hekma ya kujitolea.

Nyuki huishi kwa wastani wa siku 45. Katika kipindi hicho huzalisha asali, lakini kiwango inachokitengeneza huwenda kikawa

mara mia zaidi ya mahitaji yake. Maisha ya nyuki sio kwa faida ya nyuki mwenyewe, bali ni kwa faida yaw engine.

Matunda ya mtu wa mplamu (mti unaofanana na mzambarau) yana mbegu ambazo huifanya jamii ya mti huo uendelee kuishi. Lakini mti huo huzalisha matunda mengi zaidi ya kiwango kinachohitajika ili kuzaliana. Mti huo hutoa matunda mengi ili jamii nyingine zifaidike nayo.

Hii ni miongoni mwa mifano ya ajabu ya uungwana wa kuwajali zaidi wengine, ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameionesha ndani ya viumbe Vyake.

Mola wetu ametuletea mti wa mbuyu kutuambia maisha haya ya dunia ni kitu gani. Mti huo mkubwa hupoteza majani yake wakati wa majira ya baridi; na kwa kufanya hivyo, hutuambia kimya kimya kuwa kifo kipo. Wakati wa majira ya kuchipua, hutuonesha kuwa suala la kufufuliwa baada ya kifo ni la kweli. Mbuyu hauzai matunda, na haufai kwa mbao. Uhai wake unapofikia kikomo unaweza tu kutumika kama kuni. Mti huo unatuonya kimya kimya: “Tahadhari, na tambua kuwa wewe ni kiumbe mwenye kufa. Usiwe kama mimi nisiyekuwa na matunda!”

Tunatakiwa kuwa kama mzaituni, na kuwa na stadi mbalimbali zinazowapa faida kubwa wengine. Mzaituni hauna gogo kubwa, lakini huanza kuzaa matunda ndani ya mwaka mmoja, na huendelea kutoa matunda mpaka mwisho wa uhai wake. Waridi nalo kutuambia: “Siku zote ninatabasamu kwa rangi na harufu yangu, lakini ninavumilia miba mingi mwilini mwangu. Ninakuusia kuwa kama mimi!”

Usatawi bila kuwajali wengine, afya na madaraka au elimu bila shukrani – yote hayo ni sawa na kuwa mfu kama mti wa

mbuyu. Ni jambo muhimu sana kwa waumini kuwa kama mti wenye matunda, na kujitahidi kuzaa matunda muda wote.

Watu wenye imani wanatakiwa kujiuliza: "Ni kwa kiwango gani ninatafakari na kutenda kwa maslahi yangu binafsi? Ni kwa kiwango gani ninawafikria watu wengine wenye shida? Ninajitolea kwa kiwango gani? Vitu kama vile nyuki, mawaridi, mplamu na mzeituni vina maana gani kwangu?"

Kwa kuwa mwanadamu ana hadhi na heshima kubwa zaidi ya nyuki au mti, tunatakiwa kufanya juhudi kuwa na faida zaidi kwa viumbe kuliko nyuki au mti. Mwanadamu ndiye kiumbe mwenye hadhi ya juu kabisa kuliko viumbe wote wa Mwenyezi Mungu. Hivyo, tunapaswa kujihudumia mara moja, lakini tuwahudumie wengine mara elfu moja. Qur'an Tukufu inasema:

"...Na wanakuuliza watoe nini? Sema: Kilicho chepesi." (Baqarah, 2:219)

Tunamuomba Mola wetu atujaalie kumjua na kumshukuru kwa fadhila zote alizotujaalia, na atufanye kushikamana na matakwa yake katika kipindi chote cha maisha yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie kuwa watu watakaowafaa wengine katika nyanja zote, katika maneno yetu, katika matendo yetu na katika mwenendo wetu, na tujaalie kuwa miongoni mwa waumini wa kweli. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaaliea kutafakari na kutenda kulingana na matakwa Yake!

Amiin!

SURA YA 4

Kuwapenda Watu Wa Nyumba Ya Mtume ﷺ



Watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume ﷺ walipata fursa ya kuushuhudia kwa karibu zaidi uzuri wa wajihi wake, ufasaha wa maneno yake, na adabu na staarabu wa mwenendo wake. Walipata upendo maalumu wa Mtukufu Mtume ﷺ kwa maana aliwalea yeye mwenyewe, kimatendo na kitabia.

SURA YA 4

KUWAPENDA WATU WA NYUMBA YA MTUME ﷺ

> Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Mpendeni Mwenyezi Mungu kwa amewatendea wema na ukarimu. Nipendeni mimi kwa sababu Mwenyezi Mungu anawapenda, na ipendeni familia yangu kwa Sababu mnanipenda!" (Tirmidhi, al-Manaqib, 31/3789)

Upendo na Urafiki

Upendo na urafiki humea kutokana na hisia na matendo ya pamoja. Kadiri watu wanavyoshirikiana vitu mbalimbali baina yao, ndivyo wanavyozidi kuwa na hisia za upendo na urafiki. Upendo hujidhihirisha kikamilifu pindi unapoziona sifa zako ndani ya yule unayempenda.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anawapenda waja ambao ndani mwao anaziona sifa Zake nzuri, na huwakubalia kuwa karibu Naye. Nabii Yaqub عليه السلام alimpenda sana mwanaye Nabii Yusufu عليه السلام kuliko watoto wake kumi nambili kwa sababu aliona hisia, fikra, stadi na sifa zake mwenyewe zikijiakisi kwa Yufusu عليه السلام. Miongoni mwa Waislamu, wale ambao waliakisi sifa za Mtukufu Mtume ﷺ

walionekana sana, na kwa hivyo walipendwa mno, na watu hao ni watu wa familia yake, watu wa nyumba ya Mtukufu Mtume ﷺ.

Watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume ﷺ walipata fursa ya kuushuhudia kwa karibu zaidi uzuri wa wajihi wake, ufasaha wa maneno yake, na adabu na ustaarabu wa mwenendo wake. Walipata upendo maalumu wa Mtukufu Mtume ﷺ kwa maana aliwalea yeye mwenyewe, kimatendo na kitabia.

Watu wa Nyumba yake walitoa gharama kubwa, nyoyo na roho zao, katika kipindi chote cha maisha yao kwa ajili ya thamani ya upendo wa Mtukufu Mtume ﷺ. Walipitia njia yenye tabu na mashaka kama aliyopita Mtukufu Mtume ﷺ hapo zamani. Watu hulipa gharama ya upendo wao, hususan wale wanaopenda kwa dhati, na gharama kubwa kabisa inayotolewa katika dunia hii ni gharama ya kumpenda Mwenyezi Mungu. Watu wa Nyumba ya Mtume ﷺ walipata fursa ya kuilipa gharama hiyo. Walikuwa na dhamira kubwa, na walikuwa na unyofu wa hali ya juu kabisa wa kiroho na kimaanawi.

Watu wa Nyumba ya Mtume (Ahlul-Bayt)

Ahlulbayt ina maana ya Watu wa Nyumba – yaani nyumba ya Mtukufu Mtume ﷺ, Fakhari ya Ulimwengu. Ni watu watukufu waliolelewa moja kwa moja na hekma na maadili ya Mtukufu Mtume ﷺ. Wao ni walimu wa umma wa Kiislamu, mnara wa udhati na kushikamana na Mtume ﷺ.

Neno *Ahlul-Bayt*, mwanzo kabisa hutumika kwa wanafamilia ya Mtukufu Mtume ﷺ, na kwa msingi huu humjumuisha Mtume ﷺ na familia yake pana – Ali, Ja'far, Aqil, Abbas na familia zao – Allah awe radhi nao wote. Kama ilivyo wajibu kwa Waislamu

kumtakia rehma Mtukufu Mtume ﷺ, vivyo hivyo ni wajibu kwao kuwaheshimu na kuwapenda Watu wa Nyumba ya Mtume ﷺ.

Ni kawaida kwa mtu kukipenda chochote kinachomkumbusha kuhusu mpendwa wake. Upendo huo unaweza kwenda mbali zaidi mpaka kuvipenda vitu, tabia na sehemu zinazomtambulisha mpendwa wake. Tunapompenda mtu, humkumbuka tunapoona mtu mwenye sifa na tabia kama zake, na hivyo humuita mtu huyo kwenye vikao vyetu. Ukubwa wa jambo hili hutegemea ukubwa wa upendo wetu. Tunapompenda mtu sana, mfumo wa uvaaji wake, ukaaji wake na utembeaji wake huingia nyoyoni mwetu. Shauku ya Waislamu kwenda kuliona joho la Mtukufu Mtume ﷺ au ndevu zake ni mfano makhsusi wa taathira ya upendo huu.

Upendo wa juu kabisa ni upendo wa Mwenyezi Mungu. Kisha nafasi ya pili ni ya upendo wa Mtukufu Mtume ﷺ. Wale wanaompenda sana Mtukufu Mtume ﷺ huwapenda pia watu wa nyumba yake na kufuata mwenendo wao.

Zaydn ibn Arqam رضي الله عنه anasema: “Siku moja Mtume ﷺ alituhutubia akiwa amesimama jirani na bonde la Khum baina ya Makka na Madina. Akaanza kumhimidi Mwenyezi Mungu Mtukufu na kutuusia kwa kusema, ‘Enyi watu! Mimi pia ni mwanadamu. Muda si mrefu mjumbe kutoka kwa Mola wangu, malaika Jibril, atanijia. Nitaitika wito wa Mola wangu na kuondoka. Ninakuachieni vitu viwili muhimu. Cha kwanza ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu, ambacho kitakuongozeni kwenye njia iliyonyooka. Kifuateni kwa moyo na bidii’. Mtume ﷺ alizidi kutuusia kuhusu kuifuata Qur’an, kisha akasema, “Pia ninawaachieni watu wa nyumba yangu. Muogopeni Mwenyezi Mungu na muwaheshimu watu wa nyumba yangu! Muogopeni Mwenyezi Mungu na muwaheshimu watu wa Nyumba yangu!’”

Wasikilizaji wakamuuliza Zayd ni nani watu wa Nyumba ya Mtume na kama wake wa Mtume ni katika watu wa nyumba yake. Zayd akajibu, "Wake zake pia ni watu wa nyumba yake. Lakini walio muhimu katika watu wa nyumba ya Mtume ni Ali, Aqil, Ja'far na familia ya Abbas, ambao wameharamishiwa kuchukua Zaka." (Muslim, al-Fada'il al-Sahabah, 36)

Salman ni Katika Sisi

Mbali na watu wa Nyumba ya Mtume ﷺ kwa damu na nasaba, kuna wengine wa kiroho. Salman al-Farisi ؓ, ingawa ni mgeni, alionesha tabia na mwenendo mkubwa wa Kiislamu kiasi kwamba watu wa Makka na Madina walidai kuwa Salman anatokana na jamii zao. Lakini Mtukufu Mtume ﷺ aliposikia majadiliano hayo kuhusu Salman, aliinyanyua daraja yake kwa kusema: "Salman ni katika sisi Ahlulbayt." (Ibn Hisham, III, Waqidi, II, 446-7; Ibn Saad, IV, 83; Ahmad, II, 446-7; Haythami, VI, 130)

Maneno haya ya Mtukufu Mtume ﷺ yanaonesha kuwa sharti la msingi linalomfanya mtu ahesabiwe kuwa miongoni mwa ahlulbayt ni: kushikamana na Uislamu na maisha mema. Mlango uko wazi kwa wengine, nje ya uhusiano wa damu na ndoa, kuwa watu wa Nyumba ya Mtume ﷺ – na hii ni daraja ya juu kabisa ambayo Muislamu anaweza kuifikia.

Kisa cha Muadh ibn Jabal, aliyejulikana kwa msimamo wake, mfano mzuri. Siku moja alimsindikiza Muadh mpaka nje ya mji wa Madina. Alikuwa amemtuma kwenda Yemen kuhudumu kama gavana. Alimuusia na kisha akamwambia, "Ewe Muadh! Yumkini usinione tena. Yumkini utalitembelea kaburi langu utakaporudi!" Muadh aliposikia maneno hayo akaanza kulia. "Usilie!" alisema Mtukufu Mtume ﷺ. Kisha aligeukia upande wa Madina na kusema:

"Miongoni mwa watu walio karibu nami zaidi ni wale wanaomuogopa Mwenyezi Mungu na kushikamana na imani yao."[18]

Sehemu nyingine, Mtukufu Mtume ﷺ aliainisha sharti linalomfanya anasibiane naye, akasema: "Washirika wangu ni wale wanaoshikamana zaidi na imani yao." (Abu Dawud, al-Fitan, 1/4242).

Mfano mwingine kama huo ni ule wa Usamah ibn Zayd رضي الله عنه. Siku moja Ali na Abbas رضي الله عنهما walikuja kwa Mtukufu Matume ﷺ na kumuuliza kuwa nani anayempenda zaidi miongoni mwa watu wa nyumba yake. Mtukufu Mtume ﷺ akasema kuwa anampenda binti yake, Fatmah, zaidi ya wengine. Wakasema, "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Hatuzungumzii wanawake." Mtukufu Mtume ﷺ akajibu, "Basi nimpendaye zaidi miongoni mwa watu wa Nyumba yangu ni Usamah ibn Zayd, ambaye Mwenyezi Mungu alimneemesha nami pia nikamneemesha." (Tirmidhi, al-Manaqib, 40/3819)

Mtangazaji mkubwa wa hadith za Mtukufu Mtume ﷺ, Hakim al-Tirmidhi, ameripoti kuwa Marafiki wa Mwenyezi Mungu wa baadaye wanaaminika kuwa miongoni mwa watu wa Nyumba ya Mtume, kiroho na sio kwa nasaba, kwa kuwa wanaendelea kumdhukuru na kumkumbuka Mwenyezi Mungu, na Mtukufu Mtume ﷺ alitumwa na Mwenyezi Mungu kuaweka hali ya kumkumbua Mwenyezi Mungu ndani ya nyoyo za wanadamu. (Hakim al-Tirmidhi, al-Kitab al-Khatm al-Awliya', uk. 35-6)

Hivyo, tunatakiwa kuhakikisha kuwa upendo na khofu ya kumuogopa Allah vinakita mizizi ndani ya nyoyo zetu, na kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake nyakati zote, ili tuweze kuingia katika kikao cha kiroho cha *Ahlulbayt*. Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Watu huwa pamoja na wale wanaowapenda."

18. Ahmad, V, 235; al-Haythami, al-Majmu`a al-Zawa;id, Bairut 1988, IX, 22.

Alama ya daraja hiyo huweza kuonekana katika matendo ya mtu na kujitolea kwake.

Tabia na Mwenendo wa Watu wa Nyumba ya Mtume ﷺ

Daima Mtukufu Mtume ﷺ alitaka watu wa Nyumba yake, ambao aliwapenda sana, waishi maisha ya utii ili wawe mfano kwa wanadamu wote. Daima aliwaelekeza na kuwaongoza kwenye maisha rahisi, ya unyenyekevu, na upole, ambayo ndiyo njia ya kumpeleka mtu kwenye wokovu siku ya mwisho. Daima aliwaonya kwamba "maisha ya kweli ni maisha ya Akhera." (Bukhari, al-Riqaq, 1) Kwa onyo hili alitaka kuwaepusha na tendo dogo la kidunia, ili kuwahamasisha kushikamana na utii na kumuogopa Mwenyezi Mungu. Hakutaka wawe na mwenendo unaowalekeza kwenye mambo ya kidunia.

Mtukufu Mtume ﷺ alimpenda sana binti yake, Fatimah رضي الله عنها. Hakuna baba anayeweza kuonesha upendo kama uliooneshwa na Mtukufu Mtume ﷺ kwa binti yake, Fatimah رضي الله عنها. Hivyo, kumpa mtoto wako jina la Fatimah huleta Baraka katika familia na kuiweka karibu na Mtukufu Mtume ﷺ.

Mtukufu Mtume ﷺ anasema, "Fatimah ni sehemu ya mwili wangu. Mwenye kumuudhi atakuwa ameniudhi, na mwenye kumfurahisha atakuwa amenifurahisha."[19] Vile vile alimbashiria habari njema ya kuwa miongoni mwa wanawake bora wa Peponi.[20] Lakini kwa upende mwingine akamuonya kutobweteka kwa sababu ya kuwa binti yake, bali atahadhari kuhusu Siku ya Hukumu. "Ewe Fatimah! Fuata mwenendo utakaokuokoa dhidi ya Moto wa Jahannamu! Sina mamlaka ya kukuokoa, bali nitahusiana na wewe kwa sababu wewe ni damu yangu." (Muslim, al-Iman, 348, 351)[21]

19. Muslim, al-Fada'il al-Sahabah, 93-96.
20. Ahmad, I, 293.
21. Tazama pia: Bukhari, at-Tafsir, 26/2; Tirmidhi, at-Tafsir, 27/2

Mtukufu Mtume ﷺ alimpenda sana Fatimah ؓ kiasi kwamba alimtakia maisha ya Akhera kuliko maisha ya dunia hii. Alimtaka kushughulika na maisha ya dunia hii kwa namna ya staha kubwa kabisa, na kutoa sadaka mali zake za ziada. Daima alimuonya kutoendekeza matamanio ya dunia hii, akamhamasisha na mambo ya kiroho.

Siku moja Mtukufu Mtume ﷺ alimuona Fatimah akiwa amevaa mkufu. Hakusema kitu, lakini kwa kuwa Fatimah alikuwa mtu makini na mwenye utambuzi, alipoutazama uso wa Mtukufu Mtume ﷺ, akazielewa fikra zake. Aliuchukua mkufu huo akaenda kuuza na pesa ya mkufu huo akaitoa sadaka, licha ya kuwa alikuwa na haja ya pesa. Mtukufu Mtume ﷺ aliposikia juu ya habari hiyo alifurahi sana. (Nasa`i, al-Ziynat, 39)

Wakati fulani bibi Fatimah ؓ alidhoofika na kuchoka. Kazi za nyumbani zilimchosha, na uwashaji moto na upishi ikawa tabu. Wakati fulani cheche za moto zilikuwa zikiunguza nguo yake wakati wa kuchochea moto, na alitaabishwa na vumbi zito lililokuwa likiruka wakati wa kufagia nyumba. Mikono yake ilikuwa ikichubuka wakati wa kugeuza jiwe la kusagia nafaka.

Siku moja wafungwa wa vita waliletwa mbele ya Mtukufu Mtume ﷺ. Bibi Fatmah ؓ akamuomba ampatie mmoja wa mateka hao kama mfanyakazi, ili kumsaidia kazi za nyumbani. Mtukufu Mtume ﷺ alilikataa wazo hilo. “Ewe Fatimah! Muogope Mwenyezi Mungu! Tekeleza majukumu yako ya lazima yaliyoamrishwa na Mwenyezi Mungu kwa uwajibikaji na utii, na tekeleza wajibu wako ndani ya familia. Unapopanda kitandani wakati wa usiku omba dua kwa kusoma *subhan Allah* mara 33, *alhamdu lillah* mara 33, *Allahu akbar* mara 34 – zote kwa pamoja zitakuwa mia moja. Hiyo itakuwa bora kwako kuliko kuwa na msichana wa kazi.” Bibi Fatimah akajibu kwa utiifu na unyenyekevu mkubwa, “Hakika

nimemridhia Mwenyezi Mungu na Mtume Wake!" Hivyo, Mtukufu Mtume ﷺ hakumpatia mfanyakazi licha ya kumpenda sana binti yake. (Abu Dawud, al-Kharaj, 19-20/2988)

Riwaya nyingine kuhusu tukio hili inasema kuwa Mtukufu Mtume ﷺ alisema: "Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa siwezi kukupatia msichana wa kazi ilhali waumini maskini nje ya mlango wangu (*Ahl al-Suffah*) wanafunga mawe tumboni ili kuzuia ukali wa njaa. Fidia nitakayoipata kutokana na mateka hawa nitaitumia kwa ajili ya *Ahl al-Suffah*" (Ahmad, I, 106)

Mtukufu Mtume ﷺ alimzoesha binti yake, Fatimah, maisha ya unyenyekevu kwa sababu atakuwa mama wa kiroho wa watu wa Nyumba yake na warithi wao watukufu - Abdul-Qadir al-Jaylani, Baha'uddin al-Naqshbandi, Ahmad al-Rifa`i, na marafiki wengine wengi wa Mwenyezi Mungu – na pia awe kama mfano kwa wanawake wa Kiislamu.

Mfano mwingine wa jinsi Mtukufu Mtume ﷺ alivyoilea familia yake kiroho, tunaweza kuipata katika sura ya 33 ndani ya Qur'an Tukufu. Surah Ahzab inasema:

"*Enyi wake wa Nabii! Nyinyi si kama yeyote katika wanawake wengine. Kama mnamcha Mungu basi msiregeze sauti zenu, akaingia tamaa mwenye maradhi katika moyo wake. Na semeni maneno mema. Na kaeni majumbani kwenu, wala msijishauwe kwa majishauwo ya kijahilia ya kizamani. Na shikeni Sala, na toeni Zaka, na mt'iini Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni baarabara.*" (Ahzab, 33:32-33)

Kwa muda wa miezi sita baada ya kuteremshwa kwa aya hizo, kila siku Mtukufu Mtume ﷺ anapokwenda msikitini alikuwa akisimama kwenye mlango wa Bibi Fatmah رضي الله عنها na kuita: "Enyi watu wa

Nyumba ya Mtume! Amkeni kwa ajili ya swala! *'Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni baarabara.'*" (Tirmidhi, al-Tafsir, 33/3206)

Wakati mwingine akihisi kuwa wanaweza wasiamke wao wenyewe kwa ajili ya swala za usiku kwa sababu uchovu, alikuwa akimuamha Sayyidna Ali ؓ na bibi Fatimah ؓ kwa kugonga mlango wao.

Anas ibn Malik ؓ anasema, "Sikuwahi kumuona mtu mwema kwa familia yake kama alivyokuwa Mtume ﷺ." Maneno hayo pia yana maana kwamba hakuna aliyeweza kuwalea wanafamilia wake kikamilifu kama alivyofanya Mtukufu Mtume ﷺ. Mtukufu Mtume ﷺ aliifundisha familia yake kuishi maisha ya kujisalimisha kikamilifu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuwa mfano kwa wengine katika hilo. kama ambavyo Mtukufu Mtume ﷺ alilelewa moja kwa moja na Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuwa bwana wa mitume wote, vivyo hivyo watu wa familia yake waliolelewa naye moja kwa moja walikuwa mabwana wa watu wote.

Kwa hakika watu wa Nyumba ya Mtume ﷺ walikuwa watu wenye moyo ulioakisi tabia za Mtukufu Mtume ﷺ aliyetumwa kama rehma kwa walimwengu. Kama ambavyo upepo wa asubuhi hubeba manukato ya bustani la mawaridi, vivyo hivyo, watu wa nyumba ya Mtume, waliokulia chini ya malezi ya kiroho ya Mtukufu Mtume, waliieneza hali yake ya kiroho kwa udhati na moyo wa hali ya juu. Kama ambavyo mshumaa mmoja waweza kuwasha mishumaa mingi, hivyo mishumaa hii ya Baraka ilibeba utukufu wa Mtume ﷺ kwenda kwa kizazi baada ya kizazi. Wale waliopata bahati ya kupata nuru kutoka kwenye moja ya mishuma hii hupata ladha ya furaha ya kukifikia chanzo cha nuru, Mtume Muhammad ﷺ.

Hivyo nasaba ya kiroho ya Masufi waliozaliwa na Sayyidna Ali na Abu Bakr lazima ipitie kwa Ja'far al-Sadiq, Imam kutoka

Nyumba ya Mtume. Imam al-A'dham, muasisi wa madhehebu ya Kihanafi, alikuwa mwanafunzi mkubwa na mtoto wa kiroho wa Ja'far al-Sadiq. Imam al-A'dham anaelezea jinsi alivyofaidika kiroho kutoka kwa Ja'far al-Sadiq: "Kama si miaka miwili niliyokaa na Ja'far al-Sadiq ningeangamia."

Hivyo, watu wa Nyumba ya Mtume wamekuwa njia ya aina yake ya kueneza mwenendo na shakhsia ya Mtukufu Mtume ﷺ kwa miaka mingi.

Kuwapenda Watu wa Nyumba Ya Mtume ﷺ

Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Qur'an Tukufu:

"...Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni barabara." (Ahzab, 33: 33)

Hivyo, aya hii inatueleza wazi kuwa Mwenyezi Mungu ndiye aliyewaondolea uchafu na aibu watu wa Nyumba ya Mtume.

Mtukufu Mtume ﷺ waliwapenda sana watu wa nyumba yake na alitaka umma wake uwapende pia. Anasema: "Mpendeni Mwenyezi Mungu kwa sababu amekutendeeni wema na ukarimu. Nipendeni mimi kwa sababu nampenda Mwenyezi Mungu, na wapendeni watu wa familia yangu kwa sababu mnanipenda!" (Tirmidhi, al-Manaqib, 31/3789)

Abu Bakr ؓ aliyejipambanua kikamilifu kwa kuwa pamoja na Mtukufu Mtume ﷺ, naye pia alikuwa mfano katika kuonesha heshima kwa watu wa Nyumba ya Mtume. Alikuwa akiwahimiza watu, "Mpendeni Mtume ﷺ, na kuweni na adabu kwake! Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba ndugu wa Mtume ﷺ ni wapendwa wangu kuliko hata ndugu na jamaa zangu mwenyewe."

Kuwapenda watu wa Nyumba ya Mtume ni muhimu sana kiasi kwamba tunapomtakia rehma Mtume ﷺ katika swala zetu za kila

siku huwatakia rehma pia. Hii inaonesha umuhimu wa daraja na nafasi ya ahlulbayt katika dini. Je kuna ndugu wa mtu waliopewa heshima kama hiyo?

Imam Shafi, muasisi wa moja ya madhehebu nne za kifqhi anasema, "Enyi watu wa nyumba ya Mtume! Kukupendeni nyinyi ni faradhi iliyoteremshwa na Mwenyezi Mungu katika Qur'an. Inawatosheni kuwa fakhari kwamba hana swala asiyekutekieni rehma katika swala yake!" (Muhammad al-Farsa, al-Fasl al-Kitab, uk. 522)

Mauaji Yaliyozitikisa Mbingu

Mauaji ya Sayyidna Husayn ؓ, mjukuu wa Mtume Muhammad ﷺ aliyekuwa akimpenda sana, akimbusu kwa upendo, na hata kumuweka mabegani kwake wakati akiswali, ni miongoni mwa uovu mkubwa kabisa katika historia ya Uislamu. Tukio hili la kikatili limeendelea kuwa maumivu na kiwewe katika akili za Waislamu. Wale wote waliohusika katika mauaji haya walighadhibikiwa na Mwenyezi Mungu.

Mauaji haya ya kikatili yalilaaniwa na kuchukiwa katika ulimwengu wa Kiislamu kiasi kwamba jina la khalifa wa wakati huo, Yazid, limeendelea kutumiwa na Waislamu kama tusi. Waislamu wote, bila kujali itikadi au madhehebu zao, daima wamekuwa wakihuzunika sana kwa mauaji ya kinyama ya Sayyidna Husayn ؓ. Hivyo hakuna sababu ya uhasama, na haipaswi kuwepo uadui baina ya Waislamu wa Sunni na Shia kwa sababu ya mauaji ya Sayyidna Husayn ؓ. Hata hivyo, baadhi ya wachochezi huzidisha uchochezi wao kana kwamba kuna mfarakano wa msingi. Waislamu wa madhehebu zote mbili hawapaswi kuishi kama maadui. Leo hii, Waislamu wote wanazidi kuungana kuliko hata zamani. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an:

"Hakika waumini ni ndugu…" (Hujurat, 49: 10)

Kujiingiza katika uhasama usioingia akilini hakuleti faida. Huudhuru umoja wa umma wa Kiislamu na kuziuminya nyoyo tukufu za waliotutangulia. Ushabiki wa kimadhehebu, wakati wowote unapoibuka miongoni mwa Waislamu, umekuwa ukisababisha hasara. Hata mgongano mdogo hutoa fursa kwa wale wanaofaidika na mgawanyiko wa Waislamu. Hivyo, wakati wote tunapswa kuwa makini tusiangukia katika mtego wa mfarakano, na tuachane na mabishano yasiyokuwa ya lazima.

Ili tuweze kufanikiwa katika hili, hatuna budi kuanzisha eneo la tatu la maelewano ya pamoja sambamba na Qur'an na sunna za Mtukufu Mtume ﷺ, na eneo hilo ni mapenzi kwa *ahlulbayt* wa Mtume. Upendo huo, ambao pia umeamriwa na Mtukufu Mtume ﷺ, ni sifa ambayo Waislamu wote wanatakiwa kuiibua.

Wauthmaniyyah daima waliwajali na kuwaheshimu watu wote wnaotokana na nasaba ya Mtukufu Mtume ﷺ. Suala la kuwahudumia watu wa Nyumba ya Mtume walilipa uzito mkubwa sana kiasi kwamba ilianzishwa ofisi iliyotwa *Naqib al-Ashraf* (Kiongozi wa Dhuriya wa Mtume) katika dola ya Uthmaniya ili kulinda heshima ya watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume ﷺ.

Sisi, wazawa wa wahenga waliobarikiwa, tunapaswa kuzihuisha nyoyo zetu kwa upendo ya Qur'an na *ahlul-bayt*, ili tustahili kupendwa na Mtukufu Mtume ﷺ. Tunatakiwa kumchukuliwa Mtume ﷺ kama mfano katika matendo na mazungumzo yetu. Tujipambanauo kwa kuwa naye na watu wa nyumba yake, *ahlul-bayt*.

Mola wetu! Tunakuomba utujaalie sehemu katika hali ya kiroho ya Mtume ﷺ, ahli Zake, Maswahaba zake na ya Marafiki wa Mwenyezi Mungu!

Amiin…

SURA YA 5

Haki Na Uadilifu - 1

Hatupaswi kusahau kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, anayewaagiza waja Wake kuchunga haki na uadilifu, daima anawaunga mkono wale wanaotendewa dhulma na uonevu. Wale wanaodhani kuwa hawawezi kufanywa lolote katika dunia hii kwa wayatendayo, hawawezi kukwepa kupiga magoti na kujaribu kujiteteambele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambaye ndiye hakimu wa mahakimu…

SURA YA 5

HAKI NA UADILIFU - 1

Maadili ya Kiislamu yanajumuisha vipengele vyote vya uzuri na ukamilifu wa kibinaadamu na kuipeleka roho ya mwanadamu kwenye kilele cha mambo mema. Asili na chanzo cha maadili haya ni cha kipekee, kwa maana yamejengwa kwenye msingi imara wa haki na uadilifu. Hii ni kwa sababu amani ya mwanadamu hupatikana na kuimarika tu pale haki na uadilifu vinapochungwa na kuzingatiwa.

Sasa basi, haki na uadilifu ni nini?

Tafsiri ya jumla ya haki na uadilifu ni *"kumtendea kila mtu na kila kitu kulingana na ustahiki wake; kutoa hukumu kwa ukweli;na kuamiliana nao kwa namna ya mizania, wasitani na msimamo wa kati kwa kati."*

Kwa tafsiri hii, kumpa mtu zaidi ya haki anayostahili ni kukiuka haki za wengine, na kumpa pungufu ya kile anachostahili ni kumpokonya haki yake, na hiyo ni kwenda kinyume na uadilifu. Watu wenye imani ya kweli huwa makini sana wasifanye uhalifu huo. Yaani, muumini huhisi kuwa anawajibika kumpa kila mwanadamu anachostahiki.

Uislamu unataka uadilifu ufanywe katika kila hatua ya maisha na katika mazingira ya aina yoyote ile. Ili kuishi maisha yanayompendeza Mwenyezi Mungu ni sharti tuchunge mizania ya haki na uadilifu, kwa maana uadilifu umechukua nafasi kubwa sana miongoni mwa maamrisho na makatazo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hivyo, muumini anatakiwa kuwa muadilifu mbele ya Muumba, kisha mbele ya viumbe wenzake, kisha kujitendea uadilifu yeye mwenyewe.

Vivyo hivyo, kila muumini anatakiwa kufanya uadilifu wakati wa kupima bidhaa, wakati wa kuwahukumu watu, wakati wa kuandika kumbukumbu, na wakati wa kutoa ushuhuda mahakamni. Aidha, tunatakiwa kuchunga stahiki ya Mwenyezi Mungu katika swala na ibada zetu. Tunatakiwa kuchunga muundo stahiki wa ibada zetu, kwa sababu hiyo ni haki stahiki ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Waja wake wanawajibika kuzitekeleza na wataulizwa mbele yake.

Muumini anayeyapangilia maisha yake kulingana na uelewa huu na kulingana na vipimo vya haki na uadilifu huweza kufikia daraja ya *ahsan al-taqwim*, yaani "umbile bora kabisa." Hii ni kwa sababu kuchunga haki na uadilifu ni miongoni mwa sifa za Mwenyezi Mungu. Jina tukufu la Mwenyezi Mungu la *al-'Adl,* yaani "Muadilifu," linaonesha kuwa Mwenyezi Mungu ndiye mmiliki wa moja kwa moja wa haki na uadilifu, na pamoja na hivyo Yeye Mwenyewe ni Haki na Uadilifu. Jina hili Tukufu linajidhihirisha katika ulimwengu huu, lakini litajihidhirisha kwa ukuu wake wote wakati wa kutoa hukumu Siku ya Kiyama. Mwenyezi Mungu Mtukufu anatangza ndani ya Qur'an Takatifu:

"Nasi tutaweka mizani za uadilifu kwa Siku ya Kiyama. Basi nafsi haitadhulumiwa kitu chochote. Hata ikiwa ni uzito wa chembe ya khardali tutaileta. Nasi tunatosha kuwa washika hisabu." (Anbiya', 21:47)

Hatupaswi kusahau kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, anayewaagiza waja Wake kuchunga haki na uadilifu, daima anawaunga mkono wale wanaotendewa dhulma na uonevu. Wale wanaodhani kuwa hawawezi kufanywa lolote katika dunia hii kwa wayatendayo, hawawezi kukwepa kupiga magoti na kujaribu kujiteteambele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambaye ndiye hakimu wa mahakimu.

Tunaweza kusema kuwa katika viumbe wote, wanadamu ndio wanaobeba mzigo mkubwa wa uwajibikaji kuhusu haki na uadilifu. Mwanadamu ndiye kiumbe mtukufu kuliko viumbe wote na vumbe wote wapo kwa ajili ya matumizi yetu. Hivyo, tunabeba wajibu wa kuchunga haki na ustawi wao. Ndiyo maana mwanadamu amewajibishwa kulinda si haki zake pekee bali pia haki za kila mtu na kila kitu. Tunawajibika kwa haki za mimea, wanyama,vitu visivyokuwa na uhai na hata haki zetu wenyewe.

Tunapowatazama marafiki wa Mwenyezi Mungu tunakuta wakiwa mfano bora wa kuchunga haki za kila kitu. Siku moja, Bâyazid al-Bistâmî, ambaye alikuwa miongoni mwa Marafiki wa Mwenyezi Mungu, alipumzika chini ya mti na kupata chakula, kisha akaendelea na safari yake. Baada ya kutembea maili kadhaa alimuona mdudu (mchwa) akiwa kwenye begi lake la safari. Akasema, “Ewe Mola wangu! Nimemtenganisha mdudu huyu na makazi yake!” Hivyo akarudi kwenye mti ule aliokuwa amekaa na kumuacha hapo.

Mshairi Firdawsî ana utenzi mzuri katika kitabu chake cha *Shahnâma*: “Usimsumbue mchwa anayevuta punje ya ngano! Naye anaishi maisha yake- na maisha ni matamu.”

Siku ya Hukumu, viumbe wote watafufuliwa pamoja na wanadamu, na watadai haki zao tulizozikiuka wakati wa uhai wao duniani. Ndiyo maana imekatazwa kumtesa mnyama, kumchosha

isivyostahili, au hata kukata tawi la mti bila sababu au haja. Tunaruhusiwa kumuua mnyama hatari kwa dharura, lakini hata wakati wa kumuua mnyama hatari hatutakiwi kumsababishia maumivu yasiyokuwa ya lazima. Kwa mfano, tunapojaribu kujilinda dhidi ya nyoka, ni bora akauawa kwa pigo moja tu.

Kwa muktsarai, kila muumini anatakiwa kuielewa maana ya haki na kuwajibika na awe makini sana katika kuhakikisha anatenda uadilifu. Muamala wenye uadilifu katika mambo yote ni miongoni mwa mambo mema kabisa kwa muumini. Lakini kwa wale wenye ukomavu zaidi katika utambuzi wao, kuna jambo jema kuliko hata hili: kusamahe katika uadilifu.

Kusamehe katika uadilifu

Wale wenye imani ya kweli wanaofikia anga ya juu kabisa ya uoni hupendelea kulipa msamaha na huruma badala ya kudai kutendewa uadilifu katika kadhi zao binafsi. Hii ni kwa sababu wanafanya hivyo ili Siku ya Hukumu Mwenyezi Mungu apate kuwatendea msamaha, huruma, wema na ukarimu badala ya kuwahukumu kwa uadilifu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasifu tabia hiyo njema akisema:

"Na mkilipiza basi lipizeni sawa na vile mlivyo adhibiwa. Na ikiwa mtasubiri, basi hakika hivyo ni bora zaidi kwa wanao subiri." (Nahl, 16:126)

Je lengo letu kuu sio kupata msamaha na ukarimu wa Mwenyezi Mungu? Ndiyo maana waja wema wanapotendewa ubaya na ukali, hawapendelei kulipiza na kuadhibu. Bali hupendelea kuwa na subiri kwa ajilia ya Mwenyezi Mungu, na kuishinda hasira yao. Daima waja hao hupita njia ya uvumilifu na subira, na hulenga kupata huruma kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuwahurumia viumbe na waja wa Mwenyezi Mungu.

Kama tulivyosema, ni kwa msingi huu kwamba Abu Bakr ﷺ alimsamehe mtu aliyemzushia kashfa binti yake, bibi Aisha ﷺ, na akaendelea kumpatia sadaka na zaka. (Bukhari, Maghazi, 34; Muslim, Tawbah, 56) Alihamasishwa na aya ifuatayo:

"Na wale katika nyinyi wenye fadhila na wasaa wasiape kutowapa jamaa zao na masikini na walio hama kwa Njia ya Mwenyezi Mungu. Na wasamehe, na waachilie mbali. Je! Nyinyi hampendi Mwenyezi Mungu akusameheni?" (An-Nuur, 24: 22)

Na ndiyo maana watu wenye hekma hutenda kulingana na muongozo wa aya ifuatayo:

"Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu." (Fussilat, 41:34)

Mfano mmojawapo katika mifano mikubwa kuhusu maadili haya ndani ya Qur'an Tukufu ni kadhia ya Nabii Yusufu ﷺ aliyefanyiwa dhulama kubwa na ndugu zake. Bila kujitambulisha kwao, nabii huyu aliwakirimu na kuwapa zawadi mbalimbali walipokuja kumtaka msaada. Baada ya kupokea misaada mingi kutoka kwake ndipo walipokuja kujua kuwa anayewasaidia ni Yusufu. Wakathibitisha ukweli huu:

Wakasema: "Wallahi! Mwenyezi Mungu amekufadhilisha wewe kuliko sisi, na hakika sisi tulikuwa wenye kukosa." (Yûsuf, 12:91)

Nabii Yusufu ﷺ alionesha moyo mkubwa wa usamehevu na kuimarisha sifa hii kwa kusema:

"Akasema: Leo hapana lawama juu yenu. Mwenyezi Mungu atakusameheni, naye ni Mwingi wa kurehemu kuliko wote wanao rehemu." (Yûsuf, 12/92)

Aidha, Yusufu anamtupia lawama Shetani kwa yaliyotokea, badala ya ndugu zake:

"...Shet'ani alichochea uadui baina yangu na ndugu zangu..." (Yusuf, 12: 100)

"Niliuzwa kama mtumwa. Kwa sababu yenu pia nilikuja kujua kuwa mimi ni mtoto wa nabii!" Hayo yalikuwa maneno ya Yusufu kwa ndugu zake yaliyoonesha wema wake. Sio tu kwa aliwasamehe, bali pia hakuangalia ukatili na dhulma waliyomfanyia huko nyuma. Hilo liliwafanya ndugu zake wakosefu washikwe na mshangao na kumstaajabia ndugu yao waliyekuwa wamemsaliti.

Katika maadili ya juu ya Nabii Yusufu عليه السلام tunaweza kusema kuwa kupendelea huruma juu ya uadilifu na kuwasamehe wakosefu hujionesha kiwango kingine kabisa cha urekebishaji na muongozo. Lakini ili kupata muamalahuo, mkosaji anatakiwa kuhuzunika na kusikitikia uhalifu wake, na ayaelewe makosa. Hatupaswi kulisahau hili. Kwa maana kama mkosaji atasamehewa pasipokuhisi majuto, basi kumsamehe kutakosa ubora na wema na badala yake hugeuka kuwa ishara ya udhaifu na unyonge. Ili huruma na msamaha viwe na maana itategemea hali na tabia ya mkosaji. Kumsamehe mtu mchafu na katili huwenda kukamhamasisha kuendelea na uovu wake. Mkosaji asipobadilika baada ya kusamehe, hapo wale aliwatendea ubaya watataka aadhibiwe.

Tunaweza kumsaheme mkosaji pindi haki zetu binafsi zipokiukwa. Lakini, uhalifu unaotendwa dhidi ya umma na kuhusisha haki za watu wengine basi haki na uadilifu vinatakiwa kufanyika, vinginevyo kutochukua hatua kutahamasisha uhalifu zaidi. Jamii yote inaweza kuharibiwa na kupata hasara kwa uovu wa watu kama hao.

Kiongozi wa maisha yetu, Mtukufu Mtume ﷺ, alikuwa akisamehe makosa anayotendewa yeye kama yeye. Lakini hakuvumilia dhulma unaofanywa dhidi ya watu wengine. Alihakikisha haki za watu zinapatikana.

Hiki ndicho kipimo chenu katika kuchunga haki na uadilifu. Watu wanaofanya uadilifu kwa mtindo huo ndio wanaoufanya kwa usahihi. Tunapowatendea watu uadilifu mara ya kwanza, hutarajia kuwa nao watatutendea uadilifu. Amani na furaha yoyote inayopatikana katika maisha ya mwanadamu inategemea kiwango cha utekelezaji wa haki na uadilifu.

Uadilifu wa kidini hauna mbadala katika kudumisha nidhamu na maelewano katika jamii. Hata hivyo, uadilifu una maana nyingine katika uwanja wa uelewa na hisia ambazo wanadamu huingia mbele ya Mola wao. Uadilifu wa Kimungu unafuata kanuni za aina yake.

Kupambana na dhana ya uadilifu wa Kimungu umewapelekea wengi kupotea. Katika ulimwengu huu tunaona kwamba watu hawana fursa zilizo sawa. Baadhi yao ni matajiri, wengine ni masikini; baadhi huzaliwa na ulemavu, wengine wana afya; na baadhi huishi kwa muda mrefu ilhali wengine huishi kwa muda mfupi. Kwa kuwa mambo yote haya huamuliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, tofauti hizi zinaweza kuonekana kana kwamba zinapingana na uadilifu wa Kimungu. Hilo ni htimisho la hoja na akili mbovu na moyo wenye ujinga. Lakini, tukilitazama katika dirisha la imani na hekma, tunaweza kubaini kitu kingine kabisa. Msingi w uadilifu ni ustahiki wa kitu.

Uadilifu unahusika tu kama kitu fulani kinastahiki!

Watu hawakuumbwa kwa sababu walistahiki kuumbwa. Uumbwaji wa mwanadamu kutoka katika hali ya kutokuwa cho-

chote ni tunu kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu ambayo hakuna shukrani inayoweza kulingana nayo. Tunu iliyoje kudhihiri katika ulimwengu wa uwepo kutoka kwenye ulimwengu wakutokuwepo, na ndani ya ulimwengu wa uwepo ukaumbwa kama mwanadamu, kiumbe bora kabisa katika viumbe vyote, badala ya kuumbwa kama nyoka au tandu, jiwe au kipande cha udongo au gugu au jani. Tumepewa neema hii pamoja na nyingine nyingi, bure kabisa bila malipo. Tulitoa bei gani ili kupata neema hizo?

Kwa muktadha huu, kudai "uadilifu" kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya kutopewa vitu fulani vya mpito ni kujipeleka kwenye maangamizi. Hakuna tunachodai. Sharti la uadilifu ni ustahiki wa kitu, ikiwa na maana ya kuwa na haki halisi juu ya kitu hicho, kukipata kwa kukifanyia kazi, au kukigharamia na kukinunua. Lakini tulitoa gharama ya aina gani ili kupata fursa ya kuumbwa? Kazi gani tuliyoifanya na kutupatia sifa ya ubinadamu? Hakuna, hakuna chochote.

Mwenyezi Mungu Mtukufu alipenda maisha haya yawe na hatua au awamu mbili, awamu ya duniani na ya pili ni awamu ya Akhera. Katika awamu ya kwanza, Mwenyezi Mungu Mtukufu amejidhihirisha kwa sifa ya Mwingi wa rehma, ilhali katika wamu ya pili, amejidhihirisha kwa sifa ya Muadilifu. Mwenyezi Mungu Mtukufu aliuumba ulimwengu na wanadamu kwa Jina la Mwingi wa rehma, sio kwa Jina la Muadilifu.

Mali yote waipatayo viumbe ni tunu na zawadi itolewayo na Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu hawajibikiwi kuwapa viumbe Wake zawadi na tunu zenye kufanana. Kama viumbe wawili wangekuwa sawa katika vipengele vyote, basi uwepo wa mmojawapo usingekuwa na maana tena na utakuwa wa kipuuzi. Sifa ya Mwenyezi Mungu ya ukamilifu *al-Muta'ali,* "Mwenye Ukuu na Utakasifu", ambayo iko nje hata ya uwezo wa akili, hai-

kubali vitu visivyokuwa na maana na upuuzi. Mwenyezi Mungu Mtuukufu ameviumba vitu vyote na kuvipangilia katika mizanisahihi. Kwa hakika, Mwenyezi Mungu ametakasika dhidi ya upungufu na kasoro zote.

Hivyo, hakuna anayeweza kuuliza: "Nilifanya kosa gani lililonifanya niwe mfupi?" "Kwa nini nilizaliwa na wazazi wajinga badala ya wazazi wasomi?" "Kwa nini nilizaliwa maskini badala ya kuzaliwa tajiri?" Hali zote hizi mbalimbali hutokea kutokana na ishara mbalimbali za ukarimu wa Mwenyezi Mungu. Tunaweza kujifunza ukweli huu kutoka katika tukio moja lililotokeza Zama za Furaha:

Tha'labah alimuomba Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amuombee dua ili awe tajiri. Mtukufu Mtume ﷺ akamjibu: "Ewe Tha'labah! Mali kidogo itakayokufanya umshukuru Mwenyezi Mungu ni bora kuliko mali nyingi itakayokufanya umkufuru." Kisha akasema: "Ewe Tha'labah! Je hali ya maisha yangu haitoshi kuwa mfano bora kwako?"

Lakini Tha'labah hakuielewa maana ya muongozo huu: alisisitiza kuwa anataka kuwa tajiri. Tamaa yake hiyo ilimfanya asilione onyo alilopewa na Mtukufu Mtume ﷺ. Hivyo, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akamuombea Tha'labah awe tajiri. Alipata utajiri – lakini akaangukia katika kufuru na kutoridhika. Mwisho wa uhai wake, alijuta sana. Alisema akiwa kwenye kitanda cha maradhi yake: "Laitani ningeusikiliza wosia wa Mtume ﷺ!" Alisikitika sana kwamba aliyafuata matamanio yaliyoyabadilisha maisha yake yote kuwa jela.[22]

Ndiyo maana mja anatakiwa kuiweka akilini aya ya Qur'an isemayo:

22. Tazama: Tabarî, Jâmi u l-Bayân, XIV, 370-372.

"Tena bila ya shaka mtaulizwa siku hiyo juu ya neema." (Takâthur, 102/08)

Kutosheka na kile tunachojaaliwa na Mwenyezi Mungu ni wajibu na ni alama ya ukomavu, kwa maana kutokuwepo kwa usawa katika neema za Mwenyezi Mungu sio dhulma. Mwenyezi Mungu Mtukufu anaweza kumuumba mja katika afya kamili na akamuumba mwingine katika hali ulemavu kiasi. Anaweza kumuumba mtu mmoja na vipawa vikubwa vya kiakili, huku akimuumba mwingine na vipawa pungufu. Anaweza kumfanya kiumbe fulani kuwa nyoka anayetambaa ardhini, na akamuumba kiumbe mwingine kuwa ndege anayeruka angani. Tofauti hizi hazitengenezi msimgi wa viumbe kufanya pingamizi dhidi ya hali zao wenyewe.

Wanyamawana uelewa na hisia za kutosha kudumisha na kutunza uhai wao, na wote wana furaha kwa vile walivyo. Hawana wasiwasi wowote zaidi ya kujaza matumbo yao na kukidhi matamanio yao ya kimaumbile na ya kiasili. Hawaulizi kwa nini hawakuumbwa kama wanadamu! Na kama ambavyo mnyama au mtu hauulizi "Kwa nini sikuumbwa mwanadamu?", vivyo hivyo watu waliokosa baadhi ya mambo, kama vile ulemavu, maradhi au umaskini, hawawezi kumtuhumu Mwenyezi Mungu kuwa anatenda dhulma.

Aidha, manufaa ya mali ndogo au kubwa yataamuliwa kwenye mizani ya hisabu huko Akhera. Rasilimali ndogo zina maana ya kuwajibika kidogo, ilhali mwenye rasilimali kubwa na uwajibikaji wake utakuwa mkubwa.

Asiyeweza kuielewa hekma na siri za qadari hawezi kuelewa maana ya kujisalimisha na kuuridhia utashi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tunamkumbuka Abu Talha ﷺ na mkewe, Umm Sulaym

ﷺ, maswahaba wawili wa Mtukufu Mtume ﷺ. Abu Talha alipokuwa safarini, mwanaye wa kiume, ambaye alikuwa mgonjwa sana, alifariki dunia. Abu Talha aliporejea, alimuuliza mkewe juu ya hali ya mtoto wao. Umm Sulaym akajibu, "Maumivu yake yamekwisha. Nadhani anahisi kufarijika."

Siku ya pili Abu Talha alipotaka kutoka, mkewe Umm Sulaym akasema:

"Ewe Abu Talha! Tazama jirani yetu alivyofanya! Nilipomtaka arejeshe mali niliyomuazima, hakutaka kuirejesha!"

"Sio jambo sahihi hilo!" Abu Talha alisema.

Hapo Umm Sulaym akasema, "Ewe Abu talha! Mwanao alikuwa amana uliyopewa na Mwenyezi Mungu. Ameichukua amana yake." Mwanzo Abu Talha alishtuka, akakaa kimya kwa muda. Kisha akasema, *"Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake tutarejea."* (Tazama: Bukhârî, Janâ'iz 42, Aqîqah 1; Muslim, Adab 23, Fadâ'il as-Sahâba 107)

Tukio hilo ni mfano bora unaotufanya tutambue kuwa neema zote tunazopewa na Mwenyezi Mungu katika dunia hii ni amana ambazo tumekabidhiwa kwa muda mfupi! Msimamo huo wa kuridhika na kujisalimisha ni msimamo ambao tunatakiwa kuuonesha wakati Allah anaporupatia neema na wakati anapoamuza kuzichukua.

Kwa hakika, kuweza kufuata mfano wa Nabii Ibrahimu عليه السلام aliposema, *"Nimejisalimisha kwa Mola wa Walimwengu",* licha ya kukabiliwa na mtihani mzito, ni mojawapo katika alama kuu za kuwa muumini bora.

Mola wangu! Tunakuomba utujaalie maisha yenye kuongozwa na hali ya ikhlasi na kujisalimisha kwa dhati Kwako! Tujaalie tushikamane na haki na uadilifu! Tujaalie msamaha na huruma yako pamoja na haki na uadilifu, na utusamehe Siku ya Hukumu!

Amiin…

SURA YA 6

Haki Na Uadilifu - 2

Dunia hii ni mahali pa kutahiniwa. Hatujaja hapa bila malengo, na walahatukuachwa tu… Hatupo katika dunia hii kwa ajili tu ya kukidhi matamanio yetu ya kihayawani. Mwenye kuyafuata matamanio hayo huweza kugeuka kiurahisi na kuwa dhalimu. Kwa namna hiyo, huyahatarisha maisha yetu ya milele.

SURA YA 6

HAKI NA UADILIFU -2

Ulimwengu huu wenye mpangilio na nidhamu maridadi haukutokea kwa sadfa au bahati nasibu. Haukuumbwa kuwa zana ya kuridhisha matamanio yetu. Ulimwengu kwa lengo tukufu, na umefanywa kuwa sehemu ya kuwatahini wanadamu. Hivyo, ulimwengu na mwanadamu havikuumbwa kwa upuuzi tu.

Hakuna kinachoumbwa bure tu, bila hikma au sababu, kwa maana Jina lingine la Mwenyezi Mungu ni *al-Haqq*, yaani Haki, Ukweli, Uhalisia. Ametakasika dhidi ya kufanya kitu kwa upuuzi au bila sababu. Vitu vyote vitokavyo Kwake ni haki. Qur'an Tukufu inasema:

"Naye ndiye aliye ziumba mbingu na ardhi kwa Haki." (An'âm, 6:73)

Utazame ulimwengu wote, mtazame mwanadamu, na vitazame viumbe vingine. Kila kimoja kimetengenezwa kwa ustadi wa hali ya juu na wenye kushangaza. Uumbwaji wake unaonesha hekma na mafunzo yasiyohesabika, vipimo na mizania maridhawa. Kila mwenye akili salama anatakiwa kutafakari kwa makini na kwa undani ishara za huu ukuu wa Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anatueleza juu ya ukweli huu kwa kutuonya:

"Na mbingu ameziinua, na ameweka mizani, ili msidhulumu katika mizani." (Ar-Rahman, 55: 7-8)

"Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake kwa mchezo. Hatukuviumba hivyo ila kwa Haki, lakini wengi wao hawajui." (ad-Dukhân, 44:38-39)

"Ati anadhani binaadamu kuwa ataachwa bure?" (Qiyâmah, 75:36)

"Je! Mlidhani ya kwamba tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa?" (Mu'minûn 23:115)

Qur'an Tukufu inaeleza wazi kuwa ulimwengu huu ni sehemu ya kutahiniwa. Hatukuja hapa bila lengo, wala hatukuachwa peke yetu. Tuna utashi ambao tunaweza kuutumia kwa wema au ubaya, lakini Mola wetu ametuwekea mipaka, na akatuumuru kuichunga mipaka hiyo. Hatukuletwa katika dunia hii kwa ajili ya kukidhi matamanio ya nafsi zetu. Mwenye kufuata matamanio hayo ya kihayawani anaweza kugeuka kiurahisi kuwa dhalimu na mnyonyaji. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tunayaweka hatarini maisha yetu ya milele.

Kwa hakika, kuwa mja wa Mwenyezi Mungu humaanisha kuchunga mipaka iliyowekwa na Mwenyezi Mungu. Mja anapochunga mipaka hiyo huwa amejiokoa dhidi ya adhabu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mwenye kuivunja na kwenda kinyume na mipaka hiyo, anakuwa amejiandalia adhabu, na hivyo kuidhulumu mwenyewe nafsi yake. Ikumbukwe kuwa kinyume cha uadilifu ni dhulma.

Kinyume cha Uadilifu ni Dhulma

Ndani ya Qur'an Tukufu, Mwenyezi Mungu Mtukufu anaelezea sifa za binaadamu:

"...Hakika yeye (mwanadamu) amekuwa dhaalimu mjinga." (Ahzâb, 33:72)

Ujahiliya ni moja katika sababu kubwa zinazompeleka mtu kutenda dhulma na ukandamizaji. Kinyume cha *jahiliyyah* iliyotajwa ndani ya Qur'an Tukufu ni *'ilm*.

Maarifa na elimu ya kweli ni ile inayomuongoza mwanadamu kumtambua Mwenyezi Mungu Mtukufu – yaani kumtambua Mwenyezi Mungu ndani ya nyoyo zetu. Hivyo, kama ambavyo ujinga humpeleka mwanadamu kwenye dhulma, maarifa humpeleka kwenye wema, uadilifu na ukweli.

Kiini na asili ya ukweli na haki ni Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mwenyezi Mungu Muumba wa ulimwengu ndiye aliyetujuza Haki na ukweli. Mwenyezi Mungu Mtukufu anatuambia ndani ya Qur'an Tukufu:

"...Sema: Hakika uwongofu wa Mwenyezi Mungu ndio Uwongofu. Nasi tumeamrishwa tusilimu kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote." (An'am, 6:71)

Ni jambo baya kabisa kutojali maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume Wake, ambayo hutuongoza kwenye furaha isiyokuwa na kikomo. Anayefanya hivyo huwa anajidhulumu. Dhulma kubwa kabisa ni kufumbia macho ukweli na haki bila kushurutishwa. Kila dhulma ina adhabu yake. Adhabu ya kosa la kuufumbia haki na ukweli wa wazi na wa moja kwa moja ni *adhabu isiyokuwa na kikomo*. Hivyo kuacha kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu humpeleka mtu motoni milele, kwa sababu ndiyo dhulma kubwa kabisa dhidi ya neema alizopewa na Mola wake.

Japokuwa dhulma huwafanya wengine waumie, mwenye kuifanya humpeleka moja kwa moja kwenye adhabu kali. Madhalimu ndio wanadhurika zaidi. Ndiyo maana ndani ya Qur'an

Tukufu, mara kwa mara, tunakuta maneno *"wale wanazidhulumu nafsi zao."*

Rumi (q.s) anasema kuhusu uadilifu na dhulma: "Uadilifu ni nini? Ni kuimwagilia maji miti yenye matunda. Dhulma ni nini? Ni kulimwagilia maji waridi mwitu," na "Mtu asiyekuwa na wazo la uadilifu ni kama mbuzi jike anayemnyonyesha mtoto wa mbwa mwitu."

Yaani, dhulma ambayo mtu anaikumbatia itampeleka kwenye maangamizi. Humpeleka kwenye anguko na kutoweka.

Historia inatwambia kuwa wale wanaovunja haki za wenzao kwa manufaa yao ya mpito hujiandalia mwisho wenye kutisha. Mwishowe hujiangamiza kwa matendo yao wenyewe. Hivyo, hata kama ni jambo gumu, daima tunatakiwa kushikamana na uadilifu na kuiunga mkono haki.

Kwa lugha nyepesi kabisa, dhulma ina maana ya kuwafanya watu wateseke bila sababu.

Licha ya ukweli kwamba binaadamu wana daraja tukufu kabisa katika viumbe wote, huwa tunasahau thamani na heshima yetu kubwa na kuanza kukimbizana na anasa za mpito, matamanio ya nafsi, na tamaa za muda mfupi. Kwa njia hii watu hujiingiza kwenye adhabu ya milele, kwa kutenda dhambi na kuasi amri na makatazo ya Muumba. Lakini nani atakayebebeshwa mzigo wa hali hii?

Uwezo wa kuwatendea wengine uadilifu na huruma ni matokeo ya kwanza nay a awali kabisa ya kujitendea sisi wenyewe uadilifu na huruma. Na muongozo wetu bora wa kulifikia hili ni Mtume Muhammad ﷺ.

Mfano Bora wa Uadilifu

Mola wetu alimtuma Mtukufu Mtume ﷺ kuonesha mfano bora wa mwenendo wa mwanadamu, na kwa namna hii akayapambanua maamrisho na makatzo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Maisha safi ya Mtukufu Mtume ﷺ yanaonesha nia na makusudio ya Mwenyezi Mungu kwa wanadamu kupitia mifano hai ya kibinaadamu. Dini yetu tukufu, Uislamu, ni dini ya maisha halisi pale unapotumika hasa kwa namna bora. Misingi yake inatofautiana na mitazamo ya kiulimwengu ambayo ni ya kinadharia tu na haiwezi kutekelezeka. Hivyo, kuuelewa uadilifu ndani ya Uislamu, ingawa ni msafi, nalo pia ni jambo la msingi sana. Majukumu yako wazi kabisa.

Mtukufu Mtume ﷺ alipokuwa akiuamrisha umma wake kufanya jambo fulani, yeye na ndugu zake ndio waliokuwa wa kwanza kuitekeleza amri hiyo. Alipokuwa akiwakataza kitu, yeye na ndugu zake ndio waliokuwa wakiwajibika mwanzo kabisa kukiacha kitu hicho. Katika masuala ya uadilifu, hakuwahi kujipendelea hata kidogo, wala hakuwahi kuwapa upendeleo watu wenye mali au wenye ushawishi. Maisha ya Mtume Muhammad ﷺ yamejaa mifano ya mwenendo mwema unaowaacha watu vinywa wazi. Ifuatayo ni mifano michache tu:

Hata Kama Angekuwa Binti Yangu Fatimah…

Wakati wa zama za Furaha, mwanamke mmoja kutoka katika familia yenye ushawishi ya ukoo wa Banu Makhzuum alitenda kosa la wizi, na muathirika wa tukio hilo akamshitaki. Ndugu wa mwanamke huyo walimtafuta mtu aende kuzungumza na Mtukufu Mtume ﷺ ili mwanamke huyo asiadhibiwe. Hatimaye wakaamua kumtuma Usamah ibn Zayd رضي الله عنه, ambaye alikuwa miongoni mwa

Maswahaba wanaopendwa sana na Mtukufu Mtume ﷺ. Usamah alienda kwa Mtukufu Mtume ﷺ na kuomba mwanamke huyo asiadhibiwe. Mtukufu Mtume ﷺ alisikiliza, na uso wake ukabadilika rangi. Alimtazama Swahaba wake mpendwa na kumuuliza, "Unajadili kuvunja mojawapo katika mipaka ya Mwenyezi Mungu?"

Usamah aliposikia maneno hayo ya Mtukufu Mtume ﷺ alihuzunika sana na kujutia kitendo chake. Aliomba msamaha na kusema, "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Tafadhali niombee msamaha kwa Mwenyezi Mungu." (Bukhârî, Maghâzî, 53; Nasâ`î, Qat' al-Sâriq, 6, VIII, 72-74)

Kisha Mtukufu Mtume ﷺ alisimama na kutangaza, "Watu waliokuwa kabla yenu waliangamizwa kwa sababu ifuatayo: Mtu kutoka katika familia tukufu au tabaka la juu alipokuwa akiiba walikuwa wakimuacha huru, lakini masikini na mnyonge wanapoiba walikuwa wakiwaadhibu hapo hapo. Wallah, lau Fatimah, binti wa Muhammad, angeiba, ningemkata mkono!" (Bukhârî, Anbiyâ', 54; Muslim, Hudûd, 8, 9)

Katika Qr'an Tukufu, Mwenyezi Mungu anasema:

"Enyi mlio amini! Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ijapo kuwa ni juu ya nafsi zenu, au wazazi wawili na jamaa zenu. Akiwa tajiri au masikini Mwenyezi Mungu anawastahikia zaidi. Basi msifuate matamanio, mkaacha kufanya uadilifu…" (An-Nisâ 4:135)

Kisa hiki kinaonesha kuwa Mtukufu Mtume ﷺ, ambaye maisha yake yote ni tafsiri ya Qur'an, alisimamia utawala wa sheria na kuheshimu matakwa ya haki na uadilifu hata kama familia yake mwenyewe ingehusika. Alikataa vikali kuwapa upendeleo watu wenye ushawishi kijamii.

Kushikamana na Uadilifu

Hata kabla ya kupewa majukumu ya utume, Mtukufu Mtume Muhammad ﷺ alishiriki katika muungano wa kirai mjini Makka uliojulikana kama Muungano wa Wema (*hilf al-fudhuul*). Muungano huu ulianzishwa ili kuhakikisha uadilifu unatawala katika maisha ya kibiashara na kijamii. Kundi hili lilikuwa likiwasaidia wageni ambao haki zao zilikuwa zikipokonywa na ambao (kutokana na kukosa uhusiano wa kijamii) walikuwa hawawezi kupata haki zao. Kundi hili lilifanya kazi ya kurejesha haki za maskini kutoka kwa wenye nguvu, na kurejesha hali ya kuheshimu haki za maskini.

Hisia hii ya kuhakikisha haki na uadilifu vinapatikana inaweza kuonekana katika maisha yote ya Mtukufu Mtume ﷺ. Miongoni mwa mifano halisi ni maneno yeke yafuatayo:

"…jamii yoyote ambayo masikini hapati haki yake stahiki bila kuumizwa, haiwezi kudumu katika ustawi…" (Ibn Mâja, Sadaqât, 17)

"…Mwenyezi Mungu ataitakasa vipi jamii ambayo maskini hawarejeshewi haki zao kutoka kwa wenye nguvu?" (Ibn Mâja, Fitan, 20)

"Siku ya Kiyama, watu watakaopendwa na kuwa karibu zaidi na Mwenyezi Mungu ni viongozi waadilifu. Na wale watakaochukiwa na kuwa mbali zaidi na Mwenyezi Mungu ni viongozi madhalimu." (Tirmidhî, Ahkâm, 4/1329; Nasâ`î, Zakâh, 77)

Dakika za mwisho wakati akikaribia kufariki dunia, Mtukufu Mtume ﷺ alisema: "Shikamaneni na swala! Shikamaneni na swala! Na muogopeni Mwenyezi Mungu kuhusu haki za wale walio chini ya uangalizi wenu." (Abû Dâwûd, Adab, 123-124/5156; Ibn Mâja, Wasâyâ, 1)

Kuwa Kikwazo kwa Uadilifu: Fungu la Moto

Mtukufu Mtume Muhammad ﷺ, fakhari ya ulimwengu, anasema:

"Hakika mimi ni mwanadamu. Mnanjia na kutaka uamuzi kuhusu mambo kadhaa yanayowaleta ushindani baina yenu. Inaweza kutokea mmoja wenu akawa mahiri sana katika kuwasilisha ushahidi wake kuliko wengine. Na mimi ninaweza kutoa hukumu inayompa haki, kutokana na kile nilichokisikia kutoka upande wake. Lakini, kama atakuwa ametumia hila katika ushahidi wake nami nikatoa uamuzi unaompa haki, basi mtu huyo ajiandae kupata fungu la Moto." (Bukhârî, Shahâdât, 27; Muslim, `Aqidah, 4)

Kwa hakika, baadhi ya watu hufunika matendo yao ya kidhalimu na kuwashawishi watu kuwa hawana makosa kwa kutumia nafasi ya matatizo ya kiakili au udhaifu wa upande wa pili. Basi wasidhani kuwa wataukimbia uhalifu wao! Hata kama watazidanganya mahakama za dunia hii, mbele ya mahakama ya Mwenyezi Mungu kila kitu kitajulikana, na haki za watu zitarejeshwa. Hali ya Siku ya Kiyama itakuwa ya kutisha zaidi kuliko chochote katika ulimwengu huu.

Hivyo, yeyote anakwenda kwa hakimu ili kutendewa uadilifu anatakiwa kuichunguza dhamiri yake kama kweli ana haki katika kesi hiyo.

Suala la uadilifu ni suala muhimu sana, sio tu katika baadhi ya nyanja za maisha, bali katika nyanja zote. Uadilifu lazima utendeke katika biashara, katika elimu na katika mambo ya mazingira na ndani ya familia pia.

Kuwatendea Uadilifu Watoto

Kuwapendelea watoto wa kiume dhidi ya watoto wa kike ni kuivunjia heshima amri ya Mwenyezi Mungu, na ni ishara ya udhaifu wa imani na Uislamu wa mtu.

Sote tunafahamu kuwa watoto wa kike wamekuwa wakinyimwa haki zao nyingi na kukutana na ukandamizwaji wa aina mbalimbali. Ni dhulma kubwa kabisa kuichukulia jinsia kama kigezo cha ubora, kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu ameshatangaza kuwa kigezo pekee cha ubora ni *taqwa*- yaani uchamungu.

Siku moja Mtukufu Mtume ﷺ alifika kwa Swahaba wake mmoja. Swahaba huyo alikuwa na watoto wawili, mmoja wa kiume na mwingine wa kike. Yule wa kiume alipomkimbilia, alimkumbatia na kumkalisha juu ya paja lake. Baada ya muda kidogo akaja mtoto wa kike. Swahaba huyo akamkalisha chini badala ya kumfanyia kama alivyofanya kwa mtoto wa kiume. Mtukufu Mtume ﷺ alipoliona hilo akasema: "Je hupaswi kufanya uadilifu baina ya watoto wako?"

Hivyo alionesha kuwa haitakiwi kufanya ubaguzi baina ya mtoto wa kiume na wa kike kwa misingi ya jinsia zao. Daima unatakiwa kutompendelea mmoja kwa sababu tu ya msingi huu.[23]

Nu'man ibn Bashir رضي الله عنه anasimulia:

Baba yangu alinichukua mpaka kwa Mtume ﷺ na kusema, "Mwanangu huyu nimempatia mtumwa ambaye nilikuwa nikimmiliki."

Mtume ﷺ akasema: "Je umewapa pia watoto wako wengine?"

Baba yangu akasema, "Hapana, sijafanya hivyo."

23. Tahâwî, Sharhu Ma'ânil-Âthâr, Beirut 1987, IV, 89; Beyhakî, Shuab, VII, 468; Haythamî, VIII, 156.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema, "Basi badilisha uamuzi wako kuhusu zawadi hiyo." (Bukhârî, Hibah 12, Shahâdât 9; Muslim, Hibât 9-18)

Kutoa Haki kwa umakini kuwapa wale wanaostahiki

Baada ya ushindi wa Khaybar, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akimtuma Abdullah ibn Rawaha kwenda huko kwa ajili ya kukusanya kodi. Kila mara, Abdullah ﷺ alikuwa akitathmini kwa umakini kiwango cha tende zinazotakiwa kutozwa ushuru na kukusanya kiwango cha kodi kinachotakiwa.

Baadhi ya Mayahudi waliokuwa wakifanya shughuli za kilimo katika mashamba ya Khaybar hawakuifurahia tathmini ya Abdullah, na wakajaribu kumpa hongo ili abadilishe kiwango cha ushuru kinachotakiwa kutozwa. Walikusanya vito vya madini kutoka kwa wake zao wakampatia Ab dullah, wakasema, "Chukua vito vyote hivi ili mwaka huu usitutoze kodi!"

Abdullah akawajibu, "Siwapendi kwa sababu ya matendo yenu maovu. Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba, kutowapenda hakutanizuia kuwatendea uadilifu. Mnataka kunipa hongo. Lakini hongo ni haramu: sisi huwa hatufanyi hivyo."

Mayahudi hawa walipoona kuwa hawawezi kumhonga Abdullah ﷺ, waliuheshimu na kuukubali uaminifu wake. Walisema, "Huu ni uadilifu na uaminifu ambao huzifanya mbingu na ardhi zifanye kazi kwa nidhamu na mpangilio." (Muwatta', Musâqât, 2)

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Enyi mlio amini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mkitoa ushahidi kwa haki. Wala kuchukiana na

watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu…" (Al-Maidah, 5:8)

Utukufu ulioje wa dini yetu! Inatuamrisha kuwatendea uadilifu hata wale wanaoupinga! Muislamu mwenye kujitambua daima huheshimu haki na kutekeleza matakwa na mahitaji ya uadilifu, kwa kuwa anatambua kuwa anawajibishwa kwa kufanya dhulma, hata dhidi ya asiyekuwa Muislamu. Katka hadith moja, Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Tahadharini na dua ya aliyedhulumiwa, kwa maana hakuna kizuizi kati ya dua hiyo na Mwenyezi Mungu." (Bukhârî, Zakâh 41, 63, Maghâzî 60, Tawhîd 1; Muslim, Îmân 29, 31)

Kuna mfano mwingine wa kihistoria juu ya uchungaji wa haki na kuwafanyia uadilifu wale wasiokuwa Waislamu.

Katika siku za mwanzo za Uislamu, mji wa Hims ulikuwa chini ya ulinzi wa Waislamu. Waislamu waliposikia kuwa jeshi la Warumi lilikuwa likielekea huko, walirejesha kodi walizokuwa wamechukua kutoka kwa wakazi wa Hims. Waliwaambia, "Kwa kuwa sasa hivi tunataka kushambuliwa, hatuna uwezo wa kuwalinda. Tulikusanya kodi hizi kutoka kwenu ili tuwalinde, lakini sasa hatutaweza. Hivyo mko huru kufanya mtakavyo."

Watu wa Hims wakasema, "Tunaapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa serikali na uadilifu wenu ni bora kwetu kuliko ukandamizaji na dhulma tuliyokabiliana nayo chini ya utawala wa zamani. Tutaulinda mji huu pamoja nanyi chini ya amri ya gavana wenu."

Wayahudi na Wakristo wa miji mingine waliokuwa wamesaini mikataba na Waislamu walifanya hivyo hovyo. Mwishowe, jeshi la Kiislamu liliposhinda, raia hawa waliifungua milango ya miji yao kwa ajili ya Waislamu na kuikaribisha serikali ya Kiislamu. Waliendelea kuishi kwa amani na kutoa kodi zao.[24]

24. Balâzûrî, Futûhul-Buldân, Beirut 1987, s. 187.

Jeshi la Kiislamu lilitengeneza utamaduni huu wa uadilifu sio tu katika mji wa Hims, bali pia katika miji mingine ambayo waliifungua, na desturi hiyo ya uadilifu ikaendelea hata baada ya wao kuondoka. Kwa mfano, katika zama za Waturuki, mji wa Pleven ulipotekwa na majeshi kutoka Ulaya, Gazi Othman Pasha alirejesha kodi zilizokuwa zimekusanywa kwa Wakristo wa mji wa Pleven. Kodi hizo zilikuwa zimetolewa na wakazi hao kwa ajili kulindwa.

❁

Ni kwa sababu ya utambuzi huo kwamba wanafikra wengi wasiokuwa Waislamu katika kipindi chote cha historia wameendelea kuutambua ukuu wa uadilifu uliofundishwa na Uislamu. Wanamapinduzi wa Kifaransa walipokuwa wakiandaa Tangazo la Haki za Mwanadamu mwaka 1789, walifanya utafiti katika mifumo yote ya kisheria dunia. Lafayette, ambaye alikuwa mmoja wa wajumbe wa tume hiyo, aliidurusu sheria ya Kiislamu. Baada ya kuidurusu alishikwa na butwaa akalazimika kusema, "Ewe Mwarabu mwenye ukuu! Uligundua uadilifu wa kweli!"

Uadilifu ni nguzo kuu inayozishikilia jamii na kuzifanya serikali zifanye kazi. Kuna methali moja ya Kiarabu ya zamani inasema, "Kafiri anaweza kustawi; lakini dhalimu hawezi kustawi." Nyingine inasema, "Uadilifu ni msingi wa utawala." Ni ukweli kabisa kwamba mataifa na madola mbalimbali hufanya kazi kutokana na watawala wenye nguvu, uwezo na mamlaka. Lakini, nguvu, uwezo na mamlaka hukubaliwa na watu kwa kiwango cha uadilifu wanachokishuhudia. Nguvu bila haki huwa uadhalimu. Katika kuashiria hili, Abu Bakr ﷺ anasema, "Uadilifu bila nguvu ni udhaifu. Nguvu bila uadilifu ni udhalimu." Hii ina maana kuwa, nguvu inatakiwa kuambatana na uadilifu ili iwe na manufaa, lakini uadilifu hutolewa na nguvu ili uwe na athari.

Katika kitabu cha *Kutadgu Bilig*, Yûsuf Has Hâcip anasema, "Dhulama ni kama moto: hukiangamiza kila kinachoukaribia. Uadilifu ni kama maji: hustawisha kila yanapodondokea." Kama maji ya uadilifu hayawezi kuiokoa jamii inayoungua kwa moto wa uonevu, basi maji hayo yatakuwa yamepoteza usafi wake, sifa zake na tabia yake ya msingi na ya lazima. Mfumo wowote wa uadilifu usioweza kujibu vilio vya wanyonge ni kama maji machafu.

Baada ya mauti ya Mtukufu Mtume ﷺ, Sayyidna Abu Bakr رضي الله عنه alipochaguliwa kuwa khalifa, aliitangaza ofisi yake mbele ya watu kwa maneno ya staha ya ajabu kabisa: "Enyi watu! Nimechaguliwa kuwa Khalifa lakini mimi sio mtu bora miongoni mwenu. Nikitekeleza majukumu yangu vizuri, basi nisaidieni. Nikikosea, basi naombeni mninyooshe na kunionyesha njia sahihi…" (Ibn-i Sa'd, III, 182-183; Suyûtî, Târîkhu'l-Khulafâ, s. 69, 71-72; Hamîdullah, *Islâm Peygamberi*, II, 1181)

Tangazo hili adhimu linatuonesha kuwa ni wajibu kwa Waislamu kuwaunga mkono viongozi waadilifu, na kuwaonya bila kusita pindi wanapokosea.

Kupinga dhulma na uonevu

Mtukufu Mtume ﷺ anasema, "Jihadi bora ni kuzungumza ukweli mbele ya mtawala dhalimu." (Abû Dâwûd, Malâhim, 17; Tirmidhî, Fitan, 13) Hii ni kwa sababu ukweli usiposemwa, uongo hutawala. Unapokaa kimya ilhali ni wakati wa kuitetea haki ni kujibadilisha kuwa shetani mkimya. Kukaa kimya mbele ya mtawala dhalimu unakuwa umemuabudu kama sanamu.

Watu waliokuwa wamemzunguka Fir'auni, ambao walimhamasiha kudai uungu na kusema *"Je, mimi sio mola wenu mkuu?"* walikuwa kama mashetani licha ya kuwa katika miili ya

kibinaadamu. Kwa kuwa waliunga mkono uonevu wa Fir'auni, nao yaliwapata yaliyompata. Kumfurahia dhalimu kwa ajili ya manufaa ya kidunia husababisha fedheha na hizaya ya milele.

Wale ambao nyoyo zao huitetea na kuiunga mkono haki hubarikiwa na nguvu ya haki. Haki inapowaunga mkono kikamilifu, nao pia huiunga mkono. Wao ndio wanaowapinga madhalimu na wanaonevu.

Hivyo, Hassan al-Basri hakukaa kimya dhidi ya udhalimu wa Hajjaj Dhalimu, ambaye dhulma yake inajulikana sana. Hassan, akikabiliana na hatari, alitangaza ukweli, na kugawa kile kilichostahiki kugawiwa. Na Imam al-A'dham Abu Hanifa, ambaye hakupenda kuunga mkono sera za dhulma za khalifa Ja'far Mansur kwa namna yoyote ile, aliukataa uteuzi wake wa kuwa kadhi kuu wa Baghdad.

Maneno ya ukweli ni sauti ya imani. Kusema ukweli na kutoa kile kinachostahiki kutolewa ni miongoni mwa alama za wakomavu wa imani. Njia za udhalimu na uonevu zitafungwa kwa kuwepo kwa watu wanaosema ukweli.

Wale wanaotenda au kuunga mkono uonevu kutokana na tamaa zao, wanatakiwa kutambua kuwa siku zote urongo na mabavu hushinda kwa muda tu. Hawawezi kushida milele, kwa maana mwisho wa dhulma ni maangamizi. Kwa kuwa kuukana ukweli na kuvunja mipaka ya haki na uadlifu ni kutangaza upinzani na uasi dhidi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, watu madhalimu lazima watakutana na adhabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Historia ya dhulma na uonevu imejaa mifano ya adhabu ya Mwenyezi Mungu dhidi ya wanaotenda mambo hayo. Qur'an Tukufu inasema kuhusu jambo hili:

"...Wala hatuiangamizi miji mpaka watu wake wawe madhaalimu." (Qasas, 28:59)

Baadhi ya watu hutumia mabavu kwa sababu mwanzo dhulma huiona kuwa ni nzuri…lakini huo ni mwanzo tu. Historia inatuonesha kuwa mwisho wa dhulma hiyo ni giza nene. Kwa upande mwingine, uadilifu unaweza kuwa mgumu kuanza, lakini mwisho wake huwa salama na amani.

Muislamu anayetekeleza uadilifu – kila mahali, kila wakati na kwa kila mtu – hupenda na Mwenyezi Mungu Mtukufu na waja Wake, na hufikia utukufu na furaha duniani na Akhera. Lakini anayejitenga na uadilifu kwa ajili ya matamanio ya nafsi hawezi kupata chochote. Hata kama atapata manufaa ya muda, mwisho wake ni hasara, majuto na masikitiko.

Tunamuomba Mola wetu azilinde nyoyo zetu zisielekee kwenye dhulma kwa sababu ya manufaa ya muda mfupi. Atujaalie kuwa miongoni mwa waja Wake wenye furaha ambao wanaishi kwa misingi ya haki na uadilifu, na ambao wataingia mbele Yake wakiwa na akili yenye amani!

Amiin!

SURA YA 7

Dhima

Dhima na uwajibikaji utokanao na uelewa wa mshikamano wa kidini ni jambo muhimu sana. Licha ya umbali mkubwa uliopo baina yetu, Waislamu wanatakiwa kujiona kama viungo vya mwili mmoja, vyote vikiwa vinautegemea moyo mmoja. Kama ambavyo maumivu ya kiungo kimoja husambaa mpaka kwenye viungo vingine vya mwili wote, hivyo hivyo maumivu ya Muislmu yeyote anayeteseka ni mtihani kwa dhamiri zetu sote.

SURA YA 7

DHIMA

Binaadamu ndio viumbe bora kabisa na ndilo pambo adhimu kabisa la ulimwengu. Mwenyezi Mungu amemjaalia mwanadamu neema na vipawa vingi ambavyo hakuwapa viumbe wengine. Baada ya kujaalia vitu vyote hivi, Mwenyezi Mungu Mtukufu akamfanya mwanadamu kuwa kiumbe mwenye dhima na mwenye kuwajibika.

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka ndani mwetu silika za kuelekea kwenye utovu wa maadili na pia silika za kuelekea kwenye unyoofu na uchamungu. Na pia ametujaalia utashi wa kuchagua baina ya mambo hayo mawili, na hivyo kutoweka kwenye mtihani ndani ya dunia hii. Alitujaalia uhuru wa kuchagua jema au baya kwa sharti kwamba turidhike na matokeo tutakayoyapata.

Aliwakadiria waja Wake hali mbalimbali za maisha kama sharti la mtihani huo wa kidunia.

Binaadamu wameumbwa na uwezo na hali tofauti tofauti ili kuhakikisha maisha ya kijamii ya mwanadamu yanaendelea kwa nidhamu, uelewano na amani. Kama watu wote wangepewa sifa za aina moja, vipawa vya ustadi vya aina moja, na hali za

kimaada na kimaanawi zinazofanana, pasingekuwepo na mgawanyo wa majukumu katika jamii, na matokeo yake, pasingekuwepo na nidhamu yenye amani katika maisha ya mwanadamu. Badala yake, wanadamu wameumbwa kuhitajiana wao kwa wao, kama ambavyo mikono yetu huhitajiana ili kunawa. Mfumo wa maisha ya mwanadamu umetengenezwa katika namna ambayo watu wote wanatakiwa kushirikiana katika mambo yote, kama ambavyo vifaa vya mashine vina umuhimu kwa ajili ya utendaji kazi wa mashine husika. Hivyo, wanadamu kuwa na fursa zinazotofautiana katika maisha ya ulimwengu huu wa mitihani sio jambo lililofanywa bila hekma, bali kuna sababu maalumu ya kuwa hivyo.

Hali zinazotofautiana hutengeneza majukumu na dhima mbalimbali kwa waumini, na pia huweka haki haki tofauti tofauti. Nafasi ya mtu kijamii, vyovyote itakavyokuwa, hutengeneza mahitaji maalumu kwenye dhamiri na imani. Mwenyezi Mungu Mtukufu anawataka waja wake maskini, wanyonge na mafukara kuwa wavumilivu; watafidiwa Akhera kwa hali inayowakabili hapa duniani. Vilevile Mwenyezi Mungu anawataka waja Wake matajiri, wenye nguvu na uwezo wawe na tahadhari dhidi ya ulafi na kiburi; badala yake wanatakiwa kuwa wenye kushukuru.

Kumshukuru Mwenyezi Mungu hakufanyiki kwa maneno tu. Njia ya kweli ya kutoa shukrani ni kutoa ulichoruzukiwa kuwapa wale wenye mahitaji. Ni kuwasaidia wanyonge kwa ajili ya kumfurahisha Mwenyezi Mungu, kukidhi mahitaji yao na kupata baraka na dua zao. Matendo kama haya ndiyo njia bora kabisa ya kuelezea na kuonesha shukrani.

Daima tunatakiwa kujiuliza, “Mimi nina nguvu na afya: kwa nini fulani na fulani ni walemavu na wagonjwa? Mimi nina mali: kwa nini fulani na fulani ni masikini?” Maswali haya tunatakiwa kuyajibu kwa tafakuri, “Mwenyezi Mungu amenikabidhi amana

zote hizi, hivyo nina dhima. Ninatakiwa nijitahidi kuzitumia fursa hizi kuwasaidia wale wasiokuwa nazo."

Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Si katika sisi Yule asiyeumizwa na shida ya Musialmu mwenzake." (Hâkim, IV, 352; Haythamî, I, 87)

Dhima na uwajibikaji utokanao na uelewa wa mshikamano wa kidini ni jambo muhimu sana. Licha ya umbali mkubwa uliopo baina yetu, Waislamu wanatakiwa kujiona kama viungo vya mwili mmoja, vyote vikiwa vinautegemea moyo mmoja. Kama ambavyo maumivu ya kiungo kimoja husambaa mpaka kwenye viungo vingine vya mwili wote, hivyo hivyo maumivu ya Muislamu yeyote anayeteseka ni mtihani kwa dhamiri zetu sote.

Kasri la Ozi lilipotekwa na wakazi wake kuuawa, Sultan Abdulhamid I wa dola ya Uthmaniya alihuzunika mno. "Ewe Mola wangu, askari na watu wasiokuwa na hatia wameuawa!" alilia. Kutokana na huzuni nzito afya yake ilitetereka, akapooza na hatimaye akafariki dunia: ishara ya hisia kubwa ya dhima na uwajibikaji. Hisia kubwa iliyoje iliyotokana na imani kiasi cha kuuchukua uhai wa sultani aliyekuwa na nguvu! Tukitaka kupata ridhaa ya Mwenyezi Mungu, lazima tujitahidi kupendana, kuhudumiana, na kusaidia kwa kiwango kama hiki cha hisia na dhamiri.

Vilevile sisi waumini tunahitajiana kwa amali njema na dua. Waumini wanyonge na wanaoteseka wanahitaji amali njema za tajiri na wenye nguvu, na matajiri na wenye nguvu wanahitajia baraka na dua za masikini na wanyonge.

Mawlana Jalaluddin Rumi analielezea hili kwa uzuri kabisa:

Kama ambavyo uzuri hukihitajia kioo kizuri, ukarimu nao unamhitajia masikini. Kama ambavyo uzuri wa nje wa mtu huonekana katika kioo, vivyo hivyo uzuri wa ndani wa mtu karimu huonekana kupitia shida za watu wengine,

Kwa upande mwingine, wale wenye shida mbalimbali hawapaswi kujiona kuwa wako katika adhabu. Wanatakiwa kujua kuwa changamoto hizo ni mitihani kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Wakiweza kustahmili na kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kila hali, watafidiwa kwa tabu zote wanazozipata.

Hivyo, tajiri mwenye kushukuru na maskini mwenye kusubiri, wote wako sawa katika kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Toafuti pekee iliyopo baina yao ni kwamba, mmoja ametahiniwa kwa umasikini na mwingine ametahiniwa kwa mali na utajiri.

Katika kutuonesha mfano wa watu hao wawili, Mwenyezi Mungu Mtukufu anatusimulia kuhusu Nabii Sulayman ﷺ na Nabii Ayubu ﷺ. Japokuwa Nabii Sulayman ﷺ alikuwa na utajiri wa hali ya juu na usiokuwa na kikomo, kamwe hakuwa mwenye kiburi. Mali za dunia hazikuuteka moyo wake, na aliendelea kuwa mwenye kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hii ndiyo sababu Mwenyezi Mungu akamsifu ndani ya Qur'an Tukufu akisema: *"ni'mal-'abd"*, yaani "mja mwema!"[25]

Kwa upande mwingine, Nabii Ayubu ﷺ, ambaye alitahiniwa kwa umaskini na maradhi, daima alitambua kuwa Mwenyezi Mungu ndiye aliyemkadiria mitihani hiyo. Aliikubali hali yake na kamwe hakulalamika. Kwa sababu ya kuridhia kadari ya Mwenyezi Mungu, Nabii Ayubu ﷺ alipata sifa hiyo hiyo aliyopewa Nabii Sulayman ya *"ni'mal-'abd"* yaani "mja mwema."[26] Hivyo, jambo muhimu mbele ya Mwenyezi Mungu sio jinsi mja fulani alivyotahiniwa, bali ni jinsi anavyoupokea mtihani wake.

Ndiyo maana waumini wa kweli wanatakiwa kuwa na lengo la kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Ili kulipandikiza hasa jambo hili ndani ya nyoyo zetu, katika mambo yetu ya kiroho tunat-

25. Tazama: Surah Swaad, 38:30.
26. Tazama Surah Swad, 38:44.

akiwa kuwastaajabia na kuwaiga watu wema zaidi yetu sisi. Katika masuala ya kimaada, tunatakiwa kuwafikiria wale wenye hali duni zaidi yetu, na tuwe wenye kushukuru. Hatupaswi kulalamika kuhusu hali ngumu zilizokadiriwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, bali tunatakiwa kufarijiwa na imani yetu kwamba hali tulizo nazo zitaongeza hesabu yetu huko Akhera. Kwa maana Mwenyezi Mungu atawauliza na kuwahoji kwa undani kabisa wale aliowapa rasilimali nyingi za maisha hapa duniani. Wale waliopata neema kidogo hawatakuwa na dhima kubwa. Hivyo, uadilifu wa Mwenyezi Mungu utajidhihirisha katika namna hii.

Vivyo hivyo, mtu aliyezaliwa katika jamii ya kijima au isiyokuwa na maarifa na elimu ana dhima ndogo kwa kuikubali imani ya dini ya kweli kuliko Yule aliyezaliwa katika jamii yenye dini na iliyostaarabika: hali zao hazilingani. Hivyo, tunu alizopewa kila mja ndizo zinazoamua mipaka na kiwango cha dhima na uwajibikaji.

Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Qur'an Tukufu:

"Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya iwezavyo" (Baqarah, 2:286)

Hivyo, Mwenyezi Mungu Mtukufu humuwajibisha mja kulingana na uwezo na fursa aliyompa. Vilevile kila mmoja wetu ataulizwa kwa kila amali tuliyotakiwa kuifanya, lakini tukawa hatujaitekeleza. Tunatakiw kukumbuka kuwa tutaulizwa huko Akhera kwa kila amali njema ambayo tungeifanya lakini tukaacha kuifanya, vilevile huduma ambazo hatukuzitoa kama vile kuwausia wenzetu kuhusu imani na matendo mema, na kuwaonya dhidi ya dhulma na matendo ya uovu.

Katika hatua hii, tatizo kubwa huibuka kwa Waislamu wa dhati. Kwa maana, wakati ni rahisi kutathmini kiwango cha zaka

tunazodaiwa katika mali zetu, ni vigumu kuainisha kiwango cha huduma tunachodaiwa kwa ajili ya manufaa mengine ya kidunia, achilia mbali tunu za kiroho na kimaanawi tulizojaaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa mfano, kufanya juhudi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni jukumu ambalo Mwenyezi Mungu Mtukufu humlipa mja. Lakini, tofauti na utoaji zaka, kiwango chake hakiwezi kuainishwa.

Iwapo mali yako ni kubwa kiasi kwamba unadaiwa dola milioni moja ya Zaka, dhima yako haitaondolewa ukitoa milioni moja kwa maskini. Dhima itokanayo na tunu za kiroho na kimaanawi nayo pia iko hivyo hivyo. Baadhi ya watu hupata tunu nyingi na wengine hupata tunu chache. Tuseme kuwa uwezo wa moyo wa anayepata tunu chache ni kikombe kidogo, ilhali uwezo wa moyo wa anayepata tunu nyingi ni birika kubwa. Mtu mwenye birika kubwa akimwaga kiasi cha kikombe kimoja cha maji, ataonekana kuwa bakhili au asiyekuwa na maana kuzunguka akiwa na birika tupu. Uwezo na kipawa ni suala la mpango wa Mwenyezi Mungu, na tofauti zilizopo miongoni mwetu hutufanya tuwe na dhima tofauti tofauti.

Kwa kuwa haiwezekan kukijua kiwango hasa cha dhima itokanayo na tunu tulizopewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, tusiweke matumaini kupita kiasi kwenye swala zetu tulizozitekeleza au amali njema na sadaka tunazozitoa. Huwenda ukubwa na uwezo wa “kasha la dhima” yetu ni kubwa kuliko matendo yetu ambayo hayawezi kabisa kulijaza.

Mifano ya kanuni hii tunaipata kutoka katika Zama za Furaha. Kwa mfano, Bedui mmoja alikuja kwa Mtukufu Mtume ﷺ na kutangaza kuwa atafanya matendo ya wajibu tu. Mtukufu Mtume

ﷺ akasema: "Kama atatekeleza ahadi yake, ataokolewa."[27] Mtukufu Mtume ﷺ alisema hivyo kwa sababu huo ndio uliokuwa uwezo wa mtu huyo. Hata hivyo, Mtukufu Mtume ﷺ daima alikuwa akimuusia Muadh, ambaye alikuwa mmoja wa Maswahaba waliokuwa karibu naye zaidi, kwamba uwajibikaji wake "haukutosha." Mwishowe Mtukufu Mtume ﷺ akamwambia, "Je nikwambie jambo litakaloondosha pengo hilo?" Muadh aliiposema: "Ndiyo, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!" Mtukufu Mtume ﷺ aliushika ulimi wake na kumwambia, "Uchunge ulimi wako!"

Muadh akauliza: "Je tuna dhima kwa yale tuyasemayo?" Na Mtukufu Mtume ﷺ akajibu, "Ewe Muadh! Mwenyezi Mungu akufanye kuwa mwema! Jambo linalowapeleka watu Motoni ni maneno yatokanayo na ndimi zao!"[28]

Hatuna uhakika kama mikononi mwetu tuna kikombe au birika kubwa, ili kubaini kiwango cha dhima yetu. Kwa kweli, hatutaki hata kujua. Huwenda tuna pipa kubwa la dhima! Lakini, kila mtu anataka kusema, "Nina kikombe kidogo tu…hivyo inatosha kwangu kutoa kidogo kutoka katika kikombe chake kidogo!" Watu wengi ambao wamepewa neema nyingi na wana mapipa makubwa ya dhima bado wanajilinganisha na wale wenye vikombe vidogo na kusema kuhusu matendo yao machache kwamba "Nimeshajaza kikombe changu." Watu wengine wametoka kabisa nje ya akili zao: huilinganisha hali yao binafsi na utajiri wote wa jamii, huupunguza utajiri wao mkubwa na kuzifariji dhamiri za kwa kujiangalia wao wenyewe na kuiacha kazi yote kwa watu wengine.

27. Kwa maelezo zaidi kuhusu tukio hili, angalia Bukhârî, Imân 34; Sawm 1; Shahâdât 26; Muslim, Imân 8 na 9.
28. Kwa maelezo zaidi kuhusu tukio hili, tazama Tirmidhî, Imân, 8; Ibn Mâja, Fitan, 12.

Hata hivyo, tunatakiwa kujua kuwa tunu zinazotolewa na Mwenyezi Mungu kwa jamii na zile wanazopewa watu binafsi hazitakiwi kulinganishwa. Ndiyo maana hatutakiwi kabisa kutosha na huduma tunazozitoa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kamwe tusidhani kuwa tumetekeleza wajibu wetu kikamilifu. Ili dhima yetu ilingane na tunu tulizopewa na Mwenyezi Mungu, tunatakiwa kuendelea kufanya juhudi mpaka pumzi yetu ya mwisho.

Vilevile tunapaswa kuwa makini tusiangukie katika mtego wa kujiona kuwa hatuhusiki na kufanya juhudi katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa sababu hatuna mali au hatuna baadhi ya neema. Mfano wetu ni Abdullah ibn Umm Maktum ﷺ, Swahaba aliyekuwa kipofu. Pamoja na hali yake, alishiriki katika safari ya kijeshi ya Qadisiya, akisema, "Angalau naweza kubeba hata bendera!" Mfano mwingine unatoka katika vita ya Tabuk. Swahaba mmoja maskini alikuwa akionekana kuwa hahusiki kushiriki katika safari hiyo kwa sababu hakuwa na kipandwa. Lakini alishiriki katika safari hiyo kwa kufanya makubaliano na Swahaba mwingine amuazime kipandwa chake. Walikubaliana kwamba kama wakishinda vita naye akapona, atampa fungu lake lote la ngawira kwa kutumia kipandwa chake. Watu wa zama hizo walionesha mifano mingi kama hiyo ya kujitoa kwa moyo. Walielewa kiwango cha juhudi zinazotakiwa kufanywa ili kutekeleza amali njema inayowaongezea thawabu.

Amali zote zenye udhati zinazotekelezwa ili kumridhisha na kumfurahisha Mwenyezi Mungu ni ishara ya ukomavu wa moyo. Huwa ni matukio yanayotuweka karibu zaidi na Mola wetu. Hivyo kama tuna maradhi, ulemavu au umaskini hatutakiwi kuacha kazi ya kuutumikia Uislamu kwa kusema kuwa "Nina udhuru halali…" Badala yake, tunatakiwa kuondosha vikwazo na tujitahidi kabisa kufanya kila tuwezalo ili tuitumikie dini ya Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an Takatifu:

"Enyi mlio amini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu naye atakunusuruni na atayatilia nguvu mambo yenu." (Muhammad, 47/7)

Msijiangamize

Katika zama za Ukhalifa wa Bani Umayya, jeshi la Kiislamu lilitaka kufanikisha utabiri wa Mtukufu Mtume ﷺ kuhusu kuufungua mji wa Constantinople, mji mkuu wa Warumi, likausogelea mji huo. Miongni mwa askari hao alikuwemo Abu Ayyuub al-Ansaari, Swahaba maarufu aliyekuwa mwenye wa Mtukufu Mtume ﷺ pindi alipohamia Madina akitokea Makka. Mapigano yalikuwa makali sana, na askari wa Kirumi walikuwa wakilindwa na ukuta mkubwa wa mji huo. Askari mmoja wa Kiislamu kutoka Madina alimchochea farasi wake kupenya katikati ya jeshi la Kirumi. Wanajeshi wenzake kwa kuona hatari ya jambo hilo na kwa kuzingatia amri ya Mwenyezi Mungu isemayo, *"msiitupe mikono yenu kwenye maangamizi,"* walishtuka sana. Wakasema, "Mungu wangu! Mtazameni, anajitupa kwenye hatari!"

Abu Ayyuub al-Ansaari alipowasikia akasema, "Aya hiyo iliteremka kutuhusu sisi, Waislamu wa mwanzo wa Madina. Baada ya Mwenyezi Mungu kuikamilisha dini Yake kwa kuikomboa Makka, tukasema: "Kuanzia sasa, tushughulike na mali zetu na tuzifanye ziwe zenye faida na zenye kuzaa matunda.' Hapo aya hiyo ikateremshwa kwa Mtume ﷺ:

"Na toeni katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizo. Na fanyeni wema. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema." (Baqarah, 2/195)

"Mtu kujiangamiza kwa mikono yake inaonesha hatari ya kushughulishwa na mambo yake binafsi na kupuuza dhima na jukumu la kufanya juhudi katika njia ya Mwenyezi Mungu."

Hiyo ndiyo iliyokuwa hali ya Abu Ayyuub al-Ansari. Baada ya kulichunga onyo hili la Mwenyezi Mungu kwa uaminifu mkubwa, na kwa kushughulishwa na utekelezaji wa dhima na wajibu wake, kamwe hakuyaona matendo yake kuwa yenye kutosha na hakuacha kufanya kila awezalo katika njia ya Mwenyezi Mungu. Katika safari moja ya kijeshi, ambayo alishiriki kwa shauku ya imani, alipata heshima ya kufikia daraja ya kufa kishahidi. Wakati huo alikuwa na umri wa miaka themanini. (Tazama: Abû Dâwûd, Jihâd, 22/2512; Tirmidhî, Tafsîr, 2/2972)

Khalifa Umar ibn Abdul-Aziz, ambaye miaka miwili na nusu ya utawala wake ilijaa mafanikio makubwa, alikuwa akijitathmini kwa umakini mkubwa. Pinde mkewe anapomfariji, Umar alikuwa akisema, "Ewe Fatimah! Nitasemaje pindi Mola wangu atakaponiuliza kuhusu watu walio chini ya utawala wangu? Na nitasemaje pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu atakaponikumbusha dhimma yangu?" Anapoyatafakari masuala haya, watu walikuwa wakiona jinsi alivyokuwa akifanya juhudi kama ndege aliyeangukia ndani ya maji, akipigapiga mbawa zake…

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an Takatifu:

"Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife ila nanyi ni Waislamu." (Âl Imrân, 3:102)

"Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini." (Hijr, 15:99)

"Na ukipata faragha, fanya juhudi. Na Mola wako Mlezi ndio mshughulikie." (Inshirâh, 94:7-8)

Kutokana na aya hizo tukufu, tunatakiwa kuendelea kufanya juhudi kwa nyoyo zetu na kuongeza jitihada zetu muda wote mpaka mwisho wa uhai wetu. Katika hili, Mtukufu Mtume ﷺ ni kiigizo kwetu. Alikuwa akiswali usiku wote mpaka asubuhi akimuomba msamaha Mwenyezi Mungu Mtukufu, japokuwa alikuwa ameshasamehewa makosa yake yaliyotangulia na ya baadaye.

Pindi Maswahaba walipokuwa wakijenga msikiti, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akibeba tofali begani mwake. Alikuwa akikusanya kuni kwa ajili ya kupikia chakula cha familia yake pindi wanapokwenda mashambani. Jeshi la Kiislamu lilipokuwa safarini kwenye Vita ya Badr, alikuwa akifanya zamu ya kumpanda ngamia wake pamoja na maswahaba wake watatu. Maswahaba hao walipojaribu kumsihi apande badala yao, yeye alikuwa akikataa na kuwaambia, "Mimi ni mtembeaji zaidi yenu, na ninahitajia thawabu za Mwenyezi Mungu zaidi yenu." (Ibn Sa`d, II, 21; Ahmad, I, 422)

Kwa muktasari, kwa kuwa hatuweza kupima uwezo na fursa tulizojaaliwa na Mwenyezi Mungu, tunatakiwa kuendelea kujitolea kadiri tuwezavyo katika kuitumikia njia ya Haki mpaka mwisho wa pumzi yetu ya mwisho.

❁

Njia bora ya kulipa deni la tunu ya imani kutoka kwa Mwenyezi Mungu ni kuufikisha ujumbe wa Uislamu kwa watu wasiokuwa na imani na wakosefu. Tunatakiwa kuwaongoza kwenye Uislamu kwa njia ya heshima na yenye kukubalika. Tunatakiwa kuwa makini. Watu wakosefu ni kama ndege waliojeruhiwa – hawatibiwi kwa hasira, bali kwa huruma. Daima hatupaswi kuhamisha chuki yetu ya dhambi kwenda kwa mtenda dhambi, bali tunatakiwa tuichukie dhambi na sio mtenda dhambi. Tabia hiyo safi inaweza kupatikana zaidi katika mazingira yaliyoathiriwa na mtazamo sahihi wa Kisufi.

Siku hizi, kwa kuwa watu wengi wanasumbuliwa na udhaifu wa utashi, tunatakiwa kuwa kama madaktari hospitalini. Kumpa mgonjwa njia ya ponyo ni dhima ya kibinaadamu ya daktari, hivyo kuwaelekeza watu kwenye ponyo ya maradhi ya kiroho na kimaanawi ni dhima na wajibu wetu.

Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Dini ni nasaha." (Bukhârî, Imân,42) Aliyasema haya mara tatu ili tupate kuelewa kwamba nasaha inatakiwa kutolewa mara kwa mara.

Usiyategemee Matendo Yako pekee!

Hakuna amali ya mwanadam inayoweza kulipa deni la shukrani kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa tunu mbalimbali alizotujaalia. Ndiyo maana waja wema, na hata mitume, hataki kuhukumiwa kwa msingi wa matendo yao pekee, bali kwa msingi wa msamaha na huruma ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Siku moja, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliwataka Maswahaba wake kujiepusha na mtazamo uliopitiliza na waishi maisha ya kati na kati. "Shikeni njia ya kati na kati, songeni mbele moja kwa moja (katika dini). Angalieni! Hakuna mtu awezaye kuokolewa na matendo yake tu."

Maswahaba wakamuuliza kwa mshangao: "Hata wewe, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?"

Mtukufu Mtume ﷺ akasema: "Hata mimi pia. Mpaka huruma na ukarimu wa Mwenyezi Mungu vitakaponienea!" (Muslim, Munâfiqîn, 76, 78)

Katika hadith nyingine, Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Hata kama mwanadamu angeendelea kufanya juhudi na kuendelea kusujudi kuanzia siku aliyezaliwa mpaka atakapokufa, bado matendo yake yasingetosha Siku ya Hukumu." (Ahmad, c. IV, s. 185)

Hiyo ina maana kuwa, hata muumini mtiifu na mwema anatakiwa kuelewa kuwa matendo yake pekee hayatoshi kumuokoa.

Mtukufu Mtume ﷺ alithibitisha kuwa mwanadamu hana uwezo wa kumuabudu Mwenyezi Mungu kama inavyostahiki. Aliyasema hayo japokuwa yeye mwenyewe alikuwa akifanya ibada wakati wa usiku mpaka miguu yake ikavimba. Alikuwa akiomba: "Mola wangu! Siwezi kukusifu kama unavyostahiki! Wewe ndiwe mwenye kuweza kujisifu!" (Muslim, Salât, 222)

Kwa hiyo, jambo la msingi na lililo sahihi ni kutojifariji kwa matendo yetu, bali kumuomba Mwenyezi Mungu msamaha na huruma Yake, hata wakati tunapofanya amali na juhudi kubwa kabisa.

❁

Hakuna shaka kuwa dhima na majukumu yetu ni mazito sana katika zama hizi za mgogoro wa kiroho ambapo watu wamekandamizwa chini ya nira ya furaha za muda mpito na matamanio ya muda mfupi. Tunamuomba Mola wetu ajaalie juhudi zetu ziendane na majukumu na dhima zetu! Tunamuomba atusamehe makosa na aibu zetu na atupe heshima ya kupata Pepo Yake na Neema Zake.

Amiin…

SURA YA 8

Amana

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷻ alitangaza kuwa waumini wana wajibu muhimu na dhima kubwa wa waumini wenzao. Alituambia kuwa waumini wanatakiwa kushikana kama matofali ya ukuta na kwamba sisi sote tunatakiwa kuhisi maumivu na huzuni inayomkumba mmoja wetu. Pia alituonya kuwa kulala tukiwa tumeshiba na huku jirani yetu akiwa na njaa ni kinyume na maadili ya Kiislamu. Kwa mukhtasari, waumini wana dhima na amana kwa wenzao.

SURA YA 8

AMANA

Neno *al-mu'min,* ambalo hutumika kwa ujumla kumuelezea mtu anayemuamini Mwenyezi Mungu, ni miongoni mwa majina mazuri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Linapotumika kwa Mwenyezi Mungu, huonesha kuwa Mwenyezi Mungu ndiye chanzo na chimbuko la amani na usalama. Vilevile Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye anayewapa Mitume Wake sifa ya uumini: Yeye ndiye anayewafanya kuwa waaminifu. Kwa muktadha huu, "mtu mwenye imani" ni mtu anayeiendeleza imani, ni mtu anayeaminika na kuhamasisha hisia ya amani kwa wenzake.

Hisia ya kuheshimu kile walichokabidhiwa kama amana huwasaidia kuuendelea muungano wa imani baina ya waumini. Hadith moja ya Mtukufu Mtume ﷺ inaonya kuhusu ukweli huu:

Mwenyezi Mungu Mtukufu anapotaka kumuangamiza mja, humuondolea hayaa na staha. Baada ya kupoteza soni, mja huyo huangukia chini ya ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Baada ya kuangukia kwenye ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, hupoteza uaminifu. Bila uaminifu, atakuwa msaliti. Akishakuwa msaliti, hupoteza huruma. Huruma inapopota, hulaumiwa na kulaaniwa. Anapolaumiwa na kulaaniwa, mafungamano yake na Uislamu hukatika! (Ibn Mâja, Fitan, 27)

Kama isemavyo hadith ya Mtukufu Mtume ﷺ, uaminifu ni miongoni mwa masharti ya usalama wa imani. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuonya sehemu nyingi kuiheshimu kikamilifu. Ifuatayo ni baadhi ya mifano kutoka ndani ya Qur'an Tukufu:

"Na mmoja wenu akimwekea amana mwenziwe basi aliye aminiwa airudishe amana ya mwenzake, na amche Mwenyezi Mungu, Mola wake Mlezi…" (Baqarah, 2:283)

"Na atakaye fanya khiyana, atayaleta Siku ya Kiyama aliyo yafanyia khiyana." (al-Anfâl, 8:27)

"Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni mzirudishe amana kwa wenyewe. Na mnapo hukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu…" (Nisa', 4: 58)

Uaminifu ni miongoni mwa sifa kuu tano za mitume. Hata kabla ya Uislamu, Mtukufu Mtume ﷺ alijulikana kama mtu mwaminifu zaidi miongoni mwa Waarabu, ambao walimpa jina la "Mwaminifu" (*al-amin*) na "Mkweli" (*as-Saadiq*). Hata Abu Jahl, adui mkubwa wa Mtukufu Mtume ﷺ, alimwambia, "Ewe Muhammad! Sisemi kuwa wewe ni muongo. Lakini siukubali ujumbe uliokuja nao…" Kwa kusema maneno hayo, alikuwa akikiri kwamba anaukubali uaminifu wa Mtume wetu ﷺ, lakini alighilibiwa na matamanio ya nafsi yake. Hali hii imeelezwa ndani ya aya ifuatayo:

"…Basi hakika wao hawakukanushi wewe, lakini hao madhaalimu wanazikataa Ishara za Mwenyezi Mungu." (An`âm, 6:33)

Hakuna aliyemkaribia Mtukufu Mtume ﷺ kwa uaminifu na kutunza ahadi. Abdullah ibn Abil-Hamsa ؓ anatuhadithia kisa chenye mfano mzuri kabisa:

Kabla hajatumwa kama mtume, nilikuwa na muamala wa kibiashara na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, na alikuwa akinidai. Nilimwambia kuwa nitamlipa mara moja kama atanisubiri, nami nikaondoka sehemu ile. Lakini nilisahau ahadi yangu. Baada ya siku tatu nilikumbuka. Niliporudi sehemu tuliyozungumza, nilimkuta akiwa bado yupo. Lakini, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hakukasirika kwa kile nilichofanya. Alisema tu, "Kijana, umenisumbua! Nimekuwa nikikusubiri kwa muda wa siku tatu." (Abû Dâwûd, Adab, 82/4996)

Mtume wetu ﷺ alijulikana miongoni mwa watu wake kwa uaminifu, uadilifu na kutumainiwa. Bibi Khadija, ambaye alikuwa mwanamke mwenye kuheshimika mjini Makka, aliistaajabia sana shakhsia yake kubwa kiasi kwamba alitoa pendekezo la kuolewa naye.

Hata Mayahudi wa Madina waliokuwa wapinzani wakubwa wa kuenea kwa Uislamu walikuwa wakimtaka ushauri kila walipokuwa na migogoro baina yao, kwa sababu walikuwa na uhakika na uadilifu na uaminifu wake. Na Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akisuluhisha migogoro na migongano yao.

Barua iliyotumwa na Mtukufu Mtume ﷺ kwenda kwa Mfalme wa Rumi Heraclius, akimlingania kwenye Uislamu, ilipomfikia akiwa Damascus, Abu Sufyan pia alikuwa katika mji huo. Heraclius alimuuliza Abu Sufyan maswali mengi kuhusu Mtukufu Mtume ﷺ. Mfalme huyo alishangaa sana kusikia kuwa Mtume ﷺ hakuwahi kutuhimiwa kusema uongo au kutotimiza ahadi. Japokuwa wakati huo Abu Sufyan alikuwa adui mkubwa wa Uisilamu, alilazimika kukiri kuwa Mtume ﷺ hakuwahi kusema uongo wala kuvunja ahadi.

Hivyo, tunaona kwamba hata wale ambao hawakuuamini utume wa Mtukufu Mtume ﷺ walikiri kuwa alikuwa muadilifu na

muaminifu. Alipohama kutoka Makka, kwenda Madina, alikuwa na baadhi ya vitu alivyokabidhiwa na washirikina wa Makka kama amana. Alimteua Ali ﷺ kufanya kazi ya kuzirejesha amana hizo kwa wenye nazo.

Kwa mukhtasari, Waislamu na Wasiokuwa Waislamu walikiri uamifu wake.

Hisia yake ya ukweli wake ilikuwa kubwa mno. Siku moja mwanamke mmoja alimuita mwanaye akimwambia: "Njoo nikupe kitu!" Mtukufu Mtume ﷺ akamuuliza mwanamke huyo alichotaka kumpa mwanaye. Akamwambia kuwa alitaka kumpa tende. Mtukufu Mtume ﷺ akasema, "Kama ungempa kitu kingine ungekuwa umetenda dhambi ya kusema uongo." (Abû Dâwûd, Adab 80 / 4991; Ahmad, III, 447)

Hisia yake hiyo haikuishia kwa watu pekee bali pia kwa wanyama. Siku moja alimuona Swahaba wake mmoja akimuita farasi wake kwa kumpa ishara ya uongo kuonesha kuwa ana kitu alichotaka kumpa, alisikitika sana kiasi cha kumuita mtu huyo na kumuonya asimdanganye. (Tazama: Bukhârî, Imân, 24)

Kwa kuwa Mtukufu Mtume ﷺ aliwatazama viumbe kwa rehma aliyojaaliwa na Mola Wake, alikuwa makini na muangalifu sana kwa viumbe wote. Siku moja, wakati wa safari moja ya kivita, baadhi ya Maswahaba waliona vifanga vya ndege kwenye kiota wakavichukua. Baba wa vifaranga hao aliporudi akawa hajaviona vifaranga vyake akaanza kupiga mbawa zake kwa uchungu na huzuni. Mtukufu Mtume ﷺ alipobaini kitendo kilichofanywa na Maswahaba, aliwaamuru wavirudishe mara moja na wasimdhuru mama yao. (Tazama: Abû Dâwûd, Jihâd, 112)

Ibn Abbas ﷺ anasimulia kuwa mtu mmoja alikuwa akinoa kisu chake huku kondoo anayetaka kumchinja akiwa amelala

mbele yake. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema, "Unataka kumuua mara ngapi? Ulitakiwa kunoa kisu chako kabla ya kumlaza mbele yako." (Hâkim, IV, 257)

Aliwakataza watu wasikate matawi mabichi ya miti. Alieleza kuwa mwanamke mmoja aliyekuwa akifanya ibada za swala lakini akamuacha paka wake na njaa, alienda Motoni kwa sababu yap aka huyo, huku mwanamke mkosefu aliyempa maji mbwa aliyekuwa akikaribia kufariki dunia alipata huruma na rehma ya Mwenyezi Mungu. Aliwachukulia viumbe wote kama amana ambayo Mwenyezi Mungu amewakabidhi wanadamu, na kuwataka waumini kuwa wawakilishi wa usalama na amani ardhini.

Kila Muislamu anatakiwa kuutambua ukweli kwamba yeye ni katika umma wa mtume aliyekuwa na sifa ya Mwaminifu (*al-Amiin*) na Mkweli (*as-Saadiq*). Vivyo hivyo, muumini anatakiwa kuwa mwaminifu kwa maneno na matendo yake. Watu wengine wote, na hata viumbe wote, wanatakiwa kuwa salama dhidi ya mikono na ulimi wa muumini. Muumini anatarajiwa kuonesha mwenendo imara wa Uislamu, kwa sababu watu huwapenda wale wenye tabia na utu wa mfano, na hivyo huwafuata. Mtume wetu ﷺ aliutaka umma wake kuifanya sifa ya uaminifu kuwa sehemu ya utambulisho wake.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliwaagiza wa umini kuwa, "Rejesheni amana mlizoaminiwa (kwa wakati). Msifanye khiyana hata kwa wale wanaokufanyieni khiyana!" (Abû Dâwûd, Buyû', 79/3534) Suala la kupoteza mali za amana aliliona kama chanzo cha uovu mkubwa kabisa. Siku moja alipokuwa akizungumza na Maswahaba zake, mtu mmoja alimuuliza, "Siku ya Kiyama itafika lini?"

Mtukufu Mtume ﷺ akamjibu, "Pindi watu watakapopoteza amana walizokabidhiwa basi subiri Kiyama."

Mtu huyo akauliza tena, "Lini watu watapoteza amana?"

Mtukufu Mtume ﷺ akajibu, "Pindi mambo yatakapokabidhiwa kwa watu wasiostahiki, basi subiri Kiyama!" (Bukhârî, Ilm, 2).

Tunu zote alizojaaliwa mwanadamu kutoka kwa Mwenyezi Mungu ni amana. Katika Hotuba yake ya mwisho, Mtukufu Mtume ﷺ alisema, "…Ninakuachieni vitu viwili muhimu. Mkishikamana navyo, hamtapotea. Vitu hivyo ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna za Mtume Wake…" Hivyo, Qur'an Tukufu na Sunna za bwana Mtume ﷺ ndio vitu vyenye thamani kubwa kabisa ambavyo tuliachiwa kama amana na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake.

Vilevile Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitangaza kuwa waumini wana wajibu muhimu na dhima kubwa wa waumini wenzao. Alituambia kuwa waumini wanatakiwa kushikana kama matofali ya ukuta na kwamba sisi sote tunatakiwa kuhisi maumivu na huzuni inayomkumba mmoja wetu. Pia alituonya kuwa kulala tukiwa tumeshiba na huku jirani yetu akiwa na njaa ni kinyume na maadili ya Kiislamu. Kwa mukhtasari, waumini wana dhima na amana kwa wenzao.

Katika kuutekeleza msingi wa kuonesha huruma kwa viumbe wote kwa ajili ya Muumba, wahenga wetu wa Kiuthmaniya walianzisha zaidi ya taasisi 26,000 za hisani. Walifanya juhudi ya kuwahudumia wanadamu, wanyama na hata mimea. Hayo yalikuwa matokeo ya kuwatazama viumbe kama amana. Kama mtazamo kama huo ungekosekana, kitu gani ambacho kingewasukuma wahenga wetu kuwasaidia waumini wanaoishi huko Aceh (sasa Indonesia), eneo lililopo kwenye ncha ya pili ya dunia, kwa kuwapelekea msaada wote waliokuwa nao? Waliwasaidia Waislamu hao wa mbali kimaada, na pia kuwapatia msaada wa kijeshi dhidi ya wakoloni. Hisia yao ya uwajibikaji haikuishia kwenye mipaka ya nchi yao bali ilivuka nje na mipaka hiyo.

Nchi yetu adhimu tuliyolelewa nayo pia ni amana tukufu. Utekelezaji wa majukumu ya kidini na ulinzi wa uhai, heshima na mali, vinawezekana tu kwa kuilinda nchi yetu. Uhamaji wa Mtume wetu ﷺ kwenda Madina una hekma kubwa sana kuhusu jambo hili, kwa maana linaonesha umuhimu wa kuwa na nchi salama ili mtu aweze kuishi kwa mujibu wa dini yake.

Tunapoitazama historia yetu, tunaona kwamba ardhi tunayoishi ilibahatika kuwa nchi yetu kupitia damu za mashahidi, ambao walikufa kwa ajili ya heshima ya kuibeba amana ya Uislamu kwa watu wengine. Kutokana na kuitambua amana hii, Alparslan alijifunga katika nguo nyeupe –yaani sanda – na kuwaambia askari wake, "Leo, sisi wote tupo katika hali moja!" Aliwahamasisha askari wake kwa yeye mwenyewe kufa kishahidi. Pindi Suleiman Mkuu alipowatazama askari wake wa majini, wakiwa wameifanya Bahari ya Mediterranean kuwa sehemu ya Dola ya Uthmaniya, alisema, "Sasa sio wakati wa kujifakhiri na kujiona. Ni wakati wa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia huu ushindi!" Pindi vikosi vya Wauthmaniya vilipokuwa vikichukua chakula mashambani wakati wa safari ya kivita, pesa za malipo kwa ajili ya mazao waliyochukua walikuwa wakiacha zikining'inia juu ya matawi ya miti. Hii ni ishara kubwa ya uaminifu kwa nchi yao waliouonesha zama hizo. Na pindi Kamanda wa Kiuthmaniya, mpiganaji wa zamani wa Pleven, alipoona kuwa hawezi tena kuwalinda raia wake wasiokuwa Waislamu, aliwarejeshea kodi aliyokuwa ameikusanya kutoka kwao. Hii ni ishara nyingine yenye kushangaza inayoonesha utambuzi wa amana na uadilifu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu huwanusuru waumini pindi wanapoitetea nchi yao na dini yao. Tukio lifuatalo ni lenye kukumbukwa: linaonesha hali ya kiakili na kiwango cha imani cha mababu zetu, na kutoka wakati wa vita ya Çanakkale (mapigano ya Vita ya 1ya Dunia huko Dardanelles).

Ilikuwa siku moja kabla ya kusherehekea tamati ya mwezi mtukufu wa Ramadhan. Vehip Pasha, kamanda wa jeshi, alimuita imam kijana wa Kikosi cha 9. Akamwambia: "Ewe Imam, kesho ni Siku ya Eid. Askari wanataka kuswali swala ya idd pamoja. Licha ya juhudi zangu, sikuweza kuyabadilisha mawazo yao. Lakini hali ni ya hatari kabisa. Wakifanya hivyo, adui wanaweza kutumia fursa ya kutushambulia na kutuangamiza kwa pamoja. Ninataka kuwafafanulie askari katika namna ambayo wanaweza kuelewa!"

Mara baada ya Imam kuondoka mbele ya Pasha, mtu mmoja mwenye wajihi wenye kung'ara alimtokea.

Mtu huyo wa ajabu alimwambia, "Ewe mwanangu! Tahadhari, usiseme chochote kuwaambia askari. Ngoja tusubiri na tuone. Mambo hutokea kulingana na amri ya Mwenyezi Mungu."

Imam aliamua kumsikiliza mzee huyo na kutosema chochote. Asubuhi iliyofuata, askari wakiwa wamekusanyika kwa ajili ya swala ya idd huku nyoyo zao zikiwa zimejaa upendo wa Mwenyezi Mungu, muujiza ulitokea. Mawingu yalishuka na kuufunika mkusanyiko huo. Maadui waliokuwa wakiwatazama kwa kutumia darubini hawakuweza kuona chochote zaidi ya mawingu. Asubuhi hiyo askari waliswali swala ya idd kwa furaha mpya ya kimaanawi na kiroho. Sauti zao nzito zikitangaza na adhama ya Mwenyezi Mungu zilitikisa mbingu. Pindi mzee Yule mwenye wajihi angavu aliposoma baadhi ya aya za Surah al-Fat'hi (Ushindi), askari waliinua sauti zao kuitangaza Tawheed, imani ya Uislamu ya Umoja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Sauti hiyo iliweza kusikika mpaka kwenye kambi za maadui. Mparaganyiko mkubwa ulitokea katika vikosi vya Waingereza. Baadhi ya askari kutoka katika makoloni ya Muingereza, walipoisikia sauti hiyo ya kumhimidi Mwenyezi Mungu, wakatambua kwa mara ya kwanza kuwa walikuwa wakipigana na Waislamu wenzao. Wakafanya uasi dhidi ya makamanda

wao. Makamanda hao wa Kiingereza waliwaua baadhi yao kwa kuwapiga risasi, na wakalazimika kuwaondoa kwenye safu za mapambano wale waliobaki.

Hivi ndivyo uaminifu kwa nchi ulivyotufikia: kutoka kwenye mabega ya watu ambao nyoyo zao zilikuwa zimejaa imani, ambao walitumia matukio muafaka kwa ajili ya kupata msaada wa Mwenyezi Mungu. Askari hao wa Kiuthmaniya walioitwa Mehmetcik (yaani akina Muhammad wadogo) walijipambanua kwa upendo wao kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na kujitolea kwa dhati kwa ajili ya Ukweli. Hawakuacha usomaji wa Qur'an Tukufu, kudumisha swala au kuyadhukuru Majina ya Mwenyezi Mungu hata wakati wa vita. Walikuwa wakikimbia kutoka msitari mmoja kwenda mwingine kwa matarajio ya kufa kishahidi na kukutana na Mola wao. Walishawishika kuwa watu walioshikamana na dini, wakapita katika katika uelekeo ulioelekezwa na Qur'an Tukufu, na wakaifanya imani ya kumuamini Mungu Mmoja kuwa alama yao wataishi daima, ilhali wale wanaoiacha Qur'an na kutumbukizia katika giza la ujinga watakuwa na mwisho mwema. Kwa maana hadith ya Mtukufu Mtume ﷺ inasema, "Hakika Mwenyezi Mungu huyainua baadhi ya mataifa kwa sababu ya Kitabu hiki (Qur'an – yaani kwa sababu ya kushikana na maamrisho ya Mwenyezi Mungu yaliyo ndani yake), na kuwashusha wengine kwa sababu yake (kwa kujiweka mbali na maelekezo na muongozo wake)" (Muslim, Musâfirîn, 269)

Unaweza kubaini siri katika ukweli kwamba Wauthmaniya waliibukia katika utawala wa dunia wakitokea katika kabila la mahema mia nne kwa sababu ya kuiheshimu Qur'an Tukufu na taasisi ya kijeshi iliyoiheshimu dini kiasi cha "kujenga minara kila walipokwenda."

Kumbuka kuwa ni kutokana na heshima hii kwamba amana tukufu za vyombo vilivyokuwa vikitumiwa na Mtukufu Mtume ﷺ vililetwa mjini Istanbul wakati wa utawala wa Sultan Salim; vilitunzwa katika eneo maalumu ndani ya Kasri la Topkapi. Wauthmaniya walianzisha utaratibu wa kusoma Qur'an eneo hili na utaratibu huo umeendelea kwa karne nyingi. Na mtu wa kwanza kusoma Qur'an mahali hapo ni Sultan Salim mwenyewe.

Tusisahau kuwa siri ya utukufu wa mataifa katika ulimwengu wa nje na ndani ni juhudi zao za kuishika hekima ya ulimwengu wa kiroho. Adhama yoyote inayopatikana katika dola ya Uthmaniya, iliyodumu kwa muda wa miaka zaidi ya mia sita, ni matokeo ya Wauthmaniya kuweka msisitizo kwenye ulimwengu wa kiroho na kimaanwi.

Hivyo, kama Waislamu, dhima yetu kwenye historia yetu ni kuvilea vizazi vya vijana wenye imani, wenye kushikamana na tunu zao zao kiroho na kimaanawi, na wenye kuipenda nchi yao. Hii ni kwa sababu usalama wa imani, heshima, familia, uhai na mali unaweza kupatikana tu kwa kuilinda nchi.

Kama ambavyo mababu zetu walitukabidhi ardhi zetu za Kiislamu kwa thamani ya uhai na mali zao, hivyo hivyo nasi tunatakiwa tuzikabidhi ardhi hizo kwa vizazi vijavyo, ambapo Qur'an itasomwa kwa uwazi na adhana kutolewa kwa uhuru, zikiwa katika hali bora zaidi ya tulivyozikuta. Mwenyezi Mungu Mtukufu anatuonya kuwa:

"Tena bila ya shaka mtaulizwa siku hiyo juu ya neema (mlizofurahia duniani)." (Takâthur 102:8)

Tunu yenye kufurahiwa zaidi kuliko tunu zote ni mtu kuwa huru kutekeleza majukumu yake ya kidini ndani ya nchi yake. Muumini anatakiwa kuyaangalia mateso ya Walestina, na hali

yenye kuumiza ya Masjid Aqsa, kama ishara yenye kuhuzunisha ya kile kinachoweza kutokea pindi watu wanapopoteza utambuzi na hisia ya amana. Mshairi maarufu, Mehmet Akif anasema:

Nchi isiyokuwa na mlinzi itaangamia, kama ukiilinda, nchi hii haitaangamia!

Hata hivyo, mataifa yanaweza kubaki hai kupitia tunu za kitamaduni zinazobainisha tabia zao na zinazotengenezwa na Uislamu. Hisia yetu kuhusu dini na kuhusu historia ni amana mbili muhimu sana.

Dini ndiyo lengo la viumbe. Dini ni mkusanyiko wa kanuni na sheria za Mwenyezi Mungu zinazoweza kuyapangilia maisha ya watu kuanzia wanapokuwa watoto mpaka wanapoingia kaburini, na kuwaandaa kwa ajili ya furaha ya kudumu huko Akhera. Lugha ni nyenzo ya kufikisha ukweli ulioletwa na Uislamu. Historia ni taa inayomulika mustakbali wa mataifa kupitia uchambuzi wa vyanzo na matokeo ya matukio yaliyotengenezwa kupitia lugha na dini. Ndiyo maana utamaduni na imani haviwezi kutengana.

Tunatakiwa kujifunza historia yetu ya Kiislamu kwa ukamilifu, na tuifundishe kikamilifu. Haiwezekani kuelezea kiufasaha ustaarabu wa kiulimwengu kupitia maandishi ya wanahistoria wenye nadharia ya utaifa wanaofanya kazi kwa ushawishi wa wasomi wa Kimagharibi ambao ni maadui wa Uislamu. Historia ya Kiislamu, na hususan Zama za Furaha, hutoa suluhisho kwa kila aina ya matatizo. Tukiyafahamu vyema maisha ya Mtukufu Mtume ﷺ, daima tutapata majibu kwa ajili ya hali mpya zinazoibuka.

Ifuatayo ni jinsi Mtukufu Mtume ﷺ alivyoamimiana na maadui zake walipokuwa na shida, na jinsi alivyoamimiana na mateka wa vita.

Katika mwaka wa nane wa hijra, watu wa Makka walikumbwa na ukame mzito. Mtukufu Mtume ﷺ aliwatumia msaada wa ngano, chakula na dhahabu, licha ya ukweli kwamba hapo mwanzo walimtesa yeye na maswahaba wake kwa zaidi ya miaka ishirini. Abu Sufyan aliupokea msaada huu adhimu na kuugawa kwa Maquraysh waliokumbwa na njaa na umaskini mkali. Msaada kama huo lazima utazilainisha nyoyo za maadui wakubwa. Zawadi hiyo ilipowasili, Abu Sufyan alisema, "Mwenyezi Mungu amlipe kheri mwana wa ndugu yangu: ametekeleza dhima yake kwa jamaa na ndugu zake!" Kwa njia hii, Mtukufu Mtume ﷺ alizilainisha nyoyo za watu wa Makka. Siku hiyo baadhi yao walisilimu, huku wengine wakisilimu baadaye. (Ya'qûbî, Târ î kh, II, 56)

Mfano mwengine katika maisha ya Mtukufu Mtume ﷺ unahusu vita vya Badr. Mtukufu Mtume ﷺ alishauriana na Maswahaba wake kuhusu mustakbali wa mateka waliochukuliwa katika tukio hilo. Uamuzi ukawa kwamba mateka matajiri watajikomboa kwa fidia za mali zao, ilehali wale masikini watajikomboa kwa kuwafundisha watoto wa Madina kusoma na kuandika. Kila mateka masikini aliwekwa katika familia na kutakiwa kuwafundisha watoto kumi; Mtukufu Mtume ﷺ aliziagiza familia hizo kuwatendea wema wa hali ya juu. Ndugu wa Mus'ab in Umayr aitwaye Abu Aziz anasimulia aliyokutana nayo wakati akiwa mateka:

Nilikuwa mateka wa vita ya Badr na nilikabidhiwa kwa familia moja ya Kianswari (Waislamu wenyeji wa Madina). Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliwaambia watutendee wema. Wakati huo, mkate ulikuwa adimu sana. Ili kutekeleza maagizo ya Mtukufu Mtume ﷺ, familia hii ilinipa mkate wao mdogo waliokuwa nao, huku wao wakiishia kula tende tu. Niliona haya kula mkate ilehali wao hawana chakula. Nilitaka kuwarejeshea lakini walikataa. (Haythamî, VI, 86; İbn Hishâm, II, 288)

Kama tunataka kuufufua ustaarabu wetu adhimu, basi hatuna budi kuisoma kwa makini mifano hii, na mingine mingi katika historia ya Uislamu. Historia inatoa ushuhuda kwamba mataifa na watu binafisi huratibu maisha yao kwa mujibu wa uzoefu wao wa zamani. Historia ni kumbukumbu ya mataifa. Daima mataifa yatahitajia maonyo na muongozo wa matukio ya kihistoria. Pindi taifa linaitambua na kuiheshimu historia yake ya kweli na viongozi wake wa kimaada na kiroho, basi taifa hilo hupiga hatua na kuwa taifa adhimu. Vizazi vipya vinapokuja kuijua historia yao vizuri kuliko wageni wanavyoijua na kuzingatia uzoefu wa zamani, basi hawatakuwa na sababu ya kuhofia mustakbali wake! Ama kwa wale wasioangalia nyuma, kamwe mustakbali wao hauwi salama. Mizizi lazima izame ndani ya jana kama matawi yanataka kufika kesho.

Litakuwa kosa kubwa sana kuichukulia sayansi ya historia kama matukio madogo madogo tu ya zamani. Sayansi ya kweli ya historia imejaa hekma na siri. Hutengeneza uwanja unaotenganisha ukweli na uongo katika visa vya mataifa, ambao umejaa matukio mbalimbali. Ili kuutengeneza na kuuratibi kikamilifu mustakbali wa mataifa, uwanja huu unatakiwa kujulikana kikamilifu na masomo yake yazingatiwe. Mshairi Akif anasema:

Wanaielezea historia kama yenye kujirudia.
Kama watu wataisikiliza, basi itajirudia!

Tuna hitajio la kuijua historia ya zama za Mtukufu Mtume ﷺ. Tuna hitajio la kuujua udhaifu na nguvu za dola na serikali za Kiislamu. Na tuna hitajio la kuijua historia yetu wenyewe. Mababu zetu wa Kiislamu, Wauthmaniya, waliasisi jamii yenye msingi wa imani. Waliilinda heshima na utu wao kwa gharama ya uhai wao, na kamwe hawakutiwa utumwani. Historia yetu inatuonesha kuwa samba hawezi kuwekwa katika tundu. Pale taifa letu litakapoendelea kuutunza utambulisho wake, haitapelekwa kwenye utumwa.

Ama kwa upande wetu, tukiingia katika tunu za kitaifa na za kiroho za wazazi wetu, tutaweza kuibeba kwa heshima amana tuliyoachiwa. Tukikaa kimya ilhali tunu zetu za kitaifa na kiroho zikiharibiwa, itakuwa na maana kuwa hatuijui amana hii, na tunaweza kuipoteza. Lazima tufanye jitihada za dhati kulinda amna tulizokabidhiwa kwa gharama za roho nyingi. Tukifanya hivyo, kesho hatutahitaji kutoa gharama kubwa kuzirejesha amana hizo. Historia inatueleza kuwa amana zisizolindwa hupotea, na wale wanaostahiki ndio wanaoweza kuzirejesha.

Tunamuomba Mola wetu atufanye sisi na vizazi vijavyo kuwa wenye kufanikiwa kuzilinda amana zetu tukufu! Atulinde tusiangukie katika dimbwi la ujinga kwa kuupuuza urithi wetu. Tunamuomba atujaalie tunu ya kufika mbele Yake tukiwa na nyoyo zilizofarijika kwa kuzitunza amana.

Amiin…

SURA YA 9

Tafakuri

Tunapoutazama ulimwengu kwa tafakuri, tunaibua maswali mengi yaliyojificha katikati ya nyoyo zetu. Tumetoka wapi? Kwa nini tunaisha? Kwa nini ulimwengu unaishi? Rasilimali za riziki zetu zinatoka wapi? Tuishije? Tuamini nini? Tunakwenda wapi? Nini maana hasa ya maisha na uhai? Tutawezaje kuigundua siri ya ukweli wa kifo? Tunawezaje kuzifanya nafsi zetu ziwe tayari kwa ajili ya kifo?

Moyo ulio wazi na tayari kwa ajili ya tafakuri hutambua kwa urahisi kuwa uelekeo wa mwili wakati wa swala ni Ka'bah, lakini uelekeo wa moyo wakati wote ni kwa Mwenyezi Mungu.

SURA YA 9

TAFAKKUR

Uwezo wa kutafakari, kufikiria, ni tunu muhimu sana ambayo, sio wanadamu peke yao, bali viumbe wote wamejaaliwa. Kila kiumbe huitumia tunu hii katika ulimwengu wake kulingana na muundo wa maumbile yake. Kwa wanyama, uwezo wa kufikiri hutumika kutunza uhai wa mwili na nafsi. Mtazamao wao ni kunywa na kula, kuongeza urahisi, na kuzaliana. Hivyo, njia ya mnyama pori kufikiria hujikita kwenye uwindaji na kujamiana. Mbali na mambo hayo, mnyama hana fikra au wasiwasi: kufikiria kwake huishia hapo. Hafikirii kuhusu maumbile ya ulimwengu au mustakbali wa dunia. Lakini kwa upande wa mwanadamu, hali ni tofauti.

Tafakuri ya Kimaada na Tafakuri ya Kiroho

Kwa kuwa mwanadamu ni kiumbe mwenye hadhi na thamani kubwa kuliko viumbe wengine katika ulimwengu, dhima na wajibu wetu ni mkubwa. Hivyo tumejaaliwa uwezo mkubwa wa tafakuri.

Wanadamu wanastahiki Pepo sio kwa sababu ya akili yetu tamanifu inayojishughulisha na kula na kunywa, kupata raha na

kuzaliana, bali kwa sababu ya akili yetu ya kiroho na kimaanawi: heshima na utu ambavyo tumejaaliwa kwa namna ya kipekee.

Mwanadamu asipojitahidi kikamilifu kuongeza uwezo wa tafakuri ya kiroho, uwezo huo unaweza kupotea. Matokeo ya maisha ya kughafilika hatima yake ni majuto, kujutia umri uliokwishapita, ambao haukutumika kwa lolote zaidi ya upuuzi wakati wa utoto, ujinga wakati wa baleghe, na tamaa wakati wa ujana. Kula, kunywa, na kukusanya mali za kidunia hutupeleka kwenye kupoteza uwezo wetu wa kutafakari na kututumbukiza katika bwawa la matamanio ya kimwili na kimaada. Kuna mwanahekma mmoja anasema: "Kwa mtu mwenye hekma na busara, ulimwengu huu ni uwanja wa kutafakari usanifu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ama kwa mjinga, ni uwanja wa kujikusanyia starehe na matamanio."

Hivyo basi, kinachowafanya watu kuwa wanadamu wa kweli ni kujishughulisha na tafakuri ya kimaanawi na kiroho inayotengeneza mazingira ya utambuzi. Mwenyezi Mungu Mtukufu anawataka waja Wake kumuamini na kumuabudu kwa utambuzi mkubwa na wa kina. Na hili linawezekana tu kwa kuutafakari ukuu na adhama ya Mwenyezi Mungu.

Malezi na Makuzi ya roho

Mojawapo ya dhima na wajibu mkubwa wa waja wa Mwenyezi Mungu ni kuilea roho kwa njia ya tafakuri ya kina. Ukamilifu katika maadili, wema katika tabia, umaridadi wa moyo, na kujisalimisha katika ibada hutokana na tafakuri inayoongeza ukuaji wa roho.

Tukiutazama uzuri wa uumbaji kwa lengo la kujifunza, bila shaka tutagundua ishara za ajabu zenye hekma. Kwa mfano, tut-

amuona tembo akishindwa na mtoto wa miaka kumi. Tutamuona mpiganaji mieleka mwenye nguvu ambaye hajawahi kushindwa na mtu mwingine akidondoshwa chini na kijidudu kidogo kisichoonekana kwa macho. Sasa nani mwenye nguvu na nani dhaifu? Nini maana ya nguvu na udhaidu, kuwepo na kutokuwepo?

Tunapoutazama ulimwengu kwa tafakuri, tunaibua maswali mengi yaliyojificha katikati ya nyoyo zetu. Tumetoka wapi? Kwa nini tunaisha? Kwa nini ulimwengu unaishi? Rasilimali za riziki zetu zinatoka wapi? Tuishije? Tuamini nini? Tunakwenda wapi? Nini maana hasa ya maisha na uhai? Tutawezaje kuigundua siri ya ukweli wa kifo? Tunawezaje kuzifanya nafsi zetu ziwe tayari kwa ajili ya kifo?

Tafakuri hiyo inapoandamana na muongozo wa Qur'an na Sunna za Mtukufu mtume ﷺ, humpeleka mja kwenye kuutambua udhaifu na udogo wake mwenyewe. Tafakuri hutukumbusha kwamba hisia ya mamlaka ya kujitawala ni udanganyifu tu. Daima tunamhitajia Muumba wetu. Wanadamu huitegemea Dhati Kuu Kabisa kuwaruzuku: viumbe vyote lazima vimtegemee Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ni kosa kubwa kutoutambua ukweli huu!

Muumini anayesonga mbele kuelekea kwenye ukomavu wa roho kwa njia ya tafakuri huvuna hali ya kiroho na hekma na utambuzi katika ibada na kumtumikia Mwenyezi Mungu. Moyo ulio wazi na tayari kwa ajili ya tafakuru hutambua kwa urahisi kuwa uelekeo wa mwili wakati wa swala ni Ka'bah, lakini uelekeo wa moyo wakati wote ni kwa Mwenyezi Mungu. Sayyidna Ali رضي الله عنه anasema: "Ibada bila utambuzi, na usomaji wa Qur'an bila tafakuri, hauleti faida kubwa kama inavyotarajiwa!" Thamani ya ibada inayofanywa na moyo wenye ujinga hupungua kidogo kidogo, na wakati mwingine ibada hiyo haileti faida yoyote kwa mhusika zaidi ya kujichosha.

Kwa hivyo, marafiki wa Mwenyezi Mungu wanatuhimiza kuitekeleza kila swala kana kwamba ni swala yetu ya mwisho, kufunga swaumu kwa kutambua rehma na ukarimu wa Mwenyezi Mungu wetu, na kuendelea kuwafikiria maskini. Wanatuusia kuzitekeleza ibada zetu zote kwa tafakuri.

Abu Darda ﵁ anasema: "Saa moja ya kutafakari ni bora kuliko mikesha arobaini ya swala za sunna." (al-Daylami, II, 70-71, no: 2397, 2400) Hali hiyo ya tafakuri humfanya mtu aonje ladha ya swala zote kwa undani zaidi, na pia humfanya awajibike zaidi na azidi kuonesha shukrani kubwa kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kama ambavyo imani ni msingi katika dini, hivyo hivyo swala. Lakini swala hukubaliwa pale tu zinapotekelezwa kwa moyo wenye kutafakari na kuandamana na umakini wa kiroho. Ni hapo tu ndipo mja anaposogea karibu zaidi na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Maswahaba na waumini wa kweli wa kizazi kilichokuja baada yao walijipambanua kwa nyoyo zenye kutaamali na kutafakari. Abdullah ibn Masud ﵁ aliwaambia wenzake, "Mnatekeleza swala nyingi kuliko walivyofanya Maswahaba wa Mtume ﷺ. Lakini wao walikithirisha katika kuipa kinyongo dunia hii, nahawa kuielekea Akhera zaidi yenu."

Mola wetu anataka kuutafakari ukuu na utukufu Wake, kuzitafakari siri na hekma zilizomo ndani ya ulimwengu, na kuzitafakari neema na rehma Zake kwa waja Wake. Matokeo ya hatua yetu hiyo, tutatambua kuwa maisha haya ni ya mapito na kwamba maisha ya kudumu na ya milele yanakuja. Tutakuwa wema, wenye kuwajibika, na waja wa Mwenyezi Mungu wenye unyenyekevu.

Tafakuri ya Mtukufu Mtume ﷺ

Maisha ya mfano ya Mtukufu Mtume ﷺ yanatuonesha umuhimu wa kutafakari kwa ajili ya maendeleo ya kiroho ambayo Mola wetu anapenda kuwaona waja Wake wakiwa nayo. Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akiswali sana usiku na miguu yake ilikuwa ikivimba. Anapolala, macho yake hulala lakini moyo wake ulibaki kuwa macho. Hata wakati wa kupumzika hakuacha kuwa katika tafakuri na kumkumbuka Mwenyezi Mungu.

Bibi Aisha ؓ, mke wa Mtukufu Mtume ﷺ na Mama wa Waumini, anatueleza jinsi Mtukufu Mtume ﷺ alivyokuwa mja makini na mwenye kutafakari:

"Usiku mmoja Mtume ﷺ aliniuliza, "Ewe Aishah! Je waweza kuniruhusu nitumie usiku wote nikimuabudu Mola wangu?"

Nikajibu, "Hakika nami napenda kuwa pamoja nawe, bali ninapenda zaidi kile kinachokufurahisha."

Hivyo alichukua wudhu na kuanza kuswali. Wakati akiswali alilia sana kiasi kwamba ndevu zake, joho lake, na hata sakafuni alipokuwa akisujudu vililowa.

Bilal alipokuja kutoa adhana, alimkuta Mtume ﷺ akiwa katika hali hii. Alimuuliza, "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Kwa nini unalia hali ya kuwa umeshasamehe wa dhambi zako zilizotangulia na zijazo?"

Mtume ﷺ akamwambia, "Je, nisiwe mja mwenye kushukuru? Ninaapa kwamba usiku wa leo nimeteremshiwa aya ambazo wale wasiotafakari wanatakiwa kusikitikiwa! Kisha akasoma:

"Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na kukhitalifiana usiku na mchana ziko Ishara kwa wenye akili, ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala, na hufikiri kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi!

Hukuviumba hivi bure. Subhanaka, Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya Moto." (Al `Imran, 3:190-191; Ibn Hibban, II, 386; al-Alusi, al-Ruh al-Ma`ani, IV, 157)

Aya hizi zilipoteremshwa, Mtukufu Mtume ﷺ alilia usiku wote. Machozi yake yalitiririka kama umande unaohusudiwa na mawaridi. Na machozi ya muumini anayeutafakari ukuu na adhama ya Mwenyezi Mungu katika dunia hii yatakuwa pambo la usiku wa kifo, na nuru dhidi ya giza la kaburini.

Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akitafakari hata kabla ya kuanza kupokea ufunuo, wakati alipokuwa katika pango la Mlima Hira. Huko alimuabudu Muumba kwa kuutafakari mfumo wa mbingu na ardhi, kama alivyofanya baba yake, Nabii Ibrahimu عليه السلام.[29] Baada ya ufunuo kuanza kuteremka, aliendelea na hali hiyo ya kutafakari mpaka mwisho wa uhai wake. Mazungumzo yake yalikuwa ya kumtaja Mwenyezi Mungu na ukimya wake ulikuwa wa tafakuri. Hivyo anasema:

"Mola wangu aliniusia kuwa ukimya wangu uwe wa tafakuri." (Nami nawausia hivyo hivyo).[30]

"Utafakari uumbaji wa Mwenyezi Mungu." (ad-Daylami, II, 56; al-Haythami, I, 81)

"Hakuna ibada kama tafakuri." (Ali al-Muttaqi, XVI, 121)

Ahmad al-Rifa'i (q.s) anasema: "Tafakuri ndiyo iliyokuwa ufunguzi wa ibada ya Mtume ﷺ. Alikuwa na desturi ya kuutafakari uumbaji wa Mwenyezi Mungu na ukarimu Wake kabla ya kila swala. Hivyo, tunatakiwa kufanya tafakuri na kuitumia kujifunza."

29. Al-`Ayni, al-Umdah al-Qari, al-Sharh al-Sahih al-Bukhari, Beirut, nd. I, 61; XXIV, 128.
30. Ibrahim Canan, Hadith Ansiklopedisi, XVI, 252, namba 5838.

Hivyo basi, tuishi katika mazingira ya tafakuri. Wale wanaopenda hekma zilizomo katika ulimwengu ni vipenzi vya Mtukufu Mtume ﷺ.

Uoni wa Kipofu: Mfano wa tafakuri

Maswahaba wa Mtukufu Mtume ﷺ ambao aliwalea kiroho walionesha tabia ya tafakuri ambayo iliwasaidia dhidi ya majanga na matukio mbalimbali ya dunia hii. Ufuatao ni mfano mmoja wapo:

Abdullah ibn Maktum ؓ, ambaye alikuwa kipofu, alitaka kuungana na jeshi la Kiislamu wakati wa maandalizi ya vita ya Qadisiyah. Alipoambiwa kuwa yeye ana udhuru kisheria wa kutoshiriki, alihuzunika sana. Kisha alijitafakari kama mja mwenye dhima, akasema: "Ninaweza kufaa hata kama niko hivi. Kwa kuwa siwezoi kuona panga za maadui, ninaweza hata kubeba bendera katika kikosi cha mbele bila hofu yoyote. Askari wetu watanifuata kwa ujasiri na hamasa!" Hali ya Swahaba huyo kipofu ni mfano wenye kushtua sana kwa wale wenye macho na uwezo wa kuona…

Kusoma Kitabu cha Maisha na Uhai

Katika ulimwengu huu hakuna kilichoumbwa bure bila sababu. Kila atomu huonesha ishara na lengo la uumbaji, na kuzivuta nyoyo kwenye imani na kumpenda Mwenyezi Mungu kwa namna maalumu kabisa. "Uzungumzaji" huu wa hata vitu visivyokuwa na sauti unajulikana kama lugha ya hali (*lisaanul-haal*). Tafakuri ya kweli ni wewe kuweza kuisikia lugha hiyo kama inavyostahiki kusikika.

Kuyatazama matukio kwa macho yetu ya nje peke yake hakuwezi kuzalisha utambuzi na uelewa wenye ukomavu wa kuyajua

maisha na uhai. Utazamaji unatakiwa uandamane na tafakuri. Ni pale tu akili na moyo vinapofanya kazi pamoja ndipo utazamaji wetu unapogeuka kuwa mafunzo. Ni hapo tu ndipo uumbaji wa Mwenyezi Mungu unapozifanya nyoyo zetu kuwa na ukomavu, uimara na umadhubuti.

Hakuna kinachoweza kuikata kiu yetu ya kutafakari zaidi ya kumtambua na kumpenda Muumba wa Ulimwengu. Qur'an Tukufu inasema:

"Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!" (Ra`d, 13:28)

Mola wetu hukiruzuku kila kitu. Kila tukio katika ulimwengu huu klina sababu iliyokwisha kadiriwa, na sayansi inashughulika kugundua jinsi sababu hizo zinavyofanya kazi. Hata hivyo, Msababishi wa sababu zote ni Mwenyezi Mungu pekee. Hivyo elimu au nadharia ya kisayansi isiyomtaja Mwenyezi Mungu, muumba wa akili ya mwanadamu na kanuni za kimaumbile, itakuwa na mapungufu. Huwapeleka watu kwenye vichochoro vya upofu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anatuamuru, "*Soma!"* Kama tunataka kuepuka vichochoro vya upofu na kutumia nguvu kidogo hatuna budi kuitafakari na kuielewa amri hii. Hatuna budi kuifanya kuwa suluhisho la matatizo na hali zote katika hatua zote za maisha yetu, kwa sababu tukiifuata itatuongoza kwenye chanzo cha asili na cha kwanza kabisa cha hekma na maarifa. Kwa kuitumia njia hii, akili na nyoyo hufunguka na kuutambua mpango wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Hivyo, tuyatazame matukio yote ulimwenguni kupitia dirisha la imani, na tujifunze kutoka humo; tuzijenge roho zetu kwa tafakuri. Hapo, in shaa Allah, lulu za hekma – zinazopatikana kati-

ka mpango wa Mwenyezi Mungu juu ya matukio hayo – zitaingia ndani ya nyoyo zetu.

Kuugundua msingi: Tasawwuf

Malezi ya tasawwuf au usufi, yamewatengeneza viongozi wengi wa kiroho. Msingi wa usufi ni kuilea roho na kufikia hali ya kiroho. Tasawwuf ni njia inayokuongoza kwenye Dhati Kuu kwa kupitia ndani ya njia za kiroho kwa utambuzi. Sio njia inayokutaka kuachana moja kwa moja na maisha ya kidunia na kujitenga na watu. Kama asemavyo mshiri na mwana maarifa mkubwa Yunus Emre, Usufi sio joho lenye viraka au kilemba maalumu; usufi sio kutaja majina ya Mwenyezi Mungu tu ukaacha mambo mengine.

Pamoja na mambo mengine, tasawwuf ina maana ya mtu kuzi-tafakari dhima zake na kutafakari sababu za kushindwa kwake, na kuelekea kwenye utambuzi wa maana ya uhai na maisha. Ina maana ya kuondosha ubinafsi, kuzidisha tafakuri na kusonga mbele, hatua kwa hatua, kuelekea kwenye mwisho wenye heshima katika mafikio ya milele.

Imam al-A'dham Abu Hanifa anasema: "Ukitaka kuungana na wanamaarifa hao, kimya chako kinapaswa kuwa tafakuri, kutazama kwako kuwe kwa kujifunza, na tamaa yako iwe ya kutoa huduma. Hizo ni sifa tatu za wale wenye kumtambua Mwenyezi Mungu."

Tafakuri inatoa mchango mkubwa wa ukomavu wa kiroho na kimaanawi katika tasawwuf, kwa sababu lengo hasa sio kuswali au kutenda amali njema bila kuuhusisha moyo, bali kujisalimisha mbele ya utashi wa Muumba kwa moyo wa dhati. Hili linaweza tu kufikiwa kwa tafakuri yenye utambuzi ndani yake.

Kukitafakari kifo

Tunaweza kuzihuisha nyoyo na kufikia ukamilifu wa hali ya kiroho kwa kuacha ubinafsi. Hivyo, Mtukufu Mtume ﷺ aliusia akisema: "Kikumbuke kifo ambacho huharibu starehe zote." (Tirmidhi, al-Qiyamah, 26) Maisha ya ulimwengu huu wa mpito si chochote yakilinganishwa na maisha ya milele huko Akhera. Hivyo ni jambo la busara kuyapa kipaumbele matamanio ya mpito?

Ardhi tunayotembea juu yake leo imejaa miili ya mabilioni ya watu walioishi kabla yetu. Vivuli vyao visivyohesabika vimefunikana. Waliletwa katika soko la ulimwengu huu, wakatembea katika njia za soko hilo zilizojaa mahitaji ya kinafsi na kiroho na silika mbalimbali. Baada ya kuchukua kimojawapo, waliiacha dunia hii kupitia mlango wa mauti.

Tutapita katika mlango huo huo. Kila mmoja wetu atafikwa na siku isiyokuwa na kesho. Tarehe yake hasa haijulikani. Tangazo la Mola wetu Mtukufu inasema:

"Kila nafsi itaonja mauti. Kisha mtarudishwa kwetu" (Ankabut, 29:57)

Dunia ni chumba cha darasa ambapo tunajifunza. Ni wajibu wetu kuwa wanafunzi werevu na wa kweli katika darasa hili. Tusidanganywe na dhana kwamba tuko hapa kukaa milele!

Kukitafakari kifo ni kutafuta njia ya kuikumbuka siku isiyojulikana kabla ya kukutana nayo. Tafakuri hiyo hutusaidia kutuweka mbali dhidi ya kushughulishwa na nafsi; hutuandaa kukutana na Mola wetu na kutuwezesha kujieleza vizuri mbele Yake. Lengo lake ni kuibadilisha sura ya kifo kutoka kwenye hali ya kutisha kuwa hali yenye kupendeza. Tukifanikiwa kuishinda nafsi kwa kukitafakari kifo, tutakuwa tumejiandaa kuukabilia ulimwengu

ujao (Akhera). Kifo hutazamwa kama utangulizi usioepukika wa kukutana na Mwenyezi Mungu. Kitisho cha mauti kinachoisisimua akili hugeuka kuwa matarajio. Kifo hubadilika kuwa usiku wa harusi, kama asiemavyo Sufi mkubwa Mawlana Jalaluddin: usiku wa muungano.

❁

Hivyo tunahitajia tafakuri, huwenda kuliko chochote kile. Jinsi tunavyozidi kutafakari ndivyo tunavyofanikiwa kuzilea roho zetu, kukuza imani imara, kutekeleza swala za kweli, kutenda mema na kuamsha ndani mwetu moyo unaopanuka kuelekea kwenye anga za maisha ya milele.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie kupata utambuzi na maarifa! Atujaalie upepo mwanana wa kiroho kutoka kwenye anga tulivu ya Mtume ﷺ, Maswahaba na Marafiki wa Mwenyezi Mungu! Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaaliea kupata amani katika fikra na mawazo adhimu, na atuepushe na shari za nafsi! Tunamuomba atujaalie kuitekeleza amri Yake ya "Soma" kwa kuyapima matukio yote ya maisha kwa nuru ya imani!

Amiin…

SURA YA 10

Miale Ya Hekma Kutoka Katika Bustani Ya Moyo Wa Rumi

Marafiki wa Mwenyezi Mungu hawafi hata kama miili yao imezikwa, kwa maana nyoyo za Waislamu wa kweli hazipotelei kaburini. Badala yake, huduma zao za kimaanawi na kiroho kwa wanadamu huwa zenye kudumu. Marafiki wengi wa Mwenyezi Mungu wanaoendelea kutoa huduma zao katika ulimwengu mwengine bado wapo hai miongoni mwetu na kutuongoza kupitia vitabu vyao na taasisi zao za hisani. Wataendelea kutoa huduma ya kuwaongoza watu kwenye njia ya kweli hata baada ya kufa kwetu.

SURA YA 10

MIALE YA HEKMA KUTOKA KATIKA BUSTANI YA MOYO WA RUMI

Marafiki wa Mwenyezi Mungu ni warithi wa Mtume ﷺ ambao huitekeleza imani yao kwa upendo. Ni watu wenye bahati ambao walioziangaza nyoyo zao kupitia Qur'an na Sunnah za Mtukufu Mtume ﷺ. Watu hawa hutumika kama muongozo kwa wale ambao hawakupata bahati na fursa ya kumuona Mtume ﷺ na Maswahaba.

Marafiki wa Mwenyezi Mungu hawafi hata kama miili yao imezikwa, kwa maana nyoyo za Waislamu wa kweli hazipotelei kaburini. Badala yake, huduma zao za kimaanawi na kiroho kwa wanadamu huwa zenye kudumu. Marafiki wengi wa Mwenyezi Mungu wanaoendelea kutoa huduma zao katika ulimwengu mwengine bado wapo hai miongoni mwetu na kutuongoza kupitia vitabu vyao na taasisi zao za hisani. Wataendelea kutoa huduma ya kuwaongoza watu kwenye njia ya kweli hata baada ya kufa kwetu.

Umuhimu wa muongozo wao haupitwi na muda na mahali. Maandishi yao ni kama barua zilizotumwa kwa vizazi vya baadaye bila anuani maalumu. Barua hizo hufika kila mahali, na zinaweza kusomwa karne nyingi baada ya kuondoka kwao.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) liliuteua mwaka 2007 kuwa Mwaka wa Hadhrat Mawlana Jalaluddin Rumi, kwa maana mwaka huo ulisadifiana na kumbukumbu ya 800 ya kuzaliwa kwake. Leo hii kitabu cha Mawlana Rumi cha *Mathnawi* ni miongoni mwa vitabu maarufu zaidi kuhusu hali ya kiroho ya mwanadamu katika nchi za Amerika ya Kaskazini. Hii ina maana kuwa barua adhimu ya muongozo iliyoandikwa na Rafiki wa Mwenyezi Mungu karne nyingi zilizopita bado ina ushawishi duniani miaka mingi baada ya kifo cha mwandishi. Kitabu hicho ni kioo cha ulimwengu wa ndani wa wanadamu, kinachowasaidia kujijua vizuri na kuwasaidia kutatua matatizo ya kiroho. Huwaongoza watu wanaosumbuliwa na fikra za kimaada za zama hizi na kuwapeleka kwenye utulivu wa kiroho na kimaanawi.

Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwajaaliywa Marafiki Zake vipawa vyenye kuleta mabadiliko. Hivyo wao ni kama taa za uongofu zinazowaongoza watu kwa upendo na heshima, kuwafundisha jinsi ya kumuingiza Mwenyezi Mungu ndani ya vina vya nyoyo zao.

Baadhi ya Marafiki wa Mwenyezi Mungu wamevutwa sana na ukuu wa Mwenyezi Mungu kiasi kwamba waliishi faraghani tu, wakiyamalizia maisha yao ya mpito katika ukimya wa kiroho na kimaanawi. Ibn Abbas ﵄ anawazungumzia watu hao: “Kuna waja wa Mwenyezi Mungu ambao wanaweza kuzungumza kwa ufasaha mkubwa, lakini heshima yao kwa Mwenyezi Mungu inawafanya wakae kimya.”

Baadhi ya Marafiki wa Mwenyezi Mungu wanapendelea kuongea lakini kidogo sana. Wameelekezwa na Mwenyezi Mungu kuwaongoza wenye hekma kupitia lugha ya matendo. Utenzi ufuatao wa Baha’uddin al-Naqshabandi, aliyekuwa miongoni mwa watu hao, unaelezea hali hii:

Ulimwengu ni ngano na mimi ni pumba.
Kila mtu ni mzuri; mimi ni mbaya.

Kazi kubwa ya Baha'uddin al-Naqshabandi ni watu waliowalea na kuwatengeneza katika vikao vyake. Watu hao walijifunza kusoma misitari iliyoandikwa katika moyo wake na kuifikisha kwenye nyoyo nyingine kwa vikao vingine. Utawanyaji huu wa kimaanawi na kiroho unaendelea mpaka leo. Msingi wa mkakati wa mafundisho wa Baha'uddin al-Naqshabandi (q.s) ulitoka kwenye maelezo ya Abu Bakr ﷺ yasemayo: "Tafakari mara mbili kile unachozungumza, wakati wa kuzungumza, na Yule unayezungumza naye."

Pia kuna marafiki wengine ambao Mwenyezi Mungu aliwafanya kuwa kurumbizi wa kiroho: daima huimba tenzi za upendo wa Mwenyezi Mungu. Na aliwafanya wengine kuwa chimbuko ambalo matendo na ndimi zao kwa pamoja hutawanya hekima.

Mawlana Rumi alipewa kazi ya kuelezea ukweli wa Mwenyezi Mungu kwa maneno na matendo. Kupitia maneno yake, maandiko yake, na matendo ya moyo wake, kwa karne nyingi, ameweza kuwaangazia wale wanamtafuta Mwenyezi Mungu na kuwakurubisha Kwake.

Mawlana Rumi aliteuliwa kuwa mahali maalumu pa kumzungumzia Mwenyezi Mungu, na hivyo akawa mzungumzaji wa Marafiki wa Mwenyezi Mungu. Katika maneno yake aliweza kukusanya maarifa, siri na hekma alizojaaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hata hivyo, uwezo huo hutolewa kwa kikomo: mtu anaweza kuelezea ukweli wa Mwenyezi Mungu kwa kile kiwango tu alichoruhusiwa. Mawlana Rumi yumkini alikuwa na mengi zaidi ya yale aliyoyaandika.

Bila shaka chanzo cha elimu ya Mawlana Rumi ni Qur'an na sunna za Mtukufu Mtume ﷺ. Analielezea hili katika utenzi wake mmoja:

Mimi ni mtumwa wa Qur'an kwa muda wote wa uhai wangu.
Mimi ni vumbi la njia aliyopita Muhammad.
Mtu akipeleka ujumbe ujumbe kutoka kwangu tofauti na huu,
Ninahuzunishwa, hata kuchukizwa na uongo huo.

Hapa Mawlana Jalaluddin anajitambulisha kwa uwazi kabisa kuwa yeye ni mtumishi wa Qur'an na vumbi la njia tukufu ya Mtume ﷺ.

Kwa sababu ya hilo, Rumi ni msomi anayechukua muongozo na nuru kutoka ndani ya Qur'an na Sunnah, na pia ni chanzo cha hekma, anayetafsiri siri za Kimungu na kuziongoza nyoyo kuelekea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Mtukufu Mtume ﷺ anasema kuwa Luqman alimuusia mwanaye kwamba: "Ewe Mwanangu! Suhubiana na wasomi na ukae karibu nao! Sikiliza maneno ya wenye hekma! Mwenyezi Mungu huzihuisha nyoyo kwa utukufu wa hekma kama anayoihuisha ardhi kwa mvua." (Al-Haythami, I, 125) Ifuatayo ni baadhi ya mifano yenye kuhuisha nyoyo kutoka katika hekma za Mawlana Rumi:

Subira na Uvumilivu

Qur'an Tukufu inasema:

"Na waja wa Arrahman Mwingi wa Rehema ni wale wanao tembea ulimwenguni kwa staha, na wajinga wakiwasemeza hujibu: "Amani." (Furqan, 25:63)

Kutokana na hayo hiyo, Mawlana Rumi anasema:

- "Kaa kimya kama kitabu katikati ya wajinga."
- "Kunguru anapopiga kelele, kuumbizi hukaa kimya."
- "Tambua kuwa tabia njema ni kukaa kimya mbele ya tabia mbaya ya watovu wa tabia mbaya."

Ni kanuni muhimu katika ulimwengu huu wa majaribu na mateso kwamba kuvumilia machungu ya ulimwengu huufanya moyo kuwa na ukomavu. Subira ni ishara na alama ya imani. Mawlana Rumi anasema:

- "Akili yangu iliuuliza moyo, 'Dini ni nini?' Moyo wangu ukaliinamia sikio la akili yangu na kuinong'oneza kuwa, 'Dini ni tabia njema!'"

Mfano mkubwa kabisa wa tabia njema ni Mtukufu Mtume ﷺ. Maswahaba wanasimulia kuwa Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa na hayaa sana kuliko hata binti bikra.

- "Waridi hunukia vizuri linapokuwa pamoja na mwiba, kwa maana mwiba ni rafiki wa waridi."

Ulimwengu umepambwa kwa maelfu ya mafunzo yasiyozungumzwa. Hapa waridi limekuwa bwana wa maua yote kwa sababu ya kuuvumilia mwiba. Furaha huja baada ya kuzizoea shida na mateso. Mlango wa furaha hufunguka tu baada ya kustahmili anguko la matamanio yetu ya kidunia na mitihani migumu ya maisha.

Baadhi ya watu wanaweza kukutana na mitihani, majaribu, masaibu na kukata tamaa kiasi cha kumgeukia Mola wao na kumuomba, "Mola wangu, nisaidie!" Watu wengine, wenye mali na utajiri, wanaweza kupotea kabisa na kutomkumbuka Mola wao hata kidogo. Nafsi ya mtu ambaye hajawahi kukutana na tabu inaweza kugeuka kuwa kama farasi aliyekata kamba na kutoweza kudhibitiwa.

Ukomavu wa kiroho wa mwanadamu huimarika kutokana na vikwazo anavyokutana navyo. Shida za kidunia ni njia muhimu sana ya kutengeneza maendeleo ya kiroho. Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwafanya mitume wake wapitie mitihani mizito na tabu mbalimbali. Hivyo, wanadamu wote hupitia mitihani ili kuona wana utambuzi kiasi gani kwa neema walizopewa na Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Mtukufu huwapima waja Wake wote katika dunia hii na atatuita sote kwenda kuhesabiwa huko Akhera.

Mawlana Rumi anawausia wale watafutao furah ya kiroho waielewe mizania ya maisha.

- "Usimueleze kipofu vioo vilivyopo sokoni, wala usiimbe katika soko la viziwi."

Utambuzi na upambanuzi ni sifa bainifu ya Muislamu mwenye ukomavu. Watu wa namna hiyo huweza kuelewa hali ya wale wanaozungumza nao na kisha kuongea nao inavyostahili. Sayyidna Ali ﷺ anasema kuhusu jambo hili, "Zungumza na watu kulingana na uelewa wao." (al-Bukhari, al-`Ilm, 49) Hii ina maana kuwa unatakiwa kuzungumza katika namna ambayo inaendana na uelewa wao, sio inayoendana na uelewa wako. Kanuni ifuatayo kutoka kwa Rumi ina msaada mkubwa sana wa kutambua kiwango cha uelewa:

- "Unaweza kutambua kiwango cha maadili ya mtu kutokana na jinsi anavyocheka, na utaitambua akili yake kutokana na kile anachokicheka."

Kutafuta njia za kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu

Qur'an Tukufu inasema:

"Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli." (Tawbah, 9:119)

"Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na tafuteni njia ya kumfikilia. Na wanieni kwa juhudi kwa ajili yake ili mpate kuokoka." (Ma'idah, 5:35)

Kutokana na ujumbe huo wa Qur'an uliopiga chapa kwenye moyo wake, Mawlana Jalaluddin anasema:

- "Mtu huhukumiwa kulingana na kile anachokitafuta."
- "Kukitafuta kitu mahali kisipokuwepo ni sawa na kutokitafuta kabisa."
- "Usitembee kabla kiongozi wako hajapita. Yule atembeaye bila kiongozi ataishia kuwa mkia."
- "Ni bora kuwa mtumishi wa Rafiki wa Mwenyezi Mungu kuliko kuwa taji kwenye kichwa cha mfalme."

Sulaiman Mkuu, sultani mkubwa wa dola ya Uthmaniya, siku moja alikaribishwa kwa vifijo na vigelegele wakati akirudi kutoka katika vita aliyoshinda. Sultani huyo alihofia sana kuvutwa na hali ya ufakhari, hivyo akasoma utenzi ufuatao kuhusu umuhimu wa malezi ya nafsi:

Kuwa sultan wa dunia si chochote bali ni harakati ya kijinga.

Kumtumikia rafiki wa Mwenyezi Mungu ni heshima kubwa!

- "Vazi la hekma ambalo moyo umelipoteza linaweza kupatikana mikononi mwa watu wenye moyo."
- "Ukiungana na mtu wa moyo, utakuwa lulu hata ukiwa mgumu kama jiwe."
- "Ndege wenye manyoya huruka pamoja."
- "Yule atakaye kufika kwa Mwenyezi Mungu anatakiwa kuungana na vikao vya Marafiki wa Mwenyezi Mungu. Ukikata mawasiliano nao utaishia kuangamia."

- "Wafanye marafiki wa Mwenyezi Mungu kuwa marafiki zako, ili idadi ya msafara wao iongezeke. Kadiri msafara unavyokuwa mkubwa na imara ndivyo hatari za njiani zinavyopungua."

Imesimuliwa kuwa neno *insaan,* lenye maana ya "mwanadamu" katika lugha ya Kiarabu, linatokana na neno *uns*, lenye maana ya "urafiki au ukaribu." Hii inaonesha kuwa mwanadamu ana silika ya kimaumbile ya kujumuika na kuwa na marafiki. Hivyo, mja anatakiwa kufuata maelekezo na maagizo ya Mwenyezi Mungu na kuitumia sifa hii ya kibinaadamu kushirikiana na kusuhubiana na waumini wanyoofu na wenye imani. Kila mwanadamu ana shinikizo kutoka kwa shetani na nafsi. Imamu Shafii anasema: "Kama hushughulishwi na jambo la haki, utashughulishwa na jambo baya."

Hivyo, ili kujilinda kama mja wa Mwenyezi Mungu unayeheshimika, huna budi kusuhubiana na Waislamu wanyoofu ambao unaweza kunufaika nao kiroho na kimaanawi. Kila mwanadamu anahitaji mwongozo wa kiroho na kimaanawi. Ni kwa sababu ya hitajio hili kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu alimfanya mwanadamu wa kwanza kuwa mtume.

Sa'd al-Shirazi anaelezea kuhusu athari ya kusuhubiana na kuandamana na watu. Anasema: "Mbwa wa As-haabul Kahf saba alipata heshima kubwa na kutajwa ndani ya historian a ndani ya Qur'an, kwa sababu ya kusuhubiana na watu wema. Lakini wake wa Nuhu na Luut waliwekwa katika daraja la waliolaaniwa, kwa sababu ya kusuhubiana na watu wasiokuwa na imani." Kama kisa hiki kinavyobainisha, kusuhubiana na watu wajinga na waovu huwavuta kwenye mfumo wao wa maisha na fikra. Mawasiliano na uhusiano wa kiakili humpeleka mtu kwenye uhusiano wa kiroho, na uhusiano mbaya wa kiroho humpeleka mtu kwenye kuharibikiwa kiroho.

Kuitakasa nafsi

Qur'an Tukufu inasema:

"Hakika amekwisha fanikiwa aliye jitakasa. Na akakumbuka jina la Mola wake Mlezi, na akasali." (A`la, 87:14-15)

"Na kwa nafsi na kwa aliye itengeneza! Kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake, Hakika amefanikiwa aliye itakasa,na hakika amekhasiri aliyeiviza." (Shams, 91/7-10)

Kwa kuhamasishwa na hekma ya aya hizi, Mawlana Rumi anasema:

- "Ewe msafiri unayepita kwenye njia ya kiroho! Ukitaka kujua ukweli, tambua kuwa Musa na Fir'auni hawajafa. Wanaendelea kuishi ndani mwako; wapo ndani ya maisha yako. Wanapigana ndani mwako! Hivyo watazame wawili hao, ambao wapo katika mapambano ndani mwako."

- "Mwanadamu ni kama msitu. Kama ambavyo ndani ya msitu kuna maelfu ya nguruwe, mbwa mwitu na wanyama wengine wenye sifa nzuri na mbaya, vivyo hivyo ndani mwetu wanaishi wema na wabaya."

- "Usihangaike kuulisha mwili wako kupita kiasi, kwa maana siku moja mwili huo utaangamia. Badala yake itunze roho yako, kwa maana itapaa mbinguni na kupata heshima."

- "Istawishe roho yako kwa tafakuri na utambuzi wenye ukomavu utakaoipa nguvu katika safari yake."

- "Utakapoachana na nafsi yako, ukawajibika kikamilifu mbele ya Mwenyezi Mungu, utasafiri salama katika bahari ya siri za Mwenyezi Mungu."

- "Hakuna kioo kilichowahi kubadilika na kuwa chuma tena. Hakuna mkate uliobadilika kuwa ngano. Hakuna sharubati ya zabibu iliyorudi kuwa zabibu. Hakuna tunda bivu lililorudi kuwa bichi. Hivyo, kuwa na ukomavu na usirudi katika hali ya kutokuwa na ukomavu!"

- "Iwashie moto nafsi yako ya kihayawani, yenye giza kama usiku, kama unataka kung'ara kama mchana."

Mwenyezi Mungu Mtukufu ametujaalia uhai mara moja tu. Hatutarejeshwa hapa duniani tena. Kwa hiyo, tunatakiwa kuitumia fursa hii vizuri kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa kufikia ukomavu wa kiroho. Wale wenye kutengeneza shakhsia zenye ukomavu ndio wasiopata hasara katika maisha haya. Wale wenye kutengeneza nafsi ya kihayawani ndio watakaopata hasara kubwa hapa duniani na Akhera. Nafsi ambayo haijapitia katika mafunzo ya kiroho na utakaso ni kama farasi pori. Farasi pori humpeleka mtu kwenye mashimo, miamba na kumpoteza kabisa, badala ya kumpeleka kule anakotaka kwenda. Lakini farasi akipewa mafunzo vizuri, atampeleka mhusika sehemu anayotaka kwenda hata kama safari hiyo itakuwa na hatari na vikwazo kiasi gani.

Tamaa, saratani ya moyo

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an Takatifu:

"...Na wanao kusanya dhahabu na fedha, wala hawazitumii katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wabashirie khabari ya adhabu iliyo chungu. Siku zitapo tiwa moto katika Moto wa Jahannamu, na kwazo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao, wakaambiwa: Haya ndiyo mlio jilimbikia nafsi zenu, basi onjeni mliyo kuwa mkilimbika." (Tawbah, 9:34-35)

Kutokana na aya hiyo, Mawlana Rumi anasema:

- "Hata kama utakuwa tajiri kiasi gani, huwezi kula zaidi ya kile kinachoweza kubebwa na tumbo lako. Hata kama utazamisha gudulia lako ndani ya bahari, haliwezi kuchukua maji zaidi ya uwezo wake."

- "Kuna samaki wengi ambao, kutokana na tamaa zao, humeza chambo, licha ya kwamba bahari ingewalisha kwa amani."

- "Ulimwengu huu ni wa nini? Ulimwengu huu unahusu kutomjua Mwenyezi Mungu!"

- "Dunia hii, ambayo ni uwanja wa mitihani, ni kama sumaku kwenye matamanio ya nafsi: huyavuta kama kaharabu inavyovuta mabua. Ngano kubwa, yaani muumini mwenye busara, ambaye ulimwengu wake wa ndani umebeba siri na hekma za kiroho, ndiye anayeweza kuukwepa mvuto wa sumaku hii."

- "Manufaa ya kidunia ndiyo mtego wa nafsi. Huhadaa na kudanganya, na macho ya ndani ya baadhi ya watu hupofuka kwa sababu ya kuyatamani. Hunywa maji machungu na ya chumvi yatokayo katika udongo. Kwa kuwa hawajaonja ladha ya furaha ya kiroho, hudhani kuwa ladha ya maisha ya dunia ni yenye kuleta furaha."

- Ulafi na tamaa ya anasa za dunia hii hutupelekea kupata kile tusichostahiki."

Tamaa za kidunia ni chanzo kikuu kinachowapeleka watu kwenye ujahili. Tamaa huufanya moyo kuwa na upofu. Moyo wa aina hiyo hushindwa kuchora msitari baina ya haki na batili, halali na haramu. Mawlana Rumi anasema kuhusu upofu wa moyo: "Hata mbwa hatakula mfupa kabla ya kuunusanusa." Hivyo, Yule mwenye moyo uliopofuka kutoka na kutamani starehe na anasa za kidu-

nia ana busara ndogo kuliko mbwa. Tamaa ya kidunia husababisha janga la kiroho!

Bwana wetu, Mtume Muhammad ﷺ, alionya kuhusu matamanio na kuyaelezea kama anguko la mwanadamu. Anasema: "Mwana wa Adamu hata akiwa na mabonde mawili yaliyojaa dhahabu, bado atatamani bonde la tatu. Hakuna kitakachomtosheleza mwana wa Adamu isipokuwa kaburi." (Bukhari, al-Riqaq, 10; Muslim, al-Zakat, 116)

Wale wenye maradhi ya tamaa hata kama watapata mali na utajiri wote wa ardhini, bado watataka wapate mali zaidi kutoka mwezini au kwenye sayari ya *Mars*. Leo hii, tamaa na uozo wa kiroho wa wafuasi wa maada na dunia vinaonekana kutofikia kikomo. Hiyo ndiyo hali mbaya ya dunia yetu…

Abu Dharr, Swahaba wa Mtukufu Mtume ﷺ, anaelezea vizuri kabisa jinsi waumini wanavyoutazama umaskini. Anasema: "Kuna washikadau watatu katika mali yoyote ya kidunia. Wa kwanza ni Yule anayeimiliki, ambaye ni wewe. Wa pili ni qadari. Kadari haitakushaurisha kama mali yako itakuleta neema au shari, janga au mauti. Mdau wa tatu katika mali yoyote ni mrithi, ambaye anataka wewe ufe. Mrithi ataichukua mali yako utakapokufa, lakini wewe ndo utakayehesabiwa kwa mali hiyo. Ukiweza jitahidi usiwe mdau dhaifu kabisa kati ya wadau hao (kwa kutoa sadaka kabla hujafa). Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema, *"Hamtapata wema mpaka mtoe vile mnavyovipenda."* Mali yangu kubwa kabisa ni ngamia wangu; hivyo ninamtoa sadaka. Ninamtanguliza ili apate kunikaribisha huko Akhera." (Abu Nu`aym, al-Hilyah, I, 163)

Mali ni amana tulizokabidhiwa na Mwenyezi Mungu. Hatujui ataichukua lini amana yake. Tunaweza kupoteza mali zetu wakati wowote ule. Uhai ni kitu kinachokubwa na mambo mengi ya ghafla, na hatujui qadari italeta nini. Jambo kuu la ghafla kushinda yote

ni mauti ambayo hayaepukiki. Tunaweza kujiandaa na kuwa tayari kwa mauti kwa kuzitumia vizuri amana tulizokabidhiwa.

Sadaka: ponyo la nyonyo na furaha ya Dunia na Akhera

Qur'an Tukufu inasema:

"Na toeni katika tulicho kupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, tena hapo akasema: Mola wangu Mlezi! Huniakhirishi muda kidogo nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema?" (Munafiqun, 63:10)

Mawlana Jalaluddin Rumi anasema:

- "Roho zenye bahati mbaya ni mfano wa watu wanaoishi katika nyumba iliyojaa moshi. Sikiliza vilio vyao na kuwaitikie kwa kuwafungulia dirisha ili wapate hewa mpya. Hilo litaitakasa roho yako!"
- "Umepata nini? Umewekeza nini? Ni lulu gani uliyoipata kutoka katika kina cha bahari? Yote haya yatajulikana siku ya kifo chako."
- "Kumtembelea rafiki yako bila zawadi ni kama kwenda kwenye kunu cha kusaga nafaka bila nafaka."
- "Rejesha kile unachodaiwa kabla mauti hayajakichukua kwa nguvu."

Utenzi ufuatao kutoka kwa Necip Fazil unaelezea kwa uzuri kabisa nukta hii:

Ewe sonara bakhili, chukua mkoba mwingine!
Tunza sarafu ambayo itaweza kutumika kaburini…

Wosia na ushauri wenye busara ni muhimu sana katika kuuhuisha moyo. Wale wanaozitambua hazina za hekma huwa na hekma. Wale wanaozifuata hekma kikamilifu wataikamilisha imani yao.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie fursa ya kuishi katika anga ya hekma na kuzishuhudia siri ya ukweli. Atujaalie kuielewa maana ya Qur'an, ulimwengu na mwanadamu.

Amiin…

SURA YA 11

Mwezi Mtukufu Wa Ramadhan:

Mafunzo ya Kiroho kwa ajili ya Maisha

Uislamu sio dini ya ibada na sherehe zinazofanywa tu ndani ya mwezi wa Ramadhan au sikukuu nyingine. Ni dini ya wakati wote wa maisha.

Mwezi wa Ramadhan ni shule ya msimamo; na sikukuu ya baada yake ni shahada na cheti cha kiroho. Wakati wa sikukuu ya idd, waumini hufurahia kufaulu mtihani mkubwa wa mwezi wa Ramadhan. Katika sikukuu hiyo huonja kiasi kidogo cha ladha ya kuwa pamoja na Mola wao katika ulimwengu huu. Watafurahia tena Siku ya Hukumu.

Utii wetu kwa Mola wetu ndio sikukuu ya kweli. Tunaweza kupata sehemu ya rehma na neema za Mwenyezi Mungu tukimfurahisha maskini na mwenye shida wakati wa sikukuu.

SURA YA 11

MWEZI MTUKUFU WA RAMADHAN:

Mafunzo ya Kiroho kwa ajili ya Maisha

Mola wetu aliifanya kalenda ya maisha kuwa na siku za kupata manufaa ya kiroho. Wakati huo, neema, msamaha na rehma huongezeka. Kipindi chenye matunda zaidi ni mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

- Qur'an Tukufu, ambayo ni muongozo kwa wenye kumcha Mungu, iliteremshwa katika mwezi huu.
- Ibada ya swaumu, ambayo huimarisha ukomavu wa kiroho, hufanywa ndani ya mwezi huu.
- Usiku Wenye cheo, uliotajwa ndani ya Qur'an kuwa ni *bora kuliko miezi elfu moja,* huadhimishwa ndani ya usiku huu.
- Mikesha ya mwezi huu imebarikiwa kwa *iftaar*, kwa swala na kwa chakula maalumu.
- Nyoyo za maskini na mafukara hufurahi zaidi katika mwezi huu, kwa sababu wajibu wa kidini wa sadaka hutekelezwa mwezi huu. Sadaka za wajibu na zisizokuwa za wajibu zinazotolewa ndani ya mwezi huu huwafariji zaidi maskini.

- Milango ya pepo hufunguliwa ndani ya mwezi huu.
- Milango ya moto hufungwa kwa sababu ya kujizuia na dhambi.
- Ibilisi hufungwa minyororo ya uchaji, *taqwa,* ambayo ni utii wa muumini mwenye kujitambua.

Hivyo, mwezi wa Ramadhan sio tu hufungua milango ya furaha ya milele kwa muumini mmoja mmoja, bali pia kwa ulimwengu wote wa Kiislamu.

Qur'an na Mwezi wa Ramadhan

Qur'an Tukufu inasema:

"Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'ani kuwa ni uwongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uwongofu na upambanuzi. Basi ataye kuwa mjini katika mwezi huu naafunge…" (Baqarah, 2:185)

Kutokana na aya hii ni wazi kuwa Qur'an Tukufu ndani ya Mwezi wa Ramadhan, kwamba ni muongozo kwa wachamungu, kwamba ni muongozo unaobainisha baina na mema na mabaya, na kwamba ni wajibu kwa Waislamu kufunga katika mwezi huu.

Hivyo, Waislamu wanatakiwa kuutambua vizuri uhusiano wa karibu uliopo baina ya Qur'an na Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Abdullah ibn Abbas ﵁ anasimulia kuwa, "Mtume ﷺ alikuwa mkarimu zaidi miongoni mwetu, na ukarimu wake ulizidi pindi anapokutana na Malaika Jibril ndani ya Mwezi wa Ramadhan. Licha ya kuleta wahyi, Jibril pia alikuwa akimtembelea Mtume ﷺ kila usiku wa mwezi wa Ramadhan na kusoma Qur'an kwa pamoja. Alikuwa mkarimu zaidi kuliko upepo wa rehma [unaoleta mvua]" (Bukhari, al-Ba`d ul-Wahy 5, 6; Sawm 7; Muslim, al-Fadha'il, 48, 50)

Tunatakiwa kutekeleza kikamilifu maagizo ya kiroho yaliyoelezwa katika hadith hiyo na hasa kushughulishwa na Qur'an Tukufu wakati wa mwezi wa Ramadhan, ili tupate kufaidika na baraka za mwezi huu.

Kila siku tunatakiwa kutenga muda kwa ajili ya usomaji wa Qur'an, ambayo imeletwa kama mtengenezaji wa maisha yetu. Lakini mwezi huu wa Ramadhan tunatakiwa kukirithisha kuisoma. Tunatakiwa kushughulishwa na mazingira ya kiroho ya Qur'an, kuyafanyia kazi maelekezo yake na kuyarekebisha makosa na kasoro zetu.

Shakhsia imara na jamii salamau inaweza kuasisiwa tu kwa kufuata muongozo wa kiroho wa Qur'an Tukufu. Qur'an ni nuru itokayo kwa Mwenyezi Mungu inayouangaza ulimwengu wa ndani na nje wa Waumini. Ni muongozo wa furaha, kutukurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa hekma zake na visa vya mfano vya mitume mbalimbali.

Nguvu na uwezo wa Qur'an wa kuongoza inaweza kuleta amani na utulivu kwa watu waliokwama ndani ya mashaka ya zama hizi na wasiwasi wa baadaye, na pia wanaotatizwa na falsafa za zama hizi. Pumzi ya Qur'an ndiyo pekee inayoweza kuwafariji wenye huzuni na mkanganyiko, kuzifungua heka heka za maisha yao ya kila siku kwenye uwanja mpana wa amani na furaha ya milele.

Mwezi wa Ramadhan ni fursa ya uhai

Ndani ya Qur'an, Mwenyezi Mungu ameapa kwa muda. Anatukumbusha kwamba uwepo wetu hapa duniani sio wa kudumu wala wa kuendelea, na utafikia kikomo kabla ya kuanza kwa maisha ya kweli ya Akhera. Anatukumbusha kutopoteza muda na

kutoutumia vibaya. Kwa hali hiyo, Muislamu anatakiwa kuitambua neema ya muda na kuitumia vizuri kwa ajili ya malengo makubwa. Tunatakiwa kutambua umuhimu wa matumizi ya uhai wetu kwa kufanya mambo mema. Daima tunatakiwa kuwa wepesi katika kumuabudu Mwenyezi Mungu na kumuomba msamaha vizuri kabla ya kufikia mwisho wa uhai wetu.

Kama ambavyo maisha na uhai vina muda maalumu, mwezi wa Ramadhan nao una muda maalumu. Siku zake ni zenye kuhesabika. Hivyo jambo la busara ni kuyatumia mazingira haya adhimu ya kiroho ya siku hizo chache, kukusanya furaha yote ya milele kadiri tuwezavyo.

Bibi Aisha ﵂ anasimulia: "Mtume ﷺ alikuwa akiongoza bidii ya kufanya ibada katika mwezi wa Ramadhan kwa kiasi ambacho hatukukiona katika miezi mingine. Alikuwa akikithirisha zaidi ibada katika siku kumi za mwisho. Alitumia usiku wote akiswali, na alikuwa akiiamsha familia yake kuswali pia." (Bukhari, al-Fadl al-Laylatal-Qadr, 5; Muslim, al-Itiqaf, 8)

Wale wanaoitumia vizuri fursa ya mwezi wa Ramadhan hujaaliwa baraka nyingi. Wale wasioujali mwezi wa Ramadhan hupata hasara kubwa. Mtukufu Mtume ﷺ alionya akisema, "Jibril alinijia na kusema: 'Baraka za Mwenyezi Mungu zisimpate Yule Yule asiyeitumia fursa ya kuomba maghfira katika mwezi wa Ramadhan!' Nami nikaitikia kwa kusema 'Amiin'…" (Hakim, IV, 170/7256; Tirmidhi, Da`awat, 100/3545)

Kushikamana na Funga

Funga ndiyo amali kubwa kwa Muislamu anayetamani kuudiriki mwezi wa Ramadhan. Funga hutukumbusha kuwa sisi,

kama wanadamu, ni wasafiri tunaoelekea Akhera, ambao hatutabaki na mali wala starehe zozote mwisho wa safari yetu.

Habari njema ya raha za peponi kwa Yule mwenye kuzipa kisogo raha za dunia na akailea nafsi yake katika nuru ya moyo wa Qur'an.

Abu Usamah, swahaba wa Mtukufu Mtume ﷺ, siku moja alikuja kwa Mtume na kusema, "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ni ibada ipi ambayo nikiifanya Mwenyezi Mungu atanilipa?"

Mtukufu Mtume ﷺ akajibu: "Shikamana na funga! Hakuna ibada kama funga." (Nasai, al-Siyam 43)

Vilevile, Mtukufu Mtume ﷺ alizungumzia ubora wa daku: "Kula daku, hata kwa kunywa kiasi cha maji" (Abd al-Razzaq, al-Musannaf, IV, 227/7599); na "kuleni daku, hakika ndani yake kuna baraka." (Bukhari, as-Sawm, 20)

Funga ya mwezi wa Ramadhan hutufundisha kupunguza hata matumizi ya mambo ya halali, na hutukumbusha tunavyotakiwa kuwa makini kuhusu matendo ya haramu nay ale yenye kutia shaka.

Abdullah ibn Omar رضي الله عنه anasema, "Mwenyezi Mungu Mtukufu hataikubali ibada yako mpaka ujiepushe na matendo ya haramu na yenye kutiliwa shaka, hata kama utaswali mpaka mgongo wake ukapinda kwa sababu ya kuinama na kufunga mpaka ukawa mwembamba kama msumari."

Mawlana Rumi anasema kuhusu nukta hii ya mafunzo ya kiroho yanayopatikana ndani ya funga: "Funga husema: 'Ewe Mwenyezi Mungu! Mtu huyu hatumii hata chakula cha halali wala kinywaji cha halali, kwa kufuata maamrisho yako. Atainyoshaje mikono yake kukiuka amri zako?'"

Funga ni shule ya kiroho ya kuidhibiti nafsi. Vilevile hutengeneza njia ya kuimarisha hisia za ndani za huruma, upole na wema.

Funga ya kweli hukupa hali ya utambuzi inayokufanya uzitambue baraka ulizopewa na kushukuru kwa baraka hizo. Hutufanya tuwahurumie maskini na kuthamini huruma na upole kuliko hisia zote za kidunia. Ni shule ya mafunzo inayopunguza ulafi na kuongeza subira.

Kwa hakika, masomo muhimu katika mafunzo yetu haya ni ile mitihani tunayokutana nayo katika maisha ya kila siku. Kadiri tutakavyofaulu kwa urahisi mitihani hii ndivyo tunavyozidi kulikurubia lengo halisi la kufunga.

Miongoni mwa mitihani tunayotakiwa kufaulu wakati wa funga imeelezwa katika maneno ya Mtukufu Mtume ﷺ: "Mnapofunga msiseme maneno mabaya au kuzozana. Bali mtu anaposema vibaya au kutaka kuzozana nanyi, semeni, 'nimefunga.'" (Bukhari, as-Sawm, 9)

Kuzozana na watu sio jambo zuri. Muumini aliyefunga anapozozana, faida za kiroho za funga yake huondoka. Mwenyezi Mungu Mtukufu anabainisha namna tunavyopaswa kuwa pale tunapokasirishwa:

"Na waja wa Arrahman Mwingi wa Rehema ni wale wanao tembea ulimwenguni kwa staha, na wajinga wakiwasemeza hujibu: 'Amani'" (Furqan, 25:63)

Hivyo, funga inatakiwa kufanywa katika namna ya amani, ya kiroho na ya utambuzi. Tunatakiwa kuepuka matendo ya aibu na hata yasiyokuwa na umuhimu. Hatuwezi kufunga kikamilifu kwa kuacha kula na kunywa tu. Fanya yenye kukubalika hufanywa kwa kuidhibiti nafsi; nafsi hudhibitiwa kwa kuviepusha viungo vyote

vya mwili dhidi ya matendo ya haramu nay ale yenye kutiliwa shaka.

Ubayd, mtumwa aliyeachiwa huru na Mtukufu Mtume ﷺ, anasimulia: "Wanawake wawili walikuwa wamefunga. Mtu mmoja akaja kwa Mtume ﷺ wakati wa mchana na kumwambia, 'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Kuna wanawake wawili ambao wamefunga na wanakaribia kufa kutokana na kiu. (Tafadhali waambie waache kufunga).'

Mtukufu Mtume ﷺ akageuza uso wake, hakujibu chochote. Mtu aliyetoa ombi lake akarudia kusema, 'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, wanakaribia kufa!'

"Mara hii Mtume ﷺ akajibu, 'Waambie waje hapa!' Walipofika, Mtume ﷺ akampa mmoja wao bakuli na kumwambia, 'Tapika humu!' Mwanamke Yule akatapika damu, nyama na usaha kiasi cha nusu bakuli. Kisha Yule mwingine naye akafanya hivyo hivyo.

"Mtume ﷺ akasema, 'Wanawake hawa walifunga kwa kuacha matendo ya halali, lakini wakafungua funga zao kwa kufanya matendo ya haramu. Walikaa wakawa wanazungumza usengenyaji [kula nyama ya mtu].'" (Ahmad, V, 431, al-Haythami, III, 171)

Hivyo hatutakiwi kuacha kula na kunywa tu bali pia tunatakiwa kuwa makini na mazungumzo yetu. Ndimi zetu hazitakiwi kuwa miiba inayozichoma nyoyo za watu, bali zinatakiwa kueneza huruma. Tunahitaji kuwa na nyoyo zilizopambwa kwa hekma za Qur'an na nyuso zenye bashasha zinazoakisi tabasamu la Uislamu.

Kuwa Mja Mwenye Udhati wa Moyo (*Ikhlas*)

Mafunzo ya kiroho yanayopatikana ndani ya mwezi wa Ramadhan pia yanakusudia kutufanya kuwa waja bora. Wale wanaoshind-

wa kuwa waja wa kweli wa Mwenyezi Mungu, hatima yao ni kuwa waja wa viumbe wengine. Hali hiyo haiendani na hadhi na heshima ya mwanadamu. Muhammad Iqbal anazungumzia msiba wa wale wanaomkimbia Mwenyezi Mungu na kwenda kuwa watu wa watu wengine: "Sijawahi kumuona hata mbwa mmoja akimuinamia mbwa mwingine."

Kwa hiyo tunahitaji kuwa na utambuzi wa moja kwa moja wa kuwa waja wa kweli wa Mwenyezi Mungu pekee ili tuweze kupata raha ya kimaanawi na kiroho ndani ya mwezi wa Ramadhan. Tunatakiwa kuboresha kiwango cha hali yetu ya kiroho katika mwezi huu wa baraka.

Tunu pekee inayokubalika katika hili ni ikhlasi (udhati wa moyo). Swala zetu huthaminiwa sana na nyoyo safi, nia njema na ikhlasi yetu. Swala yoyote inayofanywa kwa madhumuni binafsi na lengo jingine kinyume na kutaka radhi za Mwenyezi Mungu haiwezi kukubaliwa. Hivyo, Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Kuna wengi wanaofunga lakini hubaki na njaa tu: hawapati faida yoyote ya kiroho. Kuna wengi wanaoswali usiku lakini wanakosa usingizi bure: hawapati faida yoyote ya kiroho." (Ibn Maja, as-Siyam 21)

Amali yoyote inayofanywa kwa lengo tofauti na kutaka radhi za Mwenyezi Mungu na ikawa haina faida yoyote Akhera huyahatarisha maisha yetu ya milele. Kutofanya maandalizi kwa ajili ya maisha ya milele hukupeleka kwenye majuto. Swala yoyote isiyoswaliwa kwa udhati wa moyo na *ikhlas* humhakikisha mhusika kuwa Akhera hana kitu na ataondoka mikono mitupu.

Swala zinazoswaliwa ndani ya Mwezi wa Ramadhan zinatakiwa kutofanywa kwa mazoea tu au kwa desturi tu, bali zinatakiwa kufanywa kwa ikhlasi na udhati wa moyo ili kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Vinginevyo, swala hazitaweza kuleta faida za kiroho, na funga itakuwa kama utaratibu maalumu wa kula

ili kupunguza uzito wa mwili, na swala za usiku zitakuwa kama mazoezi ya umeng'enyaji wa chakula.

Katika siku adhimu za mwezi mtukufu wa Ramadhan, tunatakiwa kuwa makini sana na swala zetu. Tuzitekeleze kana kwamba tunazungumza na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Swala zetu zinatakiwa kuwa fursa kwetu ya kukiri udhaifu na kasoro zetu na kueleza mahitaji yetu yote, ya kidunia na kiroho, mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hapo zitakuwa swala za kweli.

Mtukufu Mtume ﷺ anatushauri tuswali katika *jamaah*. Kuswali pamoja huongeza thamani ya swala, kwa sababu *jamaah* humpa kila muumuni undani wa kiroho wa kutafakari na kuelewa. Katika kila swala tunakariri dua hii:

"Wewe tu ndiye tunayekuabudu na Wewe tu ndiye tunayekutaka msaada" (Fatihah, 1:4)

Maneno hayo humpa muumini hamasa na moyo wa kuwa katika *jamaah*, kwa kuwa dhamiri "SISI" inaashiria kundi la watu wanaofanya kitu kimoja.

Dua ni ubongo wa ibada zote, kwa sababu humpa mja nafasi ya kukimbilia kwa Mola wake. Hutengeneza mawasiliano baina yetu na Mwenyezi Mungu. Mwenye kuyakata mawasiliano hayo hupoteza nafasi yake mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Qur'an Takatifu inasema:

"Sema: Mola wangu Mlezi asinge kujalini lau kuwa si kuomba kwenu…" (Furqan, 25:77)

Kuamka katikati ya usiku kwa ajili ya daku ni muda mwingine wa mafunzo na mazoezi ya kiroho, kwa maana tunapata baraka ya mapema kabisa. Wakati huo, Mwenyezi Mungu hutualika kwenda mbele Yake. Waumini wanatakiwa kuitika mwaliko huo,

na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hiyo. Qur'an Tukufu inawasifu watu hao kwa kusema:

"...Wanao subiri, wanao sema kweli, na wat'iifu, na wanao toa sadaka, na wanaoomba maghafira kabla ya alfajiri." (Al `Imran, 3:17)

Marafiki wa Mwenyezi Mungu huuchukulia muda wa kabla ya alfajiri kama hazina yenye thamani. Muhammad Iqbal anasema kuhusu jambo hili, "Nilipata njia ya kuvuka kuba la sayari. Niliona kuwa wakati wa kabla ya alfajiri, dua za wanadamu husafiri kwa kasi kubwa zaidi kuliko akili inavyoweza kufika kwa Mwenyezi Mungu, kwenda kuungana Naye."

Kujishughulisha na swala kwa uchangamfu kabla ya alfajiri humfanya mja asafiri mpaka kwenye anga za hekma na maarifa. Mawlana Rumi anasema, "Amka usiku na utembee kuelekea kwa Mola wako! Usiku hukupeleka kwenye ardhi ya uongofu. Siri za upendo wa Mwenyezi Mungu na raha za kiroho humwagika moyoni mwako huku wengine wakiwa wamelala. Madirisha ya moyo hufunguka sana wakati wa usiku: hapo unaweza kuchukua fungu lako kutoka katika ulimwengu wa moyo. Lakini macho ya wageni hayawezi kuyaona matukio hayo!"

Ndani ya mwezi wa Ramadhan, tumkumbuke Mwenyezi Mungu na kuzitakasa nafsi zetu kimaanawi kwa kila pumzi tunayoivuta. Tuitumie fursa ya mwezi ambao theluthi yake ya kwanza ni rehma, theluthi ya katikati ni maghfira na msamaha, na theluthi ya mwisho hutupatia wokovu. Tujitahidi kadiri ya uwezo wetu wote, zawadi hizo zitukute tukiwa na *ikhlas* na udhati wa moyo. Bila shaka, katika msimu huo wa faida, swala ndiyo nyenzo bora kabisa tunazoweza kuziandaa kwa ajili ya safari ya Akhera, kwa maana Mtukufu Mtume ﷺ anasema kuwa ibada zitakuwa pamoja nasi kaburini. "Muumini anapokufa hukuta swala zake za kila

siku zikiwa upande wa kichwani, zaka upande wa kulia, na funga upande wa kushoto.” (Haythami, III, 51)

Umar ibn Abdul-Aziz anasema, “Fanya maandalizi yako katika dunia hii kwa kuangalia safari utakayokwenda kaburini na Akhera!”

Usiku wenye Cheo Kitukufu

Usiku wenye cheo kitukufu, ni mojawapo ya hazina adhimu alizopewa Mtume Muhammad ﷺ kama zawadi na tunu maalumu ya kiroho kwa ajili ya umma wake. Habari njema za utukufu na thamani ya usiku huu zimetangazwa ndani ya sura ya Qur’an lililopewa jina la usiku huo, na pia katika hadithi mbalimbali za Mtukufu Mtume ﷺ. Mola wetu anasema kuhusu utukufu wa usiku huu katika Suratul-Qadr:

“Hakika Sisi tumeiteremsha Qur’ani katika Laylatul Qadri, Usiku wa Cheo Kitukufu. Na nini kitacho kujuulisha nini Laylatul Qadri? Laylatul Qadri ni bora kuliko miezi elfu. Huteremka Malaika na Roho katika usiku huo kwa idhini ya Mola wao Mlezi kwa kila jambo. Amani usiku huo mpaka mapambazuko ya alfajiri.” (Qadr, 97:1-5)

Usiku wa Cheo Kitukufu umeelezwa kuwa umetukuzwa sio tu kwa sababu Qur’an iliteremshwa ndani yake, bali pia kwa sababu idadi kubwa ya malaika, akiwemo Malaika Mkuu Jibril (ambaye wakati mwingine huitwa kama “Roho”), huteremka katika usiku huu. Usiku huu ni bora kuliko miezi elfu kwa sababu ni usiku wa baraka na neema ambapo waumini wenye kutubu hutolewa salamu na malaika na kusamehewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kwa kuwa ni usiku maalumu wenye hadhi na utukufu, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akiutafuta sana katika mwezi wa Ramadhan, na aliutaka umma wake kufanya vivyo hivyo. Muda wake hasa haujaainishwa. Kwa mujibu wa hadith moja ya Mtukufu Mtume ﷺ, usiku huo utafutwe katika mikesha ya siku zisizogawanyika kwa mbili katika theluthi ya mwisho ya mwezi wa Ramadhan, na hasa kwenye mkesha wa tarehe 27. Hata hivyo, hii haina maana kuwa Usiku huo lazima uangukie katika siku hizo. Imam al-A'dham Abu Hanifah na Shaykh al-Akbar Ibn Arabi kwa pamoja walitoa hoja kuwa Usiku huo sio lazima upatikane katika Mwezi wa Ramadhan pekee, bali unaweza kutokea katika usiku wowote ndani ya mwaka.

Maoni ya Imam Sha'rani kuhusu suala hili ni ya muhimu sana: "Kwangu mimi, Usiku wa Cheo Kitukufu hubadilika kutoka mwaka mmoja hadi mwingine. Nimeushuhudia mara kadhaa katika miezi ya Sha'ban, Rabi', na Ramadhan, lakini nimeushuhudia mara nyingi katika mwezi wa Ramadhan, na hasa siku za mwisho za mwezi wa Ramadhan."[31]

Kuna sababu za kutoainishwa tarehe maalumu ya Usiku wa Cheo Kitukufu, ambao thamani yake ni bora zaidi ya miaka themanini na tatu (miezi elfu moja) ya umri wa kawaida wa mwanadamu. Kuna hekma ndani ya hilo. Kwa kuwa umefichwa, Marafiki wa Mwenyezi Mungu wanatuusia kuutafuta kwa kipindi chote cha mwaka mzima. Ibn Mas'ud anasema: "Mwenye kutumia mwaka wote katika hali ya hadhari na umakini ataupata Usiku wa Cheo Kikuu." Hivyo, ushauri ufuatao umekuwa maarufu sana kwa waumini: "Usiku wowote unaweza kuwa Usiku wa Cheo Kikuu; mtu yeyote anaweza kuwa Muongozaji asiyeonekana (Khidhr, muongozaji wa Musa عليه السلام aliyetajwa ndani ya Qur'an)."

31. `Abd al-Wahhab al-Sha`rani, al-Kibrit al-Ahmar, p. 98, Izmir Ilahiyat Vakfi, 2006.

Sikukuu ya Eid

Siku na mikesha ya sikukuu za kidini hujaa baraka za Kimungu ambazo waja watiifu na wenye utambuzi ndio wanaoweza kuziona. Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Kuna watu ambao hutumia mikesha ya Sikukuu mbili (Iddi ya kufungua na Iddi ya kuchinja) wakimuomba Mwenyezi Mungu pekee. Nyoyo zao hazitakufa siku ambayo nyoyo zote zitakufa." (Ibn Maja, as-Siyam, 68)

Mwezi Mtukufu wa Ramadhan ni shule ya msimamo; na sikukuu ya baada yake ni shahada na cheti cha kiroho. Wakati wa sikukuu ya idd, waumini hufurahia kufaulu mtihani mkubwa wa mwezi wa Ramadhan. Katika sikukuu hiyo huonja kiasi kidogo cha ladha ya kuwa pamoja na Mola wao katika ulimwengu huu. Watafurahia tena Siku ya Hukumu.

Ahadi yetu kwa Mola wetu huonekana katika sikukuu hii. Tunaweza kupata fungu la rehma za Mwenyezi Mungu pindi tunapowafurahisha maskini na mafakiri wakati wa sikukuu. Mtukufu Mtume ﷺ anasema kuhusu jambo hili: "Wahurumieni walio ardhini watakuhurumieni walio mbinguni." (Abu Dawud, al-Adab, 58)

Ni muhimu kukumbuka kuwa sikukuu sio siku za sherehe binafsi au siku za kupumzika. Kama ambavyo mtu hawezi kuswali Iddi peke yake, vivyo hivyo haweza kuisherehekea peke yake au na familia yake ya karibu tu. Siku za sikukuu ni siku za kuwatembelea wazazi, ndugu, na sehemu uliyozaliwa, na pia kuwakumbuka wale waliotutangulia. Siku hizi zimewekwa ili kuufanya umma uwe imara zaidi.

Uislamu sio dini ya ibada na sherehe zinazofanywa tu ndani ya mwezi wa Ramadhan au sikukuu nyingine. Ni dini ya wakati wote wa maisha.

Imam Sha'rani anasema: "Mwezi wa Ramadhan umepewa utukufu zaidi kuliko mwezi wowote ule. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu ameuweka mwezi wa Ramadhan katika miezi ya mwaka ili baraka zake zipate kuenea kwa kipindi cha mwaka wote.[32]

Kama ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu amezifanya baraka za mwezi wa Ramadhan kuenea na kusambaa kwa mwaka wote, vivyo hivyo baraka na mafunzo tunayoyapata katika mwezi wa Ramadhan yanatakiwa kuendelea katika maisha yetu yote. Na daima tunatakiwa kuzikumbuka raha za kiroho tunazozipata ndani ya mwezi huu, kwa sababu, vyovyote tutakavyoishi, maisha yetu ni mafupi kuliko mwezi wa Ramadhan ukilinganisha na maisha yetu ya milele huko Akhera.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu azikubali swala zetu katika mwezi huu wenye baraka! Atujaalie kuishi katika mazingira maridhawa ya mwezi wa Ramadhan wakati wote. Aijaale miezi mingine kuwa kiunganishi na kutuunganisha na mwezi huu adhimu na kutuweka pamoja kwa udhati wa moyo na masimamo. Na tunamuomba Mwenyezi Mungu aifanye Ramadhan kuwa wakala wa amani na furaha katika nchi yetu, umma wetu, na Waislamu wote duniani.

Amiin…

32. Abd al-Wahhab al-Sha`rani, al-Kibrit al-Ahmar, s. 110.

SURA YA 12

Israfu -1

Katika imani, itikadi na ibada

Ubadhirifu kwa kawaida ni neno linalotumika katika masuala ya usimamizi wa fedha, lakini lina matumizi mapana zaidi yanayojumuisha mambo yote ambayo wanadamu wanaweza kupitiliza na kuvuka mipaka sahihi. Hivyo, mja akivuka mipaka iliyowekwa na Mwenyezi Mungu katika nyanja yoyote ya maisha, tendo lake hili huwa ni ubadhirifu. Tunu zote kutoka kwa Mwenyezi Mungu yumkini zikatumika bila faida, ikawa ni hasara tupu.

SURAYA 13

ISRAFU -1

Katika imani, itikadi na ibada

Tunu zote anazotoa Mola wetu kwa waja Wake ni ushahidi wa huruma, upole na upendo Wake. Tunu hizi kutoka hutolewa bure na Mwenyezi Mungu kwenda kwa waja Wake: kwa maana kwamba hakuna mja anayezilipia au anayefanya kazi inayofanya astahiki kuzipata. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an:

"Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanao fikiri." (al-Jathiyah, 45:13)

Hata hivyo, kupewa bure haimaanishi kwamba watu wanaweza kuzitumia vile wapendavyo, bila masharti au taratibu zozote. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika aya nyingine:

"Ati anadhani binaadamu kuwa ataachwa bure?" (Qiyâmah, 75:36)

Kwa hiyo, tunapotumia tunu tulizopewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu hatuna buda kuzingatia maamrisho na makatazo Yake. Tusisahau kuwa wakati matumizi ya haramu hutupeleka kwe-

nye adhabu, hata matumizi ya halali yanatakiwa kufanyika kwa maelekezo. Kama ambavyo tunatakiwa kujiepusha na matendo ya haramu, vivyo hivyo tunatakiwa kuepuka isrfu na kuangukia katika matendo mengine ya haramu pindi tunapotumia vibaya vitu vya halali. Kwa kweli, israfu ni kutumia tunu tulizopewa na Mwenyezi Mungu kwa kutojali na kuvuka mipaka aliyotuwekea katika kuzitumia. Kitendo hicho ni sawa na kukufuru neema tulizopewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Ubadhirifu kwa kawaida ni neno linalotumika katika masuala ya usimamizi wa fedha, lakini lina matumizi mapana zaidi yanayojumuisha mambo yote ambayo wanadamu wanaweza kupitiliza na kuvuka mipaka sahihi. Hivyo, mja akivuka mipaka iliyowekwa na Mwenyezi Mungu katika nyanja yoyote ya maisha, tendo lake hili huwa ni ubadhirifu. Tunu zote kutoka kwa Mwenyezi Mungu yumkini zikatumika bila faida, ikawa ni hasara tupu.

'Iyas ﷺ anasema: "Kila jambo linalovuka mipaka iliyowekwa na Mwenyezi Mungu ni israfu."

Kutokana na ushawishi wa nafsi, daima wanadamu hudhani kuwa tuna udhuru wa kufanya makosa. Hata wahalifu ambao wamefanya uhalifu mbaya kabisa huhalalisha uhalifu wao na kutaka wasamehe kwa sababu mbalimbali. Wabadhirifu na wabakhili hawatofautiani: hujitetea kwa kutoa nyudhuru mbalimbali, na huzifurahia hali zao. Ni nadra sana watu hao kutodanganyika kwamba wendawazimu wa israfu au ubakhili unaleta furaha ya kweli. Ndiyo maana dhana ya israfu ya israfu na ubadhirifu, ambayo kwa mara ya kwanza hujitokeza kama sura tu, hujaa kwa haraka sana picha itokanayo maamrisho ya Mwenyezi Mungu.

Kama ambavyo ubadhirifu wa mali tulizopewa kama amana umekatazwa na dini yetu; vivyo hivyo ubadhirifu wa rasilimali za kiroho, kama vile imani, matendo ya ibada, miundo ya maarifa

matukufu, maadili, na nyakati na misimu mitukufu, nao pia umekatazwa. Ni rahisi sana kuwa mbadhirifu na mkiukaji wa mambo hayo. Ubadhirifu na israfu katika imani ndiyo ubadhirifu hatari na mbaya kabisa kuliko aina zote za ubadhirifu. Hii ni kwa sababu, matokeo ya israfu hii ni kupoteza furaha yetu ya milele kwa sababu tu ya furaha ya mpito.

Mola wetu ameharamisha ubadhirifu na ubakhili katika mambo yetu yote, iwe ni kula, kunywa, mavazi mpaka kwenye kiwango cha juu kabisa cha maisha yetu ya kiroho. Ametuamrisha kuwa na uwastani katika kila kitu. Hivyo, kila muumini anatakiwa kuishi maisha ya kiasi na mizania ya uwastani. Mtu asiyechunga mipaka ya Mwenyezi Mungu katika matumizi ya tunu za mali na kiroho, hawezi kuepuka kuangukia katika hizi hali mbili za ubadhirifu na ubakhili.

Ningependa kuelezea kwa mukhtsari baadhi ya matendo makubwa ya israfu ambayo yatatusababishia janga na msiba mkubwa huko Akhera, na kuonesha jinsi ya kuyaepuka.

Israfu katika imani na itikadi

Hii ndiyo aina mbaya kabisa kuliko aina zote za israfu. Huharibu silika iliyo ndani ya mwanadamu ya kuuelekea Uislamu, huharibu hadhi yetu ya kiakili na kiroho kwa kuisukuma akili kwenye imani batili, uongo, imani potofu, na mielekeo hatari ya fikra. Unapokumbwa na hatari hii unakuwa umekumbwa na hasara ya kutopata furaha ya milele.

Udhaifu wa imani ni maangamizi ya kiroho ambayo mara nyingi hutokana na kusuhubiana na watu wasiokuwa wasafi. Katika aya ifuatayo Mola wetu anatuonya tusiangukie katika hali hiyo:

"Na unapo waona wanao ziingilia Aya zetu, basi jitenge nao mpaka waingilie mazungumzo mengine. Na kama Shet'ani akikusahaulisha, basi baada ya kutanabahi usikae pamoja na watu madhaalimu." (al-An'âm, 6:68)

Kuwa na uhusiano wa karibu na watu wasiokuwa wasafi hupelekea kuwapenda, kuwapenda hukupelekea kufikiri kama wao, na kufikiri kama wao taratibu huanza kuidhoofisha imani mpaka maisha ya milele yanapotoweka kabisa. Sababu ya aina hii ya israfu katika imani imeelezwa ndani ya Qur'an Tukufu kama ifuatavyo:

"Hao watakuwa katika Mabustani, wawe wanaulizana khabari za wakosefu: Ni nini kilicho kupelekeni Motoni? Waseme: Hatukuwa miongoni walio kuwa wakisali. Wala hatukuwa tukiwalisha masikini. Na tulikuwa tukizama pamoja na walio zama katika maovu. Na tulikuwa tukiikanusha siku ya malipo" (al-Muddaththir, 74:40-46)

Vilevile Mola wetu anatueleza jinsi mtu anavyoweza kuepuka mwisho huo wenye kutisha:

"Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli." (at-Tawbah, 9/119)

Aya nyingine ya Qur'an Tukufu inatukumbusha umhimu wa ishara za Mwenyezi Mungu, ikiwa ni pamoja na maamrisho na makatazo yake, na kututaka kuziangalie kwa makini kabisa na kuziweka maana zake ndani ya nyoyo zetu:

"Na wale ambao wanapo kumbushwa Ishara za Mola wao Mlezi hawajifanyi viziwi nazo, na vipofu." (Al-Furqân, 25:73)

Uwezo wa macho na nyoyo zetu kuelewa mambo ni miongoni mwa neema za Mwenyezi Mungu kwetu. Kuutumia uwezo huo

katika namna isiyoendana na malengo yake na hivyo kutoziona ishara za Mwenyezi Mungu nayo pia ni aina ya israfu, kwa maana kuzitumia vibaya neema hizo (za macho na moyo) ni kwenda kinyume na matumizi yake sahihi, na hiyo ni israfu. Katika aya ifuatayo Mwenyezi Mungu Mtukufu anatuonya juu ya mwisho mbaya utokanao na israfu na uongo:

"...Hakika Mwenyezi Mungu hamwongoi apindukiaye mipaka, mwongo mkubwa." (alMu'min, 40:28)

Vilevile kuna kadhia za upotofu wa itikadi, kwenda kinyume na mipaka iliyothibiti katika imani. Mojawapo ya kadhia hizo za upotofu wa kiitikadi hutokea pale watu wanapotembelea makaburi ya Marafiki wa Mwenyezi Mungu, na kuelekeza dua zao kwa hao Mawalii badala ya kuzielekeza kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Njia sahihi ya kuwatembelea Marafiki wa Mwenyezi Mungu ni kuchunguza matendo yao mazuri wakati wa uhai wao, na kuitafakari daraja yao kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu, na kumuomba msaada Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa daraja ya Marafiki hao. Lakini, kuweka mategemeo ya moja kwa moja kwenye uombezi (shafaa) wa waja wema na kudai kuwa "walii Yule na Yule watani-ombea na kuniokoa na adhabu" ni imani potofu. Mwenyezi Mungu ametangaza ndani ya Qur'an Tukufu kuwa wale tu waliowapa idhini ndio wanaoweza kufanya *shafaah* (uombezi):

"Siku hiyo uombezi haufai kitu, ila wa aliye mruhusu Arrahmani Mwingi wa Rehema na akamridhia kusema." (Tâhâ, 20:109)

Vilevile sio sahihi kusema kuwa waja wema wanajua kila kitu, na kuzisoma akili na nyoyo za watu. Wanajua tu kile ambacho Mwenyezi Mungu ameridhia wakijue. Vinginevyo, hata mitume hawajui kila kitu. Siku moja Mtukufu Mtume ﷺ aliulizwa jambo akajibu, "Aliyeulizwa si mjuzi wa jambo hili kushinda aliyeuliza." Wakati wa tukio kubwa la bibi Aisha h رضي الله عنها kuzushiwa kashfa, Mtu-

kufu Mtume ﷺ hakupokea ufunuo kuweka wazi jambo hilo mpaka baada ya mwezi mmoja. Katika kipindi chote hicho, hakutoa hukmu wala uamuzi juu ya jambo hilo. Mfano mwingine ni kadhia ya Maswahaba watatu ambao, kwa sababu ya uzembe, hawakushiriki katika jeshi lililokwenda kwenye vita ya Tabuk. Mtukufu Mtume ﷺ hakupokea ufunuo kuweka wazi hali yao mpaka baada ya siku hamsini.

Uthman ibn Madh'uun ﷺ alifariki dunia kwenye nyumba ya Ummul-A'laa mjini Madina. Baadaye mwanamke Yule akasema, "Ewe Uthman, ninashuhudia kuwa sasa hivi Mwenyezi Mungu Mtukufu anakutendea wema!" Mtukufu Mtume ﷺ akamkataza kusema hivyo.

"Umejuaje kwamba sasa hivi Mwenyezi Mungu anamtendea wema?"

Mwanamke huyo akajibu, "Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, sijui!"

Na hapo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema, "Uthman amekufa. Binafsi ninataraji Mwenyezi Mungu atampa rehma zake. Lakini, japokuwa mimi ni mtume niliye baina yenu, sijui kitakachonitokea mimi au nyinyi."

Ummul-Alaa anasimulia kuwa, "Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba baada ya tukio hilo sikusema tena chochote kumhusu mtu yeyote (nilikuwa nikimuombe kwa Mola wangu ampe rehma zake)." (Bukhârî, Tâbîr, 27)

Mwenyezi Mungu anatangaza ndani ya Qur'an Tukufu:

"Sema: Mimi si kiroja miongoni mwa Mitume. Wala sijui nitakavyo fanywa wala nyinyi. Mimi nafuata niliyo funuliwa tu kwa Wahyi, wala mimi si chochote ila ni mwonyaji mwenye kudhihirisha wazi." (Al-Ahqâf 46:9)

Mtu mmoja alimuuliza Nabii Ayuub ﷺ:

"Ewe Mtume mwema na mwerevu! Ilikuwaje ukahisi harufu ya Yusufu kwenye kanzu iliyoletwa kutoka Misri kabla haijakufikia, lakini ukashindwa kugundua kuwa alikuwa ndani ya kisima kilicho jirani na nyumba yako mwenyewe?"

Nabii Ayuub ﷺ akajibu: "Tunayofunuliwa na Mwenyezi Mungu ni mfano wa mwako wa nuru… Hivyo wakati mwingine huoneshwa maeneo ya mali, na tukafichwa yale yanayotokea maeneo ya karibu!"

Kumpa mtu sifa za bure na za ziada bila sababu ya msingi nalo ni israfu, na halikubaliki. Mtukufu Mtume ﷺ anasema kuwa, "Mmoja wenu akitaka kumsifu ndugu yake Muislamu, na kama kweli anazo sifa hizo, basi amsifu kama hivi: "Ninafikiri fulani ana sifa kadhaa wa kadhaa. Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi yake, siwezi kuthibitisha hilo mbele ya Mwenyezi Mungu, lakini nadhani yuko hivi na hivi." (Bukhârî, Shahâdât, 16)

Ukamilifu wa imani unategemea ukomavu na uwezo wa akili imara iliyolelewa na ufunuo. Ukamilifu wa akili unategemea nuru ya imani, ambayo ni ukomavu wa moyo. Imani na mawazo yasiyokuwa na nuru ya wahyi na badala yake yakajazwa uongo na imani potofu ni kama taa ya mafuta isiyokuwa na mafuta au taa balbu iliyokosa umeme. Vivyo hivyo, uwezo wa akili isiyoongozwa na wahyi (ufunuo) mwisho wake ni maangamizi, kama taa ya balbu inayopokea umeme usioendana na uwezo wake au mkondo wa umeme usiokuwa sahihi, na hivyo huvunjika.

Israfu katika Swala

Uwastani unatakiwa kuonekana katika matendo yote ya ibada, hata katika mambo ya kawaida yanatakiwa kuwa katika mpangilio.

Jinsi tunavyojizoesha kufanya mambo huleta athari katika tabia zetu za baadaye.

Nafasi ya kwanza ya israfu katika ibada ni mtihani wa kutumia maji kupitia kiasi wakati wa kuchukua wudhu au wakati wa kuoga, kwa sababu ya wasiwasi usiohitajika.

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alimuona Sa'd akichukua wudhu na kutumia maji mengi, akasema: "Israfu iliyoje ya maji!"

Sa'd akasema: "Je kuna israfu katika kuchukua wudhu?"

Mtukufu Mtume ﷺ akajibu: "Naam, mtu anaweza kufanya israfu ya maji hata kama anachukua wudhu mtoni!" (Ibn Mâja, Tahârah, 48)

Ni katika israfu kupuuza swala ya jamaah kama una fursa ya kuswali. Vilevile ni israfu kuswali bila utulivu na unyenyekevu wa moyo, kana kwamba unaswali tu ili umalize wajibu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema kuhusu wale wasiokuwa na utulivu na amani ya swala:

"Basi, ole wao wanao sali, ambao wanapuuza Sala zao." (Al-Mâ`ûn, 107:4-5)

Mtukufu Mtume ﷺ alizungumzia kuhusu kupoteza ubora wa swala kutokana na makosa ya ndani (moyoni), yaani swala zinazoswaliwa bila utambuzi wa kiroho. Akasema kuwa, "kuna wale wanaswali lakini wakapata thawabu nusu, theluthi, moja ya tano, moja ya sita, moja ya saba, thumni, moja ya tisa au hata moja kwa kumi ya thamani ya swala yao!" (Abû Dâwûd, Salâh, 123, 124)

Mwenyezi Mungu Mtukufu anataka akili na nyoyo zetu ziwe tayari kwa ibada wakati wa swala. Anasema:

"Nawe sujudu na ujongee!" ('Alaq, 96:19)

Anataka kuwa wakati nyuso zetu zikigusa chini, nyoyo zetu zijae unyenyekevu kutoka na utambuzi, kwa maana imani hukamilika pindi akili na moyo vinapojisalimisha kwa pamoja, vikashirikiana. Katika Qur'an Tukufu, wale wanaotekeleza swala zao kikamilifu wamesifiwa kwamba:

"HAKIKA wamefanikiwa Waumini, aAmbao ni wanyenyekevu katika Sala zao…" (Mu'minun, 23:1-2)

Aina nyingine ya israfu ni kupunguza thawabu za funga ya mwezi wa Ramadhan, ambayo ni moja katika Nguzo Tano za Uislamu, kwa kufanya mambo mabaya kama vile kusema uongo na kuwasengenya watu. Mtukufu Mtume ﷺ anasema kuwa, "Asiyeacha kusema uongo, asiyeacha kufanya biashara kwa kuwadanganya watu, basi Mwenyezi Mungu hatajali kama mtu hayo akiacha kula na kunywa." (Bukhârî, Sawm 8, Adab 51)

Funga inatakiwa kutufanya kutambua zaidi thamani ya tunu na neema mbalimbali tulizojaaliwa. Tunapoacha kula na kunywa kwa nusu siku tu, funga hutufanya tutambue jinsi gani tulivyo na udhaifu. Hutuonesha hali ya maisha ya ndugu zetu wanaoteseka kutokana na hali mbaya za umaskini, na huzihamasisha nyoyo zetu kuwaonea uchungu na kuwajali zaidi. Vilevile funga inatakiwa ituhamasishe kutoa zaka na sadaka kwa unyenyekevu na kutarajia thawabu, kana kwamba hizo zaka tunazitoa kumpa Mwenyezi Mungu mwenyewe. Qur'an Tukufu inasema:

"…Mwenyezi Mungu anapokea toba ya waja wake, na anazikubali sadaka…" (Tawbah 9:104)

Mwezi wa Ramadhan, ambao ni faradhi kufunga, umejaa nuru, hali ya kiroho, rehma, maghfira na athari za fadhila na huruma ya Mwenyezi Mungu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anatutaka tunufaike sana na nuru na neema za Mwenyezi Mungu ndani

ya mwezi huu kadiri iwezekanavyo. Katika mikesha ya mwezi huu tunatakiwa kutekeleza swala na dua za mara kwa mara kwa utulivu mkubwa, huku tukimuomba Mwenyezi Mungu msamaha, tukimdhukuru, kuzitafakri sifa Zake na kuisoma Qur'an Tukufu. Wakati wa mchana tunatakiwa kuendelea na ibada kwa moyo wote kwa kutoa sadaka na kufanya amali njema. Wakati wa kufuturu, ambacho ni kipindi cha kupokelewa swala zetu, tunatakiwa kufurahia amani itokanayo na kumuomba Mwenyezi Mungu maghfira, kumhimidi, na kupeleka chakula kwa Waislamu wenzetu ili nao wapate kufuturu. Wakati wa jioni tunatakiwa kutumia muda wetu vizuri kwa kufanya dua mbalimbali. Tusipoutumia vizuri mwezi huu, tutakuwa tumekosa faida kutoka katika bahari ya rehma na msamaha wa Mwenyezi Mungu iliyokuwa mbele yetu, na pia tutakuwa tumepoteza tunu nyingine tulizojaaliwa.

Kuna israfu na matumizi mabaya katika Hijja pale hujaji mtarajiwa anaposhindwa kujali kama anaishi kwa kipato cha halali; pale asipojali haki za wengine; pale anapojishughulisha zaidi na mambo ya kipuuzi na kujiingiza katika matendo yanayomuweka mbali na neema na nuru ya kiroho. Yote haya yanahesabiwa kuwa ni israfu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anasema kuhusu hujaji mwenye israfu na aliyechupa mipaka, "Hujaji anaposema "*Labbayk!*" (Yaani nimekuitika Mola wangu!) hujibiwa kuwa, "kelele zako hizo hazina faida! Kipato chako ni cha haramu, chakula chako ni cha haramu, usafiri wako ni wa haramu. Rudi ewe mkosefu, huna malipo yoyote! Tambua kuwa utakutana na mambo usiyoyapenda!" (Haythamî, III, 209-210)

Israfu na kutupa mipaka katika utoaji zaka na sadaka hutokea pale mtu anapomsumbua masikini kwa kumkumbusha wema aliomfanyia. Mtu akiwa na maradhi ya moyo kama vile unafiki na ufakhari, matokeo yake ni kutupa mipaka katika utoaji…Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani Qur'an:

"Kauli njema na usamehevu ni bora kuliko sadaka inayo fuatiliwa na maudhi… Enyi mlio amini! Msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na maudhi..." (Baqarah, 2:263-264)

Mtoaji anatakiwa kutafuta kwa uangalifu wale wanaostahiki kupewa zaka. Mwenyezi Mungu Mtukufu anawasifu wale wanaofanya uchunguzi huo kuwa:

…wanaofanya amali ya zaka… (Mu'minun, 23:4)

Kutoa zaka za mali na sadaka za vitu kwa watu wanaostahiki ni jambo muhimu mno. Mwenyezi Mungu anatuagiza kufanya kutafiti kuhusiana na jambo hili na kuboresha njia za kuwatafuta "ili kuwatambua wanaostahiki kwa nyuso zao."[33] Hakika, uwezo wetu wa kufikisha msaada kwa wale wanaostahiki kunategemea njia zetu za maisha. Zaka na sadaka tunazozitoa zitatuonesha iwapo mapato tuliyapata kwa njia za halali. Kama pesa zetu tulizipata kihalali, basi zitatumika vizuri na zitakwenda kwa wale wanaostahiki. Kama zilipatikana kwa njia ya haramu, basi zitatumika hovyo na kuwafikia watu wasiostahiki.

Kutakuwa na matumizi mabaya katika usomaji wa Qur'an kama mtu hatofanya juhudi za kuisoma kikamilifu au kuuelewa ujumbe wake, na kama hatayafanyia kazi maagizo na makatazo yaliyomo ndani ya kitabu hicho. Mtu huyo huifanyia ubadhirifu na israfu hazina kubwa na yenye thamani. Mwenyezi Mungu amewabainisha wale wanaoitumia vizuri na wale wanaofaidika kikamilifu na nuru ya Qur'an Tukufu:

"Kisha tumewarithisha Kitabu hao ambao tuliwateuwa miongoni mwa waja wetu. Kati yao yupo aliye jidhulumu nafsi yake, na yupo wa katikati, na yupo aliye tangulia katika mambo ya kheri, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo fadhila kuu." (Fâtir, 35:32)

33. Baqara 2:273.

Kama ambavyo umma bora kabisa ni umma wa Nabii Muhammad ﷺ, vivyo hivyo watu bora kabisa katika umma huu ni wale wanaoisoma Qur'an, wakaihifadhi, wakauchukua ujumbe wake na kufuata muuongozo na kanuni zake. Baadhi ya watu huzidhulumu nafsi zao: hawaisomi Qur'an na hawafuati muongozo wake licha ya kuwa na fursa ya kusoma. Haya ni matumizi mabaya ya kuipoteza tunu hii kubwa. Baadhi ya watu hufuata njia ya kati kwa kati, huifanyia kazi baadhi ya nyakati na kuiacha nyakati nyingine. Hata hivyo, kuna wengine hukithirisha na kubobea katika matendo mema kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.

Qur'an Tukufu ni lugha ya mbinguni na ardhini. Ni baraka kwa nyoyo na ni hazina ya hali ya kiroho. Ni muujiza wa ubainifu uliotolewa kama zawadi kwa watu. Kila moyo wenye kuishika kikamilifu hugeuka kuwa uwanja wa maajabu ya Mwenyezi Mungu. Wale wenye kusuhubiana na Qur'an Tukufu hupata utulivu wa akili na furaha ya aina yake, kwa sababu Qur'an ni mfano mdogo wa ulimwengu unaouingiza ulimwengu mkubwa ndani ya maajabu yake. Kwa wale wenye moyo, Qur'an Takatifu ni mfano wa mlango mzuri unaowawezesha kuingia ndani ya vina vya ulimwengu wa tafakuri.

Ili kuisoma Qur'a'n kikamilifu, usafi wa moyo ni muhimu kama ilivyo kwa usafi wa mwili. Kuna maradhi ya kimaanawi kwenye moyo, ambayo huwazuia watu kuamiliana na Qur'an kwa njia inayofaa. Wale wasioweza kupata rehma, ponyo na muongozo wa Mwenyezi Mungu ndani ya kitabu hicho huishia katika mazingira na hali ya hasara kubwa. Kwa kuwa Qur'an Tukufu inaelezea maagizo ya Mwenyezi Mungu, watu wema na wasafi ndio wanaoweza kuielewa. Ili mtu aweze kufaidika na neema ya Qur'an Tukufu na kupata furaha ya duniani na Akhera, lazima awe na *taqwa,* yaani Uchamungu.

Suala lingine muhimu ni suala la kuwahudumia watu. Kuwahudumia watu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, hata kwa vitu vidogo, kunaweza kuwa na thamani kubwa kuliko hata swala za sunna. Kisa kifuatacho kutoka katika Zama za Furaha kinaelezea nukta hii:

Siku moja Mtukufu Mtume ﷺ alipokuwa safarini alisimama na kuweka kambi sehemu fulani. Baadhi ya Maswahaba walikuwa wamefunga, hivyo walilala na kuchukuliwa na usingizi, kwa maana walikuwa wamechoka sana. Wengine wakaenda kuleta maji na kusimika mahema. Muda wa futru ulipofika, Mtukufu Mtume ﷺ akasema, "Leo wale ambao hawakufunga wamepata thawabu nyingi (kuliko wale waliofunga." (Muslim, Sıyâm, 100-101)

Mtu akijishughulisha na vitu visivyokuwa na umuhimu na kupuuza kutafuta kipato ili awe masikini, hii nayo ni aina ya israfu na kuituka mpaka. Mtukufu Mtume ﷺ anasema kuwa, "Mwenyezi Mungu Mtukufu anampenda mja ambaye huchoka akitafuta kipato cha halali." (as-Suyûtî, al-Jâmi` as-Saghîr, I, 65)

Aina nyingine ya israfu na kupituka mpaka ni pale mtu anapofanya dua katika kundi la watu. Wengine husoma dua ndefu sana kuliko kawaida, hususan wanapokuwa mbele ya watu. Anaweza hata akapaza sauti sana kuonesha jambo fulani, na wakati mwingine husoma kwa kughani. Kufanya hivyo huwafanya watu wakose umakini na dua inayosomwa. Yote haya yanahesabiwa kuwa ni matumizi mabaya ya ibada. Mtukufu Mtume ﷺ alikataza kusoma dua kwa kupiga kelele: "Msipige kelele mnapomuomba Mwenyezi Mungu. Kwa maana mnayemuomba sio kiziwi!" (Bukhârî, Jihâd, 131; Muslim, Dhikr, 44) Maombi hayo yasiyokuwa na uwastani ndani yake huibomoa hali ya kiroho na thamani ya matendo mema.

Israfu katika ibada huondosha faida na manufaa yake. Katika hadith nyingine, Mtukufu Mtume ﷺ anasema kuwa, "Litaibuka

kundi katika umma huu ambalo litavuka mipaka ya utakaso na dua.” (Abû Dâwûd, Tahârah, 45)

Kwa mukhtasari, Mwenyezi Mungu Mtukufu anatuonya dhidi ya kufanya matendo ya ibada kwa mazoea, bila utambuzi na bila kuzingatia. Mwenyezi Mungu anataka nyoyo zetu zizidi kumkurubia. Humkurubia pale zinapokuwa zimejazwa hali ya kiroho na nuru kupitia baraka zinazoipokea. Mwenyezi Mungu anataka nyoyo zetu zimuelekee Yeye.

Mola wetu! Tunakuomba utulinde dhidi ya matumizi mabaya na israfu katika imani, itikadi na matendo ya ibada kwa kuyapuuza au kwa kutupa mipaka. Tujaalie ladha na msisimko mkuu unaopatikana kwa kuikamilisha imani yetu, na amani na furaha itokanayo na kudumisha matendo ya ibada!

Amiin…

SURA YA 13

Israfu -2

Katika muda

Uhai ni neema yenye thamani mno ambayo Mwenyezi Mungu amewajaalia viumbe wote hai mara moja tu na kwa kipindi cha muda maalumu. Hivyo, hakuna budi kuutumia muda kwa mambo yanayolingana na thamani yake. Daima kuna vitu mbalimbali ambavyo vinaweza kufanywa kila wakati.

Huwezi kuazima muda wowote, au kumuazima mtu…unaweza kununua takriban kila kitu, lakini kamwe huwezi kununua muda ambao umeshapita.

SURA YA 13

ISRAFU -2

Katika muda

Neema zote anazozipata mwanadamu, iwe kwa juhudi au bure, ni baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa sababu Mwenyezi Mungu ndiye Muumba wa neema zote hizi, na ndiye aliyeumba uwezo na nguvu ambazo waja wanazihitajia ili kuzipata. Daima hatutakiwi kusahau kuwa sisi ni wapokeaji wa baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Daima tuishi tukijua kabisa kuwa neema zote hizi tulizopewa ni amana ambazo siku moja tutakuja kuulizwa. Qur'an Tukufu inaelezea wazi nukta hii:

"Je! Mlidhani ya kwamba tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa?" (Mu'minûn, 23:115)

Hivyo tunapotumia rasilimali za kimaada au za kiroho tulizonazo, tunatakiwa kutambua kuwa lazima tutaulizwa na kuwajibishwa. Kila tulicho nacho tunapaswa kukitumia katika kutaka radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Katika aya nyingine ndani ya Qur'an Takatifu, Mola wetu anatukumbusha kuwa bila sha tutawajibishwa hasa na kutuonesha kuwa tuna dhima kubwa:

"Tena bila ya shaka mtaulizwa siku hiyo juu ya neema." (Takâthur, 102:8)

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka taratibu na kanuni mbalimbali za jinsi ya kupata neema anazotujaalia. Vilevile ametuwekea utaratibu wa jinsi ya kuzitumia. Taratibu hizi zimebainisha vitu halali na vile vya haramu. Israfu au ubadhirifu ni miongoni mwa vitu vinavyosababisha hasara ya kutopata rehma na upendo wa Mwenyezi Mungu, na humpeleka mtu katika hali ya kughadhibikiwa na Mola wake. Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Qur'an Tukufu:

"...Wala msitumie kwa fujo. Hakika Yeye hawapendi watumiayo kwa fujo." (An`âm, 6/141)

Matumizi mabaya (israfu) ya muda

Matumizi mabaya ya muda ni miongoni mwa makosa makubwa kabisa ambayo huwakabili watu. Hayo hutokana na kukosa umakini na kughafilika. Uhai ni neema yenye thamani mno ambayo Mwenyezi Mungu amewajaalia viumbe wote hai mara moja tu na kwa kipindi cha muda maalumu. Hivyo, hakuna budi kuutumia muda kwa mambo yanayolingana na thamani yake. Daima kuna vitu mbalimbali ambavyo vinaweza kufanywa kila wakati. Hata hivyo, kanuni kuu ni kutoa kipaumbele kwa kile chenye umhimu zaidi wakati huo. Hivyo basi tunapaswa kupangilia kile kinachofuata kutokana na kiwango cha umuhimu wake.

Kwa mfano, mama kutoa kipaumbele kwenye kumnyonyesha mtoto ni jambo sahihi, kwa sababu maumbile ya huruma yake kwa mtoto yanamtaka kufanya hivyo. Lakini, akiendelea kumnyonyesha hali ya kuwa nyumba inaungua moto, atakuwa ameonesha upumbavu na ataangukia katika dhima kubwa. Hapo, kipaumbele

chake kinatakiwa iwe ni kuzima moto. Akipuuza na kutofanya lolote wakati nyumba inaungua, muda si mrefu yeye na mwanaye wataangamizwa na moto huo.

Vivyo hivyo, kwa sababu ya uozo wa maadili katika zama hizi, kutumia muda wetu kufanya juhudi ya kuhakikisha dini ya Mwenyezi Mungu inaimarika ni miongoni mwa dhima zetu.

Maswahaba wa Mtukufu Mtume ﷺ, ambao walikuwa makini sana katika matumizi ya muda, walitambua kuwa muda bora walioutumia ni pale wanapojishughulisha na kufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa watu. Swahaba mmoja alikuwa akikaribia kunyongwa na makafiri. Mtu aliyepewa jukumu la kumuua alimpa swahaba huyu muda wa dakika tatu za kutoa wosia wake wa mwisho. Swahaba huyu alimshukuru mtu huyo na kusema, "Inaonekana nina muda wa dakika tatu zaidi za kukufikishia Uislamu. Ninatarajia utaongoka."

Katika zama zetu hizi baadhi ya watu wamepotelea katika mmomonyoko wa imani na maadili. Kutokana na hali hii, ni wajibu kwa kila muumini, kutokana na imani na utambuzi wetu, kuwafikia watu hao kwa maneno laini na yenye hekma na kuwafanya waujue uzuri na wema wa Uislamu.

Kuutumia vibaya muda, ambao ndio mtaji wenye thamani mno, kwa kujiingiza katika mambo ya kipuuzi na yasiyokuwa na faida, kunaweza kuhatarisha maisha yako ya Akhera. Kwa wale ambao wameweka ujinga pembeni, muda ni neema ya kipekee, isiyolinganishwa na chochote kile. Katika Surah 'Asr' (Muda), Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Naapa kwa Zama! Hakika binaadamu bila ya shaka yumo katika khasara, Ila wale walio amini, na wakatenda mema, na wakausiana kwa haki, na wakausiana kusubiri." ('Asr,103:1-3)

Sura hii inayoanza kwa kuuapia Muda, inatangaza kuwa muda unaotumika bila imani au usiotumika katika kutenda mambo mema na kuusiana kutenda haki na subira, unakuwa umepotea bure. Muda wa namna hiyo ni muda wa hasara na huzuni. Isipokuwa kwa wale wanaoutumia muda wao vizuri wameepukana na hasara hiyo. Hivyo, sura hii inaeleza ukweli wenye kuuma kuwa watu wengi hushindwa katika suala la matumizi ya muda.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anawapa waja wake muongozo ufuatao ili kuepukana na hasara ya muda na ili waweze kupata baraka kutoka Kwake:

"Na ukipata faragha, fanya juhudi. Na Mola wako Mlezi ndio mshughulikie." (Inshirâh, 94:7-8)

Hii ina maana kuwa mtu amalizapo kazi moja anatakiwa afanye haraka kuelekea kwenye kazi nyingine. Kwa kufanya hivyo hatutaruhusu muda kupita bila kuwekeza katika ibada na matendo mema. Kwa maana muda ni hazina tuliyoazimwa ili tupate furaha ya Akhera, na kifo ndio muda wa mwisho wa kulipa deni letu.

Mfanyabiashara huchukua mkopo kwa ahadi ya kulipa deni katika muda maalumu. Muda umewekwa ili Yule anayedaiwa ajiandae kulipa deni. Maisha ya duniani ni muda tuliopewa ili kujiandaa kwa ajili ya maisha ya Akhera, ili tupate kupokelewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mfanyabiashara asipouangalia kwa makini muda wa mwisho na akawa haja jiandaa, atapata shida pindi anapotakiwa kurejesha deni…Na mwanadamu asipotumia vizuri muda aliopewa, hataweza kuiepuka hasara. Kila mtu ana dhima aliyopewa kuitekeleza kwa muda maalumu unaoanza mara tu baada ya kuzaliwa. Muda huo ukifikia ukingoni, kila mtu atakutana na Azrael عليه السلام, malaika wa mauti. Japokuwa tuna uhakika kuwa mwanadamu ataulizwa kuhusu deni lake la uhai, siku yenyewe ya kudaiwa haijulikani. Hali hii yenye kukanganya hutuhamasisha muda wote tuwe tumejiandaa kwa ajili ya kulipa deni la uhai wetu.

Ukweli kwamba uhai ni neema kutoka kwa Mwenyezi Mungu inayotakiwa kutumiwa vizuri ndiyo msingi wa kanuni muhimu ya Kisufi ijulikanayo kama *wuquf-i zamani,* yaani "kuendelea kuwa pamoja na muda." Kwa mujibu wa dhana hii, muumini anayekusudia kuisafisha nafsi yake na kuutakasa moyo wake lazima ajishughulishe na matendo sahihi na mema kila wakati, kujihesabu na kujipima muda wote. Anatakiwa kuacha yasiyo na ulazima na kuepuka mazungumzo ya kipuuzi yasiyokuwa na manufaa. Kama asemavyo Mawlana Jalaluddin Rumi, mtu huyo lazima aulinde ulimi wake usiwe "chale ya maneno." Hakika, hivi ndivyo Mwenyezi Mungu anavyowasifia waja wanaotaka wokovu:

"Na ambao hujiepusha na mambo ya upuuzi." (Mu'minun, 23:3)

"...na pindi wapitapo penye upuuzi, hupita kwa hishima yao." (Furqân, 25:72)

Muumini mwema daima anatakiwa kuutambua ulimwengu wake wa ndani. Aangalie jinsi anavyomuomba Mwenyezi Mungu msamaha, jinsi anavyomshukuru na jinsi anavyotosheka na maisha yake. Anatakiwa kuzitafakari neema zisizokuwa na kikomo anazozipata na kushukuru kwa neema hizo, na anatakiwa kutubu kwa muda alioutumia katika ujahili na ujinga. Daima anapaswa kutambua ujahili aliofanya zamani na ajiweke huru dhidi ya wasiwasi usiokuwa na maana kuhusu mustakbali wake. Anapaswa ajitahidi kutekeleza mahitaji ya zama anazoishi. Hii ina maana kwamba, anapaswa kuwa "mwana wa zama" – anapaswa kuitambua kikamilifu thamani ya uhai wake na hususan muda anaoishi kwa sasa.

Muumini mwenye ukomavu atautumia muda wake katika kujiandaa na maisha ya Akhera. Kwa hakika, kuutumia uhai wetu wenye thamani katika mambo ya kipuuzi ni mojawapo ya vyanzo vikubwa kabisa vya majuto. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ

anasema kuwa, "Watu wa peponi hawatajutia chochote bali muda uliotumika katika maisha ya dunia bila kumkumbuka na kumdhukuru Mwenyezi Mungu!" (Haythamî, X, 73-74) Hivyo anatkumbusha kuwa waumini wanatakiwa kuwekeza muda wao kama mtaji ili wavune maisha ya milele. Fursa zinapopotea, majuto hayana faida tena… Kwa hiyo basi, tunapaswa kuutumia uhai wetu vizuri wakati huu ambapo tuna fursa ya kufanya hivyo. Tufanye juhudi ya kumshukuru Mwenyezi Mungu sana kwa uwezo wetu wote. Kwa mfano, tunapaswa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya ulimi kwa kumhimidi na kumsifu kwa dhikri mbalimbali, ambazo ni ponyo na tiba ya moyo.

Mtukufu Mtume ﷺ alimuusia mkewe, Bibi Hafsa رضي الله عنها: "Ewe Hafsah! Tahadhari na kuongea sana. Kuongea sana kusikokuwa katika kumtaja Mwenyezi Mungu huua moyo. Bali mtaje Mwenyezi Mungu mara kwa mara, kwa maana hilo huuhuisha moyo." (Ali al-Muttaqî, I, 439/1896)

Mwenyezi Mungu Mtukufu anatuonya:

"Na toeni katika tulicho kupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, tena hapo akasema: Mola wangu Mlezi! Huniakhirishi muda kidogo nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema?" (al-Munâfiqûn 63:10)

Aya ifuatayo, ambayo inasimulia vilio na nyudhuru za wale wanaoishia katika hasara, inasema kwa uwazi kabisa:

"Na humo watapiga makelele: Mola wetu Mlezi! Tutoe tufanye mema sio yale tuliyo kuwa tukiyafanya. Kwani hatukukupeni umri wa kutosha kukumbuka mwenye kukumbuka? Na akakujieni Mwonyaji? Basi onjeni! Kwani walio dhulumu hawana wa kuwanusuru." (Fâtir, 35:37)

Sababu kubwa ya matumizi mabaya ya muda ni kwamba watu hukisahau kifo na kuendelea kudhani kuwa kiko mbali. Hakika huu ni msingi wa ujinga na ndiyo sababu hasa ya matumizi mabaya ya neema nyingine pia. Hadith moja ya Mtukufu Mtume ﷺ inasema kuwa, "Kikumbukeni kifo mara kwa mara! Kinabomoa ladha na raha zote." (Timidhî, Qıyâmah, 26) Mwenendo wowote unaokwenda kinyume na onyo hili la Mtukufu Mtume ﷺ siku moja utatusababishia adhabu.

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema: "Kila atakayekufa atajuta."

Maswahaba wakamuuliza:"Inawezekanaje watu wote wajute?"

Mtukufu Mtume ﷺ akajibu: "Kama ni mtu mwema, basi atajuta kwa kutofanya zaidi matendo mema. Na kama akiwa mtu muovu, basi atajuta kwa kutoacha matendo maovu." (Tirmidhî, Zuhd, 59)

Mtu anapozitafakari kwa makini athari za uwezo wa Mwenyezi Mungu ndani mwake au ndani ya ulimwengu, akazitazama kwa jicho la moyo, lazima atatafakari jinsi anavyotakiwa kuyaendesha maisha yake. Kifo ndio tukio kubwa ambalo huathiri mwelekeo wa maisha ya mtu. Tukio hilo la kuaga limejaa mafunzo yanayotakiwa kuzingatiwa. Mtu mwenye kukijua kifo hatadanganywa na raha za mpito; mwenye kutambua kuwa yeye ni msafiri katika safari ya kuelekea Akhera hawezi kulaghaiwa na kughilibiwa na midoli ya hoteli hii ya kidunia. Hatatumia muda wake kucheza na midoli hiyo. Qur'an Tukufu inatangaza kuwa:

"Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake kwa mchezo. Hatukuviumba hivyo ila kwa Haki, lakini wengi wao hawajui." (Dukhân, 44:38-39)

Hata kama tungepewa kila neema ya mpito na kuishi kwa miaka elfu moja, hazitakuwa chochote mwishoni. Je kituo cha safari yetu si ipo chini ya udongo utaoukanyaga kwa miguu yetu? Kwa nini hatutaki kutambua kuwa ujana na nguvu za vitu vyote vyenye kufa vimesagwa na kinu cha zama na wakati? Litakuwa jambo la kutisha sana, kuhusu maisha ya baadaye, iwapo mtu atajaribu kung'ang'ania mabembelezo ya kuilisha nafsi katika ulimwengu usiokuwa na uhusiano na Akhera, kama ataichukulia midoli ya uwanja huu kuwa ni kitu cha kweli!... Imam Shafii anauliza: "Je ni werevu kwa msafara unaondelea na safari kujenga nyumba barabarani?"

Tazama wale wanaozama katika raha na anasa za dunia kwa lengo la kupata amani ya akili bila kuiangalia Akhera. Hakika ni matumizi mabaya kabisa ya uhai. Ni hasara yenye kuhuzunisha na yenye kuumiza! Wale wanautumia ovyo muda wao kana kwamba hawatakufa, hapo baadaye wataijutia tabia yao na kusikitikia muda walioupoteza.

Watu wenye matamanio ya kihayawani daima hujaribu kukwepa kukifikiria kifo na yale yanayoambatana na kifo ili maisha yao ya kughafilika yaendelee bila kuingiliwa… Lakini kwa vyovyote vile kifo kitawameza. Matazamio huzalisha hofu kubwa kuhusu mustakbali, na, moja kwa moja, hugeuka kuwa jinamizi lenye kutisha. Sote tunapenda kuishi katika ulimwengu wa kufikirika unaojengwa kulingana na mapendeleo yetu wenyewe. Lakini, je, mtu mwerevu atakiuza kitu halisi kwa ajili ya kitu chenye kufikirika, ataliuza kasri kwa ajili ya gofu? Ni wazi kuwa kuna watu wengi wanaoyaangamiza maisha yao ya Akhera huku wakitaka kuendeleza maisha yao ya dunia.

Mawlana Jalaluddin Rumi anaonesha njia ya kuliepuka gereza la dunia na kuifikia furaha ya milele. Anasema kuwa,

"Usishikamane sana na mali, ili kwamba siku utakayoondoka uweze kuziacha kiurahisi. Na kama ukiweza kukiacha kitu kiurahisi, unaweza kukiacha na kupata malipo! Mng'ang'anie Yule anayekung'ang'ania: Naye Ndiye wa Mwanzo na wa Mwisho." Pia anasema kuwa, "Watu wengi wanaogopa kuwa miili yao itakufa. Lakini kitu kinachostahili kuogopwa ni kifo cha moyo."

Vitu vyote vimewekewa muda maalumu wa mwisho wa uhai wake. Muda huo hauwezi kuondoshwa au kuakhirishwa kidogo ili kurefusha uhai wa kidunia. Muda unasonga mbele, hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu alivyopanga. Huwezi kuazima muda wowote, au kumuazima mtu. Katika dunia hii unaweza kununua takriban kila kitu, lakini kamwe huwezi kununua muda ambao umeshapita.

Kama ambavyo hakuna mtu asiyechukua hatua pindi sarafu ya dhahabu inapotupwa jalalani, lakini watu wengi bado hawajali pindi muda unapotupwa kwenye vitu vya kipuuzi na visivyokuwa na manufaa.

Fariduddin Attaar (q.s) anasema: "Kuna vitu vinne ambavyo haviwezi kurejeshwa: neno linapotoka mdomoni, mshale unapoondoka kwenye upinde, ajali iliyokwishatokea na uhai uliotumika katika upuuzi."

Rafiki mmoja wa Mwenyezi Mungu anatupa wosia ufuatao: "Nenda katembelee hospitali mara moja! Utamshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu amekuepusha na maumivu na maradhi yanayowatesa wagonjwa; amekupa neema ya afya. Nenda katembelee magereza, na uyatafakari maisha ya wafungwa yaliyojaa uchungu. Tambua kuwa kosa hufanywa ndani ya dakika moja tu, kwa kutojua au kutokana na matatizo ya kisaikolojia. Tambua kuwa wakati mwingine watu hufungwa na kuteseka kwa makosa ambayo hawakuyafanya. Fikiria kama ungekuwa mmoja wao! Kisha mshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuwa amekulinda usiangukie katika

hali hizo zenye kusikitisha. Mhimidi na umsifu Mwenyezi Mungu kwa hali yako njema. Kisha nenda katembelee makaburi. Yasikilize makelele na vilio visivyotoa sauti; yatambue mazungumzo yao yenye ukimya. Tambua kuwa majuto hayana faida pindi uhai unapofikia kikomo, na hivyo itambue thamani ya muda wako. Wasomee watu wa makaburini dua na jaribu sana kuutumia uhai wako kwa kumshukuru na kumhimidi Mwenyezi Mungu pamoja na kuyadhukuru Majina Yake matukufu!"

Kwa hali hiyo waumini wanapaswa kufanya juhudi kubwa ya kuishi katika hali ya kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ndani ya Qur'an, Allah anasema:

"Wala msiwe kama wale walio msahau Mwenyezi Mungu, na Yeye akawasahaulisha nafsi zao. Hao ndio wapotovu." (Hashr, 59:19)

Abu Abdur-Rahman as-Sulami anasema kuwa kupoteza muda na kusuhubiana na wale wasiofikiria nje ya ulimwengu huu ni miongoni mwa makosa makubwa kabisa ya nafsi. Kisha anaeleza jinsi makosa hayo yanavyoweza kuondoshwa: "Uchukulie muda kuwa ndiyo kitu chenye thamani zaidi kuliko vitu vyote na utumie ipasavyo. Yaani, endelea kumhimidi Mwenyezi Mungu kwa dhikri. Daima endelea kuwa katika hali ya ibada, na usiache kukuza udhati wa moyo ndani ya nafsi yako. Kwa maana Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anasema: 'Dalili ya ukomavu wa muumini ni kuacha vitu visivyomhusu." (Tirmidhi, Zuhd, 11)

Katika hadith za Mtukufu Mtume ﷺ tunakuta maelezo yafuatayo:

- "Yathamini mambo matano kabla mengine matano hayajatokea: ujana kabla ya uzee, afya kabla ya maradhi, utajiri kabla ya umaskini, fursa kabla ya kushughulishwa, na uhai kabla ya kifo!" (Hâkim, Mustadrak, IV, 341; Bukhârî, Riqaq, 3; Tirmidhî, Zuhd, 25)

- “Baada ya kufufuliwa, unyayo wa mja hautaondoka mpaka aulizwe mambo manne. (1) Uhai wake: aliutumiaje? (2) Ujana wake: Aliushughulisha na nini? (3) Mali yake: aliupataje na aliutumiaje? (4) Elimu yake: aliifanyia nini? (Tirmidhî, Qıyâma, 1)

- “Kuna neema mbele: watu wengi hudanganyika na matumizi yake. Mali na muda.” (Bukhârî, Riqaq, 1)

Mara kwa mara Mwenyezi Mungu Mtukufu anatangaza ndani ya QUr’an kuwa siku ya Kiyama atatuhesabu na kutuwajibisha kwa neema za kimaada na kiroho alizotujaalia. Wanazuoni wa Kiislamu wana majibu yanayotofautiana kuhusu swali la kitu gani kitakachokutana na hesabu kali zaidi katika neema tulizopewa. Ibn Masu’d ﷺ anasema kuwa neema zitakazohesabiwa kwa ukali kabisa ni “amani, afya na muda.” Muawiya ibn Qurra ﷺ anasema kuwa “hesabu kali zaidi siku ya Kiyama itakuwa hesabu ya muda.” (Bursawî, X, 504)

Imam al-Ghazali anaonya: “Ewe mwanangu! Fikiria kwamba utakufa leo. Utahuzunika sana kwa muda ulioutumia kwa upuuzi. Utasema “kama ninge…” lakini hutakuwa na muda tena!”

Hadhrat Junayd al-Baghdadi anasema: “Siku moja katika dunia ina thamani kuliko miaka elfu moja ya Akhera. Hiyo ni kwa sababu kuchuma vitu na kuvipoteza ni hapa duniani. Huko Akhera hatuwezi kuchuma wala kupoteza.”

Muda unaotumika katika upuuzi ni hasara yenye kuumiza ambayo haiwezekani kuirekebisha. Majalada yote ya zamani hufungwa. Hata hivyo, bado tunaweza kufanya juhudi kurekebisha hasara kiroho kwa kumuomba Mwenyezi Mungu, kumtaka msamaha na kukimbilia kwake baada ya kujuutia muda tulioupoteza.

Mto wa uhai hutiririka kwa kasi. Siku zinazotengeneza maisha yetu, zinazohesabiwa na Mwenyezi Mungu, ni kama matone

yanayoingia kwenye kikombe. Kila siku tunasonga mbele kuelekea mwisho; tunatoka kwenye ulimwengu huu na kusogea karibu zaidi na kaburi. Kwa kuwa hatujui lini tutaondoka, tunapaswa kuzingatia kwamba tunaweza kukutana na Azrael ﷺ muda wowote, na hivyo tunapaswa kuwa tayari muda wowote kuvuta pumzi yetu ya mwisho.

Tukitafakari kwa makini, tutagundua kuwa mustakbali wetu una habari njema na pia habari za hatari. Na hatujui hatujui ni majani mangapi yaliyobaki katika kalenda ya maisha yetu…

Tunamuomba Mwenyezi Mungu, kama alivyosema ndani ya Qur'an Tukufu, atujaalie fursa ya kumuabudu mpaka *yakini* – yaani kifo- *itufike*,[34] ili tufe hali ya kuwa ni Waislamu.[35] Tunamuomba atujaalie tuyaendeshe maisha yetu pasipokuwa na israfu, yakiwa ni yenye uwastani na kuendana na hali ya ulimwengu wa ndani na wa nje. Atujaalie kuitumia neema ya Muda kwa kutenda matendo mema na yenye kumpendeza!

Amiin…

34. Tazama, Hijr, 15:99.
35. Tazama, Âl İmrân, 3:102.

SURA YA 14

Israfu -3

Katika Elimu

Moyo utakaozitengeneza jamii sio moyo wa majebi yenye ubinafsi ambayo huhifadhi vitabu vingi, bali moyo wa wale wanaozitanua nyoyo zao kwa hekma itokayo ndani ya Qur'an na ambao ni chanzo cha huruma na amani ya jamii. Huo ni moyo wa wale wanaomcha Mwenyezi Mungu, na waumini wanaopenda kuwahudumia wengine.

Kujua ni kufumbua siri za uumbaji, kuzifahamu hekma na kuwa na moyo wenye utayari wa kupokea fungu la hekma hizo kutokana na kuufahamu ukuu wa Mwenyezi Mungu na chemichemi ya uwezo Wake.

SURA YA 14

ISRAFU -3

Katika elimu

Ili maisha yetu yapate maono, umaridadi na maana, na hivyo kuwa maisha maridhawa, tunapaswa kuepuka israfu na sifa nyingine hasi. Kwa hakika israfu ndiyo chanzo kikuu cha maangamizi kwa mtu, familia na jamii kwa ujumla.

Neema zote tulizojaaliwa ni amana. Zisipofikishwa mahali panapostahiki, zikatumika katika upuuzi na matamanio, Mwenyezi Mungu Mtukufu huiondosha baraka yake.

Israfu sio tu kutumia vibaya mali, bali ni jambo la hatari katika nyanja zote za maisha. Tumeona kuwa kutumia uhai katika masuala ya upuuzi ni mojawapo ya aina za israfu na matumizi mabaya. Kujishughulisha na elimu isiyokuwa na manufaa, na kuitumia vibaya elimu kwa sababu binafsi, nayo ni israfu.

Kutafuta elimu ni kazi tukufu ambayo hukidhi maumbile yaliyo ndani mwetu: silika ya mwanadamu kujifunza. Silika hiyo ni sifa kuu kabisa katika kilele cha maumbile ya mwanadamu. Kupenda elimu ndiko kunakowafanya waumini kutaka kumjua

Mwenyezi Mungu, kumshukuru na kumtukuza kwa matendo ya ibada mbalimbali.

Aina bora kabisa ya elimu ni elimu ya kumjua Mwenyezi Mungu (*ma'rifatullah*), ambao ni uwezo wa kumtambua Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani ya moyo wako. Ulimwengu huu wa mpito ni mfano wa darasa la mtihani. Katika mazingira hayo, kujihangaisha na elimu isiyokupeleka kwenye kumtambua Mwenyezi Mungu, elimu isiyozalisha hekma na kutengeneza hali ya kuutambua ukweli moyoni, ni matumizi mabaya ya silika ya mwanadamu ya kujifunza.

Katika Qur'an Tukufu, elimu na maarifa sahihi yamehusishwa na hisia na utambuzi wa ndani, yaani kumcha Mungu na kujisalimisha Kwake. Qur'an Tukufu inasema:

"Je! Afanyae ibada nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama akitahadhari na Akhera, na akitaraji rehema za Mola wake Mlezi...Sema: Ati watakuwa sawa wale wanao jua na wale wasio jua? Hakika wanao kumbuka ni watu wenye akili." (az-Zumar, 39:9)

Tukiiangalia aya hiyo kwa umakini, tunaweza kutumia kigezo kilichowekwa na Mwenyezi Mungu kutofautsha kati ya maarifa na ujinga. Tukitaka kuwa miongoni mwa wale wanazijua hekma na ukweli, basi tutekeleza masharti yafuatayo:

1. Kumuomba Mwenyezi Mungu wakati wa usiku, kusujudu na kufanya visimamo, ili nyoyo zetu ziwe na hisia za kuwa mbele Yake.

2. Muda wote, katika hali zote, tunapaswa kutambua kuwa kuna kuhesabiwa siku ya Kiyama.

3. Tunapaswa kuendelea kukimbilia kwa Mola wetu, tukitarajia rehma Zake.

4. Kuendesha maisha kwa kuongozwa na uchamungu, na hivyo kujikurubisha zaidi Kwake.

5. Kuzilinda nafsi zetu dhidi ya sifa mbaya zinazotuweka mbali na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tujitahidi kudhihirisha sifa za uzuri, tabia zenye kupendeza zilizopo ndani mwetu, hususan ukarimu.

6. Kudumisha hali ya kutambua kuwa Mwenyezi Mungu anatuona, kana kwamba matendo yetu yanarikodiwa na kamera za Mwenyezi Mungu.

7. Kujitahidi sana kuzilinda nyoyo zetu dhidi ya ulafi na tamaa za kidunia.

8. Kuwa na subira pindi tunapokumbwa na shida na tabu wakati wa kutekeleza taratibu na mafundisho ya dini yetu.

Na ili tusiwe miongoni mwa wale "wasiojua", tunapaswa kuepuka sifa zifuatazo:

1. Ukosefu wa imani na shukurani.

2. Kumuomba Mwenyezi Mungu wakati wa shida na kumsahau wakati war aha.

3. Kufanya kitu fulani kuwa sawa na Mwenyezi Mungu kwa lengo la kuwapotosha watu au kwa matamanio na maslahi binafsi. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Je! Umemwona aliye yafanya matamanio yake kuwa ndio mungu wake?" (Furqân, 43)

Sayansi zote hulenga kugundua kanuni zilizowekwa na Mwenyezi Mungu kuviendesha viumbe na matukio. Maendeleo ya sayansi hutegemea kuongezeka kwa ugunduzi huo. Hata hivyo, kuzigundua kanuni zilizowekwa na Mwenyezi Mungu kuviendesha

vitu na matukio sio elimu inayompeleka mja kwenye utambuzi na hekma. Elemu hiyo tukufu (ya utambuzi, maarifa na hekma) ni zaidi ya kutazama vitu.

Elimu hiyo adhimu (ya utambuzi) hutufanya tuelewe sababu za kuja kwetu katika ulimwengu huu na sababu za kuondoka kwetu. Inajumuisha kuitambua na kuielewa lugha ya viumbe vyote na kuzigundua siri zake. Kujua kwa njia hii ni kufumbua siri za uumbaji, kuzifahamu hekma na kuwa na moyo wenye utayari wa kupokea fungu la hekma hizo kutokana na kuufahamu ukuu wa Mwenyezi Mungu na chemichemi ya uwezo Wake.

Kujua ni kutafuta kile ambacho ni cha lazima hasa. Na Qur'an Tukufu inaeleza kuwa kitu cha lazima kabisa kuliko vitu vyote ni kufa ukiwa katika hali ya kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.[36]

Kujua ni kujikomboa na utumwa wa nafsi ya kihayawani kabla haijafa. Na kuiamsha alfajiri ya ukweli. Kujua ni kujihoji kabla ya kuhojiwa na Mwenyezi Mungu.

Mawlana Jalaluddin Rumi alizama katika bahari ya maarifa kwa kuupanua uelewa wake wa maarifa ya nje ya kidini. Aliyazungumzia maisha yake kuwa yaligawanyika katika hatua tatu. Kipindi cha mwanzo, ambacho alifikia kilele cha maarifa ya jumla lakini akawa hajaonja ladha ya kuwa karibu na Ukweli, alikielezea kwa kusema "niliona ganda." Kipindi cha kati, ambacho alipata taarifa za hekma katika moyo wake na kupata raha ya kimaanawi, alikielezea kwa kusema "nilipikwa." Na kipindi cha ukomavu, ambacho siri mbalimbali za ulimwengu zilidhihirika mbele yake na kuzisoma kama kitabu, alikielezea kwa kusema, "nimeiva."

36. Tazama, Âl-Imrân, 3/102.

Utambuzi wa kimaanawi huongezeka kadiri maarifa yanavyoongezeka. Maarifa ya kweli humfany mtu asafiri katika bonde la maajabu. Kadiri anazijua hekma na ukweli uliowekwa ndani ya ulimwengu, ndivyo anavyozidi kutambua kuwa mwananadamu ni dhaifu, ana ukomo na si chochote… Uelewa huo ndio kujijua au kujitambua, na mwenye kujijua, humjua Mola wake.

- Mwenye maarifa, humjua mmiliki halisi wa viumbe, mfalme wa ufalme pekee. Mtu huyo hugeuka kuwa chanzo maridhawa cha wema na kuwahurumia viumbe kwa sababu ya Muumba wao.

- Mwenye maarifa, husamehe; mwenye kujua, huwa na subira; mwenye kujua huwa na upendo. Mwenye maarifa hujitahidi kumfurahisha Mola wake na kutaka kuwa karibu Naye. Kwa mtu huyo, kujitolea maisha yake ni furaha na raha.

- Mwenye maarifa hawaumizi wengine na hawezi kuumizwa na wengine. Ni mtu mwenye ulaini wa moyo na maisha yake hayaathiriwi na hisia za kutojitambua. Lugha yake ni lugha ya huruma.

- Mwenye maarifa, akiambiwa achague kati ya kumfurahisha Mwenyezi Mungu na kuwafurahisha viumbe, yeye huchagua kumfurahisha Mwenyezi Mungu.

- Mwenye maarifa hujaribu kuwa pamoja na Mola wake tu katika hali yoyote – *"akiwa amesimama, akiwa amekaa kitako na akiwa amelala."* [37]

- Mwenye maarifa daima hujishughulisha na tafakuri, anautambua ukuu wa Mwenyezi Mungu na uwezo Wake kwa kuuchunguza ulimwengu. Upole, umaridadi na utambuzi hugeuka kuwa tabia yake ya lazima.

37. Tazama, Âl-Imrân, 3:191.

- Mwenye maarifa mtu wa moyo na hali ya kiroho.
- Mwenye maarifa hutafuta amani na furaha kila mahali na katika hali yoyote.
- Mwenye maarifa ana hisia ya uwajibikaji kwa watu wengine na kwa jamii.
- Mwenye maarifa anajua kuwa nchi yake, taifa na bendera vyote ni amana. Hii ni kwa sababu usalama wa dini, familia, mali na uhai vinategemea usalama wa nchi na taifa dhidi ya taathira za maangamizi na uharibifu.
- Mwenye maarifa hujifunga kwenye maisha ya kiroho ili ajikomboe na utumwa wa nafsi ya kihayawani.
- Mwenye maarifa hachezi na midoli yenye kudanganya ya ulimwengu wa mpito. Huziweka ghururi za dunia nje ya moyo wake.
- Mwenye maarifa hujikomboa na ukaidi wa moyo, shari za umaarufu na tamaa.
- Mwenye maarifa ana ukomavu wa moyo kiasi kwamba anapokutana vishawishi vya mali, umaarufu na matamanio, husema "ninajilinda kwa Mwenyezi Mungu."[38]
- Mwenye maarifa hutambua kuwa yeye si chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Mwenye kujua hutambua kuwa hajui chochote.
- Mwenye maarifa huepukana na ujinga na anatambua anachotakiwa kukijua.

38. Tazama, Yusuf, 12:23.

- Mwenye maarifa hupata furaha kwa kuwahurumia, kuwahudumia wengine na kuwa mnyenyekevu, kwa maana haya ni matunda ya imani, na hufurahia ladha na utamu wa imani.

- Mwenye maarifa huustaajabia umaridadi na uzuri wa uumbaji wa Mwenyezi Mungu katika ulimwengu.

- Mwenye maarifa huijua lugha ya ulimwengu, kwa sababu kila kitu huzungumza na yule mwenye maarifa.

- Mwenye maarifa huuona uelewano kati ya uwezo wa akili na ule wa moyo.

- Mwenye maarifa daima hushuhudia upendo na unyoofu vikitiririka kutoka katika imani yake.

- Mwenye maarifa huwanufaisha wengine maarifa aliyonayo ya kumjua Mwenyezi Mungu.

- Mwenye maarifa huhama kutoka kwenye sababu kwenda kwa Msababishaji, kutoka kwenye taathira kwenda kwa Mwenye kuathiri, kutoka kwenye usanifu kwenda kwa Msanifu.

- Mwenye kumjua na kumtambua Mola wake ndani ya moyo wake hukitambua kila kitu. Asiyemjua hawezi kujua chochot, kwa maana watu huwa wajinga pindi nyoyo zao zinapokuwa vipofu.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ambaye ndiye mbora wa wanaomjua Mwenyezi Mungu, anasema: “Lau mngejua ninayoyajua, basi mngecheka kidogo na kulia sana…Mngeenda jangwani na kumuomba Mwenyezi Mungu kwa vilio vya dhati.” (Ibn Mâja, Zuhd, 19)

Pindi khalifa wa pili, Omar ﷺ alipofariki dunia, Abdullah ibn Mas’ud ﷺ alisema, “Mtu wa tisa katika watu kumi wenye maarifa na elimu ametutoka.”

Maswahaba wengine wakasema: "Lakini bado wapo wenye elimu kati yetu!"

Lakini Ibn Mas'ud ﷺ akasjibu, "Ninazungumzia kuhusu elimu ya ndani, sio elimu ya nje."

Katika Qur'an Tukufu, Mwenyezi Mungu anasema:

"...Kwa hakika wanao mcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wanazuoni." (Fâtir, 35:28)

Kama aya hiyo tukufu inavyosema, elimu ambayo haihusishi hisia ya kujisalimisha na kumhofu Mwenyezi Mungu ndani ya moyo wa mtu sio elimu yenye kumfurahisha Mwenyezi Mungu Mtukufu, sifa ambayo imetajwa ndani ya Qur'an na Hadith za Mtukufu Mtume ﷺ.

Kwa hakika sayansi za kidunia zinahitajika pindi zinapotumika vizuri. Sayansi za kidunia, kati maendeleo yake, zimemfanya mwanadamu apate ushahidi mpya wa utukufu na ukuu wa Mwenyezi Mungu. Hivyo zinamfanya mwanadamu kuutambua umaridadi na usanifu wa Mwenyezi Mungu na siri zake za ajabu kabisa. Katika muktadha huu, kazi za sayansi, kuanzia kwenye astrofizikia (sayansiya hali ya nyota kikemikali na kimaumbile), jenetikia mpaka kwenye maajabu yaliyofanikishwa na teknolojia, kazi zote za kitaalamu na matumizi yake, ni ugunduzi chemchem ya uwezo na ukuu wa Mwenyezi Mungu katika ulimwengu.

Katika Qur'an Tukufu, Mwenyezi Mungu anasema:

"Tutawaonyesha Ishara zetu katika upeo wa mbali na katika nafsi zao wenyewe mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli. Je! Haikutoshi kwamba Mola wako Mlezi kuwa Yeye ni Shahidi wa kila kitu?" (Fussilat, 41:53)

Hatua ya kutafuta elimu ni kujifunza siri za ulimwengu wa kimaada (physical) na kimaanawi (metaphysical) ili kuweza kufikia hatua ya juu zaidi ya kumjua Mwenyezi Mungu Mtukufu. Pamoja na kukiri uwepo wa Muumba, moyo wa mtu unatakiwa kuona namna uwezo wa Mwenyezi Mungu unavyofanya kazi ndani ya vitu na kushuhudia adhama yake ndani ya vitu hivyo. Ni masikitiko makubwa kuwa baadhi ya nyoyo zina maradhi mazito ya ujinga kiasi kwamba haziwezi kuuona usanifu wa Mwenyezi Mungu licha ya maendeleo makubwa ya sayansi na ugunduzi mwingi unaendelea kufikiwa.

Wale wanaofanya dhulma kwa kuitumia vibaya elimu yao kwa maslahi na manufaa binafsi wanaifanyia khiyana elimu yenyewe. Hii ina maana kwamba wanatumia vibaya akili na nyoyo zao wenyewe. Ili elimu iwe yenye manufaa, akili na utashi unaotokana na nayo vinatakiwa kulelewa na Qur'an Tukufu na mafundisho ya Mtukufu Mtume ﷺ. Hapo kutafuta elimu kunaweza kuwa tiba ya maradhi ya nafsi na udhaifu ambayo yanamtesa mwanadamu. Msomi akikosa malezi hayo ya mafundisho ya kidini, elimu yake inaweza kumpeleka kwenye njia hatari kiasi kwamba akawa sababu ya watu kupotea.

Kwa bahati mbaya, leo hii mwanafunzi anapofanyiwa mtihani kuamua kama anaweza kuendelea mbele zaidi katika masomo yake au la, kigezo pekee kinachoangaliwa na kukubaliwa ni uwezo wa kiakili. Hakuna anayejali kuuliza kama mwanafunzi ana sifa na uwezo wa moyo utakaomuwezesha kubeba dhima za elimu anayotaka kujifunza. Lakini , kusoma kitu kwa nje hakutoshi kufanya mtu kupata furaha na wokovu wa milele.

Chukulia mfano wa mwanafunzi wa sheria. Masomo yake yasipoongozwa na elimu au maarifa ya kiroho, anaweza kuunga mkono dhulma na ukatili kwa kutumia elimu yake ya sheria, badala ya kuunga mkono haki na uadilifu. Au chukulia mfano wa mwalimu

wa tiba: anaweza kugeuka kuwa mtaalamu wa kuua badala ya kuwasaidia watu kupona! Meneja mwenye kipawa cha kiakili cha kujifunza biashara, akikosa hisia ya huruma na upendo, anaweza kuishia kuwa dhalimu dhidi ya wafanyakazi wake. Watu hao, kwa kutumia elimu zao, wanaweza kusababisha madhara makubwa kuliko watu wasiokuwa na elimu na ambao hawawezi kuzalisha…Na kama wakiitumia elimu yao vibaya, wanaweza kuishia kwenye hasara na majuto ya milele.

Mawlana Jalaluddin Rumi (q.s) anaibainisha nukta hii ndani ya *Mathnawi*:

Mtu mwenye kipawa anaweza kuhusudiwa. Lakini lizingatie tukio la Ibilisi, na (kama elimu yako haielewani na moyo wako) usivutwe sana na nafsi yako. Usisahau kuwa Ibilisi aliyelaaniwa alikuwa mmoja wa viumbe waliokuwa karibu zaidi na Mwenyezi Mungu kwa maelfu ya miaka: alikuwa kiongozi wa malaika. Lakini alitakabari kwa elimu na ibada yake, na hivyo akachukua mwenendo mbaya kuhusu suala la kuumbwa kwa Adamu ﷺ. Ibilisi alimdharau Adamu, na matokeo yake akalaaniwa.

Iwapo elimu unayoitafuta itakuongoza kwenye ukweli, uhakika, uchamungu na matendo mema, basi hiyo ni elimu yenye manufaa. Tusisahau kuwa Ibilisi alikuwa na elimu, na Qaruun (aliyetengeneza Ndama wa Dhahabu) naye pia alikuwa na elimu. Lakini elimu zao ilighilibiwa na nafsi zao na kuwafanya watakabari na kujiona mno. Walishindwa kuyadhibiti matamanio yaliyotokana na nafsi zao, wakajiamini kupita kiasi.

Kwa hakika, elimu inayomfanya mtu awe mwenye majivuno na kiburi na kumpeleka kwenye hali ya kukata tamaa, kwa nje inaweza kuzalisha vitu vizuri na vyenye manufaa. Je hii si dhama kubwa? Ndiyo maana pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alipokuwa akimuomba Mwenyezi Mungu ampe elimu, alikuwa akisema: “Mola

wangu! Nijaalie elimu yenye mafia! Ninajilinda kwako na elimu isiyokuwa na manufaa." (Muslim, Dhikr, 73)

Kuna aina tofauti tofauti za elimu yenye manufaa. Kama ambavyo elimu ya matumizi ya msingi ya Kiislamu (*fiqh*) ni ya lazima, vivyo hivyo elimu kuhusu kurejea kwa Mwenyezi Mungu, udhati wa moyo na kujiepusha na unafiki nayo pia ni ya lazima. Iwapo mtu ataipuuza hiyo ya pili, anaweza kujuta huko Akhera. Wale wasiopatata elimu yenye manufaa zaidi, hata kama watakuwa wanajua vitu vingi kiasi gani, huwa hawawezi kufika kwa Mwenyezi Mungu.

Imam Ghazali anaonya dhidi ya matumizi mabaya ya muda na nguvu wakati wa kutafuta elimu:

Elimu unayosoma inatakiwa iwe na uwezo wa kuuangaza moyo wako na kuipendezesha tabia yako. Chukulia kwamba umebaki na wiki moja katika uhai wako. Kwa muda huo uliobaki, utaigeukia elimu yenye manufaa. Utaitafakari hali yako, utakata mahusiano yako na matamanio ya dunia na kujaribu kuwa mtu bora kabisa kuliko zamani. Lakini ni jambo lisilokuwa na shaka kwamba siku yoyote tunaweza kufa. Vivyo hivyo, masomo unayopendelea kujishughulisha nayo yanatakiwa yawe na uwezo wa kukufanya kuutambua ukuu wa Mwenyezi Mungu na kukuongoza kwenye kuimarisha hali yako ya kiroho.

Utafutaji wa elimu unahitaji kuvumilia tabu na shida mbalimbali, lakini thamani yake huoenakana inapotekelezwa katika maisha. Kutafuta elimu bila kuitekeleza ni kazi duni inayokuweka chini ya jinamizi la mzigo usiokuwa na manufaa. Humfanya msomi awe kuli, au kama isemavyo Qur'an "*punda aliyebeba vitabu*."[39] Elimu isipomeng'enywa vizuri na kutumiwa, kama haiwezi kuziathiri tabia zetu, kama haiwi sehemu ya shakhsia (personality) yetu na

39. Tazama Jum'ah, 62:5

kufikia kiwango cha kumtambua Mwenyezi Mungu, kama haimuelekezi na kumuongoza mja kwenye kuwa na soni, unyenyekevu na kuondosha kiburi, basi haitakuwa yenye manufaa na nguvu zote zilizotumika kuitafuta huwa zimepotea bure.

Tunapswa kukumbuka kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu aliuweka ukweli na siri zote ndani ya Qur'an Tukufu. Asili ya elimu zote imo ndani ya Qur'an. Chochote kinachopatikana ulimwenguni, *"kinyevu au kikavu,"* (An'am, 6/59) kimo ndani ya khazina ya Qur'an Takatifu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasma:

"Arrah'man, Mwingi wa Rehema Amefundisha Qur'ani. Amemuumba mwanaadamu, Akamfundisha kubaini." (Rahmân, 55:1-4)

Qur'an Takatifu imebeba muongozo na ujumbe mpya kabisa wa Mwenyezi Mungu kwenda kwa wanadamu. Aina ya elimu ambayo umma wetu na ulimwengu unaihitajia zaidi, leo, ni aina ya elimu inayopatikana ndani ya Qur'an Takatifu. Ndiyo maana tunapaswa kuweka uzito mkubwa kuisoma na kujifunza kikamilifu. Lakini, ili kuielewa Qur'an kikamilifu lazima uingie katika ulimwengu wake wa kiroho, na lazima uwe na uchamungu, ambayo ni sifa ya moyo. Qur'an Takatifu inawaonya waumini ikisema:

"...wanapo kumbushwa Ishara za Mola wao Mlezi hawajifanyi viziwi nazo, na vipofu." (Furqân, 25:73)

"Na bila ya shaka tumewapigia watu mifano ya kila namna katika hii Qur'ani ili wapate kukumbuka." (az-Zumar, 39:27)

Hivyo, Qur'an Takatifu inatutaka tutengeneze uhusiano madhubuti baina yake na sisi. Lakini ili kutengeneza uhusiano huo, ni lazima tuzitakase nyoyo zetu kama tunavyoitakasa miili yetu kwa ajili ya ibada. Na ili tuweze kufanya hivyo, tunahitaji malezi ya kiroho. Pia Qur'an inatwambia:

"Je! Hawaizingatii hii Qur'ani? Au kwenye nyoyo (zao) zipo kufuli?" (Muhammad ,47:24)

"Hakika amefanikiwa aliye itakasa." (Shams, 91:9)

Muongozo wetu, Qur'an Takatifu, inatuita kwenye tafakuri. Kwa kuwa Qur'an inatangaza ujumbe wa Mwenyezi Mungu, baadhi ya watu, ambao wapo karibu na Mwenyezi Mungu kiroho, huuelewa ujumbe wake vizuri zaidi kuliko wengine. Qur'an Takatifu inasema:

"...Basi mcheni Mwenyezi Mungu; Mwenyezi Mungu atakufundisheni..." (Baqarah, 2:282)

Ndiyo maana kila aya ndani ya Qur'an inakuwa wazi kwetu kulingana na daraja na kiwango cha moyo wetu.

Katika Qur'an Takatifu, Mwenyezi Mungu anauonyesha umma wote kupitia kwa Mtukufu Mtume ﷺ:

"...ukifuata matamanio yao baada ya kukujia ilimu hii, hutakuwa na rafiki wala mlinzi mbele ya Mwenyezi Mungu." (Ra`d, 13:37)

Hatua ya Mola wetu kuisifia Qur'an Takatifu kuwa ni "elimu" inaonesha kuwa somo la kwanza la wajibu kwa Waislamu ni Qur'an, na utamaduni uliojengwa kwenye msingi wa Qur'an. Hakuna maisha sahihi ya kielimu katika Uislamu yanayoweza kukubaliwa bila kurudi kwenye Qur'an. Kwa bahati mbaya, baadhi ya watu katika zama zetu wameyashusha hadhi mafunzo ya Qur'an na kulifanya kuwa jambo la ziada.

Ni jambo la kusikitisha sana kwamba baadhi ya Waislamu hudhani kwamba mafunzo ya Qur'an tunayowapa watoto wetu hayatakiwi kupewa uzito na kwa muda mrefu. Wanapendelea program za muda mfupi kama vile masomo ya majira ya joto au kozi

za mwisho wa wiki, kana kwamba wanajaribu kuondosha mzigo usiotakiwa. Vilevile wazazi wanapuuza kuwafanya watoto wao watekeleze kwa vitendo mafunzo ya Qur'an Tukufu. Wanaweka msisitizo kwenye usomaji tu, lakini sio kwenye maelekezo na mfundisho ya Qur'an.

Kuishusha thamani Qur'an Takatifu, ambayo ni neema kubwa kabisa ya Mwenyezi Mungu kwa mwanadamu, na kuzidharau shule za Qur'an huku tukiyathamini zaidi masomo ya vitu vingine, ni kutafuta mustakbali angavu katika kichochoro chenye giza. Kwa maana mwanadamu anahitajia zaidi virutubisho vya kiroho na kimaanawi kuliko anavyohitajia virutubisho vya kimwili na kimaada.

Uzuri ulioje wa maneno ya Mawlana Rumi:

Usipupie kuulea mwili kupita kiasi. Mwisho wa mwili huo ni kafara itakayotolewa kwa ardhi. Ilee roho yako kwa maana ni roho yako ndiyo itakayopata heshima na kufika katika viwanja vitukufu. Usiupe mwili wako mafuta au vitu vitamu kupita kiasi, kwa sababu wanaoupa chakula kupita kiasi hutumbukia katika shimo la kutekeleza haja za kinafsi na mwishoni hupata fedheha. Upe moyo wako chakula cha kiroho. Upe tafakuri zilokomaa, hukumu za sawa na maandalizi ya kiroho ili iweze kufika mwisho wa safari yake ikiwa kama msafiri wa milele aliye imara na mwenye nguvu.

Matamanio ya kidunia ni mfano wa minyororo inayoyafunga maisha yetu ya kiroho. Kama moyo wako umejazwa tamaa za nafsi, huwezi kufika mbele ya Mwenyezi Mungu. Kuyapendelea matamanio ya kidunia ni mfano wa jiwe lililofungwa mgongoni mwako: kwa muda wote litakapokaa hapo hutaweza kuogelea wala kuruka. Muislamu asipojishughulisha na ukweli, atajishughulisha na uongo. Sa'di wa Shirazi amelielezea hili vizuri kabisa: "Roho za walioghafilika ambao hufuata matamanio yao ya kihayawani hujichafua zenyewe."

Utakuwa unajikanganya sana kutafuta furaha kwa kufanya matendo machafu yaliyo kinyume na maadili! Lengo litakalotuhakikishia furaha yetu ya baadaye sio kupata vyeti tunavyopewa na wanadamu kama sisi, bali radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mwenyezi Mungu anaonya:

"...Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye khazina za mbingu na ardhi, lakini wanaafiki hawafahamu." (Munafiqûn, 63:7)

Tusisahau: Moyo utakaozitengeneza jamii sio moyo wa majebi yenye ubinafsi ambayo huhifdhi vitabu vingi, bali moyo wa wale wanaozitanua nyoyo zao kwa hekma itokayo ndani ya Qur'an na ambao ni chanzo cha huruma na amani ya jamii. Huo ni moyo wa wale wanaomcha Mwenyezi Mungu, na waumini wanaopenda kuwahudumia wengine.

Mshairi Mehmet Akif anaelezea dawa inayoweza kutibu matatizo ya mwanadamu:

Kwa kuchota muongozo wa moja kwa moja kutoka kwenye Qur'an,

Tunaweza kuzifundisha zama hizi kuijua thamani ya Uislamu...

Mola wetu! Tunakuomba utulinde dhidi ya mateso ya wale wanaouchukua uchafu kuwa ndiyo furaha, kwa sababu ya kukosa furaha ya kweli itokayo katika Qur'an! Tujaalie fursa ya kuzihesabu nafsi zetu kabla hujatuhesabu siku ya Kiyama na utujaalie kuwa waja wenye nyoyo zenye ukomavu! Tulinde tusiyafanyie israfu na kuyapoteza maisha yetu ya milele kwa tamaa zetu za mpito na ujinga wetu katika dunia hii!

Amiin…

SURA YA 15

Israfu - 4

Katika maadili

Mola wetu ametuagiza tuyapangilie maisha yetu kulingana na kanuni njema za kimaadili, kwamba tuishi na nyoyo zenye kuitambua hadhi ya kuwa wanadamu. Mwenyezi Mungu Mtukufu ametupambanua sisi na viumbe wengine kwa maadili mema yenye kusifika, kwa sababu kwa upande wa viumbe wengine, tafakuri ya kimaadili ni jambo lisilowezekana.

Maisha ya kidini bila uendelezaji wa maadili ni jambo lisilowezekana kabisa. Kuwa na imani bila kuiwekea ulinzi wa tunu za kimaadili ni kama kuwasha mshumaa katika upepo bila kuulinda kwa kioo. Imani hiyo isiyolindwa daima itakuwa katika hatari kubwa kabisa mbele ya matamanio ya kidunia na vishawishi vya Shetani.

SURA YA 15

ISRAFU– 4

Katika maadili

Tunu za kimaadili ni sifa njema za kitabia ambazo Mwenyezi Mungu anazikubali na anapenda kuziona katika matendo yetu. Ni miongoni mwa zawadi zenye thamani kubwa kabisa ambazo mwanadamu amejaaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hadith moja ya Mtukufu Mtume ﷺ inasema, "Jipambeni kwa sifa za Mwenyezi Mungu." (Munâwî, at-Ta`ârif, uk.564) Hivyo tabia njema kielelezo cha sifa nzuri za Mwenyezi Mungu.

Kwa muktadha huu, kuwa na tabia njema ni dhima yetu kama waja, na ni miongoni mwa alama kubwa kabisa zinazoonesha ukaribu wetu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tabia njema hutengeneza na kuonesha hadhi na daraja kubwa kabisa ya wanadamu. Ndiyo maana kushughulika na tabia njema ni sifa inayomtofautisha mwanadamu na viumbe wengine wote.

Binadamu kamili huonesha mifano safi ya usanifu wa Mwenyezi Mungu katika ulimwengu huu wa majaribu. Mtu huyo husimama kwenye kilele cha uumbaji. Mwanadamu ambaye ni kiumbe wa aina yake mwenye vilele visivyofikika na vina visivyopimika,

anaweza kuilinda thamani yake ya juu ndani ya ulimwengu kwa kujitoa kwa dhati kuwa mja anayeangazwa na tunu za kimaadili.

Moyo ni bahasha ambayo ndani yake tunu za tabia njema zimetunzwa. Umeumbwa na kujaaliwa uwezo wa kufikia hatua ya kuwa kioo kinachotazamwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa kuwa na uwezo huo, ni jambo la kusikitisha sana kama watu wanatumia uhai wao wote wakiyatafuta matamanio ya mpito na kuacha kuzipa nyoyo zao nuru wa maadili. Safari yao hiyo huishia kuisaliti hadhi ya mwanadamu inayomstahiki mja wa Mwenyezi Mungu. Watu hao hupoteza daraja ya juu waliyochaguliwa na Mola wao. Hii ina maana kwamba japokuwa mwanadamu ameumbwa katika umbile bora kabisa kuliko viumbe wengine wote, na Mwenyezi Mungu akampa daraja tukufu, bado watu wanaweza kuitumia vibaya na kuipoteza kabisa nafasi hiyo.

Lengo la elimu ya maadili ni kutusaidia kufikia nafasi yetu, yaani mwanadamu kamili, kwa kuendelea kutukumbusha kwamba muda wote tunaangaliwa na Mwenyezi Mungu na pia kwa kututakasa dhidi ya sifa chafu. Inalenga kupandikiza sifa tukufu ndani ya nyoyo za watu, kama vile usafi, utambuzi, wema, ukarimu, staha na huruma, ili ziweze kustawi ndani maumbilie yetu ya asili. Kwa muktadha huu, maadili ni kiungo cha lazima cha imani na dini; ndiyo moyo na msingi wake. Kwa kuutambua ukweli huu, kiongozi wetu Mtukufu Mtume ﷺ, ambaye Mwenyezi Mungu amemuelezea kuwa alitumwa kuwa *rehma kwa walimwengu,* yeye mwenye anaielezea kazi yake kuwa: “Nimetumwa kuja kukamilisha tabia njema.” (Muwatta’, Husn al-Khulq, 8)

Kwa hali hiyo, Maisha ya kidini bila uendelezaji wa maadili ni jambo lisilowezekana kabisa. Kuwa na imani bila kuiwekea ulinzi wa tunu za kimaadili ni kama kuwasha mshumaa katika upepo bila kuulinda kwa kioo. Imani hiyo isiyolindwa daima itakuwa katika

hatari kubwa kabisa mbele ya matamanio ya kidunia na vishawishi vya Shetani.

Tunu za kimaadili huilinda dini na imani yetu kama ngao ya kiroho. Mtume wetu ﷺ, fakhari ya ulimwengu, anasema, "Jibril aliniambia kuwa Mwenyezi Mungu anasema: 'Dini hii ni dini niliyoichagua kwa ajili Yangu. Kwa dini hii, ukarimu na wema ni vitu muhimu zaidi. Kwa muda wa maisha yako kama Muislamu, iinue dini hii kwa vitu hivi viwili!" (Haythamî, VIII, 20; Ali- al-Muttaqî, Kanz, VI, 392)

Huo ndio umuhimu wa tabia njema kwenye dini yetu. Maisha yasiyoongozwa na tunu za kimaadili hujiharibu na kuiharibu dini. Lakini wale ambao nyoyo zao zina fungu katika maadili huifikia furaha inayotokana na kuonja ladha na utamu wa kweli wa imani. Ufuatao ni mfano wa jinsi tabia njema inavyokuwa kama daraja la kiroho kwa mwanadamu.

Kuna swahaba aitwaye Hakim ibn Hizam ambaye alijitahidi sana kuwa na tabia njema. Alikuwa ndugu wa bibi Khadijah رضي الله عنها. Hakim alikuwa mkarimu na mwenye huruma mno, na alikuwa akipenda kuwasaidia watu wengine. Wakati huo, katika zama za Jahiliya, ilikuwa ni ada na desturi kuwazika watoto wa kike wakiwa hai. Hakim alikuwa akiwanunua watoto hao ili kuwalinda wasiuawe. Siku moja alimuuliza Mtukufu Mtume ﷺ: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Katika kipindi cha kabla ya Uislamu nilifanya matendo mema, kama vile kutoa sadaka, kuwaacha huru watumwa na kuwatembelea jamaa. Je, nitapata thawabu kwa matendo hayo?"

Mtukufu Mtume ﷺ akajibu: "Matendo mema uliyoyafanya hapo zamani ndiyo sababu ya kupata heshima ya kuingia katika Uislamu!" (Bukhârî, Zakâh, 24; Muslim, Îmân, 194-196)

Kuna mifano mingine mingi inayoonesha uhusiano mkubwa baina ya tabia njema na imani. Tunakumbuka wachawi wa Fir'auni, aliyedai kuwa ni Mungu, walipoletwa kuja kushindana na Musa عليه السلام. Kabla ya mashidani hayo, wachawi hawakuwa na wazo la kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu. Lakini walibahatika kupata fungu katika siri ya tabia njema kuwa ndio ufunguo wa imani. Walikuwa na adabu kwa kuanza kuonesha ufundi wao wakati wa kushindana na Musa. Hili litakuwa lilimfurahisha Mwenyezi Mungu, kwa sababu wakati huo walianza kuegemea upande wa Nabii huyo. Na baadaye, baada ya kushuhudia miujiza, nyoyo zao zilitoa mwangwi wa hali ya juu uliofanya wapate heshima ya kuwa waumini – imani imara mno kiasi kwamba walikuwa tayari kuyatoa maisha yao kwa ajili yake.

Fir'auni na wapambe wake nao pia waliishuhudia miujiza iliyowafanya hao wachawi kuamini. Lakini miujiza hiyo hiyo iliwafanya wapambe wa Fir'auni kung'ang'ania msimamo wao wa kumkana Mwenyezi Mungu. Mwishowe, Fir'auni aliwaua kikatili wachawi waliomumini Musa, na hivyo wakafikia daraja ya kufa kishahidi. Vilevile walipata neema nyingine kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kwa maana kisa chao kimetajwa ndani ya Qur'an Tukufu na hivyo wataendelea kuwa kumbukumbu tukufu kwa waumini wote mpaka Siku ya Kiyama.

Kwa hiyo, manufaa ya kiroho yatokanayo na tunu za kimaadili kama vile wema, umaridadi, usafi wa moyo, ukarimu na huruma hupata kuonekana wazi. Tabia njema ni jambo muhimu sana katika kukubaliwa na Mwenyezi Mungu kiasi kwamba huwasaidia wale wenye nayo kupata imani, ambayo ndiyo neema yenye thamani zaidi kuliko zote. Fikiria jinsi uendelezaji wa tabia njema unavyoweza kuwasaidia wale wenye imani kukwea kwenye kilele cha juu cha kiroho!

Kwa upande mwingine, tabia za kifasiki hupelekea kuziharibu jamii na kuibua masaibu mengi mazito na kisha hasara kubwa huko Akhera. Maisha ya amani ya mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla yatawezekana tu kwa kuvilea vizazi vya baadaye katika maadili mema. Tunahitaji kizazi chenye Uchamungu kinachoipenda nchi yao na kina umaridadi na usafi wa moyo. Kama asemavyo Muhammad Iqbal: "Waislamu wana dhima kwa njia ambayo dunia inapitia sasa."

Kwa muktadha huu, Mola wetu ametukataza tusiwafuate wale wanaoangukia katika wendawazimu wa israfu kwa kuvuka mipaka ya tabia njema.

"Wala msit'ii amri za walio pindukia mipaka, ambao wanafanya ufisadi katika nchi, wala hawatengenezi." (ash-Shu'arâ, 26:151-152)

Katika aya nyingine Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Kwa hakika wale wanao penda uenee uchafu kwa walio amini, watapata adhabu chungu katika dunia na Akhera. Na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui." (an-Nûr, 24:19)

Ukosefu wa haya/soni na adabu, ambayo ni miongoni mwa tunu muhimu mno za kimaadili, ni matukeo ya udhaifu wa imani na mmommonyoko wa kidini. Mtukufu Mtume ﷺ alielezea uhusiano uliopo kati ya tunu za kimaadili na imani pale aliposema kuwa "Haya ni sehemu ya imani." (Bukhârî, Imân, 3) Basi, wale wanaohamasisha kushuka kwa maadili, kama vile kuenea kwa hali ya utovu wa haya na uchafu katika jamii, huwa wamefanya kosa hatari sana dhidi ya imani ya jamii hiyo. Kwa hakika, lengo la kwanza la dini yoyote ya kweli ni kueneza imani ya Mungu mmoja duniani kote, na lengo la pili ni kutengeneza muundo wa kijamii unaoundwa na maadili mema.

Historia ya dunia imeshuhudia matukio mengi ambapo adhabu ya Mwenyezi Mungu iliwashukia wale ambao hawakuziheshimu tunu za kimaadili na wakapindukia mipaka. Hivyo, historia imejaa mafunzo kwa wale wenye kuzingatia. Inatosha kujifunza kwa kusafiri duniani kutafuta ishara hizo zenye mazingatio. Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Qur'an Tukufu:

"Je! Hawatembei katika ardhi ili wapate kuwa na nyoyo zao za kuzingatia, au masikio ya kushikilia? Kwani hakika si macho yanayo pofuka, lakini zinazo pofuka ni nyoyo ziliomo vifuani." (Hajj, 22:46)

Jamii inapoangukia katika wazimu wa israfu kwa kupindukia mipaka yao wenyewe ya tunu za kimaadili, ni moja ya alama za ujio wa Siku ya Hukumu, ambayo ni maangamizi ya dunia nzima. Hicho ni kiwango cha hatari kinachoambatana na israfu ya tabia ya mwanadamu. Kuna hadith nyingi za Mtukufu Mtume ﷺ zinazotueleza kuhusu utovu wa maadili na kupindukia mipaka ambako kutatokea wakati Siku ya Hukumu itakapokuwa ikikaribia. Ifuatayo ni mifano michache tu:

"Zitakuja zama ambazo juhudi na nguvu zote za watu zitaelekezwa kwenye matumbo yao. Mtu mtukufu ataangaaliwa kwa msingi na kigezo cha mali. Wanawake ndio watakaokuwa qibla cha swala zao, na pesa ndiyo itakayokuwa dini yao. Tahadharini! Hao ndiyo viumbe hatari kabisa. Hawatakuwa na nafasi mbele ya Mwenyezi Mungu." (Ali al-Muttaqî, Kanzu'lUmmâl, XI, 192/31186)

"Zitakuja zama ambazo watu hawatajali kama chumo lao ni la halali au la haramu." (Bukhârî, Buyû', 7)

"Zitakuja zama ambazo wale watakaosema ukweli watakataliwa na wale watakaosema uongo watakubaliwa. Wale wenye kuaminika wataonekana kuwa wahaini, na wahaini watakuwa wenye

kuaminika. Watu watatoa ushuhuda bila kuitwa, kutoa viapo bila kutakiwa kufanya hivyo.” (Tabarânî, XXIII, 314)

“Zitakuja zama ambazo watu wataacha kutekeleza dhima yao ya kuamrisha mema na kukataza mabaya.” (Haythamî, Majma`az-Zawâ’id, VII, 280) Kwa maana kwamba hawatahamasisha matendo mema na kukataza matendo mabaya.

Na siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema: “Zitakuja zama ambazo nyoyo za waumini zitayeyuka kama chumvi inavyoyeyuka ndani ya maji!”

Wakauliza, “Kwa nini ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?”

Akajibu: “Kwa sababu hawataweza kuondosha uovu wanaokutana nao.” (Ali a-Muttaqî, Kanz, III, 686/8463)

Abdullah ibn Umar رضي الله عنه anasimulia:

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alitugeukia na kusema: “Enyi *Muhajiruun* (Waislamu waliohama kutoka Makka)! Kuna mambo matano ambayo ninamuomba Mwenyezi Mungu yasiwapate. Mambo hayo ni:

1. “Zinaa ikienea katika jamii kiasi cha kufanywa waziwazi, maradhi mbalimbali kama vile tauni, na mengine ambayo hayakuwahi kushuhudiwa kabla, yataenea baina watu hao.” (Kwa maoni yangu, maradhi kama Ukimwi yanaweza kuwa yanathibitisha onyo hili lililotolewa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.)

2. “Pindi watu watakapofanya upunjaji katika vipimo vya biashara zao watakumbwa na njaa, kupoteza maisha, na dhulma kutoka kwa watawala wao.

3. “Watu watakapoacha kulipa Zaka ya mali zao watanyimwa mvua. Kama si kwa sababu ya wanyama, Mwenyezi Mungu asingewapa hata tone moja la mvua.

4. "Watu hao watakapoacha kutekeleza ahadi zao kwa Mwenyezi Mungu na kuacha kufuata mwenendo wa Mtume Wake watatumiwa maadui wa nje watakaozitwaa mali zao.

5. "Pindi viongozi watakapoacha kufuata muongozo wa Qur'an wakajichagulia wanayopenda, Mwenyezi Mungu atawaadhibu kwa adhabu itokayo miongoni mwao wenyewe." (Ibn Mâja, Fitan, 22; Hâkim, IV, 583/8623)

Mwenyezi Mungu Mtukufu ametoa maonyo mengi ndani ya Qur'an Tukufu ili tusiangukie katika hali hizo. Pia ametukumbusha kwamba hatujaachwa tu, bali muda wote tunaangaliwa:

"Hatamki neno ila karibu yake yupo mwangalizi tayari." (Qâf, 50:18)

Hivyo basi Mwenyezi Mungu anatutaka tuwe macho na tuchunge mipaka ya Mwenyezi Mungu katika tabia zetu. Anataka tuache kupindukia mipaka, tuache ushenzi, kufanya kupita zaidi ya kiasi na chini zaidi ya kiasi, tuache kujishughulisha na mambo yasiyokuwa na faida yatakayoyaharibu maisha yetu…

Kuna aya nyingi ndani ya Qur'an Tukufu zinazotuagiza kuwa na kiasi katika matendo yetu na kutuusia kuwa na rasilimali za maadili mema. Ifuatayo ni baadhi ya mifano:

"…Na ambao hujiepusha na mambo ya upuuzi…" (Mu'minûn, 23:3)

"Na ushike mwendo wa katikati, na teremsha sauti yako. Hakika katika sauti mbaya zote bila ya shaka iliyo zidi ni sauti ya punda." (Luqmân, 31:19)

Kwa hakika ufidhuli ni miongoni mwa mambo ambayo humpelekea mwanadamu kupoteza tabia njema. Ufidhuli hutokana kuzitelekeza sifa njema za kimaadili kama vile utambuzi na wema. Ni kama kuyakana maumbile ya mwanadamu, kuyaacha yale

yanayotufanya tuwe wanadamu, kama mfano wa punda aliyetajwa ndani ya Qur'an Tukufu unavyoonesha.

Adabu ya maongezi inayomfaa mwanadamu ni kutumia msemo wa Qur'an, *qawl layyin*: lugha laini. (Tâhâ, 20:44) Mwenyezi Mungu Mtukufu alipomtuma Nabii Musa ﷺ kwenda kwa Fir'auni alimwambia atumie kauli laini. Na Mola wetu anasema:

"Waambie waja wangu waseme maneno mazuri, maana Shet'ani huchochea ugomvi baina yao. Hakika Shet'ani ni adui aliye dhaahiri kwa mwanaadamu." (Isra', 17:53)

Kwa maana hiyo, Mwenyezi Mungu anatukumbusha kuchunga kanuni za adabu wakati wa kuzungumza na watu. Katika aya nyingine, Mwenyezi Mungu anaelezea moja wapo ya kanuni hizo, japokuwa anamwambia Mtukufu Mtume ﷺ:

"Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungeli kuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia." (Âl-Imrân, 3:159)

Kwa upande mwingine, muumini anatakiwa kuwa na mwendo wa katikati katika maadili yake kama ilivyo katika mambo mengine. Mwenendo huwa mzuri pale unapokuwa wa katikati, na huwa mbaya pale unapopindukia au unaposhuka chini zaidi katika utekelezaji.

Kwa mfano, unyenyekevu ni jambo zuri. Lakini mtu akizidisha katika kuonesha unyenyekevu hubadilika na kuwa majisifu. Hii ni kupindukia mpaka katika kuonesha unyenyekevu.

Kuna watu ambao hutaka kuwaonesha watu wengine kuwa wana unyenyekevu: moja kwa moja haya ni majisifu. Ni unafiki kutumia maadili kwa ajili ya kutaka kitu fulani. Kwa hakika ni unafiki wa wazi kujionesha kuwa una unyenyekevu na ni jambo

linalopingana na maadili. Kwa mfano, angalia maneno haya: "Huwa natumia muda wa siku tatu pekee kuisoma Qur'an yote." "Niliweza kujenga msikiti mmoja tu kwa sababu ya umaskini" au "niliwapa chakula watu kadhaa wa kadhaa." Yote haya ni maneno yanayoonesha unafiki na ufakhari chini ya kivuli cha unyenyekevu. Pia kujinyenyekeza mbele ya mtu mwenye kiburi asiyestahili kuoneshwa heshima, kiasi kwamba unajifedhehesha, nayo ni aina nyingine ya matumizi mabaya ya unyenyekevu.

Kujiweka mbali sana na watu kwa ajili ya kulinda heshima yako na ukaribu uliopitiliza katika uhusiano wa kibinaadamu na urafiki, hususan katika maisha ya familia, ni israfu katika ukaribu. Hali zote mbili zinaweza kuwa na hasara. Kuna kiwango ambacho pia kinatakiwa kuchungwa wakati wa kuwasaidia wengine. Kutoa msaada kupita kiasi na kutoa kidogo kupita kiasi vinatakiwa kuepukwa kama tunataka kujizuia na israfu.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa makini sana kuhusu suala la heshima na hadhi ya mwanadamu. Anasema: "Yeyote miongoni mwenu asiwaite wale walio chini ya mamlaka yake "mtumwa wangu" au "kijakazi wangu." Nyote ni waja wa Mwenyezi Mungu. Wake zenu pia ni waja wa Mwenyezi Mungu. Mnapowaita watu katika familia yenu, tumieni maneno kama vile "mwanangu," "binti yangu" au "mpendwa wangu." (Muslim, Alfâdh, 13)

Hata hivyo pia, Mtukufu Mtume ﷺ anatuambia tuzungumze na watu waharibifu, ambao wameufisidi ulimwengu kwan yoyo zao na kustahiki adhabu ya Mwenyezi Mungu, kulingana na hadhi yao. "Usimuite mnafiki "bwana". Kwa maana ukimchukulia kama mheshimiwa, utaghadhibikiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu." (Abû Dâwûd, Adab, 83; Ahmad b. Hanbal, V.346)

Hivyo ni wazi kuwa kutumia mienendo ya kimaadili kama vile unyenyekevu na staha katika hali moja tu, bila kuangalia

mazingira, ni kama kuvaa miwani ya macho bila kuangalia maelekezo ya daktari. Huu ni ubadhirifu katika maadili. Kwa hakika, maadili yanatutaka kuyakubali matendo yanayostahiki kukubaliwa, kuyakataa matendo yanayostahiki kukataliwa, na kuamiliana na watu kulingana na nafasi zao. Jambo la muhimu ni kuchunga mizania ya Mwenyezi Mungu na kufuata njia ya katikati katika masuala ya kimaadili kama tunavyopaswa kufanya katika masuala mengine. Hapo ndipo tutakapoweza kuonesha tabia na sifa za Muislamu mwenye ukomavu.

Mtume wetu ﷺ alizitekeleza tunu za maadili ya Kiislamu katika maisha yake kwa namna nzuri iliyojaa staha na utambuzi. Kwa kutumia shakhsia yake tukufu na tabia yake ya mfano aliulea umma wake katika namna nzuri na maridhawa. Kwa mfano, Mtukufu Mtume ﷺ hakuwa akizungumzia makosa ya watu waziwazi. Badala yake, katika mkusanyiko wa hadhara alikuwa akisema, "Nina nini leo, mbona naona hili na hili?" (Bukhârî, Manâqib 25; Muslim, Salât 119) Alikuwa akikosoa jambo kana kwamba macho yake ndiyo yaliyokuwa yanakosea kuliona.

Ufuatao ni mfano mwingine wa njia aliyoitumia kwa umakini katika malezi. Siku moja wakati wa chakula, Mtukufu Mtume ﷺ alibaini kuwa kuna mtu aliyekuwa ametoa hewa chafu. Akasema, "Wale waliokula nyama ya ngamia wanapaswa kuchukua wudhu upya!" Hivyo hakumtaja mtu mmoja. Tendo lisilopendeza likawa jambo lisilofaa, kwa kuwa aliwataka Maswahaba wote waliokuwepo kutawadha upya.[40]

Hakika viwango vya maadili ya Mtukufu Mtume ﷺ daima vilionesha huruma, umakini, usafi na upole. Ndiyo maana alikuwa

40. Ni jambo lenye kuvutia kwamba madhehebu kongwe ya kifiqhi ya Zahiri waliichukulia hadith hii kumaanisha kuwa ulazi wa nyama ya ngamia hutengua wudhu! Inaonekana kuwa wanazuoni hao hawakuelewa hekma iliyokuwa nyuma ya maneno hayo ya Mtukufu Mtume ﷺ.

mpole sana kwa Mabedui waliokuwa wakija kutoka jangwani. Walikuwa wakimuita kwa sauti ya juu, "Muhammad! Muhammad!" Lakini alikuwa akiwaitikia kwa upole, "Karibu tafadhali. Ungependa kuuliza nini?" (Muslim, Nuzur, 8; Abû Dâwûd, Aymân, 21/3316)

Tunatakiwa kuwa kama yeye, tuangalie viwango vya uelewa wa watu pale tunapowaelekeza jambo na kujaribu kuwarekebisha. Pia tunapaswa kuangalia mifano mingine ya Mtukufu Mtume ﷺ katika adabu na maadili mema.

Wakato wa kutoa sadaka ni muhimu mno kuchunga adabu za kutoa. Hili ni jambo muhimu sana linaloonesha tabia njema. Kujiingiza katika matendo mabaya kama vile kuwakumbusha watu msaada wetu tuliowapa, kuwafanya watulipe fadhila, kuzivunja nyoyo zao, kuwaonesha kiburi…yote haya hutufanya tukose thawabu za matendo yetu na hivyo hupotelea hewani. Mababu zetu walikuwa waangalifu sana wasije kupoteza thawabu za amali zao njema kwa njia hii.

Mababu zetu wa Kiuthmaniya walikuwa makini sana kutozivunja nyoyo za walemavu. Walikuwa wakiwaita kwa kusema, "Enyi waheshimiwa!" Kamwe hawakuuchukulia ulemavu kuwa ni adhabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu (kama ilivyokuwa ikiaminiwa na watu wa Ulaya wakati huo), bali waliuchukulia ulemavu kama mtihani kwa wale wenye uwezo, ili kuwaangalia kama watawasaidia. Vilevile mababu zetu waliwasaidia watu wenye ukoma pindi jamii ilipowafukuza. Waliwajengea makazi maalumu yaliyojulikana kama Miskinler Tekkesi (makazi ya maskini).

Vilevile walianzisha taasisi mbalimbali kulinda heshima ya wazee wasiokuwa na ndugu, kwa sababu ya staha na heshima yao watu hao walishindwa kukidhi mahitaji yao wakiwa pamoja na watu wengine. Baadhi ya taasisi ziliwapatia wazee wa kike

sufu/ pamba iliyochambuliwa ili waweze kutengenezea nyuzi na vitambaa. Kisha taasisi hizo huzinunua kazi za wanawake hao kwa bei ya juu, ili wanawake hao waweze kukidhi mahitaji yao kwa kipato cha mikono yao.

Mababu zetu pia walitengeneza masanduku maalumu na kuyaweka msikitini ambapo watu walikuwa wakiweka au kuchukua pesa, kiasi kwamba hakuna anayejua mtoaji na mchukuaji.

Wakati wa usiki walikuwa wakiwapelekea masikini chakula katika vyombo vilivyofungwa, ili hisia za maskini zisiumizwe kwa kujulikana na watu.

Bezmialem Valide Sultan alianzisha taasisi maalumu kwa ajili ya kulipa fidia za vyombo au mali inayoharibiwa na wafanyakazi wa ndani kwa bahati mbaya. Alitaka kulinda heshima ya wafanyakazi wa ndani ambao walikuwa wakifanya kazi kwa watu wenye ufedhuli na utovu wa maadili.

Kwa hakika, Mwenyezi Mungu Mtukufu hakubali mja Wake kufedheheshwa na kudhalilishwa. Nyoyo, ambazo hutazamwa na Mwenyezi Mungu, hazipaswi kuumizwa. Mababu zetu walilijua hili vizuri sana. Adabu, umaridadi, ulaini na utambuzi walioutumia kuitekeleza misingi ya maadili ya Uislamu ni mfano mwema ambao wametuonesha.

❀

Mola wetu ametuagiza tuyapangilie maisha yetu kulingana na kanuni njema za kimaadili, kwamba tuishi na nyoyo zenye kuitambua hadhi ya kuwa wanadamu. Mwenyezi Mungu Mtukufu ametupambanua sisi na viumbe wengine kwa maadili mema yenye kusifika, kwa sababu kwa upande wa viumbe wengine, tafakuri ya kimaadili ni jambo lisilowezekana.

Kwa hali hiyo, kuipoteza sifa inayotupambanua kama wanadamu na kuishi kama wanyama, au chini kabisa ya wanyama, ni hasara kubwa kwa heshima ya ubinaadamu na ni wazimu wenye kutisha kwa israfu na ubadhirifu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atulinde dhidi ya shari zote na israfu inayoweza kuyapoteza maisha yetu ya Akhera. Tunamuomba atujaalie nyoyo zilizobarikiwa kwa dua hizi zilizotoka katika kinywa adhimu cha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu: "Mola wangu! Ipambe tabia yangu ya ndani kama ulivyonipamba kwa tabia ya nje! "Mola wangu! Niongozo ili nipate tabia njema! Hakika Wewe ndiwe uwezaye kuniongoza!"[41]

Amin...

41. Ibn Hajar, Fath al--Bârî, X, 456.

SURA YA 16

Israfu - 5

Katika Tafakuri

Tafakuri ya kweli hutokea pindi akili na moyo, vilivyoangaziwa na ufunuo, vinapoungana.

Marafiki wa Mwenyezi Mungu huyatafakari maajabu ya usanifu wa Mwenyezi Mungu katika ulimwengu kama mtu anavyochungulia ndani ya kisima. Hutoka huko na kuelekea kwenye himaya ya ulimwengu wa moyo. Maneno hayawezi kuielezea hali ya moyo unaotambua na kuona; ndimi haziwezi kuifafanua. Wale wanaoyatazama maumbile ya ulimwengu kwa hisia kuu ya moyo hupata ladha ya raha ya maajabu yanayopatikana katika usanifu huo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

SURA YA 16

ISRAFU -5

Katika tafakuri

Mwenyezi Mungu Mtukufu alimpa mwanadamu sifa maalumu kama vile akili, mantiki na uwezo wa kutafakari. Alimuinua mwanadamu juu ya viumbe wote. Qur'an Tukufu hukielezea kila kitu kwa mifano, na imeweka wazi kuwa inazungumza na wale wenye akili tu. Daima Mwenyezi Mungu anawataka waja wake kujishughulisha na tafakuri, kuvitazama vitu vyote kwa jicho litakalowafanya wapate hekma, na kuchukua mafunzo kutoka humo. Ndiyo maana katika aya nyingi za Qur'an Tukufu, Mwenyezi Mungu anatuita kwenye tafakuri kwa kusema, *"Je hamfikiri?", "...ili mpate kutafakari," "...huwenda mkatafakari," "Tazameni!"*

Qur'an Tukufu inaonesha kuwa akili iliyoongozwa na wahyi (ufunuo), ni kitovu sahihi cha tafakuri, na inawaita wanadamu kwa kusema "Enyi wenye akili!" Ndiyo maana watu wenye akili ambao wanataka kuishi kulingana na heshima na hadhi ya mwanadamu wanapaswa kuingia katika ulimwengu wa tafakuri ulioangazwa na nuru ya Qur'an Tukufu.

Waislamu tusingeweza kugundua siri nyingi kwa akili, kama Uislamu ungetuonesha anga ya tafakuru. Mbaya zaidi, huwenda tungezitumia akili zetu katika kutafuta matamanio ya kidunia tu. Ili kuzilinda nafsi zetu dhidi ya janga hilo, tunahitaji muongozo na maonyo ya Qur'an Tukufu na Sunna za Mtume ﷺ. Vitu hivi viwili ndio muongozo pekee unaoweza kuipeleka tafakuri kwenye muelekeo sahihi, na ndio muongozo unaoweza kuielezea misingi ya maisha kuafikiana na njia iliyonyooka.

Tafakuri ni miongoni mwa ibada muhimu mno. Ili kuishi kama waja wa Mwenyezi Mungu, tunapaswa kuzitafuta hekma na siri za ulimwengu na kuyaduru matukio yanayotokea ndani yake. Ili tufikie lengo hilo, tunapaswa kuzizamisha nyoyo zetu ndani ya tafakuri. Litakuwa jambo bora na lenye matumaini iwapo kila Muumini atajaribu kuyapatanisha mawazo yote yaliyomo akilini mwake na radhi za Mwenyezi Mungu, kuzipatanisha hisia zake zilizopo moyoni – hata pumzi anayoivuta au kuitoa - ni ridhaa ya Mwenyezi Mungu. Kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu alituumba ili tumuabudu na kumtumikia. Kitu chochote kinachopingana na asili ya uwepo wetu kitaangukia katika fungu la israfu.

Akili, ambayo ni mojawapo ya neema za kushangaza sana alizopewa mwanadamu, peke yake haitoshi kuwaongoza watu kwenye ukweli. Thamani ya tafakuri ya mwanadamu inategemea utendanji kazi wa pamoja baina ya akili na moyo. Akili pekee inaweza kutosha tu kwa masuala ya kidunia na kutafuta manufaa binafsi. Lakini ili tuwe na ukomavu katika imani, moyo ambao ni kitovu cha utambuzi na hisia, unapaswa kulelewa katika masuala ya kiroho, ili uwe muongozo kwa akili. Moyo huitawala akili, na tafakuri huitawala dhamira. Hii ina maana kwamba nguvu iliyo nyuma ya matendo yote ya sunna ni moyo na utambuzi uliopandikizwa ndani ya moyo huo. Hivyo kuhakikisha moyo unalelewa

kulingana na maamrisho ya Mwenyezi Mungu ni muhimu zaidi kuliko malezi ya vipawa vingine vyote.

Uwezo wa kutafakari wa mtu ambaye moyo wake umeangazwa kwa nuru ya Qur'an na sunna za Mtukufu Mtume ﷺ unahitaji kuwa wenye kufahamiana na siri husika.

Akili na moyo vimeumbwa katika namna ambayo huwaongoza watu kwenye mema na ukweli kwa sharti kwamba view vimepata nuru ya muongozo wa Mwenyezi Mungu. Tafakuri ya kweli hutokea pindi akili na moyo, vilivyoangaziwa na ufunuo, vinapoungana.

Kujaribu kupata ufumbuzi wa mambo yaliyo nje ya uwezo wa akili ni aina ya israfu ya tafakuri. Tumeagizwa kutafakari siri za sifa za Mwenyezi Mungu na katika maajabu ya Qur'an, ulimwengu na maumbile ya mwanadamu. Lakini, kujaribu kutafakari mambo yaliyo nje ya uelewa wa mwanadamu, kama vile asili ya Mwenyezi Mungu au siri za qadari, ni matumizi mabaya ya vipawa vyetu vya kiakili. Majaribio hayo yameharamishwa na Qur'an Tukufu na hadith za Mtukufu Mtume ﷺ.

Kama ambavyo kuna kikomo cha mwanga ambao macho yanaweza kuuona, na kikomo cha sauti ambayo masikio yanaweza kuusikia, vivyo hivyo kuna kikomo cha kiwango cha mambo ambayo akili inaweza kuyaelewa. Ndiyo maana akili inahitaji kuongozwa na ufunuo. Kama ambavyo ni msiba kutotafakari ukweli mbalimbali, vivyo hivyo ni msiba kuipuuza mipaka yetu ya kimaumbile na kujaribu kuisukuma akili kwenda nje ya uwezo wake. Juhudi hii ni matumizi mabaya ya akili, na inaweza kusababisha majuto huko Akhera.

Mara nyingi akili ya mwanadamu hufanya kazi kwa kushawishiwa na matamanio ya kidunia pamoja na maradhi mbalimbali

ya moyo kama vile majivuno na kiburi. Akili inapokosa muongozo wa moyo salama, hupotoka. Tafakuri inayofanywa katika mazingira hayo huweza kuwa na hitimisho potofu. Mawlana Jalaluddin Rumi (q.s) anasema: "Kama Shetani angekuwa na upendo mkubwa kama alivyokuwa na akili kubwa, asingeangukia katika hali ya laana aliyonayo sasa hivi."

Hivyo akili ipo kimya: yenyewe binafsi haina thamani chanya. Lazima iongozwe na hisia kutoka moyoni. Hisia zinazotokea nyoyoni mwetu zikiweza kupata sifa ya kiroho kupitia malezi ya kiroho, basi hisia hizo zinaweza kuiongoza akili yetu.

Kudhibiti hisia ni jambo gumu mno. Lakini, tunawajibika kuendelea kufanya juhudi ya kuziweka hisia zetu ziendane na radhi za Mwenyezi Mungu. Tunachotakiwa kufanya ni kuingia ndani ya tafakuri kwa mujibu wa maagizo ya Qur'an na mfano hai kutoka kwa Mtukufu Mtume ﷺ. Anga zinapotanuliwa na tafakuri hiyo, kwa huruma ya Mwenyezi Mungu mawazo na hisia zetu zitaenda sambamba na radhi Zake.

Moyo huo huo ambao ni makazi ya hisia, vilevile ni makazi ya imani. Imani ni hisia tukufu, kuhisi kwa hali ya juu. Basi, imani ni kukiri kwa moyo, sio kukiri kwa akili. Siri za Mwenyezi Mungu zilizopo ndani ya ulimwengu zinazoweza tu kugunduliwa na akili inayofanya kazi chini ya muongozo wa moyo uliojazwa imani. Ndiyo maana jambo muhimu na nyeti kabisa kuhusu dini ni suala la imani. Imani haiwezi kuishi mahali palipo na matamanio ya kidunia. Hata mpasuko mdogo wa kioo huzidi kupanuka, na hatimaye kioo chote husambaratika. Katika ulimwengu wa moyo, daima tunapaswa kuwa waangalifu kwa mambo yanayoonekana kuwa madogo. Hata doa dogo linapotua moyoni hatuna budi kuliondosha kabisa.

Unyenyekevu katika ibada huongeza thawabu za ibada. Kughafilika katika ibada hupunguza thawabu. Hata hivyo, mtu akiyatazama tu manufaa yake binafsi, na mpasuko ukatokea ndani ya moyo wake, imani yake itakuwa hatarini. Uzembe katika masuala ya imani, huwapeleka watu kwenye maangamizi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atulinde nayo.

Kuna mifano na matukio mengi juu ya jambo hilo. Qaruun ni mfano mzuri. Mwanzo alikuwa mtu mwema. Baada ya Mwenyezi Mungu kumjaalia kiwango kikubwa cha utajiri, aliharibika na kujawa na kiburi. Alianza kuhisi kuwa alizipata mali hizo kwa nguvu zake mwenyewe. Alijifakhiri na kujiona kiasi kwamba alijaribu kumpinga Musa ﷺ. Mwishowe, Mwenyezi Mungu Mtukufu alimdidimiza yeye na mali zake ardhini. Hatima yake imeelezewa ndani ya Qur'an kama ifuatavyo:

"Basi tukamdidimiza yeye na nyumba yake katika ardhi; wala halikuwepo kundi lolote la kumnusuru kwa Mwenyezi Mungu, wala hakuwa miongoni mwa wanao jitetea." (Qasas, 28:81)

Moyo unaopoteza msingi wake wa imani huwa kama kisu kinachoteleza pindi mtu anapokata mkate: akizembea kidogo tu kinamkata. Kisu kinapotukata, hapo hapo hisia zetu huibuka.

Moyo wenye hisia ndio kiungo huru zaidi katika mwili. Mwelekeo wake hubadilika wakati wowote. Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Moyo upo mikononi mwa Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma, na huugeuza apendavyo." Moyo una sehemu ya sifa ya Mwenyezi Mungu ya Muongozaji, na pia ina sehemu ya sifa Yake ya Mgeuzaji. Hakuna ajuaye wakati gani sifa mojawapo itaitawala nyingine.

Mfano mwingine ni Bal'am ibn Bawrah, ambaye kisa chake kimetajwa ndani ya Qur'an Tukufu. Mkondo wake wa kuelekea

kwenye matamanio ya kidunia uliotokana na nafsi yake ya kihayawani ulimharibu na kumuangamiza. Mwanzo alikuwa miongoni mwa waja wema wa Mwenyezi Mungu. Aliweza kuonesha hata miujiza mbalimbali, na dua zake zilikuwa zenye kukubaliwa na kujibiwa. Lakini matamanio ya nafsi yaliidhibiti akili yake na matokeo yake akaangamia. Qur'an inaelezea kisa chake kama ifuatavyo:

"Na wasomee khabari za yule ambaye tulimpa Ishara zetu, naye akajivua nazo. Na Shet'ani akamuandama, akawa miongoni walio potea. Na tungelitaka tungeli mtukuza kwa hizo Ishara, lakini yeye aliushikilia ulimwengu na akafuata pumbao lake. Basi mfano wake ni mfano wa mbwa. Ukimhujumu hupumua na kutoa ulimi na ukimwacha pia hupumua na kutoa ulimi. Huo ni mfano wa kaumu wanao zikanusha Ishara zetu. Basi simulia hadithi, huenda wakatafakari." (A'râf, 7:175-176)

Kama nilivyosema hapo mwanzo, kujaribu kutumia akili nje pasipo muongozo wa wahyi na kwa ajili ya kupata manufaa binafsi huwafanya wanadamu kuwa wapumbavu, na huwapeleka kwenye mkanganyiko uliotajwa katika aya iliyotangulia. Ndiyo maana Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akiomba kwa kusema: "Mola wangu! Usiniache peke yangu hata kwa muda wa mpepeso wa jicho."[42] Maneno haya yanaonesha hali ya kiroho ya muumini wa mfano.

Kwa hivyo, ili tuweze kuiokoa imani yetu, yatupasa kupitia mafunzo ya utambuzi na hisia inayoendelea kutuweka katika hali ya hofu na matarajio, na kuiongoza tafakuri yetu ipasavyo. Kama tunataka kufa tukiwa na nyoyo zenye imani, yatupasa kuzifanya nyoyo zetu kuwa zenye hisia na utambuzi katika maisha yetu yote. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an:

42. Jâmi` as-Saghîr, v. I, uk. 58

"Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife ila nanyi ni Waislamu." (Âl-Imrân, 3:102)

Kwa mfano, kama hatupendi na kuchukia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, tutapenda kitu tunachopaswa kukichukia na kukichukia kitu tunachopaswa kukipenda, na hapo janga la kiroho litatusibu. Yatupasa kujifunza kuyapeleka mapenzi na chuki kule vinakostahili. Kusuhubiana na wachamungu humpeleka mtu kwenye furaha. Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Qur'an Tukufu:

"Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli." (at-Tawbah, 9:119)

Kwa upande mwingine, kushikamana na adui wa dini ni mwanzo wa kukumbwa na janga. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema kuhusu jambo hili:

"...baada ya kutanabahi usikae pamoja na watu madhaalimu." (An'âm, 6:68)

Kwa muktadha huo, ili tujiingize katika tafakuri salama, hisia zetu zinatakiwa kuangazwa kwa nuru kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Katika aya nyingine, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Kwa hakika Sisi tulikadimisha amana kwa mbingu na ardhi na milima; na vyote hivyo vikakataa kuichukua na vikaogopa. Lakini mwanaadamu akaichukua. Hakika yeye amekuwa dhaalimu mjinga." (Ahzâb, 33:72)

Kwa kuwa wanadamu tumeshindwa kuutambua ipasavyo uzito wa amana tuliyokabidhiwa, katika aya hii tumepewa sifa za *dhaluum* (dhalimu) na *jahuul* (mjinga mno). Maneno haya yamekusudiwa kubainisha umuhimu wa amana hiyo na kuwataka watu wazingatie. Ili tuepukane na sifa hizo za *dhaluum* na *jahuul*,

yatupasa kufanya matendo mema na tuweze kuigeuza elimu yetu ya ndani na ya nje kuwa utambuzi wa moja kwa moja wa uwepo wa Mwenyezi Mungu kwa njia ya tafakuri. Katika hili, Mola wetu anatueleza katika suratul-Asr kuwa ili wanadamu waweze kuepukana na hasara lazima wawe na imani, wafanye matendo mema, na wausiane kutenda haki na subira – ambayo ni ibada inayotokana na kuihudumia jamii. Akionesha maana ya ndani kabisa ya aya za sura hiyo, Imam Shafii anasema, "Kama watu wangeitafakari Suratul-Asr na kuchambua ipasavyo, ingewatosha." (Ibn Kathîr, Tafsiri ya Suratul-Asr)

Ndani ya Qur'an Tukufu, Mola wetu ametufungulia anga pana ya tafakuri. Miongoni mwa aya zinazotakiwa kuzingatiwa kuhusu hilo ni hii ifuatayo:

"Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala, na hufikiri kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Subhanaka, Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya Moto." (Âl-Imrân, 3:191)

Maajabu mbalimbali yanayoonesha uwezo wa Mwenyezi Mungu katika ulimwengu wa anga (kama vile maajabu ya mbingu na ardhi) na ulimwengu wa muda (kama vile mabadiliko ya usiku na mchana) – yote haya yanawaita watu wenye akili ya kutafakari kumkurubia zaidi Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anataka tuielewe lugha ya ulimwengu. Katika ulimwengu huo vitu vyote huzungumza na wale walio tayari kwa ajili ya kupata nuru ya Mwenyezi Mungu. Vitu vyote, kuanzia kwenye chembe ya atomu mpaka kwenye sayari, humkumbusha mwanadamu juu ya utukufu na ukuu wa Mwenyezi Mungu.

Tunapozitafakari siri za utukufu wa Mwenyezi Mungu zinazopatikana ndani ya ulimwengu, hutupeleka kwenye unyeyekevu na hatimaye kutambua kuwa sisi si cochote. Ukomavu wa muumini upo katika uelewa wa kwamba yeye ni dhaifu na mnyonge

mbele ya Mola wake. Kuukubali ukweli huu – wa kwamba sisi si chochote na si lolote mbele ya ukuu na utukufu wa Mwenyezi Mungu – ndiko pekee kunakoweza kuyaondosha maradhi hatari ya majivuno na kujiona.

Katika hili, Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akimuomba Mwenyezi Mungu msamaha, "Mola wangu! Hatuwezi kukujua kama unavyostahiki kujulikana…" (Munâwî II, 520)

Nafsi ya mtu ambaye hajaonja unyonge na kukata tamaa ni kama farasi mwitu. Fir'auni, Namrudh (aliyemtesa Nabii Ibrahimu), Qarun na Haman walikuwa kama hivi. Watu hao walifurahia mateso ya watu wengine. Kwao, vilio vya wanyonge vlikuwa kama ala zenye kufurahisha.

Kwa upande mwingine, mtu akipatwa na maradhi, majanga au msiba katika dunia hii, lakini akaweza kupata mazingatio, maumivu atakayoyapata yatageuka kuwa neema kwake. Kwa sababu unapokutana na matatizo, hali ya kukata tamaa na kuhisi kuwa si chochote hukuongoza kwenda kwenye staha na unyenyekevu, na kukufanya ulie "Ewe Mola wangu!" kutoka ndani ya kina cha moyo wako.

Aidha, watu hufikia kilele cha ukomavu kulinagana na mateso wanayopitia na shida wanazokabiliana nazo. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwafanya Mitume Wake pamoja na waja wema wapitie misukosuko katika safari zao za kiroho. Misukosuko hiyo ikageuka kuwa ishara ya neema za Mwenyezi Mungu, wakaitumia kama njia ya kuzikamilisha hali zao za kiroho.

Sheikh Sa'di Shirazi anasema: "Kwa wale wenye kutafakari, kila jani la kila mti, hata likiwa dogo kiasi gani, huwa kama kitabu kikubwa kinachotoa maarifa kuhusu Mwenyezi Mungu (yaani,

moyo kumtambua Mwenyezi Mungu). Kwa wajinga wasiojitambua, miti yote duniani huonekana kama haina jani hata moja."

Ili viungo vyetu vya fahamu na akili yetu viweze kuzielewa siri za Mwenyezi Mungu katika ulimwengu, akili zetu zinapaswa kuwatengenezwa kwa tafakuri na moyo wetu unapaswa kuwa na kina cha kiroho. Maajabu ya uumbaji wa Mwenyezi Mungu ndani ya ulimwengu ni kama ushairi wa kimaanawi usiokuwa na sauti wala maneno. Ushairi wa kimaanawi ladha na kina chake huongezeka kadiri moyo unavyozama ndani yake.

Marafiki wa Mwenyezi Mungu huyatafakari maajabu ya usanifu wa Mwenyezi Mungu katika ulimwengu kama mtu anavyochungulia ndani ya kisima. Hutoka huko na kuelekea kwenye himaya ya ulimwengu wa moyo. Maneno hayawezi kuielezea hali ya moyo unaotambua na kuona; ndimi haziwezi kuifafanua. Wale wanaoyatazama maumbile ya ulimwengu kwa hisia kuu ya moyo hupata ladha ya raha ya maajabu yanayopatikana katika usanifu huo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Watu hao huyageuza macho yao kwenye maajabu yanayopatikana katika tofauti za majani na maua ya mimea, ambayo humea katika ardhi moja, lakini matunda yanatofautiana rangi, harufu, ladha na umbile. Huwatazama vipepeo, ambao huonesha ruwaza ya ajabu katika mbawa zao licha ya umri wao kutozidi wiki mbili tu. Huusikiliza ujumbe wa siri unaotangazwa na vitu vyote hivyo katika lugha ya maumbile yake. Kwa watu hao, ulimwengu ni kitabu kinachotakiwa kusomwa.

Wakati huo huo, watu wajinga ambao wana vina vifupi vya bahari ya akili na moyo, huviangalia vitu kwa upande wa nje. Hawajui lulu za kiroho zilizomo ndani ya vina hivyo. Mawlana Jalaluddin Rumi anawaelezea kuwa:

Wale ambao nyoyo zao zimejaa mapenzi ya dunia ni kama wawindaji wa vivuli. Mtu anawezaje kumiliki kivuli? Mwindaji mmoja mjinga alidhani kivuli cha ndege kuwa ni ndege mwenyewe, na akajaribu kukikamata. Hata ndege aliyekuwa akining'inia juu ya tawi la mtu alishangazwa na kitendo cha mwindaji huyu mjinga!

Rafiki mmoja wa Mwenyezi Mungu anasema: "Kwa mtu mwerevu, huyaona maisha haya kuwa ni fursa ya kuangalia utukufu wa Mwenyezi Mungu. Kwa mtu mjinga, maisha haya ni ya kukidhi matamanio ya nafsi."

Watu wenye moyo huutazama ulimwengu huu kwa lengo la mazingatio na kujifunza siri za vitu vyote. Wanatambua kuwa kuna siri katika kila kitu, na hivyo hupata maarifa kutoka ndani ya ulimwengu. Wale wajinga husema, "Achana nayo, jitahidi sana kufurahia chochote uwezacho: tunakuja hapa duniani mara moja tu!" Msimamo kama huo huongeza giza na kutu katika nyoyo zao.

Mawlana Jalaluddin Rumi anatutaka tuzinduke, tuitafakari hali yetu, na tuchunguze hekma ya uwepo wetu ulimwenguni:

Mtazame mwanadamu kwa hekma! Kwa nini unayaona matamanio ya mwili wako na manufaa binafsi kuwa ni muhimu kama milima mikubwa? Kwa nini unamuona mwanadamu mwenye tafakuri salama kuwa asiye na umuhimu kama sisimizi? Kwa nini unakuwa kipofu na mjinga, japokuwa unauona ukuu na uwezo wa Mwenyezi Mungu katika ulimwengu? Ewe uliye chini kabisa kuliko wa chini! Kama ambavyo jiwe halijui chochote, hujui chochote cha tafakuri. Hasara kiasi gani uliyo nayo! Kwa kuwa umepoteza tafakuri, umenyimwa neema kubwa kabisa kuliko zote.

Ni jambo la kusikitisha sana pale neema ya tafakuri inapowekwa chini ya matamanio ya nafsi. Kuishi bila tafakuri ni ishara ya uvivu na ujinga uliopitiliza. Kukosa hisia ni kuufanya moyo

uwe kipofu na kiziwi, na moyo kutojali mbele ya siri zote hizi za Kimungu ni jambo lisilopatana na hadhi ya mwanadamu. Kuutazama ulimwengu kwa mtazamo wa kijinga na macho na upofu wa moyo ni janga kubwa la kiroho. Hali hii imeelezwa ndani ya Qur'an Tukufu:

"Je! Hawatembei katika ardhi ili wapate kuwa na nyoyo zao za kuzingatia, au masikio ya kusikilia? Kwani hakika si macho yanayo pofuka, lakini zinazo pofuka ni nyoyo ziliomo vifuani." (Hajj, 22:46)

Mawlana Rumi anaona kuwa matumizi mabaya ya tafakuri ni kama "kuweka takataka ndani ya bakuli la dhahabu." Hiyo ndiyo taswira kamili ya matumizi mabaya ya neema za tafakuri na utambuzi kwa kuzitumia kwa ajili ya matamanio duni na dhalili ya kihayawani.

Tunatakiwa kufanya tafakuri kwa njia sahihi na katika mazingira sahihi. Vinginevyo, tafakuri huenda mrama, na inaweza kumsababisha hasara ya kiroho. Wale wasiozingatia maonyo ya Mwenyezi Mungu watajuta sana siku ya Kiyama kwa kuitumia vibaya neema ya tafakuri kwa kuipeleka kwenye kukidhi matamanio ya nafsi zao. Qur'an Tukufu inasema:

"Na humo watapiga makelele: Mola wetu Mlezi! Tutoe tufanye mema sio yale tuliyo kuwa tukiyafanya. Kwani hatukukupeni umri wa kutosha kukumbuka mwenye kukumbuka? Na akakujieni Mwonyaji? Basi onjeni! Kwani walio dhulumu hawana wa kuwanusuru." (Fatir 35:37)

Hivyo basi, tunapaswa kutumia akili zetu ipasavyo ili kupata wokovu huko Akhera. Tunapaswa kuziangaza hisia zetu na mawazo yetu kwa nuru kutoka kwa Mwenyezi Mungu, sio mawazo ya kishetani ya majivuno au matamanio ya nafsi. Mawlana Rumi

anasema kuwa mja anatakiwa kuwa makini sana katika suala hili: "Mawazo, fikra na mitazamo ya kishetani inayoibuka ndani mwetu ni kama miiba katika nyoyo zetu. Miiba hii haitoki kwa mtu mmoja tu, bali maelfu ya watu, na kupenya ndani ya nyoyo zetu."

Tunapaswa kujilinda dhidi ya mitazamo itokanayo na nafsi zetu za kihayawani au Ibilisi, kwa sababu huharibu upeo wa kiroho wan yoyo zetu na kuviangamiza vipawa vyetu vya tafakuri na utambuzi. Redio iliyowekwa kwenye mkondo mbaya haiwezi kupokea matangazo ya kituo kingine cha utangazaji, na vivyo hivyo kwa upande wa moyo. Moyo ukiendelea kubaki katika ujinga, hautaweza kupata uongofu na hatima yake ni kuangamia. Samaki huishi vizuri baharini, na viumbe bara huishi vizuri nchi kavu. Vivyo hivyo, roho ya mwanadamu hupata furaha ndani ya mazingira yenye nuru ya Qur'an Tukufu na Hadith za Mtume ﷺ.

Anga kuu kabisa ya tafakuri ni tafakuri ya kifo. Tafakuri hii hutuokoa dhidi ya ulaghai wa mitihani ya nafsi na ulevi wa anasa za kimwili, na hivyo humfanya mwanadamu awe na moyo wenye utambuzi. Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Qur'an Takatifu:

"Na uchungu wa kutoka roho utamjia kwa haki. Hayo ndiyo uliyo kuwa ukiyakimbia." (Qâf, 50:19)

Katika hadith moja, Mtukufu Mtume ﷺ alisema: "Kikumbuke sana kifo, kwa maana kinakata raha zote." (Tirmidhî, Qiyâmah 26)

Watu wenye ukomavu huzitafsiri taarifa kuhusu maisha baada ya kifo na kujiandaa kwa ajili ya maisha ya baadaye wakiwa hapa hapa duniani. Mtu hawezi kuzijua siri za mustakbali wetu wa baadaye mpaka ayatafakari maisha ya baada ya kifo. Mtu yeyote mwenye tafakuri salama lazima atafakari ipasavyo, katika mazingira ya utambuzi, kuhusu maana ya safari yetu fupi tokea utotoni mpaka anapoingia mwanandani.

Haiwezekani kulifumbua fumbo la mustakbali kwa kutumia tafakuri nyepesi ya mwanadamu. Tunaweza kulifikia hilo pale tu tunapojisalimisha mbele ya muongozo wa wahyi (ufunuo). Vinginevyo tutajichosha bure kwa kujaribu kukikwepa kifo.

Mwenyezi Mungu anataka tuingie kwenye Pepo Yake. Ndiyo maana anatuonya tusighafilike. Anasema ndani ya Qur'an Tukufu:

"Je! Mlidhani ya kwamba tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa?" (Mu'minûn, 23:115)

Katika muktadha huu, Mtukufu Mtume ﷺ alimuomba Mwenyezi Mungu amlinde asipoteze tafakuri na utambuzi kutokana kuvamiwa na matamanio ya kidunia: "Mola wangu! Usiifanye dunia kuwa fikra na lengo letu kuu wala mwisho wa utambuzi wetu…." (Tirmidhî, Da'awât, 79)

Vilevile, Mtukufu Mtume ﷺ anatutaka tutafakari hata wakati wa dua anazoomba kabla ya kulala. Alionesha shukrani na kumsifu Mwenyezi Mungu katika kwa utambuzi wa hali ya juu: "Himidi na sifa njema ni kwa Mwenyezi Mungu anayetulisha na kutunywesha, anayetulinda na kutuhifadhi, kwa maana kuna wengi ambao hawana ulinzi wala hifadhi." (Muslim, Dhikr, 6) Ni wajibu mkubwa kwa waja wa Mwenyezi Mungu kuzitafakari neema anazowajaalia kila siku na kumshukuru kwa neema hizo. Yatupasa kutafakari umuhimu wa kuwa na uwezo wa kwenda kulala tukiwa tumeshiba ilhali kuna watu wengi duniani ambao huenda kulala wakiwa na njaa na kiu; kulala tukiwa na hisia ya raha na usalama, ilhali kunwa watu wengi wanaokandamizwa na umasikini na njaa; na kulala kwa amani, ilhali kuna watu wengi ambao usiku hawapati utulivu kwa sababu majanga na masaibu yanayowakumba.

Unapopewa neema nyingi na kubwa unakuwa umepewa dhima kubwa. Hivyo hivyo hesabu ya kile ambacho tumekipata kwa siku

nzima kabla ya kwenda kulala kina nafasi ya lazima katika maisha ya tafakuri. Ni lazima ujihisabu kwa kile ulichopata kwa siku nzima kabla ya kwenda kulala. Khalifa wa pili, Umar ﷺ anasema: "Ihesabu nafsi yako kabla hujahesabiwa." Alikuwa akiihisabu nafsi yake na kuitathmini kwa umakini na undani kabisa. Nafasi ya uongozi aliichukulia kwa uzito mkubwa. Siku moja alisema: "Kama kondoo atazama katika mto Tigris, Mwenyezi Mungu atamuuliza Umar." Na alikuwa akiiambia nafsi yake: "Ewe Umar, leo umefanya nini kwa ajili ya Mwenyezi Mungu?"

Ninauliza: lini tumekuwa na hisia kama hizo? Tunajichosha kutafuta maisha, lakini ni mara ngapi tumezihesabu nafsi zetu? Ni mara ngapi tunatumia muda kufikiria juu ya sababu za kuumbwa kwetu, tumetoka wapi, tunakwenda wapi na ni kwa kiwango gani maisha yetu yanaridhiwa na Mwenyezi Mungu? Ni muda kiasi gani tunautenga kwa ajili ya kutafakari kikamilifu kama tumeweza kutekeleza mafundisho na wajibu wa dini yetu? Ni kwa kiwango gani tunayatengeneza maisha yetu kulingana na maamrisho y Mola wetu? Ni kwa kiwango gani tumeweza kuingia ndani ya ulimwengu wa kiutamaduni na kiroho wa Qur'an Takatifu, ambayo ni ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwetu? Na ni kwa kiwango gani tumeweza kuiga mifano bora katika maisha ya Mtukufu Mtume ﷺ, ambaye maisha yake ni Qur'an iliyo hai? Ni kwa kiwango gani tumeweza kuyaangalia mapungufu yetu katika masuala haya? Au tumepoteza hazina yetu bora ya kutafakari?

Qur'an Tukufu inatusimulia kisa cha Habib an-Najjar aliyepigwa mawe na watu wa kabila lake lakini akaiokoa imani yake; kisa cha watu wa Ukhduud waliowekwa katika mahandaki wakachomwa moto; na kisa cha wachawi walioteswa na Fir'auni baada ya kupata muongozo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tumepewa

mifano yote hii, lakini ni kwa kiwango gani tunatambua thamani ya neema ya Mwenyezi Mungu, neema ya imani?

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atuepushe na hali ya kunyimwa tafakuri, na atuepushe tusiifanyie israfu neema hii kubwa! Azifanye nyoyo zetu, akili zetu na hisia zetu zifuate njia anayoikubali Yeye!

Amiin…

SURA YA 17

Israfu - 6

Katika Riziki na Sadaka

Inafahamika vyema kuwa chanzo cha mgogoro wa kiroho wa zama zetu na mapato ya haramu, kukiuka haki za wengine, mtu kutoridhika na kile alichonacho, na tamaa ya kupata zaidi. Ili kuondosha misukumo hasi, tunapaswa kuchunga kanuni za Kiislamu zinazotuonya dhidi ya kuvunja haki za wengine na kutuhamasisha kupata riziki zetu kwa njia za halali.

❀

Katika jamii yoyote kutakuwa na watu ambao wanaweza kuwa wanafanya chini ya kiwango ambacho fursa zao zinawalazimisha kufanya. Tukiyalinganisha matendo yetu na matendo ya watu hao na kujihesabu kuwa ni wakarimu kwa ulinganisho, ulinganisho huo utakuwa wa makosa. Ndiyo maana tunapaswa kukilinganisha kiwango cha ukarimu wetu na matendo ya Mtukufu Mtume ﷺ na Maswahab zake.

SURA YA 17

ISRAFU -6

Katika Riziki na Sadaka

Maisha ya duniani, ambayo ni mtihani kwetu, yamepambwa kwa neema zisizohesabika, zinazoonesha hekma ya uwezo na ukuu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Neema hizi zinaweza kuwahamasisha watu kuwa waja wema. Vilevile zinaweza kusababisha fitna na hasara, iwapo waja hao wataendelea kuwa wazembe. Itakuwa ni israfu kubwa kuzitumia vibaya neema tulizoaminiwa na Mwenyezi Mungu kinyume na malengo yake sahihi, au kwa ajili ya matamanio ya nafsi na tamaa za kishetani.

Hakika, Mwenyezi Mungu Mtukufu aliviweka vitu vyote vilivyo baina ya mbingu na ardhi chini ya utawala wa mwanadamu. Lakini pia akatuambia kuwa tutaulizwa na kuwajibishwa kwa neema hizi siku ya Kiyama. Mwenyezi Mungu anatuambia ndani ya Qur'an Tukufu:

"Tena bila ya shaka mtaulizwa siku hiyo juu ya neema." (at-Takâthur, 102:8)

"Hapana shaka yoyote mtapata misukosuko katika mali zenu na nafsi zenu…" (Âl-Imrân, 3:186)

"Je! Mlidhani ya kwamba tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa?" (Mu'minûn, 23:115)

Aina mbaya kabisa ya israfu (yaani kupindukia na kukiuka mipaka iliyowekwa) ni ile inayotokana na kuvuka mipaka iliyowekwa na Mwenyezi Mungu, na hivyo ukabadilisha furaha ya milele huko Akhera kuwa hasara.

Kwa sababu ya ujinga, mara nyingi watu hudhani kuwa israfu inahusu tu ubadhirifu wa rasilimali za kimaada, na hivyo kuitumia dhana hii ndani ya maana finyu. Lakini, kama ambavyo imekatazwa kutumia vibaya rasilimali zinazoshikika, vivyo hivyo imekatazwa kutumia vibaya rasilimali za kiroho. Aidha, israfu katika rasilimali za kiroho inaleta dhima nzito zaidi na hupelekea mtu kukhasirika.

Miongoni mwa maeneo muhimu ambayo watu hufanya israfu kimaada na kiroho ni yale yanayohusu mapato ya kila siku, matumizi na utoaji wa sadaka.

Mwenyezi Mungu ameshakadiria riziki za waja Wote. Ndani ya Qur'an Tukufu, Mwenyezi Mungu anaeleza kuwa riziki ya waja imeshakadiriwa:

"Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi. Na sitaki kwao riziki, wala sitaki wanilishe. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuruzuku, Mwenye nguvu, Madhubuti." (adh-Dhaariyât, 5156-58)

"Na wanyama wangapi hawawezi kujimilikia riziki zao! Mwenyezi Mungu anawaruzuku hao na nyinyi pia. Na Yeye ndiye Mwenye kusikia Mwenye kujua." (`Ankabût, 29:60)

"NA HAKUNA mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Naye anajua makao yake na mapitio yake. Yote yamo katika Kitabu chenye kubainisha." (Hûd, 11:6)

Katika aya hizi, Mwenyezi Mungu Mtukufu anatuhakikishia kuwa ujuzi, nguvu, uwezo na rehma Zake havina kikomo. Kwa kweli hatuwezi hata kuwaza idadi ya viumbe vinavyoishi chini ya udongo, chini ya matabaka ya ardhi, na katika vina vya bahari. Lakini Mwenyezi Mungu anajua kila kitu kuhusu viumbe hao na anawapa chakula na riziki yao. Hivyo, tunapotafuta riziki zetu, tunapaswa kutafakari jinsi tunavyoweza kutengeneza usuhuba wa moyo na Mgawaji Mkuu wa riziki, yaani Mwenyezi Mungu Mtukufu, anayegawa riziki kwa kila kitu.

Ukweli kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anawahakikishia viumbe riziki zao ni ishara ya uwezo Wake Mkuu. Hili limeelezwa vizuri katika kauli ya Mtukufu Mtume ﷺ: "Usikate matumaini ya riziki muda ambao unaweza kuinua kichwa chako. Kwa maana mwanadamu huzaliwa na mama yake akiwa mtupu, na akiwa mwekundu kutoka kichwani mpaka kwenye kidole gumba cha mguu. Baadaye Mwenyezi Mungu Mtukufu humpatia kiwango kikubwa cha riziki." (Ibn Mâja, Zuhd, 14) Vilevile anasema: "Mwenyezi Mungu ni mwenye kujitosheleza. Kile ambacho wanadamu hula na kunywa hakipunguzi chochote katika utajiri wake. Ni mkarimu mno, na hutoa neema bila kikomo, usiku na mchana. Fikiria vile ambavyo Mwenyezi Mungu amewajaalia viumbe tokea zilipoumbwa mbingu na ardhi! Hakuna kilichopunguza utajiri wake." (Bukhârî, Tawhid, 22)

Kwa kulitambua hili, kama tunahofia mno kuhusu riziki zetu na kuvuka mpaka katika juhudi zetu, tutakuwa tunaupa nafasi wasiwasi utokanao na nafasi zetu za kihayawani, na tunatakiwa kuondokane na wasiwasi huo. Tunapaswa kutafuta riziki tuliyokadiriwa na Mwenyezi Mungu kwa njia sahihi na za halali. Tunapaswa kuyachukulia matokeo ya juhudi zetu za halali kuwa ni uamuzi wa Mwenyezi Mungu, tuyatambue kuwa ni kheri kwetu, na tuyakub-

ali. Tukikimbilia kwenye wasiwasi usiokuwa na msingi kuhusu utafutaji wa riziki tukamsahau Mtoa riziki, na kama tutatumia njia za haramu kupata zaidi ya kile tulicho nacho, tutakuwa tumevuka mipaka na kuangukia katika israfu.

Wakati huo huo, tunapaswa kutodhani kwamba, kwa kuwa Mwenyezi Mungu ameshakadiria riziki, hatuhitaji kufanya juhudi. Mawazo hayo mabovu yanayowahamasisha watu kuwa wavivu, nayo pia yanatokana na uovu wa nafsi zetu za kihayawani. Mawazo hayo, hutupeleka kwenye hali nyingine uzembe uliopitiliza.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anaielezea hali ya huko Akhera kwa wale wanaovuka mipaka aliyoiweka kwa kuwa na ulafi na ubakhili, na kuzitoa mhanga nafsi zao kwenye mapenzi ya mali za dunia hii:

"Aliye kusanya mali na kuyahisabu. Anadhani ya kuwa mali yake yatambakisha milele! Hasha! Atavurumishwa katika H'ut'ama. Na nani atakujuvya ni nini H'ut'ama? Moto wa Mwenyezi Mungu ulio washwa. Ambao unapanda nyoyoni. Hakika huo utafungiwa nao Kwenye nguzo zilio nyooshwa." (Humazah, 104:2-9)

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alielezea wasiwasi wake kuwa umma wake unaweza kuangukia katika israfu kwa kuacha mwenendo mwema katika kutafuta mali. Anasema: "Ninahofia kwamba baada ya kuondoka, mtaletewa maua (mali) na mapambo ya dunia (nanyi mkaangukia katika kuvipenda)!" (Bukhârî, Zakâh, 47)

Ni jambo lisilofaa kwetu kushughulishwa mno na riziki zetu kiasi cha kupuuza swala na huduma kwa jamii. Vilevile haifai kwa wavivu na wazembe wa kutafuta riziki za familia zetu, kiasi kwamba wanakuwa katika hatari ya kuangukia katika umasikini na maangamizi. Njia inayokubalika na yenye baraka, isiyokuwa na israfu, ni ile isiyowafanya watu wapuuze kufanya matendo yao ya

ibada, na sio inayoharibu ustawi wa mtu, bali ni ile inayoweka utaratibu wenye uwiano wa kufanya kazi inayopelekea kupata riziki ya halali inayoleta furaha kwa familia.

Kwa upende mwingine, ni jambo zuri kutafuta mali ya dunia ili kutoa sadaka kwa maskini, wanyonge na wale wanaoishi katika mazingira yasiyokuwa salama. Mtu wa aina hiyo anaweza kupata amani ya moyo na furaha ya Akhera, kwa maana ukarimu na huruma ni miongoni mwa sifa za muumini.

Huruma ni tunda la imani lenye thamani mno. Huruma hujitokeza wazi pindi tunapojitahidi, kwa kutumia njia zote za halali, kuwasaidia watu wenye shida kuwaondoa kwenye umaskini. Neema tunazopewa na Mwenyezi Mungu tunazihamishia kwa masikini kwa kutoa sadaka.

Uzuri ulioje wa maneno ya Mawlana Rumi! "Maisha haya ya duniani ni ndoto. Kuwa tajiri katika dunia hii ni kama kupata hazina ndotoni. Utajiri wa dunia hii hubaki hapa hapa, huhama kutoka kizazi kimoja kwenda kizazi kingine."

Tukiziacha mali zetu zote kwa warithi na watoto wetu, hatujui zitafanywaje. Wanaweza wasiwe na mafunzo sahihi ya kiroho, na hivyo hatuwezi kukisia jinsi watakavyoutumia urithi huo. Kukusanya utajiri wa familia ni kujibebesha dhima kubwa na nzito huko Akhera. Hatua hiyo inaweza isiwe ya busara, kwa wale wenye kujitambua. Qur'an Tukufu inatuonya:

"...Na wanao kusanya dhahabu na fedha, wala hawazitumii katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wabashirie khabari ya adhabu iliyo chungu." (at-Tawbah, 9:34)

Siku moja Mtukufu Mtume ﷺ aliwauliza Maswahaba zake: "Nani kati yenu anayependa mali ya warithi wake kuliko mali yake mwenyewe?"

Maswahaba wakajibu: “Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Sote tunapenda mali zetu zaidi kuliko mali za warithi wetu!”

Hapo Mtukufu Mtume ﷺ akasema: “Chochote ambacho mtu anakitanguliza Akhera, kwa kukitoa sadaka, hiyo ndiyo mali yake ya kweli. Kile asichokitoa hubaki na kuwa mali ya warithi wake!” (Bukhârî, Riqâq 12)

Shaykh Sa’di anatoa ushauri ufuatao kuhusu matumizi sahihi ya mali: “Usidhani kuwa kwa kuzirundika mali hadhi yako itapanda! Maji yasiyotembea hutoa harufu. Jaribu kusamehe na kutoa sadaka. Mbingu hufunguka kuyasaidia maji yanayotembea; huyasaidia kwa mvua na mafuriko. Watu werevu huzichukua mali zao wakaenda nazo pindi wanapoelekea Akhera. (Yaani huzitoa kama sadaka wakati wakiwa hai ili zipokelewe na Mwenyezi Mungu). Watu wenye ubakhili ndio wanazipoteza mali zao sana kiasi cha kuziacha nao wakaondoka!”

Abu Hurayrah ﵁ anasimulia kuwa mtu mmoja alikuja kwa Mtukufu Mtume ﷺ na kumuuliza: “Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ni sadaka ipi itakayokuwa na thawabu nyingi zaidi?”

Mtukufu Mtume ﷺ akajibu: “Sadaka itakayokuwa na thawabu nyingi zaidi ni ile iliyotolewa wakati ukiwa na nguvu, uwezo, afya na utashi wa kushikamana nazo, kwa kuwa unakuwa huna hofu ya kuwa masikini au kutamani kuwa tajiri. Usiakhirishe kutoa sadaka mpaka unapokaribia kufa, kisha ukaanza kusema, “Kiasi hiki kitapelekwa kwa fulani na fulani, na kiasi kile kitapelekwa kwa fulani na fulani!’ Hakika, wakati huo mali hiyo haitakuwa yako tena bali itakuwa imeshachukuliwa na warithi wako.” (Bukhârî, Zakâh 11)

Abdullah ibn Shihhir ﵁ anasimulia kuwa: “Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa akisoma Surah at-Takaathur. Ali-

pomaliza kusoma, akasema: “Wana wa Adam huendelea kusema ‘Mali yangu, mali yangu!’ Enyi wana wa Adamu! Je mna mali yoyote zaidi ya ile mliyokwisha itumia kwa kuila na ikachakaa, au kwa kuitanguliza Akhera kwa kuitoa sadaka, ili mpate kulipwa thawabu kwayo?” (Muslim, Zuhd, 3-4)

Siku nyingine, Mtukufu Mtume ﷺ alisema: “Kama mmoja wenu akifika asubuhi akiwa uhai na mali iliyosalimika sana kiasi cha kumpa afya na mlo wa kila siku, atakuwa kama aliyepewa dunia nzima.” (Tirmidhî, Zuhd, 34)

Akasema tena: “Furaha iliyoje kwa mwenye kuongozwa kwenye njia ya Uislamu, akawa na riziki ya kutosha na kutosheka na kile alicho nacho!” (Tirmidhî, Zuhd, 35)

Abu Umaamah ‘Iyaas ibn Tha’labah ؓ anasema: “Siku moja Maswahaba walikuwa mbele ya Mtume, wakawa wanazungumzia mambo ya kidunia. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akasema, “Sikilizeni, sikilizeni? Kutafuta maisha ya wastani ni katika imani! Kutafuta maisha ya wastani ni sehemu ya imani!” (Abû Dâwûd, Tarajjul, 2)

Simulizi ya Tha’labah ni simulizi yenye mazingatio kwa waumini wenye ukomavu. Alianza kama mtu mwema, lakini akashikwa na tamaa ya kupata mali za kidunia. Hakusikiliza maonyo na muongozo wa Mtukufu Mtume ﷺ, hatimaye mali za dunia zilimlevya, na mwisho wake ukawa wenye hasara na majuto.

Mtukufu Mtume ﷺ anasema: “Mwana wa Adamu anaweza asipate chochote zaidi ya nyumba ya kuishi, nguo ya kuusitiri mwili wake, kipande cha mkate na kikombe cha maji.” (Tirmidhî, Zuhd, 30)

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ waliwausia waumini kutafuta maisha bila kufanya israfu, kutosheka na kile walicho nacho,

na kuwa na mwendo wa katikati. Yeye mwenyewe aliishi hivyo, ili apate kuwa mfano kwa umma wake. Mfumo wa maisha yake unaakisiwa katika dua yake ifuatayo: "Mola wangu! Wapatie riziki inayowatosha familia ya Muhammad." (Bukhârî, Riqâq, 17)

Inafahamika vyema kuwa chanzo cha mgogoro wa kiroho wa zama zetu na mapato ya haramu, kukiuka haki za wengine, mtu kutoridhika na kile alichonacho, na tamaa ya kupata zaidi. Ili kuondosha misukumo hasi, tunapaswa kuchunga kanuni za Kiislamu zinazotuonya dhidi ya kuvunja haki za wengine na kutuhamasisha kupata riziki zetu kwa njia za halali.

Kwa hakika, mali iliyochumwa kwa njia halali au haramu huathiri uhusiano wako na Mwenyezi Mungu na uhusiano wako na watu, na hivyo huathiri majaaliwa yako. Pato la halali au la haramu mara nyingi pia huwa na athari chanya au hasi kwenye mwenendo wa watoto wetu. Kama tunataka watoto wa mfano wasioathiriwa na mambo mabaya, tunapaswa kuhakikisha mali zetu zinapatikana kwa njia halali.

Moyo ukishikamana hasa na maamrisho ya Mwenyezi Mungu na sunna za Mtukufu Mtume ﷺ, utahitaji riziki ya halali, na mwili uliostawishwa kwa riziki hiyo huwa chanzo cha nuru na mambo mema. Ama miili iliyochafuliwa kwa vyakula vya haramu au vyenye kutiliwa shaka, basi miili hiyo huwa chimbuko la shari na uovu. Kwa hali hiyo, wale wanaompenda Mtume ﷺ watafuata wosia na ushauri wake. Watajiepusha na israfu na ubakhili, na watakuwa makini kuhakikisha riziki yao inapatikana kwa njia halali. Kwa kuifuata njia ya Mtukufu Mtume ﷺ yenye nuru, watapata furaha ya kusuhubiana naye huko Akhera.

Tambua kuwa mahitaji yanatofautiana kutoka wakati mmoja kwenda mwingine. Mahitaji yanapaswa kushughulikiwa kulingana na kiwango cha udharura wake. Kama tukitoa pesa na juhudi katika

sadaka lakini ikawa sio katika mahitaji stahiki, matendo yetu hayo yatachukuliwa kuwa ni israfu, kwa sababu tutakuwa tumeshindwa kutathmini mahitaji halisi. Kwa mfano, kama jamii inahitaji sana waumini waliolelewa kwa hisia ya heshima, watu wanaowapenda Waislamu wenzao, kama tukitumia sadaka zetu kwenye eneo jingine tofauti na hile, basi tutakuwa tunazipoteza bure na yatakuwa ni matumizi mabaya. Katika zama ambazo utekelezaji wa misingi ya kidini na maendeleo ya kiroho kwa pamoja vinadhoofika, hitajio kuu ni kuwaunga mkono na kufanya jitihada za kuongeza kiwango cha malezi ya kidini, kimaadili na kiroho.

Waumini wanapaswa kuongeza uwezo wao wa kuainisha mahitaji. Mwenyezi Mungu Mtukufu anaelezea umuhimu wa kuhakikisha kuwa sadaka zinawafikia wale wenye mahitaji zaidi. Anasema ndani ya Qur'an Tukufu:

"Nawapewe mafakiri walio zuilika katika njia za Mwenyezi Mungu, wasio weza kusafiri katika nchi kutafuta riziki. Asiye wajua hali zao huwadhania kuwa ni matajiri kwa sababu ya kujizuia kwao. Utawatambua kwa alama zao…" (Baqarah, 2:273)

Wakati kuna watu wengi sana ambao ni wenye kuhitaji, haitakuwa sahaihi kuwapa watu ambao tunawajua kabisa kuwa sio wahitaji. Yaani, tunapaswa kuwapa sadaka wale wenye kuhitaji kabisa kulingana na mahitaji yao.

Mawlana Jalaluddin Rumi (q.s) anasema:

Kuna watu wengi wenye mali ambao, kama wakiacha kuwapa sadaka wale wasiostahiki, wangefaidika na kujizuia kwao kuliko wanavyofaidika na sadaka zao. Tumia mali ulizojaaliwa na Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa sheria zake! Kutoa sadaka bila misingi sahihi hukufanya uwe mtumwa muasi ambaye hutoa mali za bwana wake kuwapa wezi huku akijifanya ni mkarimu.

Wale wanaohusika na taasisi za misaada ya kibinaadamu wanapaswa kuutambua msingi huu na wawe makini sana wanapopeleka misaada kwa masikini.

Kuna nukta nyingine muhimu ambayo inahitaji kuangaliwa. Tendo fulani linalofanyika katika mazingira tofauti linaweza kuonekana kuwa ni lile lile, lakini litahesabiwa vingine kabisa kulingana na mazingira. Wakati matendo fulani yanaweza kuhesabiwa kuwa ni israfu baada ya kufanywa na mtu mmoja, matendo hay ohayo yanaweza kuhesabiwa vingine iwapo yatafanywa na mtu mwingine, kwa maana watu wana fursa zinazotofautiana kutokana na neema za kiroho na kimaada walizonazo. Hivyo, dhima ya kila mtu kwa Mwenyezi Mungu inategemea vipawa vya mtu husika. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Qur'an:

"Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya iwezavyo..." (Baqarah, 2:286)

Hivyo tunaona kuwa kwa mujibu kipimo cha Mwenyezi Mungu, hakuna jukumu la mtu linalolingana na la mtu mwingine.

Mwenye uwezo mkubwa anapaswa kutoa kiwango kikubwa zaidi cha sadaka kulingana na uwezo na mali yake. Sote tuna wajibu, na tutaulizwa kwa amali njema ambazo tutakuwa tumezifanya na zile ambazo hatukuzifanya.

Hata hivyo, katika jamii yoyote kutakuwa na watu ambao wanaweza kuwa wanafanya chini ya kiwango ambacho fursa zao zinawalazimisha kufanya. Tukiyalinganisha matendo yetu na matendo ya watu hao na kujihesabu kuwa ni wakarimu kwa ulinganisho, ulinganisho huo utakuwa wa makosa. Ndiyo maana tunapaswa kukilinganisha kiwango cha ukarimu wetu na matendo ya Mtukufu Mtume ﷺ na Maswahaba zake. Tunapaswa kuufanya mwenendo wao kuwa kigezo chetu cha kutathmini matendo yetu ya

hisani, na kujitahidi kuwaiga. Wale wanaoonekana kuwa wakarimu mbele ya watu wanaweza wasiwe hivyo mbele ya Mwenyezi Mungu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atujaalie tujiepushe na ya haramu na yale yenye kutiliwa shaka katika mambo yote! Azilinde nyoyo zetu zisielekee kwenye ubadhirifu au ubakhili! Atujaalie kuzitumia neema Zake kulingana na ridhaa Yake, na tuweze kufika mbele Yake tukiwa na nyuso zenye kung'ara na akili zenye amani!

Amiin!...

SURA YA 18

Israfu - 7

Katika Afya na Matumizi ya Chakula na Vinywaji

Mtu hushtuka sana anapoona israfu ikitawala tabia zetu za matumizi ya chakula na vinywaji, katika maisha yetu ya kila siku na hususan wakati wa sherehe za harusi na karamu mbalimbali. Kuandaa karamu za kibadhirifu ili kuonesha ufakhari na uwezo, kuhamasisha ulafi kwa vyakula kayaya, kuvaa mavazi ya mitindo ghali mno – tabia zote hizi za kibadhirifu zitasababisha majuto huko Akhera, kwa maana tutaulizwana kuhisabiwa kuhusu matumizi haya kulingana na kipimo na mizani ya Mwenyezi Mungu.

SURA YA 18

ISRAFU– 7

Katika Afya na Matumizi ya chakula na Vinywaji

Afya ni miongoni mwa neema za Mwenyezi Mungu zisizothaminiwa na kushukuriwa. Mtukufu Mtume ﷺ anaonya juu ya ujinga na upuuzaji wa watu kuhusu neema hii: "Kuna neema mbili ambazo watu hawazithamini ipasavyo: afya na wakati." (Bukhârî, Riqâq, 1) Hivyo anatuonya, sisi umma wake, dhidi ya hasara tunayoweza kuipata kwa kutozijali tunu hizi mbili zenye thamani.

Ibn Umar رضي الله عنه ameripoti kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema: "Unapofika asubuhi, usiisubiri jioni. Unapofika jioni, usiisubiri asubuhi. Unapokuwa na afya, chukua tahadhari kwa ajili ya muda ambao unaweza kuumwa. Katika kipindi chote cha maisha yako, chukua tahadhari kwa ajili ya muda utakaokufa." (Bukhârî, Riqâq, 3)

Mwenyezi Mungu alitupa amana ya mwili, na miili yetu ina haki juu yetu. Ili tuweze kuishi maisha ya unyoofu kikamilifu, ni lazima kuitunza afya ya mwili na ya kiroho pia. Matendo ya ibada yanaweza kufanywa pale tu mtu anapokuwa na mwili wenye afya.

Je mtu asiyekuwa na afya anaweza kuswali kwa utulivu au kufunga kwa amani ya moyo? Ibada nyingi na amali njema zinazofanya nyoyo za watu kuwa karibu zaidi na Mwenyezi Mungu hutegemea neema ya afya. Mtu anapokosa afya, ibada na huduma mbalimbali nazo pia hukosa uzima. Hivyo, tunapokuwa na fursa ya afya, tunapaswa kumshukuru Mwenyezi Mungu kikamilifu kwa neema hii na kuziwekea maanani ibada zetu na utoaji wa sadaka pia.

Kama ilivyo kwa neema nyingine, afya nayo inaweza kufanyiwa israfu iwapo mhusika hatafuata maagizo ya Mwenyezi Mungu yanayohusu kuitunza. Uvutaji wa sigara unaweza kuonekana kuwa jambo dogo, lakini linaweza kuiharibu afya, kama ilivyo kwa matendo mengine ya haramu. Kuitupa afya yako ni kuamiliana na mwili wako kwa israfu na bila kujali. Ilikuepuka israfu ya afya zetu, tunapaswa kuilinda kwa kufuata muongozo wa akili na maamrisho ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hii inahusisha kutafuta virutubisho vyenye afya, lakini pia kuilinda miili yetu dhidi ya sababu za kiasili kama vile joto na baridi iliyopitiliza, na dhidi ya uzembe na upuuzaji, kama vile ajali za barabarani.

Dini yetu inajumuisha mafundisho mbalimbali ya kimwili na kiroho yanayohusu ulinzi na utunzaji wa afya. Yanatuagiza kuwa makini katika ulaji wa vyakula. Yanatuusia kwamba tusiende mahali ambako kuna maradhi ya kuambukiza, lakini pia kama sisi wenyewe tuna maradhi ya kuambukiza, tusitoke mahali tulipo. Dini yetu inatupatia kanuni za msingi za kinga kupitia ngao ya maamrisho na ushauri mbalimbali.

Dini yetu inatuambia kuwa ili tuzilinde afya zetu, tahadhari za kiroho ni muhimu pia. Tahadhari hizi ni pamoja na kutoa sadaka na zaka katika mali zetu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliashiria kiwango cha hadhari za kimaanawi na kiroho kinachohitajika kulinda afya zetu: “Kila kiungo cha mwanadamu kinatoa sadaka.

Ndiyo maana kumhimidi Mwenyezi Mungu ni sadaka; kumshukuru Mwenyezi Mungu ni sadaka, kusema "laa ilaha illallah" ni sadaka; kusema "Allahu Akbar" ni sadaka; kutoa ushauri mzuri ni sadaka; kukataza mabaya ni sadaka. Rakaa mbili zinazoswaliwa kabla ya adhuhuri, nazo pia ni sadaka." (Bukhârî, Sulh, 11)

Kwa hakika, afya na furaha ni neema kubwa ambazo tunawajibika kumshukuru Mwenyezi Mungu. Wajibu huu huweza kutekelezwa kikamilifu kwa kutoa sadaka na zaka katika mali zetu. Vilevile unaweza kutekelezwa kwa kumhimidi Mwenyezi Mungu, kwa kufanya ibada, na kwa kufanya mambo mbalimbali ya kuwahudumia watu ili kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Maswahaba watukufu wa Mtume ﷺ, ambao wamefanywa kuwa mifano kwetu kwa sababu ya maadili yao ya hali ya juu,[43] walifanya juhudi kubwa katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa sababu neema walizojaaliwa na Mwenyezi Mungu walizichukulia kama mtaji wa kuwekeza kwa jili ya maisha ya Akhera. Mwenyezi Mungu Mtukufu akazibariki juhudi na jitihada zao. Maswahaba wa Mtukufu Mtume ﷺ hawakuishi maisha ya anasa tunayoishi sasa, ambayo yamejaa ulazi kupita kiasi, ulafi, starehe na ubadhirifu. Waliishi huku wakitambua kuwa "makazi ya roho kesho ni kaburi."

Mwili, tulioaminiwa kwa muda fulani, isipolishwa ipasavyo, ima kwa sababu ya ubakhili au kwa sababu nyingine, utakumbwa na aina mbalimbali za udhaifu na maradhi. Vilevile, matatizo hayo hujitokeza pindi tunapoupa chakula kupita kiasi. Ukiulisha kwa chakula cha halali au cha haramu, utapata maradhi ya kimaada. Hata hivyo, ukiulisha kwa chakula kilichopatikana kwa njia ya haramu, utapata matatizo ya kimwili na pia utapoteza afya ya kiroho.

43. Tazama: at-Tawbah, 9/100.

Kadiri hali ya kiroho inavyopanda, ndivyo unavyozidi kuwa makini kuhusu vyakula na vinywaji. Kwa mfano, kwa mujibu wa sheria za dini, kuendelea kula baada ya kushiba huhesabiwa kuwa ni israfu na uharibifu. Kwa mujibu wa mafunzo ya Kisufi, kuendelea kula *mpaka* ukashiba huchukuliwa kuwa ni israfu. Kwa ngazi ya ukweli, kula bila kukumbuka uwepo wa Mwenyezi Mungu ni israfu. Na kwa ngazi ya utambuzi wa kumtambua Mwenyezi Mungu, kula bila kutafakari ukuu wa Mwenyezi Mungu katika neema ya chakula huhisabiwa kuwa ni israfu.

Khidhr عليه السلام alimtembelea Abdulkhaliq Gujduwani (q.s), aliyekuwa miongoni mwa Marafiki wa Mwenyezi Mungu. Mazungumzo baina ya wawili hao kuhusu matumizi ya chakula na vinywaji yamejaa mafunzo, kwa sababu yanaonesha kilele cha utambuzi wa kiroho.

Abdulkhaliq Gudjuwani katika kuonesha ukarimu alimkirimu Khidhr chakula, lakini Khidhr عليه السلام alikataa kula, na kuondoka kwenye meza ya chakula. Abdulkhaliq Gudjuwani alishangazwa sana na hali hiyo, akasema: “Hiki ni chakula kilichopatikana kihalali, kwa nini hutaki kula?”

Khidhr akajibu: “Ndiyo, kimepatikana kihalali, lakini aliyekiandaa alikipika akiwa mwenye hasira na mwenye kughafilika.”

Hivyo kiwango cha kiroho katika chakula chetu hakiletwi tu kwa chakula hicho kupatikana kihalali, bali pia kwa hali ya kisaikolojia ya wale wanaokiandaa. Kiwango cha kiroho katika sifa zetu za ndani na katika ibada zetu hutengenezwa na kiwango cha kiroho kinachopatikana katika chakula chetu. Hivyo, tazama jinsi tunavyopaswa kuwa na umakini kuhusu chakula tunachokitumia.

Vyakula vinavyouzwa hadharani huonekana na macho ya watu, baadhi yao ni maskini ambao wangetamani kuvipata lakini

hawawezi kumudu. Watu hawa wana haki fulani fulani juu ya chakula hicho kwa sababu ya wao kuoneshwa chakula hicho. Vilevile, hatujui jinsi vyakula vinavyoandaliwa kibiashara. Kwa bahati mbaya, mara nyingi watu hawajali kuhusu madhara yanayoweza kusababishwa na chakula hicho. Lakini, historia ya chakula tunachokitumia, yaani jinsi kilivyoandaliwa na kutufikia, hutuathiri.

Chakula kilichopatikana kihalali kina nafasi muhimu katika kuutakasa moyo. Abdulqadir Jaylaani (q.s) anasema: "Chakula kisichopatikana kihalali huua moyo; chakula kilichopatikana kihalali huupa uhai. Kuna chakula kinachokufanya ushughulishwe na dunia. Pia kuna chakula kinachokufanya ushughulishwe na Akhera. Kuna hata chakula kinachokufanya umpende Mwenyezi Mungu Mtukufu."

Mawlana Jalaaluddin Rumi (q.s) anasema: "Usiku wa jana baadhi ya vipande cha chakula chenye kutiliwa shaka viliingia tumboni mwangu na kuziba njia ya zinduko na muongozo." Maneno yake yanaonesha kuwa tunapaswa kuwa makini kuhusu kiwango cha kiroho katika chakula tunachotumia kama tunavyokuwa makini kwenye viwango vya kimaada vya chakula hicho.

Vilevile Mawlana Rumi anasema: *"Usipupie kuulea mwili kupita kiasi. Mwisho wa mwili huo ni kafara itakayotolewa kwa ardhi. Ilee roho yako kwa maana ni roho yako ndiyo itakayopata heshima na kufika katika viwanja vitukufu…Usiupe mwili wako mafuta au vitu vitamu kupita kiasi, kwa sababu wanaoupa chakula kupita kiasi hutumbukia katika shimo la kutekeleza haja za kinafsi na mwishoni hupata fedheha."*

Kukithirisha katika mambo hayo ni jambo linalokwenda kinyume na hadhi na heshima ya mwanadamu.

Mababu wetu wema walisema: "Mwenyezi Mungu aliiweka elimu ya tiba katika nusu ya aya moja ya Qur'an isemayo:

"...kuleni, na kunyweni na wala msifanye ubadhirifu..." (A'raf, 7:31)

Walisisitiza juu ya umuhimu wa kujiepusha na yubadhirifu wakati wa kula na kunywa ili kuwa na maisha yenye afya kiroho na kimwili.[44]

Hadith moja ya Mtukufu Mtume ﷺ inasema: "Kula, kunywa, vaa na toa sadaka bila kuangukia katika israfu na kiburi." (Bukhârî, Libâs, 1) Kauli hii inaonesha mipaka ambayo watu wanatakiwa kuichunga wakati wa kukidhi mahitaji yao. Katika hadith nyingine ya Mtukufu Mtume ﷺ, tunasoma: "Ni israfu kula kila kitu unachokitamani!" (Ibn Mâja, At`ima, 51)

Kula kila kitu kwa uroho hujulikana kama ulafi, na dini yetu imekataza jambo hilo. Vilevile, maneno haya yanaonesha kwamba kuwa na fursa ya kupenda jambo hakutoi uhalali wa kuliendekeza. Pindi Umar ؓ alipokutana na Jabir ؓ, ambaye alikuwa na kipindi cha nyama mkononi mwake, alimuuliza: "Ni nini hiyo?"

Jabir ؓ akajibu: "Ni kipande cha nyama nilichokinunua kwa sababu nilikitamani."

Umar ؓ akasema: "Unanunua kila kitu unachokitamani? Je, huogopi kuwa miongoni mwa wale waliosifiwa katika aya: *'Nyinyi mlitwaa vitu vyenu vizuri katika uhai wa duniani, na mkastareheshwa navyo...'"* (Ahkâf 46:20)" (Ibn Hanbal, Zuhd, uk.124)

Mtukufu Mtume wetu ﷺ alieleza kipimo ambacho mtu anapaswa kukichunga kuhusu ulaji: "Mwanadamu hajakizaja kikombe hatari zaidi ya tumbo lake. Kwa hakika vipande vichache vya chakula vinatosha kuishi. Lakini kama mtu akilazimika kula, basi atenge theluthi ya tumbo lake kwa ajili ya chakula, theluthi

44. Tazama: Ibn Kathîr, Taf s î r , II, 219.

nyingine kwa ajili ya kinywaji, na theluthi ya tatu kwa ajili ya pumzi!" (Tirmidhî, Zuhd, 47)

Tukio lifuatalo lililotokea wakati wa Zama za Furaha, linaonesha wazi umuhimu wa kufuata muongozo wa Mtukufu Mtume ﷺ kuhusu utumiaji wa chakula na vinywaji.

Katika zawadi nyingi zenye thamani zilizotumwa na gavana wa Alexandria kwa Mtukufu Mtume wetu ﷺ ni pamoja na tabibu. Mtukufu Mtume ﷺ alimwambia tabibu huyo: "Rudi kwa familia yako. Sisi ni watu ambao hatuli bila kuwa na njaa, na tukila hatujazi matumbo yetu." (Halabî, Insân al-`Uyûn, III, 299)

Maneno haya ya Mtukufu Mtume ﷺ yanajumuisha maelekezo ya kuponya maradhi mbalimbali yatokanayo na ulaji kipita kiasi na israfu inayoshuhudiwa katika zam zetu.

Umar رضي الله عنه anatoa wosia ufuatao kuhusu jambo hili: "Epuka kulijaza sana tumbo lako wa chakula na vinywaji. Vinginevyo itausababishia madhara mwili wako, litaibua maradhi na kukufanya uwe mvivu wa kutekeleza swala zako. Fuata njia ya katikati katika utumiaji wa chakula na vinywaji! Hiyo itakuwa na manufaa kwa mwili wako, na pia itakuepusha na israfu." (Ali al-Muttaqî, Kanz, XV, 433/41713)

Thevenôt, msafiri wa Kimagharibi, aliandika kitabu cha uchunguzi alioufanya wakati wa safari zake mbalimbali na kukichapisha mwaka 1665 mjini Paris. Katika kitabu hicho aliandika jinsi mababu zetu, waliobeba bendera ya Uislamu kwa karne nyingi, walivyoyapangilia maisha yao. Alibaini usafi, wepesi na mfumo wao wa kati na kati katika ulaji, na jinsi utamaduni huu ulivyozaa jamii ya watu wenye afya. Anasema: Waturuki wanaishi maisha yenye afya na ni nadra kuugua. Hutakuta magonjwa yenye uhusiano na figo na magonjwa mengine ya hatari tunayokumbana nayo katika nchi yetu. Hawayajui hata majina ya magonjwa hayo.

Ninadhani kuwa sababu ya Waturuki kuwa na hali hizo nzuri za kiafya ni kwamba wanaoga mara kwa mara na wana kiasi katika utumiaji wa chakula na vinywaji. Wanakula kiasi kidogo tu cha chakula. Na hawatumii vyakula mchanganyiko, tofauti na aina ya vyakula vinavyotumika miongoni mwa Wakristo.[45]

Kuna methali moja inatukumbusha: "Mtu hapaswi kuishi kwa ajili ya kula, bali ale kwa ajili ya kuishi!" Kanuni hii inaelezea sifa muhimu ya waumini. Kisa kifuatacho kinaielezea mizani hii ya maadili ya Kiislamu. Ni kisa kilichojaa mafunzo na mazingatio:

Siku moja, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alijiwa na mgeni, ambaye hakuwa Muislamu. Mtukufu Mtume ﷺ akaagiza mgeni huyo aandaliwe maziwa ya kondoo. Walimkamua kondoo huyo na maziwa yakaletwa. Mgeni alikunywa maziwa yote aliyoletewa. Hivyo wakaleta maziwa mengine, na mgeni akayanywa yote. Hili lilijirudia mara saba; mgeni alikunywa sufuria saba za maziwa. Siku iliyofuata mgeni yule alisilimu. Kwa mara nyingine Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliagiza wamletee mgeni maziwa. Walileta sufuria moja la maziwa, na mgeni akayanywa yote. Mtukufu Mtume ﷺ akaagiza aletewe sufuria nyingine, lakini mara hii mgeni yule hakuyanywa yote. Hapo Mtukufu Mtume ﷺ akasema: "Muumini hunywa kwa utumbo mmoja, ilhali kafiri hunywa kwa matumbo saba!" (Muslim, Ashriba', 186)

Mwenyezi Mungu Mtukufu anatutaka tuwe watu wa wastani katika utumiaji wa vyakula na vinywaji na tujiepushe na desturi inayofuatwa na wasiokuwa Waislamu katika jambo hili. Anatuonya:

"...walio kufuru hujifurahisha na hula kama walavyo wanyama, na Moto ndio makaazi yao." (Muhammad, 47:12)

45. M. De Thevenot, *Relation d'un Voyage Fait au Levant*, s. 58, Paris, 1665.

Tabia zote zinazoondosha baraka ya chakula ni katika israfu. Hivyo unapoanza kula bila kunawa mikono na bila kumkumbuka Mwenyezi Mungu, na asipomshukuru Mwenyezi Mungu mwisho wa chakula chake, hiyo haitakuwa tu ukosefu wa shukrani, bali pia itakuwa israfu.

Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Baraka ya chakula inapatikana katika kuosha mikono kabla na baada ya kula." (Tirmidhî, At`ima, 39)

"Mwenye kulala bila kunawa mikono yake baada ya kula, akipata madhara, asimlaumu yeyote bali ajilaumu mwenyewe!" (Abû Dâwûd, At'ima, 53)

Mababu zetu walikuwa makini sana kuhusu kuosha mikono kabla na baada ya kula. Ricaut, katibu aliyekuwa akifanya kazi katika Ubalozi wa Uingereza mjini Istanbul katika karne ya kumi na saba (na ambaye alikuwa adui wa Waturuki), aliuelezea umakini wa mababu zetu kuhusu afya ya chakula. Alisema: "Kunawa mikono ni desturi mashuhuri sana miongoni mwa Waturuki kiasi kwamba wana msemo kuwa Mwenyezi Mungu aliumba chakula ili watu wapate kuosha mikono!"[46]

Hivyo kuchunga kanuni za afya wakati wa kula au kunywa ni nyenzo ya kuongeza baraka na husaidia katika afya na amani ya kimwili na kiroho. Aidha, watu wanapoanza kula kwa kusema *bismillaah* (kwa jina la Mwenyezi Mungu) na kumalizia kwa kusema *Alhamdulillah* (himidi ni za Mwenyezi Mungu), chakula hicho huwa ni ponyo, ilhali chakula kinacholiwa bila kumtaja na kumshukuru Mwenyezi Mungu huzalisha uzembe na uzito kupita kiasi. Mtukufu Mtume wetu ﷺ anasema:

Mtu akisema *bismillah* anapoingia nyumbani kwake na anapoanza kula, Shetani huwaambia askari wake, "Hapa hamtapata mahali pa kulala wala chakula." Lakini asiposema *bismillah*

46. Ricaut, *Histoire de l'état Présent de l'Empire Ottoman*, s. 285, Paris, 1670.

wakati wa kuingia nyumbani kwake, Shetani huwaambia askari wake, "Hapa ni sehemu nzuri kwenu kuutumia usiku wa leo." Na asiposema *bismillah* anapoanza kula, Shetani huwaambia askari wake, "Mmepata sehemu ya kukaa na kula usiku huu." (Muslim, Ashriba', 103)

Bibi Aisha ﵂ anasimulia:

Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikaa kwa ajili ya chakula pamoja na Maswahaba zake. Bedui mmoja akaja; alikula chakula chote kwa mikupuo miwili. Hapo Mtume wetu ﷺ akasema: "Kama angesema *bismillah,* chakula hiki kingetutosha sisi wote. Hivyo mmoja wenu atakapoanza kula, aseme *bismillah*. Akisahau kusema mwanzo, basi aseme *bismillah fi awwalihi wa akhirihi,* (yaani, kwa jina la Mwenyezi Mungu mwanzo na mwisho)."

Adabu za kunywa maji ni kusema *bismillah* na kunywa kwa mikupuo mitatu; na mwishoni tuseme *Alhamdulillah*. Mtume wetu ﷺ alikuwa akinywa maji na vinywaji vingine kwa kuvigawa sehemu tatu. Alisema: "Usinywe vitu kwa mkupuo mmoja, kama ngamia. Kunywa kwa mikupuo miwili au mitatu. Sema *bismillah* kabla ya kunywa; na mwisho sema *Alhamdulillah*. (Tirmidhî, Ashriba, 13) Vilevile Mtume wetu ﷺ alikataza kupuliza ndani ya kinywaji kwa sababu yoyote ile.

Mtu mmoja alimuuliza: "Nifanye nini nionapo kitu kimedondokea katika jagi la maji?"

Mtukufu Mtume ﷺ akasema: "Kimwage kitu hicho!"

Kisha mtu huyo akasema: "Sioni kama kiu yangu inakatika ninapokunywa." Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akamshauri anywe maji kwa mikupuo mitatu na kusema: "Kisha kiondoshe kikombe cha maji kinywani mwako!" (Tirmidhî, Ashriba', 15)

Vilevile kula peke yako hupunguza baraka ya chakula, na ni aina ya israfu… Mtume wetu ﷺ anasema kuwa, “Umoja ni rehma, na upweke ni moto.” Alituusia kuwa pamoja wakati wa kula.

Wahshi ibn Harb ﷺ anasimulia kuwa baadhi ya Maswahaba walimwambia Mtukufu Mtume ﷺ: “Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Tunakula lakini hatuhisi kutosheka.”

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akauliza, “Labda mnakula peke yenu?”

Waksema, “Ndiyo, tunakula peke yetu!”

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akawaambia, “Kule pamoja na mseme *bismillah*, ili chakula chenu kipate kubarikiwa.” (Abû Dâwûd, At`ima, 14)

Mtukufu Mtume ﷺ pia alituonya, “Iwapo mmoja wenu akidondosha kipande cha chakula kikachafuka, basi auondoshe uchafu hule na kukila kipende hicho. Msimuachie Shetani.” Akiendelea kutuonya, alituhamasisha kula chakula chote kilichopo kwenye sahani, akasema: “Hamjui mahali baraka inapopatikana ndani ya chakula.” (Muslim, Ashriba’, 136)

Mtu hushtuka sana anapoona israfu ikitawala tabia zetu za matumizi ya chakula na vinywaji, katika maisha yetu ya kila siku na hususan wakati wa sherehe za harusi na karamu mbalimbali. Nyakati hizo kiwango cha israfu huwa ni kikubwa sana. Tunaweza kufikiria kiwango cha israfu yetu kwa kuangalia ulaji wetu wa mkate. Ingawa ni ngumu kupima kiwango cha israfu kinachohusishwa katika matumizi mengine, tunaweza kukitathimini kwa kutazama kinachotokea kwenye vipande vya mkate. Kwa kweli matokeo ya tathimini yanatisha sana.

Kuandaa karamu za kibadhirifu ili kuonesha ufakhari na uwezo, kuhamasisha ulafi kwa vyakula kayaya, kuvaa mavazi ya mitindo ghali mno – tabia zote hizi za kibadhirifu zitasababisha

majuto huko Akhera, kwa maana tutaulizwana kuhisabiwa kuhusu matumizi haya kulingana na kipimo na mizani ya Mwenyezi Mungu.

Sherehe za harusi na karamu ni njia muhimu ya kuimaisha hisia za umoja. Kwa bahati mbaya, sherehe hizo zinapoandaliwa kwa ajili ya maonesho, hazifanyi tena kazi ya kujenga hisia za umoja. Badala yake husukuma watu kwenye hisia za uovu kama vile ufakhari, kiburi, wivu na husda, vitu ambavyo huwapeleka kwenye majuto na hasara. Jamii ambazo sherehe hizo huhamasishwa hujiweka mbali na rehma na baraka za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kwa mukhtasari, mwisho wa maisha yaliyotawaliwa na ubadhirifu na israfu ni hasara kubwa ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Hakika wabadhirifu ni ndugu wa Mashet'ani." (Isrâ, 17:27)

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anatukumbusha kuwa huko Akhera tutaulizwa juu ya neema na amana zote tulizopata wakati wa uhai wetu duniani. Alitutaka tujiepushe na mghafala na uzembe. "Unyayo wa mja hautaondoka kabla hajaulizwa walivyoutumia uhai wake, aliitumia vipi elimu yake, alizipata wapi na alizitumia vipi mali zake, na alizitumia vipi nguvu za mwili wake." (Tirmidhî, Qiyâmah, 1)

Hivyo hatupaswi kusahau kwamba kuvuka mipaka tuliyowekewa na Mwenyezi Mungu kuhusu matumizi ya chakula na vinywaji ni israfu. Kuipuuza neema ya afya na kuipoteza ni israfu. Kutumia kipindi cha uhai wetu katika mambo ya kipuuzi ni israfu. Kuacha kuzitunza amana za kimaada na za kiroho tulizoaminiwa, kuzielekeza fikra na hisia zetu kwenye uelekeo mbya – yote haya ni israfu. Katika eneo la malezi, ambayo huitengeneza shakhsia ya mwanadamu, kuacha kuwasaidia watu kuelewa kuwa ni viumbe wanaoheshimika zaidi kuliko viumbe wote, na hivyo kuwapoteza, ni israfu mbaya kabisa.

Hakika ni jukumu la lazima kwa wazazi kuwapatia watoto wao malezi ayatakayowahamasisha kuishika Qur'an na sunna za Mtukufu Mtume ﷺ. Malezi haya yanatakiwa kuwa yale yatakayowazuia watoto kupoteza maisha yao ya kiroho. Vilevile, jitihada katika eneo hili huonesha ni kwa kiasi gani tunaipenda Qur'an na Mtukufu Mtume ﷺ, na ni kwa kiasi gani tunashikamana navyo. Kama asemavyo Mtukufu Mtume ﷺ: "Nimewaachieni vitu viwili: Kitabu na Sunnah." (Muwatta', Qadar, 3)

Hivyo yatupasa tujitahidi kuongeza mapenzi yetu kuipenda Qur'an Takatifu. Na yatupasa kuweka umakini kubwa kwenye malezi ya kiroho na kimaadili kwa watoto wetu, kwa kuwa haya ni mambo yanayopuuzwa sana katika maisha rasmi ya malezi.

Kwa hakika, urithi mkubwa ambao tunaweza kuwaachia watoto wetu ni utamaduni wa Qur'an Takatifu na Sunna za Mtukufu Mtume ﷺ. Tunapaswa kufanya juhudi kuwaongoza watoto wetu kwenye kushikamana na sifa za kimaadili za Mtukufu Mtume ﷺ, ambazo ni utekelezaji wa miongozo ya Qur'an kikamilifu. Hatupaswi kuyapoteza maisha yao ya milele kwa sababu ya wasiwasi kuhusu maisha yao ya mpito.

Katika muktadha huu, kama tunawapenda watoto wetu, kama tunataka kuwalinda dhidi ya aina zote za hatari, na kama tunataka tuwe nao Akhera, tunapaswa kuhakikisha wanapata malezi yanayowaweka katika imani. Mwenyezi Mungu Mtukufu anaelezea jinsi juhudi hizi zinavyoweza kuwa sababu ya kupata furaha Akhera:

"Na walio amini na dhuriya zao wakawafuata kwa Imani tutawakutanisha nao dhuriya zao, na wala hatutawapunja hata kidogo katika vitendo vyao. Kila mtu lazima atapata alicho kichuma." (at-Tûr, 52:21)

Waumini wanaopata baraka hii watakuwa pamoja na dhuriya zao wenye imani huko Akhera. Hii ni neema ya pekee watakayopewa, kwamba wataishi Peponi wakiwa pamoja na watoto wao. Kwa namna hii raha na furaha ya wazazi hupata kukamilika. Sharti

la kupata neema hiyo ni kwa watoto wetu kulelewa kama waumini, walelewe katika mazingira ya Qur'an Takatifu na sunna za Mtukufu Mtume ﷺ.

Kutekeleza wajibu wetu kwa watoto wetu kuhusu maisha ya Akhera ni dhima nzito iliyopo mabegani mwetu. Tujiepushe na "israfu ya rasilimali za kibinaadamu" ambayo ndiyo israfu mbaya kabisa kuliko aina zote za israfu.

❁

Iwapo shughuli zetu muhimu zitaangaliwa kwa mwanga wa vipimo tulivyoviainisha kuhusu israfu, tutaona jinsi matumizi ya dhana hii yalivyokuwa makubwa. Israfu inahusisha kiwango kikubwa cha tabia zinazoonekana katika mifumo mbalimbali katika kila eneo la maisha yetu, kuanzia kwenye kuchukia sana mpaka kwenye kupenda sana, na kwenye ubadhirifu katika sherehe na karamu.

Tulichofanya hapa ni kujaribu kuainisha viwango muhimu na kuonesha kwa ujumla matumizi yake kwa kuchambua masuala machache yenye umuhimu. Lakini viwango na misimamo tuliyojaribu kuainisha hapa hayajifungi kwenye mada tulizozieleza tu: bali yanaweza kuhusika kwenye aina zote za matendo ya mwanadamu. Hivyo, hatupaswi kusahau kuwa ni wajibu wetu kuvitumia viwango hivi popote panapofaa kuvitumia, na hivyo kuepuka aina zote za ubadhirifu na ubakhili.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atuepushe na kufanya mambo kupita kiasi au kutofanya kupita kiasi! Atujaalie kupata maisha ya utiifu anayoyaridhia! Atuongoze ili tutumie neema Zake kwa mujibu wa kanuni kuu ya uwastani, na tuweze kumshukuru kikamilifu kwa neema hizo!

Amiin…

SURA YA 19

"Hakuna Udhuru Wa Kukiuka Mpaka Wa Halali Na Haramu"

Mahojiano kuhusu Utambuzi wa Kiislamu Katika Ulimwengu wa Biashara

Pato la haramu ni mfano wa puto linalopasuka ghafla. Baadhi ya Maputo haya hupasuka katika maisha haya, na mengine yatapasuka Akhera. Ongezeko kubwa la pato hilo linaweza kukupa furaha sana, lakini ukweli wake wa kiroho ni wenye kutia hasara sana. Pato la haramu hukufanya ufilisike milele.

Ili kutathmini kiwango cha kiroho cha pato letu,tunaweza kuangalia tunalitumia mahali gani. Kuna methali isemayo, "Pesa ni kama nyoka: hutokea shimo lililoingilia."

SURA YA 19

"HAKUNA UDHURU WA KUKIUKA MPAKA WA HALALI NA HARAMU"

Mahojiano kuhusu Utambuzi wa Kiislamu Katika Ulimwengu wa Biashara

Mheshimiwa Ustadh! Siku hizi watu wanazungumzia uhusiano uliopo baina ya Uislamu na ubepari, na kuhoji kwamba Waislamu wanaanza kuunga mkono ubepari. Una maoni gani kuhusu suala hili?

Mahali ambapo ubepari hutokea na kustawi ni mahali ambapo mitazamo kama vile kutosheka na kumtegemea Mwenyezi Mungu imedhoofika, na badala yake tamaa ya dunia na vishawishi vya mapato ya haramu vimekuwa na nguvu na kujiimarisha. Kwa sababu ya nguvu ya vishawishi hivyo, Waislamu wanapaswa kupitia katika malezi ya Kisufi ili kuzidhibiti tamaa na wasiwasi wao. Kuzidhibiti hali hizi kunaweza kufikiwa kwa kuimarisha hali ya kutosheka na kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kutosheka ndio utajiri wa kweli. Kutosheka hutuweka huru dhidi ya tamaa ya pesa na mali, tamaa inayowafanya watu kuwa watumwa. Lakini Muislamu asipoisafisha nafsi yake na kuutakasa

moyo wake, anaweza kujikuta amenasa katika njia za kibepari ambazo hazitambui mipaka yoyote zaidi ya pesa.

Si ubepari wala usoshalisti unaoruhusu kuwepo kwa sifa za moyo na maadili ya dhamiri. Mfumo mmoja kati ya hiyo unadai kuwa mali ni milki ya jamii; mwingine unadai kuwa ni miliki ya watu binafsi. Mifumo yote miwili inatengenezwa na mawazo ya umini na unyonyaji. Katika mifumo yote miwili, watu wanakuwa kama meno ya gurudumu.

Kwa mujibu wa Uislamu, mali ni milki ya Mwenyezi Mungu. Mtu anapokuwa na mtazamo huo, hakuna nafasi ya umimi na unyonyaji. Uchumi wa Kiislamu unaanza na kutatua tatizo la maisha ya mwanadamu. Kushirikiana na kuwasaidia wengine, hususan maskini, ni sharti la dini, ni wajibu. Mwenyezi Mungu Mtukufu ametangaza kuwa maskini wana haki kwenye mali za matajiri:

"Na katika mali yao ipo haki ya mwenye kuomba na asiye omba." (Dhâriyât 51:19)

Msingi hii ni aina ya malezi na matunzo kuhusu matumizi ya pesa, na ni njia ya kuwaweka watu pamoja. Kwa maana kwamba, katika Uislamu pesa sio kitu kinachotamaniwa kukusanywa na kulimbikizwa, bali ni amana inayotakiwa kutolewa au kutumiwa. Ikitolewa au kutumiwa ipasavyo, kama fungu la maskini limetolewa, hapo mali huwa nyenzo kubwa ya kumtumikia Mwenyezi Mungu Mtukufu. Lakini, kama sharti la kutekeleza haya, ni muhimu kuzingatia pesa hizo zimepatikana wapi na kwa vipi. Kwa maana kila kitu kinachotafutwa lazima kutakuwa na njia iliyotumika kukitafuta. Moyo wa mtafutaji hutengenezwa na jinsi pesa husika ilivyotafutwa. Kisha matumizi ya pesa hiyo yanategemea jinsi moyo ulivyotengenezwa, shakhsia ya yule anayeitoa au kuitumia. Hivyo tunapaswa kuwa makini mno kuhusu njia tunayoyumia kuchuma maisha yetu.

Kuna aina Ngapi za Kipato?

Yaonekana kuwa aina mbili za kipato. Ya kwanza ni kipato kinachopatikana kwa mujibu wa taratibu za kidini na misingi ya utambuzi, ambayo msingi wake ni uchungaji wa misingi iliyowekwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hii inajumuisha biashara, ambayo ina taratibu na misingi yake ya kimaadili.

Uhalali katika aina yoyote ya chumo ni jambo la lazima: hakuna udhuru wa kuwa na umimi unaopelekea kuwahadaa wengine. Hata kama chumo la mtu linaweza lisiongezeke kwa haraka pindi linapotengenezwa kihalali, thamani yake ya kiroho daima huongezeka. Mali hiyo hutenga kiasi fulani kwa ajili ya sadaka, kusaidia mambo mema na mazuri. Jambo hili humpa mhusika amani ya moyo na adhamiri. Waislamu wanaziendesha mali zao kulingana na taratibu hizo huwa na huruma kwa viumbe wote, na kwa mwanadamu kuonesha huruma ndiye njia pekee ya kupata huruma ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anasema: "Wahurumieni walio ardhini, ili wale walio mbinguni wapate kukuhurumieni!" (Tirmidhî, Birr, 16)

Historia ya pesa kimaadili huwa na taathira kwenye hisia za mwenye nayo. Ili kutathmini kiwango cha kiroho cha pato letu,tunaweza kuangalia tunalitumia mahali gani. Kuna methali isemayo, "Pesa ni kama nyoka: hutokea shimo lililoingilia.

Aina nyingine ni ipi?

Aina ya pili ya pato ni ile inayopatikana kwa njia ya mabavu au nguvu. Kwa ujumla aina hii ya pato ni ya haramu. Hukusanywa kwa dhulma na kutumia na kupokea hongo. Kimsingi ni mali hatari.

Pato la haramu ni mfano wa puto linalopasuka ghafla. Baadhi ya Maputo haya hupasuka katika maisha haya, na mengine yatapasuka Akhera. Ongezeko kubwa la pato hilo linaweza kukupa furaha sana, lakini ukweli wake wa kiroho ni wenye kutia hasara sana. Pato la haramu hukufanya ufilisike milele.

Mali kama hiyo ni nadra sana kutumika kwa ajili ya sadaka, kusaidia mambo mema na mazuri. Kwa kiwango kikubwa ni sehemu ndogo ya mali hiyo ndiyo inayoweza kuwa na upekee…

Kwa bahati mbaya, siku hizi aina hii ya pili ya pato inaonekana kumshawishi kila mtu. Mfumo wa kibepari unahamasisha aina hii ya mali. Inasikitisha sana kwamba Waislamu wengi wanaonekana pia kuiweka katika nyoyo zao. Watu wengi wamepetwa na uchu wa pesa.

Jambo la kufanya kabla ya kutafuta kipato ni kufikiria utakavyokwenda kujibu huko Akhera. Pindi nyoyo zinapokosa hisia na watu wakaacha kujali kuhusu Akhera, ni rahisi sana kugeuka kuwa wanyama wasiotambua mipaka au sheria, na hugeuka kuwa wapokonyaji wasio na huruma wa haki za watu. Kwa kutumia wasiwasi na tamaa ya mwanadamu, ubepari unawasukuma watu kuwa wanyonyaji. Tunaweza kupata mifano mengi ulimwenguni inayounga mkono hili. Watu wanadhalilishwa kwa sababu ya pesa. Mtazamo huo unawezaje kukaa pamoja na thamani ya mwanadamu? Husababisha utengenezaji na utumiaji wa mabomu yasiyobagua: mimea na wanyama, watoto na wakubwa, wagonjwa na wazee wote hugeuka kuwa wahanga na walengwa. Hakuna huruma, hakuna upole. Je pesa iliyopatikana kwa damu za watu wasiokuwa na hatia na masikini zinaweza kujenga au kutengeneza ubinadamu? Lakini hizo ndizo mali za ubepari usiokuwa na huruma zinazomdhalilisha mwanadamu siku hadi siku. Umeifanya pesa kuwa sanamu linaloabudiwa.

Uislamu unapendekeza njia gani?

Kama ilivyo katika mambo mengine, Uislamu unaona kuwa waja wanawajibika kwa Mwenyezi Mungu kuhusu mali. Kwa sababu Mwenyezi Mungu alimpa kila kitu mwanadamu kama amana. Qur'an Tukufu inasema:

"Tena bila ya shaka mtaulizwa siku hiyo juu ya neema." (at-Takâthur 102:8)

Hivyo mtu anapaswa kutafuta mali kulingana na vipimo vya kanuni na uwajibikaji. Hakuna udhuru wa kukiuka mipaka ya halali na haramu. Kusema "Ninachukua mali hii niweze kufanya mambo mema hapo baadaye," ni njia mbaya: ni kujidanganya. Uislamu hauikubali kanuni ya "chuma upendavyo na tumia upendavyo!" Hivyo Waislamu wanapaswa kuukataa, moja kwa moja, msingi wa nadharia ya ubepari: kukusanya na kutumia bila mipaka.

Leo hii, katika zama ambazo mali zimewatia wanadamu utumwani, Muislamu anapaswa kujipamba kwa maadili ya hali ya juu kuliko hata huko nyuma. Anapaswa kujipamba khofu ya kumuogopa Mwenyezi Mungu, kuheshimu sana haki za wengine, na kudumisha hisia ya uwajibikaji na dhima.

Kwa mfano, Waislamu wanapaswa kuepuka kuingia mikataba ya kidhulma ili kuepuka matatizo ya kibiashara au mgogoro wa kiuchumi. Tunapaswa kuyakabili matatizo yetu ya kiuchumi kwa kutaka msaada katika taasisi za kifedha za Kiislamu. Kujiepusha na kutoa au kupokea riba ni jambo muhimu sana katika dhima ya maisha yetu ya duniani na hali ya maisha yetu ya Akhera.

Suala jingine ambalo tunapaswa kulitazama ili kuzifanya nafsi na mali zetu kuwa safi kiroho ni kujiepusha na hongo zinazotolewa kwa ajili ya mikataba chini ya kivuli cha takrima au

zawadi. Unaweza kubadilisha jina la kitendo, lakini asili ya tendo hilo itabaki kuwa ile ile. Majina mapya kwa matendo haramu ya zamani ni jaribio lisilokuwa na manufaa la kujifariji kuhusu kile tunachokifanya: majina hayo ni mbao za Moto zinazotuzuia kuhoji matendo yetu. Abdullah ibn Amr ﵁, mmoja wa Maswaba wa Mtukufu Mtume ﷺ, anasimulia kuwa Mtukufu Mtume ﷺ aliwalaani wale wanaochukua hongo na wale wanaozitoa. (Abû Dâwûd, `Aqdiyyah, 4:3580)

Kwa bahati mbaya, siku hizi mali imewekwa sumu ya utamaduni huu, na tamaduni nyingine zinazohusiana nao, kutoka kila upande. Muislamu asipokuwa mwangalifu, makini na mwenye kutambua kama ambavyo angekuwa pindi mtu anapotembea katika sehemu iliyotapakazwa mabomu ya kutega, hawezi kuilinda mali yake dhidi ya sumu hizi.

Unashauri uangalifu, umakini na hatua zipi?

Hatupaswi kuyatengeneza maisha yetu ya kibiashara kulingana na unyonyaji na umimi wa ubepari, bali kwa kuchunga mipaka ya halali na haramu.

Aidha, tunapaswa kuepuka kuratibu mambo yetu katika kuutumikia mfumo wa kiuchumi unaohamasisha israfu. Kuongezeka kwa ubadhirifu na anasa zitaiharibu vibaya jamii yetu. Kadi za mikopo, ambazo husababisha ongezeko la matumizi, nazo pia ni mitego ya kiuchumi: ni nyenzo za unyonyaji. Kuwa mwenye mahitaji hakulalishi matumizi ya kadi hizo. Uislamu umetoa suluhisho bora kwa wale wenye shida lakini sio pesa: *qard hasan* (mkopo mzuri kwa ajili ya Mwenyezi Mungu). Aina hii ya mkopo umewekwa maalumu kwa ajili ya kuwafariji wale wenye matatizo ya kifedha na kuwasaidia kurejesha hali zao. Aina ya mkopo

unaotolewa na kadi za mikopo, huwasababisha wale wanaozitumia kufilisika. Ni mfumo ambao wanaofaidika ni wale wanaokufanya utumie, sio wale wanaotumia.

Matangazo hukusukuma kutumia ili kwamba watu wengine usiowaona wapate kukutumia kutengeneza pesa. Katika hili humnyonya hata masikini, bila kuhisi dhima yoyote. Watu wengi baada ya kuvutiwa na matangazo hayo yenye kudanganya, hubaki kuwa waathirika wa mifumo isiyokuwa ya kihalali wala kisheria. Kwa mfano, tangazo linaweza kuja na ujumbe, "Binti ataonekana mrembo na mwenye mvuto iwapo atatumia bidhaa hii nah ii! Ukifanya hivyo, utakuwa na mvuto sana na kufuatwa!" Binti anapoliona tangazo hili hutamani sana kupata bidhaa hizo. Lakini kwa kuwa hana pesa ya kuweza kuvigharamia, anaweza kuanza kwenda kinyume na maadili na kuyaharibu maisha yake…

Hivyo basi, tunapaswa kukumbuka kuwa utajiri mkubwa kabisa ni kuridhika na kutosheka na kile ulicho nacho. Mwenyezi Mungu Mtukufu kutuamrisha: "Tajirika!" bali alituamrisha: "Tafuta riziki yako kihalali, itumie kihalali, na toa sadaka!" Tusipowasahau masikini na wenye shida, tutatengeneza maisha yetu ya kiuchumi kwenye misingi halali.

Inaonekana kwamba Waislamu wanaoshikamana na maagizo ya kidini sasa wanabadili msimamo wao.

Kwa bahati mbaya, leo ubepari umeuharibu sana ulimwengu wetu wa kiroho kiasi kwamba hata katika makampuni ambayo wamiliki wake wana hisia za kidini, imekuwa ni kawaida kufanya biashara katika namna inayokinzana na maadili na taratibu za Kiislamu. Kuna watu wengi ambao huswali kila siku na wameenda Hijja, lakini husema, "Lazima nipate zaidi ili niweze kutoa sadaka

zaidi!" Lakini hoja yao hiyo haiwezi kuhalalishwa. Katika maeneo mengi utakuta mchanganyiko wa halali na haramu. Kwa mfano, tangazo linalotangazwa bila kujali maadili, au makatibu muhtasi wa kike wanaoajiriwa maalumu kwa ajili ya kuvutia wateja. Haya yote ni mambo yasiyokubalika kabisa. Tunapoweka mkazo kwenye utajiri wa dunia kuliko mapato ya Akhera, siku zote umimi na ubinafsi wetu utatoa udhuru kwa kusema, "Hivi ndivyo mambo yalivyo!" Ni bomu la kufilisika litakalolipuka huko Akhera.

Kwa hiyo, katika maisha ya kibiashara na kiuchumi, kila kitu kinatakiwa kudurusiwa na kushughulikiwa kwa makini na uangalifu mkubwa. Tunapaswa kuwa makini kuhusu wale tunaowaajiri, hatupaswi kabisa kuvunja na kukiuka taratibu za Uislamu kwa sababu yoyote ile. Hatupaswi kuwalazimisha wanawake kufanya kazi za wanaume, au kuwalazimisha wanaume kufanya kazi za wanawake: watu hawapaswi kulazimishwa kufanya kila kitu kinachokinzana na maumbile yao. Maadili na misingi ya Kiislamu iliyoweka viwango vitukufu na vya hali ya juu kabisa ndiyo inayotakiwa kuwa muongozo wetu. Tunapaswa kuwa makini na wajibu wetu kama waja na kuchunga haki za wengine.

Mtukufu Mtume ﷺ kabla hajafariki aliusia kuwa, "Shikamaneni na swala, na muogopeni Mwenyezi Mungu kuhusu haki za wale walio chini ya uangalizi wenu!" (Abû Dâwûd, Adab, 123-124/5156; Ibn Mâja,Wasâyâ, 1) Katika uhai wake alikuwa makini sana kuhusu haki za viumbe vyote, lakini muda mfupi kabla ya kifo chake alifanya kitu kilichoonesha umuhimuwa haki za watu wengine. Licha ya kuwa dhaifu sana, alikwenda msikitini na kuwaambia Maswahaba zake: "Enyi watu! Kama kuna tu niliyemchukulia mali yake bila kujua, basi mali yangu hii hapa na aje achukue haki yake! Na kama kuna mtu niliyempiga, basi huu hapa mgongo wangu na aje anipige!..." (See Ahmad, III, 400)

Baada ya kusikia maneno haya, Maswahaba walianza kulia.

Maneno haya yanatuonesha umuhimu wa haki za watu wengine. Kwa tukio hili, Mtukufu Mtume ﷺ alitoa mfano kwa umma wake – mfano ambao unaweza kuigwa na umma wake mpaka Siku ya Mwisho. Ni wajibu wetu kutenda kwa mujibu wa miongozo hii iliyotolewa na mfano huu.

Uvunjaji wa haki za wengine ni aina ya ujinga na dhulma mbaya ambayo itaendelea mpaka Siku ya Hukumu, na hiyo itawapeleka wahusika kwenye maangamizi ya milele.

Leo hii, ubepari hauheshimu haki za wengine. Unawakandamiza zaidi wale ambao tayari ni wanyonge. Mabepari hukichukulia kila kitu kuwa ni halali. Lakini kwa Waislamu, kuna vitu ambavyo ni haramu.

Kwa mukhtasari, leo hii tunahitaji kujikosoa sana, hali itakayotuzindua! Kwa wakati huu, mali zimewaghilibu watu. Hata hivyo, watu wanatakiwa kuzighilibu na kuzitawala mali badala ya wao kutawaliwa na mali.

Tunawezaje kufanikisha hili, ilhali pesa ni msingi wa ubepari na kila kitu kinatawaliwa na ubepari?

Ili kufanikisha hili tunatakiwa kuitawala pesa badala ya kutawaliwa na pesa. Na hili linaweza kufikiwa kwa kufuata maagizo na maamrisho Mtawala wa watawala.

Tazama jirani yako. Kuna watu wenye fursa nyingi za kimaada, lakini hawana amani. Baadhi yao hupatwa na wendawazimu. Ukilinganisha maisha ya sasa na ya zamani, kiwango cha utajiri na ustawi kimeongezeka sana – lakini matukio ya msongo na wendawazimu yameongezeka. Maisha ya kifamilia yameharibika.

Matukio ya talaka yameongezeka. Watoto wanakumbana na hali za kutisha. Kizazi kisichokuwa na mazingira ya familia yenye amani hutafuta furaha mitaani. Wanabaki kusubiri huruma ya mitaani. Mfumo wa kibepari wenye umimi, ambao hautambui tofauti ya halali na haramu, umeshindwa kuleta amani katika jamii yetu.

Nurettin Topçu, niliyosoma naye wakati nikisoma katika shule ya Imam Hatib High school, alikuwa akituuliza, "Nani mwenye furaha zaidi, watu wa sasa au wale walioishi zamani?" Kisha alikuwa akilijibu swali hilo kwa undani, akifafanua jinsi watu wa zamani walivyoishi kwa furaha na jinsi watu wa sasa walivyokosa amani na huruma.

Mheshimiwa Ustadh! Kuwa tajiri inaonekana kuwa mtihani mgumu.

Kuwa tajiri na kuwa maskini, vyote viwili ni mtihani mgumu, inategemea na mazingira. Hakuna kilicho rahisi kuliko kingine. Hivyo sikumaanisha kuwa ili uwe na amani lazima uwe masikini! Msisitizo wangu juu ya dhima zetu na umuhimu wa kuchunga mipaka ya Mwenyezi Mungu kusikupelekee kudhani kuwa umasikini unatakiwa kuhamasishwa. Unatakiwa kujua kuwa Uislamu hauwakatazi watu kuchuma mali. Kinyume chake, amri ya *"toa sadaka*" imerudiwa mara mia mbili ndani ya Qur'an Tukufu. Huu unaweza kuchukuliwa kama ushauri kwamba watu watafute mali za kutosha ili waweze kutoa sadaka. Nukta ambayo tungependa kuibainisha hapa ni kuwa, mtu hapaswi kwenda mbali zaidi ya mipaka ya Mwenyezi Mungu ya ugawaji wa riziki, ambayo ni mipaka ya qadari. Hapaswi kudhani kuwa nyenzo zote zinaruhusiwa katika kupata mali. Bali ni muhimu kuchuma kiwango cha riziki ya halali tuliyotengewa na Mwenyezi Mungu, na tujitahidi kuwa na sifa za kutuwezesha kutoa sadaka.

Kwa hakika, tunahitaji watu wakarimu wenye mapato ya halali wanaoweza kukusanya mali za kutosha ili kuwasaidia masikini na wenye shida. Watu hao walihitajika zamani, na leo hii wanahitajika pia.

Nukta ya muhimu ni kwamba hatupaswi kupoteza amani ya moyo kwa ajili ya mali. Hatupaswi kuiharibu amani ya moyo inayotokana na neema za Uislamu. Tunatakiwa kuwa watu wa upendo, na tusisahau kuwa utajiri wa kweli na usiokuwa na kikomo unapatikana katika uhai wa moyo.

Je, hatuwezi kuchukua mfano wa Abu Hanifah, ambaye alijishughulisha na biashara na pia alikuwa mwanazuoni mkubwa wa Kiislamu?

Ndiyo, ni hakika kabisa. Abu Hanifah (muasisi wa madhehebu kifiqhi ya Hanafi inayofuatwa na idadi kubwa ya Waturuki), ni mtu wa mfano katika matendo mema, na pia katika uanazuoni. Mwenendo wake wa mfano katika miamala yake kibiashara, unaonesha sifa tukufu ambazo mtu angependa kuiona katika shakhsia ya Muislamu. Tunaweza kusema kuwa tunahitaji kufanya kampeni ya kushikamana na tunu za kimaadili kama za Abu Hanifah katika jamii ya leo, ambayo hisia za mshikamano zimedhoofika, amani na utulivu wa kijamii vimepotea, na chuki na uhasama vimeenea. Kuna visa vingi kumhusu, lakini hapa nitatoa kisa kimoja tu:

Abu Hanifa alikuwa mtu mwenye mali ambaye alijipatia riziki yake kupitia shughuli zake za kibiashara. Kwa kuwa alikuwa ameshughulishwa na kusoma na kufundisha, aliwaajiri mawakala kumfanyia shughuli za biashara kwa niaba yake. Abu Hanifah alikuwa akifuatilia kuona kama shughuli za mawakala hao zinaendana na taratibu za kidini. Alikuwa makini sana katika suala hili. Siku moja alimtuma mshirika wake wa biashara Hafs ibn Abdurrahman kwenda kuuza nguo. Akamwambia: "Ewe Hafs! Mzigo huu wa nguo

una mapungufu haya na haya. Hivyo hakikisha wateja wanaelewa kuhusu mapungufu haya, na uuze kwa kiasi kadhaa cha punguzo."

Hafs aliuza mzigo huo kwa bei iliyoelekezwa na Abu Hanifah! Lakini, alisahau kumwambia mnunuzi kuhusu mapungufu ya nguo husika. Abu Hanifah alipogundua hali hiyo, akamuuliza Hafs ibn Abdurrahman, "Unamfahamu mteja aliyenunua nguo ile?" Hafs akasema kuwa hakuwa akimfahamu…

Imam Abu Hanifa aliposikia hivyo, aliitoa sadaka pesa yote iliyokuwa imepatikana kwenye nguo hiyo. Alihofia kuwa pesa iliyopatikana kwa bidhaa ambayo mapungufu yake hayakuainishwa isije ikaharibu uhalali wa mapato yake. Mwenendo wa aina hii, uliotokana na khofu yake kwa Mwenyezi Mungu, ulileta baraka kwenye biashara ya kimaada na ya kiroho ya Abu Ahanifah.

Ili kuelewa kama mtu fulani ni mwema, mwenye udhati wa moyo na mwaminifu, tusiangalie ibada anazofanya, bali hali ya kiroho anayofanyia ibada zake hizo. Yaani, tunatakiwa tuangalie kama mwenendo wake unaendana na maadili ya Kiislamu na kama kipato chake kimepatikana kwa njia za halali. Siku moja mtu mmoja alimsifu mtu fulani mbele ya Umar ﷺ, akamuuliza mambo matatu: "Umewahi kuishi na mtu huyo? Umewahi kusafiri pamoja naye? Umewahi kufanya naye biashara?" Mtu huyo akajibu: "hapana". Umar akamwambia: "Hivyo basi usimsifu, kwa sababu humjui vizuri."

Vilevile, Abu Sufyani ath-Thawri (q.s) anasema: "Kiwango cha hali ya kiroho ya mtu husadifiana na kiwango cha uhalali wa mkate wake." Siku moja, mtu fulani akamuuliza, "Ewe mwalimu! Tafadhali waweza kutwambia thamani ya kuswali katika safu ya kwanza msikitini?" Badala yake, alianza kuzungumzia kuhusu umuhimu wa chumo la hahali. Kisha akasema: "Ndugu yangu! Kwanza angalia jinsi unavyopata chakula chako! Kama chumo

lako ni la halali, basi nenda kaswali katika safu yoyote unayotaka. Hutapata ugumu wowote kuhusu jambo hilo."

Marehemu baba yangu, Musa Efendi (q.s) alikuwa akihadithia kisa kifuatacho kuonesha umuhimu na baraka inayopatikana pindi watu wanapopata riziki yao kwa njia za halali, na kuacha kuchanganya mapato yao ya halali na yale ya haramu:

Tulikuwa na jirani asiyekuwa Muislamu. Baadaye akasilimu. Siku moja nikamuuliza kwa nini alifanya hivyo, akaniambia: "Nilisilimu kutokana na maadili matukufu ya Rebî Molla katika biashara zake. Mimi nay eye tulikuwa na ardhi zinazopakana. Rebî Molla alikuwa akipata riziki yake kwa kuuza maziwa. Jioni moja alikuja nyumbani kwetu na kutuambia, "Chukua maziwa haya ni yako!"

Nilishangazwa, nikasema: "Hilo linawezekanaje? Sikukuomba maziwa!"

Alikuwa mtu mnyoofu na mwenye utambuzi. Akasema: "Nilimuona mmoja wa mifugo yangu akila katika shamba lako. Sikuweza kusema alipoingia katika shamba lako, au alikwenda kwa umbali gani. Ndiyo maana ndoo hii ya maziwa ni yako. Mpaka mwisho wa mzunguko wa umeng'enyaji wake nitakuwa nikikuletea maziwa."

Nikasema: "Hakuna tatizo jirani yangu! Hayo ni majani na mimea tu. Sitaki kukudai chochote!"

Lakini Rebî Molla akasema, "Hapana, hapana, siwezi kulikubali hilo. Haya maziwa ni haki yako!" Aliendelea kutuletea maziwa ya mnyama yule mpaka mwisho wa mzunguko wa umeng'enyaji wake.

Tabia ya mtu huyo mwema ilinigusa na kuondosha vifuniko kwenye macho yangu. Hivyo jua la muongozo wa Mwenyezi Mungu likachanua. Nilisema moyoni: "Bila shaka dini ya mtu mwenye tabia tukufu kama hiyo itakuwa ni dini bora. Nani anayeweza kuutilia shaka ukweli wa dini ambayo wafuasi wake ni wanyoofu, wenye kujali haki za wengine, wakamilifu na wenye udhati wa moyo kiasi hicho?" hivyo nikatamka maneno ya shahada na kuwa Muislamu mimi mwenyewe."

Mifano hii inaonekana kuwa ya hali ya juu sana kueleweka katika ulimwengu wetu unaoongozwa na pesa. Bila shaka pia kuna mifano mingi mizuri! Mwisho, una wosia upi wa moja kwa moja kwetu?

Visa hivi vyenye hekma vinaonesha wazi ni kwa kiwango gani tunatakiwa kuwa makini katika suala la chumo na mapato ya halali na haramu. Mapato ya halali ni sehemu muhimu sana ya *taqwa*, yaani Uchamungu. Ndiyo maana Mtukufu Mtume ﷺ anasema: "Kibarua mwaminifu na mwenye kuaminika atakuwa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, wakweli na mshahidi." (Tirmidhî, Buyû', 4) Kwa sababu mtu mfanyakazi mwenye moyo wenye hisia huwa wakala wa amani na baraka kwa wote wanaokutana naye. Kwa sababu hiyo anapata furaha ya duniani na Akhera. Lakini, kwa wale walioshindwa na tamaa ya dunia, hali ni tofauti. Japokuwa wanaweza kuonekana kuwa wana maisha mazuri ya kidunia, hakika watu hao ni masikini na mafukara wa maisha ya milele huko Akhera.

Mtukufu Mtume ﷺ hakuwahesabu kuwa katika umma wake wale wenye ulafu katika biashara na wenye kuwadanganya wengine. Aliwatoa kabisa katika umma wake. Soma kisa kifuatacho:

Siku moja Mtukufu Mtume ﷺ alimtembelea mfanyabishara mmoja sokoni. Aliuingiza mkono wake kwenye fungu la ngano na kuhisi kuwa ulikuwa umeloa. Akauliza, "Nini hii?"

Mtu yule akajibu: "Mvua ndiyo iliyoulowesha, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!"

Mtukufu Mtume ﷺ akasema: "Kwa nini sehemu iliyolowa hukuiweka upande wa juu ili wateja waione? Wale wenye kutudanganya sio katika sisi." (Muslim, Imân, 164)

Vilevile, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ﷺ anasema: "Kila umma una mtihani. Mtihani wa umma wangu ni mali." (Ahmad ibn Hanbal, IV, 160)

Akasema tena: "Zitakuja zama ambazo watu hawatajali kama wanapata mali zao kwa njia za halali au za haramu." (Bukhârî, Buyû', 7, 23)

Vilevile akasema: "Ninahofia baada ya kuondoka kwangu kuwa mtaletewa maua (mali) na mapambo ya dunia. Na mnaweza kuangukia katika shimo la kuvipenda!" (Bukhârî, Jihâd, 37; Muslim Zakâh, 121-123)

Siku moja, wakati akizungumza na Maswahaba, alisema: "Sihofii kwenu umasikini. Bali ninahofu kwamba dunia itatandazwa mbele yenu, kama ilivyotandwa kwa wale waliokuwa kabla yenu. Na ninahofu kwamba mtaishindania kama walivyofanya waliokuwa kabla yenu. Na ninahofu kwamba itawaangamizeni kama ilivyowaangamiza waliokuwa kabla yenu." (Bukhârî, Riqâq 7, Jizya 1; Muslim, Zuhd, 6)

Maneno haya yanaonekana kuelezea kwa mukhtasa hali ya sasa ulimwenguni. Watu wanaoonesha mghafala ulioelezewa katika maneno hayo ya Mtukufu Mtume ﷺ wanaweza kuona tabu sana

kuacha matendo ya haramu. Na kama nyoyo zao haziwezi kuacha ya haramu, itakuwa changamoto kubwa, na wakishikamana na halali itahesabiwa kuwa ni ibada.

Waislamu wa sasa wanapaswa kufanya juhudi kubwa ya kujilinda na shari za ubepari. Tujihadhari dhidi ya kuifanya pesa kuwa hima na matamanio yetu! Badala yake, tushikamane na sifa zinazowastahiki waja wema. Tumche Mwenyezi Mungu, kwa hali yoyote ile, tutafute radhi zake, tuwe wenye huruma katika jamii, kuing'ang'anie misingi ya maadili ya Kiislamu, tuheshimu haki za wengine, na tuchunge mipaka ya halali na haramu.

Kumbuka kuwa, kutokana na hali ya sasa, kila moyo mnyoofu na wenye huruma unapaswa kuwahurumia na kuwasikitia maskini, wanyonge na wenye huzuni. Lakini wale wanaostahiki kusikitikiwa zaidi ni:

- Madhalimu wasiojitambua, wanastahiki kusikitikiwa kuliko hata wanyonge wanaowaonea;
- Watumwa wa nafsi zao, hata kama wanaishi maisha ya anasa;
- Wanyonyaji wenye roho za ulafi, wanatakiwa kusikitikiwa kuliko hata masikini wanaowanyonya.

Kwa hakika hawa ndio watu wanaotakiwa kuonewa huruma kuliko wengine. Masikitiko yetu ni njia ya kuwaokoa kutokana na hali mbaya ambazo wameangukia, na kuwasaidia kupata muongozo wa kuwapeleka kwenye njia ya haki na kweli.

Mtume wetu ﷺ anasema: "Ewe Mola wangu! Ninajilinda kwako kutokana na elimu isiyokuwa na manufaa, moyo mgumu, tumbo lisilotosheka na swala isiyokubliwa." (Muslim, Dhikr, 73)

Akasema pia: "Fanya haraka, kabla hujaangukia katika umaskini unaowafanya watu wasahau, au katika utajiri unawafanya watu wapotee!" (Tirmidhî, Zuhd, 3/2306)

Hivyo daima tukumbuke kilichoelezwa na Mtukufu Mtume ﷺ hapa: kwamba umaskini unaowafanya watu wamsahau Mwenyezi Mungu, na utajiri unaowafanya watu wapotee, vinaweza kuwa sawa.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atujaalie tuishi tukiwa tumezungukwa na neema Zake! Atuepushe na vitu vyote vya haramu au vyenye kutiliwa shaka!

Amiin!

FOR FREE IN PDF FORMAT

ISLAMIC WORKS

YOU CAN DOWNLOAD IN PDF FORMAT

1350 BOOKS IN **60 LANGUAGES** FOR FREE

Islamic books in different languages are waiting
for you in PDF format at the web site
www.islamicpublishing.org

ERKAM PUBLICATIONS | islamicpublishing.org |